

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Thelathini na Nne - Tarehe 27 Julai, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

MHE. HASSAN RAJAB KHATIB - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 315

Ugawaji wa Chakula cha Msaada - Nanyumbu

MHE. ARIDI M. ULEDI aliuliza:-

Kwa kuwa katika msimu wa mwaka 2003/2004 Jimbo la Nanyumbu lilikumbwa na upungufu mkubwa wa chakula kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za ukame na wanyama waharibifu wa mazao na kwa kuwa Serikali ilisambaza chakula cha msaada katika baadhi ya vijiji vilivyomo katika Jimbo la Nanyumbu na vijiji vingine kukosa mgao huo na kwa kuwa ule upungufu wa chakula ulivikumba vijiji vyote vya Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali ilitumia mwongozo gani katika kugawa chakula hicho cha msaada?

(b) Je, ni vijiji vingapi vilipata chakula hicho na ni kiasi gani na ni vijiji vingapi havikupata msaada huo na ni kwa sababu gani?

(c) Kwa baadhi ya vijiji kukosa chakula hicho cha msaada Serikali haioni kuwa haikuwatendea haki wananchi wa vijiji hivyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aridi Mwananche Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ilitumia taarifa ya tathmini iliyofanywa na wataalamu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo na Chakula, wadau mbalimbali na Sekretariati za Mikoa kuanzia tarehe 29 Juni hadi tarehe 13 Julai, 2003. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi chini ya usimamizi wa Mkuu wa Wilaya ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maafa ndio waliohusika katika ugawaji wa chakula cha msaada katika vijiji vilivyobainika kuwa na uhaba mkubwa wa chakula.

(b) Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nanyumbu lina vijiji 72. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na wataalamu, vijiji 43 ndivyo vilivyoonekana vina upungufu mkubwa wa chakula na vyote vilipata chakula cha msaada wa jumla ya tani 1,582. Vijiji ambavyo havikupata msaada wa chakula cha njaa ni 29 na hii ni kutokana na hali ya chakula katika vijiji hivi kuwa ya kuridhisha.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika majibu ya sehemu (a) na (b), vijiji ambavyo havikupatiwa msaada havikuachwa kwa makusudi, bali vijiji hivi vilionekana vinajitosheleza ukilinganisha na vijiji vingine. Hivyo suala la kutotendewa haki halipo kwani Serikali ilifanya kila jitihada ili kuwapatia wananchi wote waathirika wa chakula

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwa kuwa njaa katika msimu wa mwaka 2003/2004 ulikumba Vijiji na Kata na Tarafa zote za Jimbo la Nanyumbu, kwa kuwa mahindi ya bei nafuu ya shilingi 50/= kwa kilo yaligaiwa kwa ubaguzi kwa vijiji vichache na kuviacha vijiji vingi havina msaada huo na kwa kuwa wananchi katika vijiji ambavyo walikosa mahindi hayo waliwatupia lawama viongozi wao wa Vijiji na Kata kuwa ndiyo waliosababisha wao kukosa mahindi hayo ili rafiki zao ambao ni wafanyabiashara waweze kuuza.

SPIKA: Uliza swali, je?

MHE. ARIDI M. ULEDI: Je, Serikali haioni kuwa viongozi wa vijiji na Kata wanaolaumiwa kwa mapungufu yaliyotokea katika ugawaji wa mahindi hayo ni kwamba wanaonewa kwa sababu hawakuhusika katika ugawaji huo?

La pili, je, Serikali kama hivyo ndivyo haioni kuwa ni juu yake iwaombe radhi viongozi hao ambao wengi wao waliibiwa mazao yao mashambani na wananchi wenye njaa? (*Makofit*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB): Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali ilitoa mwongozo maalum kwa nchi nzima namna ya kutambua wale watu ambao wameathirika na njaa na mwongozo huu uliwafikia viongozi wa Wilaya, viongozi wa *ward* na viongozi wa vijiji. Siamini kwamba viongozi wa eneo hilo wataweza kuwanyima watu wao wenyewe ili kupata chakula hiki, haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni kwamba hatuna taarifa kwamba palikuwa na ubaguzi katika eneo hilo na dhamana kubwa ya ugawaji huu ni ya Mkuu wa Wilaya ya Masasi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aridi Uledi, hatuamini kwamba viongozi wa Serikali hii, viongozi wa Chama Tawala wataweza kuwanyima watu wao chakula, wafe na njaa ambapo chakula hicho kinatolewa na Serikali ili kuwasaidia wao.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kila msimu wa kilimo wa mwaka 2004/2005 huwa kuna njaa, je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na tatizo hili hasa kwa sasa yanapokuwa mahindi yapo mengi lakini *SGR* hainunui?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB): Mheshimiwa Spika, sijui utafiti wake kaufanya wapi, lakini siamini kwamba kila mwaka kipindi hiki kunakuwa na njaa katika nchi hii haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali imejiandaa, katika hotuba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, amesema kwamba mwaka huu tayari ametengewa fedha kwa ajili ya kuweka akiba angalau ya tani 100,000 kwa ajili ya kukabiliana na hali ya njaa nchini kwetu.

Na. 316

Madalali Wasio Waaminifu Kuwatapeli Wakulima

MHE. ESTHERINA KILASI aliuliza:-

Kwa kuwa soko la Tandale, lililoko Jijini Dar es Salaam ni moja kati ya masoko makubwa ya mazao ya chakula kwa wakulima wetu, wakiwemo wakulima toka Wilaya

ya Mbarali na kwa kuwa hivi karibuni soko hilo limekumbwa na wimbi kubwa la kuwatapeli wakulima unaofanywa na madalali wasio waaminifu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni jukumu lake la Kikatiba kulinda haki ya wakulima hao ili kuikomesha tabia hiyo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti hali hiyo ili isiendelee kuwaathiri wakulima?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli soko la Tandale ni moja kati ya Masoko makubwa ya mazao ya chakula kwa wananchi wengi wa Jiji la Dar es Salaam. Soko hili hutumiwa na wakulima wa Wilaya mbalimbali ikiwemo ile ya Mbarali na ni kweli kulitokea wimbi la utapeli lililofanywa na madalali wasio waaminifu kwa kuwatapeli wakulima mazao yao. Serikali inakiri kuwa inalo jukumu Kikatiba kulinda haki ya wakulima pamoja na mali zao. Kutokana na jukumu hili hatua kadhaa zimechukuliwa kudhibiti utapeli huo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003 Serikali imechukua mikakati mbalimbali kuhakikisha kuwa wakulima hawatapeliki mazao yao kama ifuatavyo:-

(i) Vyama vya ushirika vitatu vimeimarishwa sokoni Tandale vyama hivyo ni *Tandale Marketing Grains Sellers Association and Investment (TAMAGRASAI)*, *Tandale Vegetable Cooperative Society* na *Tandale Food Cooperative Society*.

(ii) Zoezi la kusajili madalali sokoni hivi sasa linaendelea. Usajili unachukuwa muda mrefu kidogo kukamilika kutokana na utaratibu uliozoleka ambapo wafanyakishara huwakopesha wakulima pembejeo pamoja na gharama za uvunaji na usafirishaji wa mazao hadi sokoni hapo kwa makubaliano ya kurejesha gharama hizo wakati wa mauzo.

(iii) Jumla ya madalali 11 walibainika kuwatapeli wakulima kutoka Mikoa mbalimbali walichukuliwa hatua zifuatazo:-

Madalali watatu walilipa madeni yao kuitia Kamati ya Soko la Tandale na madalali wanane walipelekwa Kituo cha Polisi cha Magomeni ambapo kati yao wanne walipelekwa Mahakamani na wale wote walibainika kutapeli wamepigwa marufuku kupokea mizigo ya wakulima sokoni Tandale.

(iv) Ili kuimarisha usalama, Kamati ya Soko la Tandale imeweka utaratibu wa kuhakiki malipo yote ya nauli wanazolipa wapokeaji wa mazao kwa niaba ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali hali ya utapeli kwa wakulima Sokoni Tandale hivi sasa imepungua kwa kiasi kikubwa na tunaamini kabisa juhudhi hizo zitakavyoendelea udhibiti huo utazidi kuimarika.

MHE. ESTHERINA KILASI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza. Majibu ni mazuri sana ya Naibu Waziri wa TAMISEMI. Pamoja na majibu mazuri na pongezi nzuri za kazi nzuri ambazo anazifanya kuhakikisha udhibiti wa utapeli, lakini nina swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ni moja, sababu kubwa ambazo zinapelekea wakulima wa Mbarali pamoja na wakulima wengine wanaolima mazao haya ya chakula ni kukosekana kwa soko la karibu au kukosekana wafanyabiashara ambao wangeweza kuwasaidia kununu kupunguza gharama za usafiri, je, Serikali ina mpango gani wa kushawishi wafanyabiashara wakubwa ambao wanapatikana Tandale na sehemu zingine ili kuweza kuwasaidia wakulima hao wapate soko kwa karibu? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, ombi la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na tunaweza kabisa tukaliwakilisha kwenye Halmashauri zinazohusika kujaribu kufanya hiyo kazi. Lakini nataka nimkumbushe kwamba biashara ni biashara. Wafanyabiashara hawa wanafanya kazi hiyo ili waweze na wao kupata pato wanadolitegemea. Kwa hiyo, kwa sehemu kubwa itategemea na wao namna watakavyochukulia gharama hizo popote pale watakapoanzisha lile soko na ndiyo maana soko la Tandale lina mvuto kwa sababu kwao linawapa nafuu zaidi.

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa soko la Tandale kimazingira na kimajengo ni soko la zamani sana na kwanza limepitwa na wakati na kwamba ukarabati au ujenzi mpya wa soko hilo unahitajika ili kupunguza matatizo kama hayo ya matapeli, je, Serikali inasemaje juu ya kukarabati au kujenga soko la Tandale upya ili kuhakikisha kwamba liwe la kisasa? Nashukuru sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peter Kabisa ni shahidi kwamba zipo juhudhi kubwa sana katika Jiji la Dar es Salaam kujaribu kuboresha masoko yetu na tumefanya hivyo katika masoko ya Temeke, tumefanya hivyo katika soko la Makumbusho na ni azma yake kuendelea kukarabati na kutengeneza masoko ya ziada ili kuwezesha Jiji hili kuwa na masoko yenye hali nzuri, likiwemo soko la Tandale.

Matatizo ya Barabara Jimboni Morogoro Kusini - Mashariki

MHE. SEMINDU K. PAWA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa muda mrefu imeyafahamu matatizo yaliyopo katika barabara za Ubena-Ngerengere-Kidunda, Ngerengere-Tununguo hadi Bwira, Mtegowasimba-Ngerengere, Lubungo-Mikese-Msomvizi, Madamu-Tegetero-Hewe:-

(a) Kwa kuwa swali hili nimeliuliza mara nyingi lakini halipatiwi majibu ya kuridhisha, je, sasa Serikali itatoa majibu juu ya matatizo yaliyopo ndani ya barabara nilizozitaja?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuzitembelea barabara hizo na kuungana nasi katika kupongeza *MVIWATA*, *TASAF* na Vikosi vya JWTZ kwa kazi nzuri waliyofanya ya kusaidia utengenezaji kwenye baadhi ya maeneo ya barabara hiyo?

(c) Je, ni lini barabara hizo zitapatiwa fedha kwa ajili ya kuzitengeneza na hatimaye kufungua mawasiliano kwa wananchi wa Mifulu, Kidunda, Tununguo, Kikunde, Kungwe, Tandai, Kalundwa na Usungura?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini - Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa sehemu nyingi hapa nchini Serikali inafahamu matatizo yaliyopo katika barabara zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Matatizo makubwa ya barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge ni pamoja na madaraja mabovu, upungufu wa makalvati, utelezi katika sehemu za milima na sehemu nyingine kutopitika kwa sababu ya kuwa ni maeneo yenye unyevunyevu mwangi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo yaliyolezwa hapo juu, Serikali pamoja na wadau wengine wakiwa ni pamoja na *TASAF*, *MVIWATA* na *JWTZ* kwa mwaka 2003/2004 wamejitahidi sana kuzifanyia ukarabati barabara za Halmashauri ya Morogoro kama ifuatavyo:-

Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro nyenyewe imetengeneza barabara ya Ngerengere - Kidunda kwa gharama ya shilingi 53,126,400/=, *TASAF* imefanya ukarabati kwenye barabara za Kibaoni-Maskati kwa shilingi 80,054,373 /=, Mngazi-Karonga shilingi 48,272,876 /=, Tandai-Tegetero shilingi 49,367,715/=, Karenge-Tande shilingi

49,038,100 /=, Tande-Singisa shilingi .45,411,200/= na Tingeni-Mnyenzo shilingi 76,709,360/. Barabara zote zimekamilika isipokuwa barabara mbili nilizozitaja mwisho.

Mheshimiwa Spika, Mtando wa Vikundi vya Wakulima (*MVIWATA*) nayo imesaidia sana katika ukarabati wa barabara hizi kwa kushirikiana na Serikali. Barabara hizo ni Madamu-Kinole kwa shilingi 366,006,300/=, Lengali-Nyandira kwa shilingi 638,963,501/= na Nyandira-Tchenzeme kwa shilingi 49,316,400/=.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la wananchi nalo limechangia kwa kufanya matengenezo katika madaraja ya Ubena na Kizuka katika barabara ya Ubena-Ngerengere. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza *MVIWATA*, *TASAF* na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi nzuri waliyoifanya na wanazoendelea kufanya za ukarabati wa barabara za Halmashauri ya Morogoro. Serikali ipo tayari kabisa kuzitembelea barabara hizo na kuungana na wananchi wa Wilaya ya Morogoro katika kuwapongeza wadau wote na tayari tumeshawasiliana na Mkuu wa Mkoa ili niweze kufanya ziara hiyo katika Mkoa wa Morogoro.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye sehemu ya (a) Serikali inaendelea kufadhili matengenezo na ukarabati wa barabara kwenye maeneo yaliyotajwa na kwa mwaka 2004/2005 barabara zifuatazo zimeombewa fedha:-

Kwanza ni barabara ya Ubena-Ngerengere kwa gharama ya shilingi 12,052,000/=, barabara ya Mtegwasimba-Ngerengere kwa shilingi 126,8000,000/=, barabara ya Madamu-Kinole kwa shilingi 185,102,000/=, barabara ya Kinole-Tegetero kwa shilingi 3,658,000/= na barabara ya Ngerengere-Kidunda kwa shilingi 295,166,000/=.

Aidha, barabara ya Tegetero-Hewe imepangwa kufanyiwa ukarabati katika awamu ya pili ya mradi wa *TASAF* kwa gharama ya shilingi 50,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini-Mashariki, kwa ufuatiliaji wa karibu sana katika masuala yanayohusiana na barabara katika eneo lake. (*Makofi*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza ni kwamba katika majibu yake alieleza barabara za Jimbo la Kaskazini tu yakiwemo Nyambila na maeneo mengine, je, nani kajibu swali hili ambalo lilikuwa linaelekeza maeneo mengine yalifanywa mafanikio bila kutaja barabara ambazo zimo katika hili swali la msingi, mfuatilie na ichukuliwe hatua za kinidhamu.

Halafu pili, kwa kuwa napongeza nimeshapata fedha, wananchi wamesikia kwamba zipo fedha za kutengeneza barabara hizi na wananchi wanafuatilia hii, je, ushauri Halmashauri hii kutumia kandarasi maeneo hayo na ye ye mwenyewe aje azitembelee barabara hizo baada ya Bunge hili? Ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa pengine baadhi ya barabara tumeziacha wakati wa kujibu swalii hili kwa kuwa swalii lenyewe lilikuwa na maeneo mengi ambayo alikuwa ametaka tuyazingatie. Lakini tutalifanyia kazi ya ziada na tutakupa majibu kwa maandishi kuhusiana na hayo maeneo ya nyongeza. (*Makofi*)

Kuhusu swalii la pili, nimekwishasema nitajitahidi kufanya ziara hiyo mara tu baada ya Bunge hili na tutashirikiana na Mheshimiwa Semindu Pawa, kwa karibu katika suala hili.

Na. 318

Uharibifu wa Mazingira Kutokana na Uchimbaji Holela wa Mchanga Dodoma

MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF aliuliza:-

Kwa kuwa Dodoma ni mji mteule wa Makao Makuu ya Serikali na kwa kuwa moja ya majukumu ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mazingira ya Dodoma yanatunzwa na kuendelezwa na kwa kuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma Mjini wameshindwa kudhibiti uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji holela wa mchanga katika maeneo ya Medeli, Dodoma Makulu, Ipagala, Kisasa, chini ya madaraja na kwenye makorongo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvisaidia vyombo hivyo viwili katika kuthibiti uchimbaji huo wa mchanga unaosababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye maeneo niliyotaja?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini ikiwa ni pamoja na mchanga, kokoto, mawe, kifusi unasimamiwa na Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Kwa mujibu wa sheria hiyo ni makosa kufanya shughuli za uchimbaji wa Madini bila leseni ambayo huonyesha maeneo yanayoruhusiwa kufanya uchimbaji. Manispaa ya Dodoma kwa kushirikiana na uongozi wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu tayari wametenga maeneo maalum kwa ajili ya uchimbaji wa mchanga. Maeneo hayo ni Mtumba, Kikombo, Nzuguni, Michese, Mkonze na Ntyuka.

Kwa kutumia sheria ya Madini Manispaa ya Dodoma kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Ofisi ya Madini na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini wana wajibu wa kudhibiti uchimbaji holela wa mchanga katika maeneo yaliyopimwa viwanja na makorongo unaosababisha uharibifu wa mazingira.

Hata hivyo kuna wakorofii wachache wanakiuka sheria na taratibu hizo zilizowekwa. Manispaa kwa kushirikiana na vyombo vyaa dola isisite kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaopatikana wakichimba mchanga katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo ya Serikali kuwa wananchi katika maeneo yao wataendelea kushirikiana na Serikali katika udhibiti wa uharibifu wa mazingira ya maeneo wanamoishi.

MHE. NJELU E. M. KASAKA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Samahani, sikumwangalia Mheshimiwa Hashim Saggaf, lakini ameridhika. Endelea.

MHE. NJELU E. M. KASAKA: Mheshimiwa Spika, nilitaka niulize kwamba kwa kuwa uchimbaji wa mchanga ni moja tu ya mambo ambayo yanaharibu mazingira. Lakini pia kuna suala la uchafu wa mifereji ya maji machafu hapa mjini Dodoma pamoja na utupaji hovyo wa mifuko ya lambo ya *plastic* pamoja na chupa za *plastic*, je, Serikali katika umoja wake kwa ushirikiano na TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuzingatia hili suala la usafi wa mazingira kuna hatua gani zitachukuliwa kuhakikisha kwamba angalau Mji wa Dodoma licha ya kuwa na barabara mbaya lakini angalau usafi wa mifereji unazingatiwa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Spika, suala la usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na tatizo kubwa tunalolishuhudia sote la kuzagaa kwa mifuko ya *plastic* au mifuko ya *rambo*. Tunapouliza kwamba hivi Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na tatizo hili, nilikuwa naangalia Katiba yetu katika Ibara ya 27, inatamka juu ya kile tunachokisema juu ya haki na wajibu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa upande wa Serikali tuna wajibu wa kuhimiza na kuhamasisha uelewa wa suala la umuhimu wa utunzaji wa mazingira. Lakini pia Katiba hii hii inatamka dhahiri kwamba kila raia, kila mwananchi ana wajibu wa kutunza mazingira. Ninachoomba tushirikiane tutekeleze Katiba yetu.

SPIKA: Mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa sheria zikishapitishwa na Bunge ni Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa hiyo, swali hili litajibiwa na Waziri Mkuu au kwa niaba yake na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Na. 319

Sheria zilizopitishwa na Bunge katika Kipindi cha 2000-2004

MHE. MOHAMED H. MISSANGA aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge katika kipindi cha 2000 hadi 2005 limetunga sheria kadhaa kukidhi matakwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii:-

- (a) Je, ni sheria ngapi zilizotungwa na kupata kibali cha Mheshimiwa Rais?
- (b) Je, ni sheria zipi kati ya hizo zimeanza kutumika?
- (c) Je, ni sheria ngapi ambazo zimepata kibali cha Mheshimiwa Rais lakini hazijaanza kutumika na kwa nini?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge limekwisha kutunga jumla ya Sheria 103 na zote zimepata kibali cha Mheshimiwa Rais.

- (a) Sheria zilizoanza kutumika ziko 91 na kwa kuwa orodha ni ndefu nitampatia Mheshimiwa Mohamed Missanga, nakala ya orodha hii.
- (b) Sheria zilizokwisha pata kibali cha Rais lakini bado hazijaanza kutumika ziko 12. Baadhi ya Sheria hizo zimepitishwa na Bunge na kupata kibali cha Rais hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Ofisi yangu itafanya kila lililo ndani ya uwezo wake ili kuhakikisha kwamba kila Waziri mwenye dhamana kwa kila sheria ambayo haijaanza kutumika anakamilisha mapema maandalizi yanayohitajika na kila sheria husika ikiwa ni pamoja na kuunda vyombo mbalimbali vinavyohitajika kusimamia na kutekeleza sheria hiyo. Baada ya kukamilisha maandalizi hayo, kitakachofuata ni wa Waziri mwenye dhamana na sheria husika kutoa tangazo katika Gazeti la Serikali kuhusu tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya kuridhisha kwa wastani yaliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Katika swali langu la msingi (c) nilitaka kujua sababu ambazo zimepelekea hizo sheria 12 ambazo amezitaja hazijaanza kutumika. Hajaeleza ni sababu zipi zimepelekea mpaka sheria hizo hazijaanza kutumika?
- (b) Kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekiri kuwa zipo sheria ambazo hazijaanza kutumika ambazo ni 12, je, hii haidhahirishi kwamba kuna udhaifu katika maandalizi ya kuwasilisha Miswada ya Sheria hapa Bungeni au haidhahirishi kwamba

wakati mwingine kuna baadhi ya Miswada inaletwa kutokana na shinikizo kutoka nje ya nchi? (*Makofî*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nikianza na swali lake dogo la pili. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Serikali huru na wala haipati shinikizo kutoka mahali popote inapoleta Miswada hapa Bungeni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Miswada inayoletwa hapa Bungeni inaandaliwa kwa makini kwa kuzingatia mahitaji na mazingira ya wakati wa nchi yetu. Kuhusiana na swali lake dogo la kwanza sababu kwa nini zile sheria 12 zimepata kibali cha Rais lakini hazijaanza kutumika.

Kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi na nimeahidi kumpatia Mheshimiwa Mohamed Missanga, orodha ya sheria hizo lakini katika hizi sheria 12 kama atakavyoona sheria hizo zinahitaji maandalizi mazuri sana kwanza kwa upande wa Kanuni ukichukua mathalani sheria ya Makampuni. Sheria ya Makampuni inahitaji maandalizi makubwa sana.

Kwa upande wa kanuni, ina kanuni nyingi sana pia inahusisha wadau wengi sana mfano Wahasibu, Wanasheria, Wakaguzi na Idara ya Mahakama. Ili uweze kuhakikisha kwamba sheria inaanza vizuri, kwa kishindo, maandalizi yote haya ni ya muhimu sana katika kufanikisha azma ya kutunga sheria husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna aina ya udhaifu wowote lakini ni nia njema tu ya kutaka kuhakikisha kwamba sheria hizi zinapoanza kutumika zitumike vizuri.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba sheria nyingi tunazozipitisha hapa Bungeni na kusainiwa na Mheshimiwa Rais mara nyingi zinakuwa henzieleweki kwa wananchi walio wengi ambao kimsingi ndio walengwa wanaotungiwa sheria hizi, je, Serikali inalitambua jambo hilo na iwapo inalitambua ni taratibu gani ambazo Serikali inaziandaa kuwezesha sheria hizo kueleweka kwa wananchi katika njia rahisi na inayoteklezeka?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, wakati anawasilisha hoja yake hapa Bungeni alisema Serikali inatambua tatizo hilo na ndio maana imeahidi kupitia Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba tutaongeza kasi ya kutafsiri sheria zinazopitishwa na Bunge lako katika lugha ya Kiingereza ziweze kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kwa kuimarisha Kitengo cha Tasfiri katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunajibu swalí linalofanana na swalí la nyongeza la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, humu Bungeni tulisema kwamba kwa sasa hivi na hata kwa kipindi kinachokuja sheria nyingi zitaendelea kuandikwa katika lugha ya Kiingereza kwa sababu Kiingereza ndio Kiswahili cha dunia na pili ni lazima tutambue kwamba uhandishi wa sheria ni taaluma maalum ambayo lazima tuendelee kuijenga katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili tunapotunga sheria katika lugha ya Kiswahili kweli ziendane na misingi inayokubalika ya uhandishi wa sheria.

Na. 320

Idara ya Maendeleo ya Jamii

MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii ni dira kwa Idara nyingine inayoelekeza njia sahihi ya kupita wakati wa kupeleka mpango wa Idara yoyote kwa jamii (*approaches*) na kwa kuwa ili ishauri *approach* sahihi ni lazima Idara ifanye utafiti na hata kutoa elimu kwa jamii juu ya mpango husika na pia Idara huwa kama kiungo kati ya Halmashauri na jamii na kati ya Idara na Idara:-

(a) Je, kwa kuzingatia umuhimu wa kazi hizo, Serikali haioni haja ya kuhakikisha kwamba kila Kata inapatiwa Afisa Maendeleo ya Jamii?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiweka Idara hiyo katika Idara nyeti ili zipate ruzuku toka Serikali Kuu kama ilivyo Idara ya Afisa Kilimo na kadhalika ili shughuli zake zisikwame na pia Serikali haioni umuhimu wa kuagiza Halmashauri katika Mpango wa *Local Government Reform* kutouunganisha Idara hiyo na zingine ili shughuli za Idara zisimezwe na Idara nyingine?

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuwapa pipipiki, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swalí la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo umuhimu wa kila Kata kupatiwa mtaalam wa Maendeleo ya Jamii. Kwa hakika, hilo ndilo linaloelekezwa na sera yetu ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 ambayo imesisitiza kuwepo na angalau mtaalam mmoja wa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti na Serikali kusitisha ajira katika baadhi ya sekta, watumishi wengi katika Idara mbalimbali ikiwemo Idara ya Maendeleo ya Jamii hawajaweza kuajiriwa. Hali iliyopo katika Mkoa wa Mtwara ambao una jumla ya Kata

107 unao Maafisa wa Maendeleo ya Jamii 54 tu, mmoja akiwa Mkoani, 18 katika Makao Makuu ya Wilaya na 35 tu ndiyo waliopo kwenye ngazi ya Kata. Hivyo itachukua muda mrefu kabla azma yetu ya kuwa na Afisa Maendeleo ya Jamii kwa kila Kata kutimia.

Aidha, suala la ajira limekuwa likishughulikiwa kwa umakini mkubwa na Halmashauri kwa kuendelea kuomba na kujaza nafasi zilizo wazi katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(b) Mheshimiwa Spika, kimsingi katika Halmashauri za Wilaya, hakuna Idara nyeti na zisizo nyeti kwani Idara zote zinategemeana na zina umuhimu sawa. Katika kutekeleza mkakati wa kuondoa umaskini na kuinua hali ya uchumi wa wananchi, Serikali ilibainisha sekta za kipaumbele ambazo ni afya, elimu, maji, kilimo, barabara vijijini.

Mheshimiwa Spika, sekta hizi hupewa kipaumbele katika mgawanyo wa raslimali ya Taifa kwa kutengewa ruzuku (*OC*) toka Serikali Kuu na Idara nyingine zilizobakia ikiwemo ya Maendeleo ya Jamii zinahudumiwa na Halmashauri kutokana na vyanzo vya mapato vya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua katika mpango wa maboresho wa Serikali za Mitaa kupitia *Local Government Reform* ni kupitia upya muundo wake kulingana na mazingira halisi. Hivyo basi, zipo Halmashauri zilizoamua kuunganisha Idara zake kwa lengo la kuleta ufanisi zaidi. Uamuvi wa kuunganisha Idara hizo hufanywa kwa makini kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Hivi sasa zoezi la kuangalia upya miundo ya Halmashauri linaendelea katika Halmashauri 38 za maboresho awamu ya kwanza. Hakuna sera ya jumla ya kuunganisha Idara ya Maendeleo ya Jamii na Idara nyingine bali kila Halmashauri huamua kadri wanavyoona inafaa na pale ambapo Idara hii imeunganishwa na Idara nyingine shughuli za Maendeleo ya Jamii zitaendelea kufanyaika chini ya Idara mpya kwa kutumia watumishi waliopo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata kupewa vyombo vya usafiri ili waweze kuwafikia wananchi vijijini kwa urahisi. Hali ya uchumi itakapokuwa nzuri, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI zitaangalia uwezekano wa kuwapatia wataalam wa Maendeleo ya Jamii na wataalam wengine kwenye Halmashauri vitendea kazi kama vile vyombo vya usafiri na zana zingine za kufanyaika kazi.

MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ila nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa shughuli za maendeleo ya jamii ni *coordinative* kati ya Idara na Idara nyingine, Idara ya Maji wanaweza kwenda kijijini kuchimba bwawa, Idara ya Afya kufukia bwawa kwa sababu ya mbu, Idara ya Maendeleo inabidi ifanye *coordination*, bwawa liwepo na ngao itumike, je, Serikali iko tayari kuwapa semina wataalam wa Idara

zote ili wasione Idara ya Maendeleo ya Jamii inaingilia kila kazi wakati ni kazi yake?
(*Makofi/Kicheko*)

(b) Serikali iko tayari kuweka Idara ya Maendeleo ya Jamii kwenye Mipango ili iwe na nguvu ya kuwaita Wakuu wa Idara wote kabla hawajaenda kuwachanganya wanakijiji kupeana msimamo bwawa liwepo lakini ngao itumike ili wasiwachanganye wananchi mara hawa wachimbe bwawa hawa wafukie? (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, kwanza amezungumzia suala la semina. Suala la semina lipo na litaendelea kuwepo. Kwa hiyo, linawezekana kwani Idara ya Maendeleo ya Jamii ni mtambuka na inaingia kila sehemu.

Swali lake la pili, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba hakuna *uniformity*, ni kwamba kila Halmashauri itaona mazingira yake. Napenda kutoa mfano mmoja mdogo, ukipeleka Idara ya Nyuki Morogoro Mjini kwa kweli ni kichekesho kwa sababu hatuna mambo hayo, miti ile hakuna pale Mjini, ndio maana nimesema kwamba kila Halmashauri itategemea na mazingira yake.

MHE. RAPHAEL N. MLOLWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba wataalam wa Maendeleo ya Jamii wana utaalam wa sekta mtambuka na kwa kuwa katika ngazi za vijiji na Kata masuala ya *specialization* sio muhimu sana katika kushughulikia maendeleo ya wananchi, je, Serikali itawapandisha hadhi hawa wataalam wa Maendeleo ya Jamii na kuwapa hadhi ya raslimali kuwezesha kufanya kazi zao vizuri zaidi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwamba wote tunaafikiana kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii wana umuhimu wao. Ndio maana hapo mwanzoni nimekataa kwamba Idara hii sio nyeti bali Idara zote ni nyeti. Kama ndio hivyo, naelewa kabisa Maafisa wote walioko katika Wilaya zetu wana nafasi zao na wote watapata nafasi sawa katika utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vitendea kazi, kama nilivyojibu kwamba hali ikituruhusu basi sio tu Maafisa Maendeleo ya Jamii bali Maafisa wote watasaidiwa.

Na. 321

Matumizi ya Maji ya Mto Malala na Nduruma

MHE. TALALA B. MBISE aliuliza:-

(a) Je, maji yanayochukuliwa kutoka katika Mto Nduruma na Malala (Arumeru) kwenda katika Manispaa ya Arusha yataathiri vipi na kwa kiasi gani maeneo yanayotegemea maji ya Mito hiyo kwa kunywa, kumwagilia na kunyweshea mifugo?

(b) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kukabiliana na athari hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mizania katika Mito ya Nduruma na Malala yaani maji yanayochukuliwa Mtoni kwa matumizi mbalimbali na maji yanayoingia Mtoni kwa njia ya vijito na chemchem, kama ilivyobainishwa na Wizara yangu mwezi Novemba, 2003 inaonyesha kuwa kwa Mto Nduruma maji yanayoingia ni mita za ujazo 77,933,000 kwa siku wakati yanayochukuliwa kwa matumizi mbalimbali kwa ajili ya umwagiliaji yakiwemo ya wenze hati na mifereji ya asili ni *cubic meter* 53,136,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hivyo, kiasi kinachobaki bila kutumika ni lita 24,797,000 kwa siku, sawa na asilimia 31 ya maji yote.

Kwa upande wa mto Malala maji yanayoingia mtoni ni lita 58,406,000 kwa siku, wakati yanayochukuliwa ni lita 39,917,000 kwa siku. Hivyo yanayobaki bila kutumika ni lita 18,490,000 kwa siku, sawa na asilimia 31 ya maji yote. Kiwango kinachobaki katika mito yote miwili cha asilimia 31 ni mara tatu ya kile kinachotumika na Mataifa mengine yenye usoefu wa muda mrefu wa menejimenti ya maji, kwa mfano Marekani, Brazil, New Zealand, Spain na Chile ambao wote hao wako kwenye asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, maji yanayokusudiwa kuchukuliwa kutoka Mto Nduruma kwenda Manispaa ya Arusha ni lita 3,802,000 tu kwa siku kiasi ambacho ni asilimia 4.8 ya maji yanayoingia kwenye Mto huo. Hii itafanya maji yanayobakia Mtoni bila kutumika kuwa lita 20,995,000 kwa siku sawa na asilimia 26. Hali kadhalika, maji yanayokusudiwa kuchukuliwa kutoka Mto Malala ni lita 3,110,000 kwa siku. Hii itafanya maji yanayobakia Mtoni bila kutumika kuwa lita 15,380,000 kwa siku sawa na asilimia 26. Hivyo, uchukuaji wa maji hayo hautaathiri watumiaji wengine waliopo hivi sasa ikiwa ni pamoja na matumizi kwa ajili ya hifadhi ya mazingira.

(c) Pamoja na kwamba uchukuaji wa maji kwa ajili ya Manispaa ya Arusha hautakuwa na athari kwa watumiaji wengine, Wizara yangu imepanga kusajili na kuvipa uwezo vyama vya watumiaji maji katika Mito ya Nduruma na Malala ili viweze kufanya yafuatayo kwa kushirikiana na Ofisi ya Bonde la Mto Pangani pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru:-

(i) Kusimamia uhifadhi wa ardhi na mazingira katika mabonde ya mito hii miwili kwa kutumia sheria zilizopo.

(ii) Kusimamia ujenzi wa milango kwenye mifereji yote ili kudhibiti matumizi ya maji.

(iii) Kutafiti na kubaini mifereji isiyo na hati na kudhibiti ongezeko holela la mifereji.

(iv) Kufanya mapitio ya hati zote.

(v) Kusimamia na kuhakikisha kuwa watumiaji wanachukua maji kutoka mitoni kiasi walichoruhusiwa tu.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuchukua hatua hizi ni kuhakikisha kuwa maji ya kutosha yanaendelea kuwepo katika mito hii miwili kwa ajili ya matumizi mbalimbali na pia kwa kuzingatia athari za ukame zilizowahi kujitokeza mara kadhaa katika maeneo hayo.

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza.

(a) Wakati mradi huu ukitekelezwa, kuna watu ambao waliswekwa mahabusu, je, Wizara iko tayari kuhakikisha kwamba hao watu wanarudi kama bado wako kwenye mahabusu wakawa huru na wakarudi kwenye shughuli zao za maendeleo?

(b) Wizara iko tayari kuhakikisha kwamba mji ulio karibu na maeneo ambayo yanachukuliwa maji hayo, Mji wa Tengeru pamoja na taasisi zilizopo pale sasa unapata maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, moja, nchi yetu inaendeshwa kwa sheria, kanuni na taratibu. Kama kuna watu ambao wanatuhumiwa kuvunja sheria, upo utaratibu watafikishwa Mahakamani kama walitenda kosa na Mahakama ndio ya mwisho kufanya maamuzi.

Pili, kuhusiana na Vyuo ambavyo viko karibu na eneo hilo kupata maji, kama nilivyoleza bado hata baada ya maji kuchukuliwa na Manispaa ya Arusha kutabakia 26% ambayo ni karibu mara 2.5 ya kawaida ya maji yanayotakiwa kubaki kwa ajili ya *ku-balance ecology* kwenye mto na viumbe hai kubakia kwenye eneo la mto. Kwa hiyo, nina hakika kwamba hata tukichukua 5% nyingine bado maji ya kutumika yatakuwa mengi lakini sasa hiyo inategemea sana na uwezo wao wa *ku-invest* katika kuchukua maji hayo.

Na. 322

Mpango wa Kutengeneza Bwawa Wilayani Massasi

MHE. RAYNALD A. MROPE aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya 1980 Serikali ilianzisha mpango wa kutengeneza bwawa kubwa katika makutano ya Mito miwili ya Mbangala na Msanjesi, Wilayani Masasi ili kuhifadhi maji kwa wingi ambayo yangeweza kunufaisha vijiji vya Namalembo, Chingulungulu, Namatutwe na hata vijiji vya Kata ya Namajani na kwa kuwa mpango huo ulisitishwa baadaye bila maelezo:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha Serikali kuacha kutekeleza mpango huo ambaa ungeleta ufumbuzi wa tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika eneo la Masasi Magharibi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kuleta maji safi na salama katika eneo hilo?

(c) Je, kuna mpango gani wa kujenga bwawa kubwa katika chanzo cha Mto Lukuledi, ili kupunguza matatizo ya ukosefu wa maji Masasi Magharibi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba katika miaka ya 1980, Serikali ilipanga kujenga bwawa kubwa katika kijiji cha Mbagala Wilayani Masasi ili kupata ufumbuzi wa tatizo la ukosefu wa maji katika eneo hilo la Masasi Magharibi. Mradi huu ulitarajiwa kuvinufaisha vijiji vya Namalembo, Chingulungulu, Namatutwe na baadhi ya vijiji katika Kata ya Namajani. Gharama za ujenzi wa bwawa hilo kwa wakati huo zilikadiriwa kuwa na shilingi milioni 2.

Mheshimiwa Spika, kutohana na ukosefu wa fedha Serikali ilisitisha utekelezaji wa mpango huo na badala yake ilichimba visima vifupi viwili na visima virefu nane katika baadhi ya vijiji viliviyotajwa.

(b) Eneo la Masasi Magharibi lina miradi 13 ya maji ya visima virefu inayotumia mashine za dizeli. Miradi hiyo ni Nanyumbu, Mangaka, Nandembo, Lukuledi, Mikangaula, Kilosa, Mkwajuni, Nangomba, Namajani, Namatutwe, Chikowe, Mlingula na Namkungwi. Miradi 12 kati ya 13 niliyoitaja haifanyi kazi kutohana na kuharibika au kuchakaa kwa injini au pampu ya kusukuma maji.

Katika kukarabati miradi hiyo, Serikali ilitenga shilingi milioni 13 katika mwaka 2003/2004 kwa mradi wa Ndwika utakaohudumia vijiji vitatu vya Mangaka, Ndwika na Kilimahewa. Ukarabati wa mradi huo utakamilika katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Serikali pia ilitenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa Nandete katika mwaka huo wa fedha. Katika mwaka 2004/2005, Serikali imetenga shilingi milioni 40 kwa ajili ya mradi wa Mkuula utakaohudumia vijiji vitatu vya Mkuula, Nanyumbu na

Chungu. Mradi wa Nandete nao umetengewashilingi milioni tatu katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo, Wilaya ya Masasi ni miongoni mwa Wilaya 38 ambazo ziko kwenye Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia utakaoteklezwa kuanzia mwaka huu wa 2004/2005. Chini ya mradi huu, wananchi watawezeshe kujenga miradi yao ya maji watakayopendekeza wenyewe katika Wilaya nzima ya Masasi ikiwa ni pamoja na eneo la Masasi Magharibi. Wilaya ya Masasi pia ni miongoni mwa Wilaya zitakazoteklezwa mradi wa maji vijijini unaofadhiliwa na Serikali ya Japan. Katika eneo la Masasi Magharibi, mradi huo utatekelezwa katika vijiji vya Namkungwi, Kilosa, Nanyumbu na Namasogo. Mradi huo unaohusu uchimbaji wa visima virefu utaanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi hiyo utapunguza tatizo la maji katika eneo la Masasi Magharibi kwa kiwango kikubwa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kama nilivyo sema jana, ajihusishe kikamilifu katika kuchagua miradi itakayoteklezwa chini ya programu hii.

(c) Serikali haijapanga kujenga bwawa katika Mto Lukuledi katika mipango yake. Hata hivyo, kama nilivyo eleza Mheshimiwa Mbunge namshauri wakae na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ili kuona kama mradi huo unaweza kuingizwa katika programu hiyo ya Benki ya Dunia ili utekelezwe kwa kiwango watakachokua wameamua wenyewe.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Kwa kuwa jana Waziri alisema kwamba mradi wa Mbwinji utaleta maji ya kutosheleza Mji wa Masasi na hatimaye kupeleka Nachingwea, je, haoni ingefaa sana kuwapa matumaini watu wa Masasi Magharibi kwamba hatimaye maji yatatoka katika mradi huu mkubwa wa Mbwinji ili kuondoa tatizo hili kabisa? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kwa bahati mbaya toka Uhuru huu mradi wa mabwawa haujafanikiwa katika Wilaya ya Masasi, je, Waziri haoni kwamba ingekuwa bora au busara kwa Wizara yake kuchukua maji kutoka vyanzo mbalimbali vya chemchem ambavyo vimejaa katika Wilaya ya Masasi hasa kutoka sehemu za Nahinga, Mbwinji, Liputo, Ndanda, Mwena na sehemu nyingine ambapo maji ya chemchem yapo kwa wingi ili kuondoa tatizo la maji katika Wilaya hii ya Masasi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kama tulivyo eleza Mheshimiwa Raynald Mrope, ni Mbunge maarufu, mradi wa Mbwinji *uta-supply* maji Masasi na Nachingwea. Najua tatizo lako, mnataka muonekane kwamba ninyi ndio mmesaidia Nachingwea kupata maji, sisi tunasema mradi huo ni kwa ajili ya maeneo yote mawili.

Mheshimiwa Raynald Mrope, msilette *local politics* hapa itatuletea matatizo, mradi huu ni wa Serikali na utasaidia sehemu zote mbili sio moja inasaidia nyingine. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pili, vijiji alivyovitaja chini ya Mpango wa Benki ya Dunia, nina hakika kwamba wakiviingiza vitafaidika na mradi utajengwa kulingana na uwezo wa wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Na. 323

Upatikanaji wa Hatimiliki

MHE. ALI SAID SALIM (k.n.y. MHE. MASOUD ABDULLA SALIM) aliuliza:-

Kwa kuwa suala la hatimiliki kwa ujumla limekuwa kero kubwa kwa wakulima wa mashamba makubwa ya kilimo kama *Katani Limited*, vile vile kwa wakulima wadogo wadogo na hata maeneo ya ufugaji na kwa kuwa upatikanaji wa hatimiliki ungeshawishi wawekezaji kuwekeza zaidi na hatimaye kupelekea vijana kupata ajira kwa lengo la kuondokana na umaskini:-

(a) Kwa nini Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuyapatia hatimiliki mashamba ya Mkumbara, Gomba, Mwenga, Kituo cha Utafiti Kibaha na shamba la uzalishaji mitamba Ngerengere?

(b) Je, Serikali inatueleza nini juu ya hatimiliki ya Kampasi ya *Solomon Mahlangu* katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (*SUA*) baada ya kuondoka kwa Wapigania Uhuru wa Afrika ya Kusini (*ANC*)?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, kabla ya kujibu napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi mashamba ya Mkumbara, Gomba na Mwenga ni mionganii mwa mashamba yaliyowekwa chini ya *Presidential Parastatal Sector Reform Commission (PSRC)* ili yabinafsishwe. Mashamba hayo, yalikuwa na hatimiliki (*Certificates of Title*) kabla ya kuwekwa kwenye mpango wa kubinafsishwa. Hata hivyo, wakati mpango wa kuyabinafsisha mashamba hayo ukiwa unaendelea kuandaliwa, Serikali iliona ni vema kuyamega baadhi ya mashamba kwa lengo la kuwagawia ardhi wanavijiji wanaozunguka mashamba hayo. Zoezi la umegaji lilisimamiwa na *PSRC*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, napenda sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina kigugumizi cha kuyapatia hatimiliki mashamba yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge. Kilichochelewesha utoaji wa hatimiliki mpya katika mashamba ya Mkumbara, Gomba na Mwenga baada ya zoezi la umegaji kufanyika ni hatimiliki za awali za mashamba hayo zinatakiwa zifanyiwe marekebisho chini ya utaratibu wa ama kutoa hatimiliki mpya endapo hatimiliki za zamani zitakuwa nimemaliza muda wake, kurudisha sehemu ya ardhi (*part surrender*) au kuhamisha miliki (*transfer of the right of occupancy*). Aidha, baadhi ya hatimiliki ziliwa zimebekwa rehani na Mabenki kwa sababu ya mikopo. Hivyo, inatakiwa mikopo ilipwe ili kukomboa ardhi hiyo iweze kutolewa kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la ardhi linalotumiwa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Miwa, Kibaha ni kwamba, kituo hiki kiko ndani ya eneo la *Kibaha Education Centre* ambalo limepimwa na lina hatimiliki. Endapo Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Miwa kitahitaji kupatiwa hatimiliki, kinatakiwa kishirikiane na Wizara ya Kilimo na Chakula, kuomba kibali cha kumega eneo hilo kwa Mheshimiwa Rais. Kufanya hivyo ni kutekeleza tamko la Mheshimiwa Rais alilotoa mwaka 2000 kwamba eneo hilo limemegwa kwa idhini yake. Aidha, kwa upande wa shamba la kuzalisha mitamba la Ngerengere, shamba hilo limepimwa na lina Barua ya Toleo Na.129 (*Letter of Offer No.129*). Hivi sasa hatimiliki inaandaliwa ili wakabidhiwe.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaona umuhimu wa Kampasi ya Solomon Mahlangu ya Chuo Kikuu cha Sokoine (*SUA*) kuwa na hatimiliki. Hivyo, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kushirikiana na Mkoa wamekwishawasilisha mapendekezo ya kufuta hatimiliki za mashamba ya mkonge yaliyopo kampasi hiyo na ufutaji uko katika hatua za mwisho. Aidha, sambamba na zoezi hilo, Halmashauri hiyo inaendelea kufanya mchanganuo wa matumizi halisi ya ardhi inayohitajika kwa ajili ya kampasi hiyo kabla ya upimaji kuanza.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Halmashauri zenyetanu mashamba ya aina hii kuharakisha hatua za ufutaji wa Hatimiliki zilizo hai ili upimaji na utoaji wa Hatimiliki mpya ufanyike haraka na kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la hatimiliki limekuwa likilalamikiwa na wananchi wengi katika suala la mashamba na nyumba, je, Wizara ina mpango gani wa kulitafutia ufumbuzi suala hili ili wananchi waweze kupata hatimiliki za mashamba na nyumba kwa muda muafaka? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimeeleza taratibu zinazopaswa kufuatwa kwanza wanaanzia kijijini kukubali kwamba eneo hili liweze kugawiwa, Wilaya ishirikishwe hata Mkoa ndipo maelekezo hayo yaje Wizarani tuweze kuyafanya kazi na kuweza kumega kisheria lakini sio kwamba tuhimize bila kushirikisha watu wote wanaohusika na eneo lile. Lakini kama bado anahitaji maelezo zaidi, afike Wizarani, kila wakati yuko pale tutamwelekeza zaidi na kwa kutumia sheria.

Mashine ya Kuchambulia Pamba

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha pamba kimeongezeka kwa zaidi ya hekta 12,000 kwa wanaojishughulisha na kilimo hicho na kwa kuwa mashine ya kuchambulia pamba iliyopo Kilosa ni ndogo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mashine kubwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu tulizonazo katika msimu wa 2003/2004, Wilaya ya Kilosa ililima jumla ya hekta 8,704, wakulima wadogo walilima hekta 6,906 na wakulima wakubwa walilima hekta 1,798. Wilaya hiyo inatarajia kuvuna tani 2,516 za pamba ya mbegu. Nawapongeza sana wakulima, viongozi wa Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Kilosa kwa mafanikio haya makubwa hususan yakilinganishwa na hekta 359 zilizolimwa katika mwaka wa 2002/2003 ambazo zilitoa tani 107 tu za pamba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha Kilosa kilikarabatiwa kwa shilingi milioni 20 na kukifanya kiwe na uwezo wa kuchambua tani 1,800 za pamba kwa msimu. Katika msimu wa mwaka 2003/2004, Bodi ya Pamba imepanga kukarabati vinu kumi zaidi na kukifanya kiwanda kiwe na uwezo wa kuchambua tani 5,500 za pamba ya mbegu kwa msimu. Ukarabati huo unatarajiwa kugharimu shilingi milioni 23.6.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kampuni ya *New Msowero Limited* imeanza kutekeleza hatua za awali za ujenzi wa Kiwanda kipyaa cha Kuchambulia Pamba katika Kijiji cha Msowero, Tarafa ya Magore. Ujenzi wa kiwanda hicho unatarajiwa kukamilika mwaka wa 2005/2006 na kitakuwa na uwezo wa kuchambua tani 8,000 za pamba mbegu kwa msimu. Juhudi hizo zitafanya uwezo wa kuchambua pamba mbegu katika Wilaya ya Kilosa kufikia tani 13,500 kwa msimu.

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kwa kukarabati vinu vingine. Je, ni lini atapeleka pesa huko ili ziwahi msimu? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, tunalo tatizo la bei ya pamba. Pamba imeanza na shilingi 320/=, sasa imeshuka mpaka shilingi 250/=. Je, Serikali inatamka nini kuhusu ubabaishaji wa bei hiyo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ongezeko la vinu linafanyika sasa hivi, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, pesa zipo, zitafika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la bei ya pamba, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Christopher Wegga, kuwa Serikali ya CCM inalitambua jambo hili na inalishughulikia kwa umakini sana. Tunaomba awe na subira, jibu litapatikana mapema iwezekanavyo. (*Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibwa na muda wa maswali umekwisha. Sasa tunaendelea na matangazo ya vikao vya leo vya Kamati. Kamati tatu za kudumu zimepangiwa kufanya vikao leo, ya kwanza ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athuman Janguo, anawajulisha wajumbe wake kwamba mara baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, Kamati hiyo itakutana katika ukumbi Namba 133, ghorofa ya kwanza.

Ya pili ni Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Njelu Kasaka, anawaomba wajumbe wake wakutane chumba Namba 231, saa tano asubuhi hii. Kamati ya tatu ni ya Hesabu za Serikali, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, anawajulisha wajumbe wake kwamba, kikao kitafanyika saa nne na nusu chumba Na. 227, ghorofa ya pili. Hizo ni Kamati za Bunge.

Halafu kuna Chama cha Hiari cha Wabunge kinachohusu masuala ya idadi ya watu na maendeleo, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Paul Kimiti, anawatangazia Wabunge ambao ni wajumbe wa Chama hicho wabaki humu ndani mara baada ya kuahirisha kikao cha asubuhi, anataka kuwapa taarifa muhimu. Hao ni Wabunge wa masuala ya idadi ya watu na maendeleo.

Mwisho wa matangazo tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 Wizara ya Maliasili na Utalii

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako kabla ya kusoma hotuba ya bajeti ya Wizara yangu niseme yafuatayo:-

Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza katika historia ya maisha yangu ya kisiasi kusoma bajeti bila mume wangu Profesa Ramadhani Meghji, ama kuwepo hapa Dodoma, ama kunipigia simu asubuhi na mapema ya kunitakia kila la kheri popote anapokuwa,

namwomba Mwenyezi Mungu amrehemu na kuiweka roho yake mahali pema peponi.
Amin.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira, leo asubuhi naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kwa kujadili Makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2004/2005. Wizara yangu itazingatia na kutekeleza mapendekezo ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa sekta ya utalii kumetokana na kuwepo kwa hali ya amani na utulivu chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamshukuru binafsi kwa kusaidia pia kukuza sekta ya utalii. Mheshimiwa Rais amekuwa ni alama nzuri ya utambulisho wa Taifa letu ikiwemo ndani na nje ya nchi. Tunampongeza kwa kuteuliwa kwenye Tume ya Tony Blair kuhusu masuala ya Afrika na pia kuendelea kuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Kimataifa ya athari za Kijamii na Utandawazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aidha, niruhusu niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu na marafiki katika kuwafariji na kuwapa salaam za rambirambi, familia, ndugu na wapiga kura wa Majimbo ya Mbeya Vijijini na Ulanga Mashariki, kufuatia vifo vya Mheshimiwa Yeté Sintemule Mwalyego na Mheshimiwa *Comrade Capt.* Mstaaful Theodos James Kasapira. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa, kuchaguliwa na kushinda nafasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Ni matumaini yetu kuwa uzoefu wenu katika uongozi utakuwa chachu ya maendeleo kwa maslahi ya umma na taasisi hizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopatwa na matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kushinda uchangazi mdogo wa Ubunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kwa kujadilia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2004/2005, Wizara yangu itazingatia na kutekeleza mapendekezo ya Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Sekta ya Maliasili na Utalii iliendelea kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Kwa kutumia vigezo vya

kawaida nya mafanikio, wananchi wengi wameendelea kupata ajira ya moja kwa moja katika shughuli za maliasili na utalii na vile vile wengine kujajiri wenyewe katika biashara mbalimbali kutokana na mazao ya maliasili hasa uvuvi, misitu na shughuli zinazoimarisha utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kigezo cha mapato ya fedha za kigeni, katika mwaka 2003, ukiachia mbali mapato kutokana na utalii, uuzaaji wa mazao ya samaki pekee nchi za nje uliingizia Taifa Dola milioni 129.6 ikilinganishwa na Dola milioni 121 mwaka 2002 na Dola 95.4 milioni mwaka 2001. Ili kufaidika na ufanisi huu, Serikali imeamua kwamba kuanzia mwaka 2004/2005, samaki wakubwa wa mapezi wa maji ya chumvi wasioliwa sana na wananchi wa mwambao, nao watachakatwa (*process*) na kuuzwa nchi za nje kama vile ilivyo Sangara. Hatua hii itatoa fursa kwa wananchi wa mwambao kuboresha zana zao za uvuvi ili kuwavua samaki hao kwa wingi, na muhimu zaidi, kuwapanulia wigo wa uvuvi na kuongeza mapato yao katika vita ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililoonyesha mafanikio mazuri ni katika ukusanyaji wa maduhuli katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara. Lengo la mwaka 2003/2004, lilikuwa kukusanya shilingi bilioni 21.3. Hadi mwezi Mei, 2004 Wizara ilikwishakusanya shilingi bilioni 22.9. Makusanyo ya maduhuli yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kwani katika mwaka 2002/2003, lengo lilikuwa shilingi bilioni 17.7 lakini makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 22.4. Ongezeko hili, bila kubadilisha viwango nya ushuru pia ni ishara ya kuboresha utoaji huduma na kusimamia uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ni lazima nikiri kuwa pamoja na mafanikio hayo, pametokea pia changamoto ambazo Wizara yangu inalazimika kuzishughulikia. Kwa mfano, tumefanikiwa katika kuboresha uhifadhi wa wanyamapori na hivyo idadi ya wanyama imeongezeka kama vile tembo, simba na kadhalika. Hali ya usalama na wingi wa wanyama hao umewafanya wasogelee zaidi sehemu chache za makazi na mashamba ya wananchi na kuwaondolea amani. Suala hili linashughulikia.

Matatizo mengine yaliyoendelea katika mwaka 2003/2004, ni pamoja na uchomaji ovyo wa misitu, uvunaji haramu wa mazao ya maliasili, uvamizi wa maeneo ya hifadhi ya wanyamapori na misitu kwa ajili ya kilimo, makazi na malisho ya mifugo, ubovu wa miundo mbinu katika maeneo ya hifadhi na uchache wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba pamoja na mafanikio na matatizo niliyoyaeleza, katika kusimamia uhifadhi endelevu, Wizara iliendelea kufanya mapitio katika Sera, Sheria na Kanuni za sekta zake ndogo na kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha sekta hizo. Vile vile, utangazaji wa utalii uliimariswa kwa kutafuta masoko mapya na kuongeza ushirikiano na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2003/2004 na malengo ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya wanyamapor ni msingi wa biashara ya utalii nchini na inachangia maendeleo ya wananchi kwa kutoa asilimia ya mapato kugharamia miradi ya kijamii. Sekta imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia ushirikishaji wa wananchi katika kuhifadhi na kunufaika na uhifadhi huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, moja ya kazi za sekta hii ilikuwa kufanya mapitio ya sera ya wanyamapor pamoja na kufanya marekebisho ya sheria ya wanyamapor ili iendane na marekebisho yaliyoko kwenye sera.

Katika kipindi cha 2004/2005, sekta hii itakamilisha mapitio ya sera na sheria husika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu kwa kutumia wataalamu wake ilitoa elimu juu ya Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor (*Wildlife Management Areas Regulations - WMAs*) za mwaka 2002 kwa baadhi ya viongozi Watendaji wa vijiji na Halmashauri za Wilaya 13 kati ya 16 ambazo zimo kwenye majaribio ya matumizi ya Kanuni hizo. Wilaya hizo ni Monduli, Kiteto, Ngorongoro, Kilolo, Morogoro, Rufiji, Tunduru, Songea, Tarime, Urambo, Sikonge, Namtumbo na Babati ambazo zimehusisha jumla ya vijiji 73. Katika Wilaya ya Serengeti, elimu ilitolewa pia kwa wananchi kwenye mikutano ya hadhara katika vijiji vitano vinavyounda eneo la Majaribio la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor la Ikona.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya majaribio ya Wilaya za Rufiji na Morogoro tayari yameshawasilisha maombi rasmi ya kutangazwa na Jumuiya za Jamii kutambuliwa kisheria kuwa zitasimamia wanyamapor katika ardhi za Vijiji vya Tapika na Ngarambe kwa Wilaya ya Rufiji na eneo la Ukutu linalohusisha vijiji 23 kwa Wilaya ya Morogoro. Wilaya zilizobaki zenye Vijiji vilivymo kwenye mpango wa Majaribio ya *WMA*, zimo katika hatua za kuandikisha Jumuiya za Jamii (*Community - based Organisation - CBO*) kwa mamlaka husika. Aidha, Wilaya kumi kati ya Wilaya 17 zimeunda Bodi za Wilaya za ushauri wa masuala ya maliasili.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa viashiria na mpango wa utekelezaji wa viashiria hivyo kwa ajili ya ufuataliaji wa utekelezaji wa Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor, ili kuwezesha tathmini ya utekelezaji wa Kanuni ifikapo miaka mitatu tangu zianze kutumika.

Katika kuendeleza uhamasishaji na elimu kwa umma vipindi vya radio 20 vilirushwa hewani na Redio Tanzania, picha za *video* 14 zilioneshwa katika Mikoa 7 na kipindi kimoja kilirushwa kupitia Televisheni ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 Wizara itatoa mafunzo kwa watumiaji viashiria kuhusu ufuataliaji wa mabadiliko kwenye *WMA* na utekelezaji wa mpango wa viashiria. Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuhusu Kanuni za *WMA* katika vijiji na Jumuiya za Jamii na itaendelea kufuatalia kwa karibu uendeshaji na usimamizi wa Maeneo 16 ya majaribio ya kanuni za hifadhi ya wanyamapor.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa wanyamaporii uliimashwa kwa kuapatia watumishi mafunzo maalum pamoja na kuapatia vitendea kazi. Hadi Aprili, 2004, doria zilizofanyika zilinasa watuhumiwa 1,700 na nyara mbalimbali za Serikali ikiwemo kilo 587.8 za meno ya tembo, kilo 79 za meno ya kiboko na ngozi 64 za wanyama. Vile vile, bunduki 349 za aina mbalimbali zilikamatwa.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi kwa kuimarisha doria, kuapatia watumishi 160 mafunzo kuhusu kupambana na ujangili pamoja na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, kuhusu ulinzi wa maisha na mali za wananchi, siku 1,122 za doria zilitumika kusaka wanyamaporii waharibifu katika Wilaya 24. Risasi 23,350 za aina mbalimbali zilinunuliwa kwa ajili ya kudhibiti wanyama waharibifu na kati ya hizo 3,080 zilitolewa kwa Halmashauri za wilaya 24.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itaendeleza ulinzi wa maisha na mali za wananchi dhidi ya wanyamaporii kwa kuhakikisha upatikanaji wa risasi na kuapatia mafunzo ya mbinu mbalimbali za kudhibiti wanyama waharibifu askari wa Vijiji kwenye maeneo ya majoribio ya Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamaporii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilikamilisha mipango ya uendeshaji wa mapori ya Akiba ya Burigi/Biharamulo na Ibanda/Rumanyika. Kazi ya kupitia mipango ya uendeshaji wa mapori ya akiba ya Ugalla na Mkomazi/Umba inaendelea. Barabara mpya zenye urefu wa kilometra 1,753 zilitengenezwa na nyingine zenye urefu wa kilometra 2,756 zilifanyiwa ukarabati. Viwanja vipyta vya ndege vitano vilijengwa katika mapori ya akiba ya Selous, Moyowosi/Kigosi, Mpanga/Kipengere, Lukwika/Lumesule na Ugalla.

Vile vile, viwanja 17 vilifanyiwa matengenezo ya kawaada. Mipaka ya mapori ya Lukwika/Lumesule, Rungwa/Kizigo, Ugalla, Mpanga/Kipengere, Moyowosi/Kigosi na Liparamba imepitiwa na kuchorwa upya. Kilometra 1,033 za mipaka ya mapori zimefanyiwa ukarabati. Katika mapori ya Usangu na Mpanga/Kipengere mipaka iliwekwa alama za kudumu. Aidha, nyumba 10 za watumishi zimejengwa na 42 kukarabatiwa katika vituo mbali mbali.

Vile vile, Wizara iliwahamisha wafugaji waliokuwa wanaishi ndani ya Pori la Akiba la Moyowosi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itaendelea kupanua mtandao wa barabara katika mapori ya akiba kwa kulima barabara mpya zenye urefu wa kilomita 350 na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 1,000. Aidha, Wizara itakamilisha kupitia mpango wa uendeshaji kwa mapori ya Akiba ya Ugalla na Mkomazi na itaandaa mipango ya Uendeshaji mapori ya Rukwa/Lukwika na Mpanga/Kipengele. Mpango wa uwekezaji wa pori la Akiba la Rungwa/Kizigo utafanyiwa mapitio na maandalizi ya mipango ya uendeshaji ya mapori ya Lukwika/Lumesule, Swagaswaga na Mkungunero yataanza. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ilikamilisha kuorodhesha eneo la Bahari la Rufiji-Kilwa-Mafia kuwa eneo la ardhioevu yenye umuhimu wa Kimataifa (*Ramsar site*). Hivyo tangu nchi yetu iliporidhia mkataba wa *Ramsar* mwaka 2002 ilishatenga maeneo manne muhimu yenye hadhi kama hiyo. Vile vile, katika kuratibu masuala ya ardhioevu Wizara iliunda chombo cha juu kabisa cha kutoa maamuzi kuhusiana na uendelezaji wa ardhioevu kinachowahusisha Makatibu Wakuu wanane

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, wizara itaanza hatua za awali za kuorodhesha vinamasi (*swamps*) vya Bonde la Mto Kagera kuwa eneo lenye umuhimu wa Kitaifa na itakusanya maoni ya wadau ili kuandaa mkakati wa Kitaifa wa Ardhioevu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori, utafiti wa wanyamapori umelenga kutathmini wingi wa rasilimali pamoja na kubaini magonjwa kwa lengo la kuwa na rasilimali endelevu ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Taasisi ilifanya sensa za wanyamapori katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Mapori ya Akiba ya Moyowosi/Kigosi na Ugalla. Aidha, Taasisi iliendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti wa ufugaji nyuki katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Dar es Salaam na Tabora, utafiti wa magonjwa ya wanyamapori na utafiti wa wanyama wanaokula nyama.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Taasisi itaendelea kufanya sensa ya wanyamapori na ndege wa majini (*water birds*) pamoja na kuendeleza miradi ya utafiti. Taasisi pia itakarabati majengo ya kituo cha Tabora pamoja na kujenga Ofisi ya Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori umekuwa ukitegemea mapato toka kwa wahisani na wakereketwa wa uhifadhi wa wanyamapori. Fedha zinazopatikana zinatumika kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Mfuko ulitarajia kukusanya shilingi bilioni 3.9. Hadi kufikia Aprili, 2004, Mfuko ulikuwa umekusanya shilingi bilioni 3.7. Fedha hizo zilitumika kuimarisha doria za uzuiaji ujangili, miradi ya maendeleo, kugharimia utafiti na mafunzo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Mfuko umekadiria kukusanya shilingi bilioni 3.8. Fedha hizo zitatumika kuimarisha na kuboresha usimamizi wa uhifadhi wa wanyamapori na mazingira pamoja na ushirikishaji wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Hifadhi za Taifa, Hifadhi za Taifa zimekuwa zikisimamia mbuga za wanyama zilizotengwa maalum kwa ajili ya utalii wa kuona na kupiga picha.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 hadi Februari, 2004, Shirika liliendesa doria za kuzuia ujangili na kufanikiwa kukamata majangili 1,799 na silaha mbalimbali 36 na mbao 2,104. Aidha, wanyama 326 wa aina mbalimbali waliuawa na majangili.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2004, Watalii 304,105 walitembelea Hifadhi za Taifa. Idadi hii ni pungufu kwa asilimia 11.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2002/2003. Kupungua kwa watalii kunatokana na tishio la ugaidi na vita vya Iraq. Licha ya idadi ya watalii kupungua, mapato yaliongezeka ambapo Shirika lilikusanya shilingi bilioni 17.6 kutokana na shughuli za utalii ikilinganishwa na shilingi bilioni 17.5 zilizopatikana kufikia Februari, 2003. Ongezeko hili linatokana na kuanzishwa kwa shughuli mpya za utalii kama utalii wa mitumbwi katika hifadhi ya Arusha pamoja na utalii wa kutembea kwa miguu kwenye hifadhi za Tarangire na Ruaha. Jumla ya kampuni 107 za utalii ziliendesa biashara ya utalii katika hifadhi za taifa.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango wake wa Ujirani Mwema, Shirika lilitumia shilingi milioni 102.5 kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Shirika liliendesa warsha tatu kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ili kuandaa mipango ya uendeshaji ya Hifadhi za Serengeti na Mahale. Aidha, Wizara itawasilisha Muswada kwa ajili ya kuanzisha hifadhi za Saadani na Kitulo pamoja na kupandisha hadhi ya Misitu ya Meru/Ngrudoto, Kilimanjaro/Marang na mashamba namba moja mpaka tatu ya Manyara kuwa sehemu za hifadhi.

Mheshimiwa Spika, mipango na matarajio ya Shirika kwa mwaka 2004/2005, itaelekezwa katika kuboresha miundo mbinu kwa ajili ya utalii, kupanua wigo wa shughuli za utalii na kukamilisha mipango ya uendeshaji wa hifadhi za Mahale, Serengeti na Gombe.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inasimamia uhifadhi wa bonde la Ngorongoro ambalo ni kivutio maarufu cha utalii duniani. Eneo hilo linajumuisha hifadhi ya wanyamapor na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2004, watalii 219,761 walitembelea eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Kati ya hao, 160,541 walitoka nje na 59,220 walikuwa watalii wa ndani ya nchi. Jumla ya Shilingi bilioni 8.5 zilikusanya kutokana na watalii hao na kuvuka lengo la shilingi bilioni 6.9 la mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Mamlaka ilikamilisha ujenzi wa barabara kutoka Makao makuu ya Hifadhi hadi Kata ya Naiyobi, Olbalbal na Kakesio pamoja na barabara kutoka kata ya Endulen hadi kijiji cha Olpiro.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Mamlaka inatazamia ongezeko la asilimia 10% ya watalii watakatembelea Hifadhi ambao wataingiza shilingi bilioni 7.7. Ili kuhakikisha mapato endelevu, Mamlaka itajenga jengo la kitega uchumi mjini Arusha, pamoja na kununua vitendea kazi kwa ajili ya ujenzi na kuimarisha barabara.

Aidha, Mamlaka itakamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Embarway kwa kujenga madarasa nane na nyumba tano za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki Sekta hii katika kutekeleza majukumu yake imetoa kipaumbele katika kutekeleza Sera na marekebisho ya sheria, usimamizi shirikishi wa misitu pamoja na uendelezaji wa mashamba ya miti na hifadhi za nyuki. Ili Sera ya Taifa ya Misitu ya 1998 na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya 1998 ileweke kwa wadau, Wizara iliweka sera hizi katika tovuti ya Wizara ili wadau wengi waweze kuzipitia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara iliendesha mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu katika wilaya 15. Vile vile, vijiji 39 katika wilaya za Mpwapwa, Same, Kondoa, Dodoma Vijijini, Lindi na Kilwa viliwezeshwa kuandaa Mipango ya Usimamizi Shirikishi wa misitu na hifadhi za nyuki. Katika kuboresha uhifadhi wa Misitu ya Hifadhi ya vyanzo vya maji na mikoko, uhamasishaji ulifanyika katika vijiji 72 kwenye Wilaya 28.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara itatekeleza mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu katika wilaya 37 kwenye Mikoa ya Morogoro, Lindi, Iringa, Mbeya, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida, Dodoma, Tabora, Kigoma, Rukwa, Mwanza, Kagera na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 hadi Aprili, 2004, magogo yenye mita za ujazo 24,866 yalivunwa katika misitu ya asili, na mita za ujazo 309,100 katika mashamba ya miti.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, magogo yenye mita 25,000 za ujazo katika misitu ya asili na mita za ujazo 350,000 katika mashamba ya miti yatavunwa. Ili kuboresha usimamizi wa uvunaji wa mazao ya misitu, utoaji wa leseni za kuvuna miti utashirikisha wilaya na serikali za vijiji. Utaratibu huu utaanza katika wilaya 20 ambazo zitaunda kamati za kujadili maombi ya leseni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara ya nje ya mazao ya misitu na nyuki kwa mwaka 2003/2004, Wizara ilikadiria kuwa sekta binafsi itauza mazao ya misitu yenye thamani ya shilingi bilioni 9.8. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2004, mazao ya misitu na nyuki yenye thamani ya shilingi bilioni 11.6 yaliuzwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara inatarajia sekta binafsi itauza mazao ya misitu na nyuki yenye thamani ya shilingi bilioni 10.9. Aidha, kuanzia tarehe 1 Julai, 2004, usafirishaji wa magogo nje ya nchi hautaruhuswa. Madhumuni ni kuendeleza sekta ya viwanda, kuongeza ajira na thamani ya bidhaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na uendelezaji wa mashamba ya miti, maandalizi ya upigaji picha za anga katika mashamba ya *Sao Hill*, Kiwira, Buhindi, Meru na Kilimanjaro Kaskazini yalikamilika ikiwa ni sehemu ya kukamilisha taratibu za kuwashirikisha wadau katika kusimamia mashamba hayo.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara itakuza miche milioni 7.5 na kupanda miti hekta 5,000. Vile vile, itapogoa miti katika hekta 3,000 na kupunguza miti katika hekta 1,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa ufugaji nyuki, mwaka 2003/2004, Wizara iliwezesha kutenga na kuchora ramani za Hifadhi za Vijiji vya Tura na Kizengi katika Wilaya ya Uyui. Shughuli za ugani zilifanyika katika Wilaya za Newala, Lindi, Masasi, Kahama, Songea, Dodoma, Manyoni, Mpanda na Uyui.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itatoa huduma za ugani katika Wilaya 10 na kutangaza hifadhi nne za nyuki za vijiji.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Misitu ililenga kuendeleza usimamiaji na uratibu wa utafiti wa misitu kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa, pamoja na kutoa ushauri ili kuendeleza raslimali za misitu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Taasisi itapanua na kuimarisha utafiti wa kilimo misitu katika mikoa ya Pwani, Shinyanga, Mwanza, Tabora na Tanga, kwa lengo la kuwafikia wakulima 1,000. Vile vile, itafanya utafiti wa kuzalisha vyahuso (*cloning*) ya mikaratusi inayokua haraka katika vitalu vya majaribio vilivyoko Arusha, Lushoto, Mombo, Korogwe, Kibaha, Morogoro, Dodoma na Mufindi.

Madhumuni ya Wakala wa Mbegu za Miti ni kuwezesha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira kwa kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi vingine.

Hadi kufikia Aprili, 2004, Wakala ulikusanya kilo 13,500 za mbegu, ambapo kilo 10,582 ziliuzwa nchini na 38 nchi za nje. Vile vile, miche 20,000 ilikuzwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wakala inalenga kupanua upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za miti kwa kukusanya kilo 12,500 za mbegu za miti, kuuza kilo 10,000 nchini na kilo 50 nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya uvuvi ina mchango mkubwa katika upatikanaji chakula nchini. Katika kuzingatia hilo, mpango kamambe wa kutekeleza sera ya uvuvi umeanza kwa kuanzisha miradi mbalimbali. sekta ndogo ya uvuvi imelenga kuimarisha masoko na vituo vya kupokelea samaki, kuhamasisha ufugaji wa samaki na mazao ya baharini pamoja na kudhibiti ubora wa mazao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilianza kutekeleza mpango kamambe wa kuendeleza sekta ya uvuvi kwa kuanza ujenzi wa soko la kisasa la Kirumba katika Manispaa ya Mwanza. Vile vile, ilianza kutekeleza mradi wa kuhifadhi mazingira ya Ziwa Tanganyika pamoja na kuendeleza huduma za kiuchumi kwa wavuvi na huduma za jamii, ambao unahuishwa nchi zinazomiliki Ziwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliendeleza juhudi za kuboresha ufugaji samaki pamoja na ukulima wa mwani. Wizara ilitoa mafunzo ya uhamasishaji juu ya ufugaji bora wa samaki kwa wananchi 1,472. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wasimamizi wa vituo vya kuzalisha mbegu bora ya samaki aina ya perege katika Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga. Jumla ya wananchi 153 walinufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza kilimo cha Mwani, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itatoa mafunzo kwa wakulima wa mwani 70.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa ubora wa mazao na masoko, mwaka 2003/2004, Wizara ilikagua viwanda 26 vya kusindika mazao ya samaki na meli za uvuvi 25. Washiriki 4,838 kutoka sekta binafsi walipewa semina kuhusu njia bora za kusindika na kusafirisha mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, sampuli 2,842 za minofu zitachukuliwa kuhakiki ubora, 562 za minofu na maji zitapimwa kuchunguza uchafuzi utokanao na dawa za kuua wadudu wa mimea. Vile vile, sampuli 2,000 za minofu zitapimwa kudhibiti uchafuzi utokanao na mionzi viwandani. Kagazi 16 zitafanyika viwandani kuhakiki kiwango cha usafi unaokubalika kimataifa. Pia, Watumishi 40 watapatiwa elimu ya ukagazi wa mazao ya uvuvi na wadau 1,480 watapata mafunzo ya uzalishaji bora wa mazao ya uvuvi. Vituo vitano vya ukagazi wa mazao vya Mafia, Kilwa, Bukoba, Musoma na Mwanza vitaimarishwa na maabara ya Nyegezi itakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kwa mara ya kwanza kuanzia Juni 2004 kuruhusu kuuza nje ya nchi samaki wa mapezi wa baharini ili kuinua kipato cha wavuvi wadogo wadogo na pato la Taifa. Uamuzi huu ulifikiwa kutokana na matakwa ya wananchi wa Ukanda wa Pwani. Mawasiliano ya kina yalifanywa na wadau kabla ya kufikia uamuzi huu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, doria zilifanyika kwenye maeneo mbalimbali ambapo watuhumiwa 31na nyavu 2,143 zenye ukubwa tofauti zilikamatwa na kuharibiwa kwa amri ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, doria 12 zilifanyika pia kwenye Bahari ya Ndani na kwenye Ukanda wa Uchumi ambapo 6 zilikuwa ni kwa meli na 6 ni kwa ndege na meli tatu zilishikwa kwa tuhuma ya kukiuka masharti ya leseni na kusafirisha mizigo kinyume na sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itaendesha doria ya siku 12,500 za kazi ili kudhibiti uvuvi haramu na kuzuia biashara ya magendo. Mtambo maalum wa kompyuta utanunuliwa kwa madhumuni ya kuratibu mwenendo wa meli zinazovua kwenye Ukanda wa uchumi wa Bahari.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilitoa elimu kwa umma kuhusu uvuvi bora kwa kurusha vipindi 160 vya redio na 10 vya *television*. Ukusanyaji wa takwimu uliimariswa kwa kuwapa masomo ya muda mfupi watumishi 86 na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Wizara itatoa elimu kuhusu uvuvi bora kwa umma kwa kurusha hewani vipindi 138 vya redio na 10 vya *television*. Sensa ya wavuvi na zana itafanyika kwenye Ukanda wa Pwani na Maziwa makubwa pamoja na kutoa mafunzo kwa wakusanya takwimu 60 ili kuimariswa matumizi endelevu ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ilikamilisha upembuzi yakinifu kuona jinsi gani Hifadhi za Bahari na maeneo tengefu, pamoja na rasilimali za Bahari na Mwambao zinavyoweza kuchangia katika juhudhi za kuondoa umaskini. Matokeo ya upembuzi huo ni utayarishaji wa mpango ambao utahusika na usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari na mwambao. Mpango huu vile vile utahusisha sehemu ya Tanzania Visiwani (Zanzibar). Aidha, Wizara yangu ilikamilisha ujenzi wa Ktuo cha Taifa (*Visitors Information Centre*) katika Maeneo Tengefu ya Visiwa vya Bongoyo na Mbudya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itakamilisha utayarishaji wa mpango wa mchakato wa muda mrefu (*Long Term Strategic Plan*). Aidha, Wizara itakamilisha utayarishaji wa Mkakati wa usimamizi wa fukwe za bahari na visiwa vidogo, Hifadhi za Bahari ya Ghuba ya Mnazi na maingilio ya Mto Ruvuma na maeneo tengefu ya Dar es Salaam Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, Wizara itakamilisha kanuni za kutekeleza sheria ya Hifadhi za Bahari Na. 29 ya mwaka 1994 katika Hifadhi za Bahari ya Mafia na Ghuba ya Mnazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi, utafiti wa uvuvi umekuwa ukifanyika kwa lengo la kubaini wingi wa rasilimali na kutoa ushauri kuhusu matumizi endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, taasisi ilifanya utafiti wa Kamba katika maeneo ya Pwani ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara ili kubaini wingi wa samaki katika maeneo hayo. Kutokana na utafiti huo msimu wa uvuvi wa kamba ulipangwa kuanza rasmi tarehe 1 Aprili, 2004 na utaishia Septemba, 2004 badala ya Machi - Novemba ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, samaki aina ya Kisukuku anayesadikika kuishi miaka takribani milioni 60 iliyopita alipatikana kwa mara ya kwanza kwenye maji ya Tanzania. Taarifa za kuaminika ni kwamba tokea samaki huyu apatikane huko Kilwa Masoko, idadi ya watalii imeanza kuongezeka. Taasisi za Utafiti za nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi zimeweka mkakati wa kufanya utafiti wa samaki huyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, ujenzi wa Makao Makuu ya Taasisi na Kituo cha Utafiti cha Dar es Salaam utaanza.

Mheshimiwa Spika, utalii ni sekta ambayo inaweza kuchangia ukuaji wa kasi wa pato la taifa. Katika kutekeleza majukumu yake, sekta hii itakamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Sera ya Utalii na pia itatilia mkazo kukuza na kuimarisha utalii wa ndani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, biashara ya utalii ulimwenguni iliathiriwa na vita vya Iraq, ugonjwa wa mafua (*SARS*) na ugaidi. Mataifa mbalimbali hasa yale ambayo ni masoko ya utalii duniani yalitoa tahadhari ya usafiri kwa wananchi wake kutotembelea maeneo fulani kwa hofu ya kutokuwa salama. Kutokana na hali hii, watalii 576,198 waliingia nchini ikilinganishwa na matarajio ya watalii 603,990 na kuliingizia Taifa dola za Kimarekani milioni 731.

Mheshimiwa Spika, Watalii wa ndani waliongezeka kutoka 270,934 mwaka 2002 hadi 297,077 mwaka 2003, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, lengo ni kupokea watalii 607,000 kutoka nje ya nchi, watakaoliingizia Taifa dola za Kimarekani milioni 750.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ilibaini na kutathmini vivutio na maeneo ya uendelezaji utalii katika Mikoa ya Singida, Mtwara, Mwanza na Mara. Aidha, taarifa na picha za vivutio mbalimbali katika Mikoa hiyo ziliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itafanya semina za uhamasishaji katika mikoa ya Singida, Lindi na Mtwara na kuandaa taarifa na picha za vivutio vya utalii katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa Amani kupitia Utalii uliohudhuriwa na washiriki 350. Vile vile, Wizara ilishiriki kwenye mikutano ya Shirika la Utalii ya nchi za Jumuiya ya Madola na *Africa Travel Association* iliyofanyika Malaysia na Cameroon sawia kwa madhumuni ya kukuza ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itakuwa mwenyeji wa semina ya Shirika la Utalii Duniani kuhusu Maendeleo ya Utalii na Kupunguza Umaskini (*Regional Seminar on Tourism Development and Poverty Alleviation*) itakayofanyika Septemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara iliteua Kampuni ya *DCDM Consulting Group* kutoa ushauri kuhusu masuala ya uwekezaji katika sekta ya utalii. Randama (*Memorandum*) ya maeneo yanayofaa kwa uwekezaji na ripoti ya mpango wa kudhamini wawekezaji wadogo vimekamilika. Vile vile, Wizara ilitayarisha kanzidata ya wawekezaji watarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itatayarisha jarida litakalotoa habari za kina za fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ilikamilisha rasimu ya vigezo vya kupanga hoteli, migahawa na loji za kitalii katika daraja. Aidha, watumishi wanenamemba mafunzo kuhusu taaluma ya kusimamia zoezi hilo nchini Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itaendesha semina kwa wadau kuhusu vigezo hivyo na kuanza kuendesha zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilikamilisha ripoti ya matokeo ya utafiti wa wageni wanaotoka nje. Vile vile, iliendelea na ukusanyaji wa takwimu mbalimbali kutoka kwa watoa huduma za kitalii kwa ajili ya kutengeneza mfumo mapya wa ukusanyaji takwimu unaojulikana kama *Tourism Satellite Account*. Utafiti huo ulifanyika katika Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Iringa, Singida na Mtwara. Aidha, Wizara ilianzisha tovuti inayoitwa www.tourismtanzania.go.tz ambayo inatoa taarifa muhimu za sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kukusanya takwimu za watoa huduma za utalii katika vituo vyote vya maingilio ya watalii pamoja na kuboresha tovuti.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii imekuwa na jukumu la kutangaza utalii kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuharakisha ukuaji wa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Bodi ilifanya ziara 22 za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi. Vile vile, ilichapisha nakala 75,000 za majarida na 150,000 za vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005, Bodi itaendelea kutafuta masoko mapya ya watalii hasa kutoka Bara la Asia, China na Urusi kutokana na matatizo ya ugaidi yanayozikumba nchi za Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Serikali wa Chuo cha Taifa cha Utalii unatoa mafunzo ya Cheti katika fani ya utalii na hoteli.

Mwaka 2003/2004, Wizara ilipata milki ya viwanja viwili vilivyopo Mtaa wa Shaaban Robert, Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Utalii kitakachotoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada. Aidha, Serikali imesaini Mkataba wa Ushirikiano na Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo hicho ambacho kitatoa elimu ya ngazi ya juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara inatarajia kuanza ujenzi huo utakaogharimu shilingi bilioni tano. Chuo kitakapokamilika kitakuwa na

uwezo wa kutoa wahitimu wa ngazi ya usimamizi katika fani ya hoteli ili kupunguza waajiriwa wageni katika hoteli nyingi hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya mambo ya kale ina jukumu la kulinda, kutafiti na kuhifadhi urithi wa mambo ya kale. Utekelezaji wa jukumu hili umezingatia mwono na wito wa sera ya utamaduni ya mwaka 1997, sheria ya mambo ya kale ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya 1979. Kutokana na sekta ya mambo ya kale kutokuwa na sera yake, katika mwaka 2004/2005 Wizara yangu itaandaa sera ya mambo ya kale.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilienendelea kufanya utafiti wa akiolojia huko Kinole na *Kola Hill*, Mkoani Morogoro. Aidha, Wizara iliratibu na kusimamia utafiti wa akiolojia huko Ngorongoro katika Bonde la Olduvai, eneo la Laitoli, Engaruka, Ziwa Eyasi, Hifadhi ya Taifa Serengeti na Ziwa Natron.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itafanya utafiti wa kuboresha historia ya maeneo ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aidha, Wizara itakamilisha mpango wa uhifadhi endelevu wa Mji Mkongwe wa Bagamoyo na kuanza kuboresha baadhi ya vivutio vilivyoko kwenye njia ya kati ya utumwa kutoka Ujiji hadi Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ilikamilisha ujenzi wa vituo vya kumbukumbu na habari vya Isimila Mkoani Iringa na Kolo Mkoani Dodoma. Vile vile, Wizara ilikamilisha ukarabati wa jengo la Caravan Serai, Bagamoyo Mkoani Pwani litakalotumika kama kituo cha habari na kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo vya kumbukumbu na taarifa vya Ujiji, Mkoani Kigoma na Kaole, Mkoani Pwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara ilikamilisha ukarabati wa nyumba ya Kijerumanii, uimarishaji wa gofu la Msikitii Mkuu na jengo la Kireno huko Kilwa Kisiwani. Aidha, Wizara ilikamilisha ujenzi wa gati, kuweka umeme wa mionzi ya jua na mawasiliano ya redio ya upepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itafanya tafiti za kiakiolojia, historia, usanifu majengo, elimu jamii na kuandaa mpango wa uendeshaji wa Kilwa Kisiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhifadhi wa Mji wa Kihistoria, Bagamoyo, katika mwaka 2003/2004, Wizara iliingia Mkataba na Serikali ya Sweden kugharimia mradi wa uboreshaji njia ya kati ya biashara ya utumwa, vipusa na meno ya tembo ili iingizwe kwenye orodha ya Urithi wa Dunia. Katika mwaka 2004/2005, Wizara itaanza kutekeleza Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Makumbusho ya Taifa linatekeleza jukumu la kukusanya, kuhifadhi na kutafiti vitu vyote vya urithi wa kihistoria, kiutamaduni,

kisayansi na kiteknolojia. Taarifa za urithi huo huhifadhiwa na kutumika kuelimisha Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Shirika lilifanya uhamasishaji wa jamii ili zihifadhi na kuuensi utamaduni wao. Jamii ya Wamwera ilihamasishwa na kufanya tamasha la Siku ya Utamaduni wa Mtanzania katika Kijiji cha Makumbusho. Aidha, katika mwaka 2003/2004, Shirika liliendelea na maandalizi ya ujenzi wa Jumba la Utamaduni kwa kuwashirikisha wadau ambapo warsha mbili zilifanyika kupata maoni yao. Watendaji wa Makumbusho pia walipata fursa ya kutembelea nchi nyingine kupata usoefu wa uendeshaji wa majumba ya Makumbusho. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Shirika litaendelea na mpango wa maandalizi ya ujenzi wa jumba la utamaduni na kutafuta wafadhili wa ujenzi wa jumba hilo. Mwaka 2003/2004, Shirika lilianza kufanya utafiti wa akiolojia Wilaya ya Iringa na utafiti wa Viumbe Bahari huko Kaole, Wilayani Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Shirika litaendelea na mpango wa akiolojia Wilaya ya Iringa na utafiti wa viumbe bahari katika Wilaya ya Mafia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Wizara ilikuwa na watumishi 3,484. Pamoja na idadi hiyo, bado kuna upungufu wa watumishi. Matarajio yalikuwa ni kuajiri watumishi 166 lakini watumishi walioajiriwa katika ajira mbadala ni 20 tu.

Katika Mwaka 2004/2005, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 152.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara ilitegemea kuwapandisha cheo watumishi 286 wa kada mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2004, watumishi 150 walikuwa wamepandishwa cheo. Mapendekezo mengine yako Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara inatarajia kuwapandisha cheo watumishi 326.

Mheshimiwa Spika, jumla ya watumishi 323 walipatiwa mafunzo ya taaluma mbalimbali ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi katika mwaka 2003/2004. Aidha, katika kuendana na mabadiliko ya teknolojia na utandawazi Wizara imefanya zoezi la kubaini mahitaji ya mafunzo kwa watumishi na kuandaa mpango wa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara itaanza kutekeleza mpango wa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ustawi wa watumishi, Wizara imeingia mkataba na Benki mbalimbali unaowawezesha watumishi kukopa fedha. Hata hivyo, tatizo lililojitokeza ni riba kubwa inayotozwa kwa mikopo. Wizara pia ina mipango ya kukabiliana na janga la ukimwi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara iliendelea kuboresha vyuo kwa kukarabati majengo na kuboresha mitaala pamoja na kuvipatia vifaa vya kufundishia ili vilingane na mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua mbalimbali zilichukuliwa na vyuo ili vipate usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Usajili wa Vyuo vya Elimu ya Ufund. Chuo cha Wanyamapor Mweka ambacho kilithibitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa kituo cha mafunzo bora *Centre of Excellence* katika fani ya wanyamapor, kinatarajia kupanua soko lake kwenye nchi za maziwa makuu na kupanua wigo wa mafunzo ya muda mfupi pamoja na kuridhia mikataba ya ushirikiano na vyuo, taasisi za elimu na utafiti ndani na nje ya nchi.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vyuo vya Elimu ya Ufund Stadi itakamilisha mtaala wa kitaifa wa fani ya Utalii ambao utawezesha kudhibiti na kuboresha kiwango cha elimu kinachotolewa na vyuo vya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uvuvi Mbegani kimefikia katika hatua za mwisho za kupata usajili wa awali wa Baraza la Taifa la Usajili wa Vyuo vya Elimu ya Ufund. Pamoja na mafunzo ya kawaida, lengo la Wizara ni kuinua hadhi ya Chuo hiki ili kiwe taasisi ya kuendeleza shughuli za uvuvi katika Ukanda wa Bahari (*Fisheries Development Centre*) kama kilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambao ulizinduliwa mwaka 2002, kila Idara imeandaa mkataba wake wa jinsi ya kuwahudumia wateja kwa ufanisi. Katika mwaka 2004/2005 Wizara itaendelea kutekeleza Mkataba huo. Aidha, Taasisi na Mashirika yaliyo chini wa Wizara yametakiwa kuandaa mikataba ya Huduma kwa wateja wao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara iliandaa mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa vyuo, taasisi, mashirika na wakala wa Serikali. Wakuu wa vyuo na Maafisa Maliasili wa Mikoa walipata mafunzo hayo yaliyolenga kubaini namna na kuzuia vitendo vya rushwa na kuimarisha utendaji unaozingatia misingi ya utawala bora. Kila Taasisi, Mashirika na Wakala wameagizwa kuwa na mipango ya kupambana na rushwa na kuimarisha utawala bora katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya utawala bora kwa watumishi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2004, Mashirika 27 kati ya 33 yaliyokuwa chini ya Wizara yalikuwa yamerekebishwa au kubinafsishwa. Mashirika 19 yamesaini mikataba ya mauzo na mashirika 8 yamesaini makubaliano ya awali. Kati ya Mashirika 6 yaliyobaki, 4 yamefilisiwa, moja shughuli zake zimefungwa na moja bado halijafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itaendeleza urekebishaji wa mashirika yaliyosalia pamoja na kufuatilia maendeleo ya uendeshaji kwa yale yaliyorekebishwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wananchi na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa shukrani kwa washirika wetu wa maendeleo wafuataao kwa michango yao ya kifedha na kitaalamu kama ifuatavyo:-

Norway, Denmark, Finland, Marekani, Sweden, Japan, Ufaransa, Ujeruman, Ubelgiji, Uingereza, Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*), *ADB*, *AWF*, *FAO*, *FZS*, *GTZ*, *IUCN*, *KfW*, *Trade Aid*, *MIGA*, *AFRICARE*, *UNESCO*, *UNDP*, *World Bank*, *WWF*, *ICCROM* na mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu, Bwana Solomon Odunga, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa ushirikiano walionipa na kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2003/2004. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu ili iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha 2004/2005, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya shilingi 47,123,892,100. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,970,499,400 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi 28,153,392,700 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa iko tayari kujadiliwa. Wasemaji wanne wa mwanzo watakuwa Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, hawa hawajachangia kabisa tangu tumeanza.

Halafu atafuatia Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Esha Stima, wajiandae. Lakini kwanza namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Makadirio haya atoe maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira.

MHE. HASSAN RAJAB KHATIB - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu Na. 81(1) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2004, nachukua fursa hii kukushukuru

kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2003/2004, pamoja na maoni juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii kwa masikitiko makubwa kuwapa pole za dhati familia na wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini Mkoani Mbeya, kwa kufiwa na Mbunge wao, Mheshimiwa Yetet Sintemule Mwalyego, tarehe 24 Juni, 2004 hapa MJINI Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapa pole familia na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, Mkoani Morogoro, kwa kufiwa na Mbunge wao, Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, kilichotokea usiku wa kuamkia tarehe 22 Julai, 2004 hapa MJINI Dodoma. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Napenda pia kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikaa Dar es Salaam tarehe 1 Juni, 2004 kupitia Taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2003/2004 na kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, aidha, masuala yafuatayo yalijitokeza :-

- Dira ya Wizara ya Maliasili na Utalii;
- Muundo wa Wizara;
- Majukukmu ya Wizara;
- Utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka 2003/2004;
- Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2003/2004;
- Mpango wa maendeleo na Bajeti ya mwaka 2004/2005; na
- Maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara hii ni kusimamia, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza raslimali za Maliasili na Mambo ya Kale na kukuza utalii kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, majukumu haya ya Wizara ni mapana na makubwa na yanagusa sekta nyingi za kiuchumi, kibiashara na kijamii katika ngazi za Kitaifa na Kimataifa. Kamati inaipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kumudu utekelezaji wa majukumu hayo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kutekeleza ipasavyo maagizo karibu yote ambayo ilipewa na Kamati mwaka 2003/2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na maelezo, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Wizara nchini ambayo ilitembelewa na Wajumbe wa Kamati katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Wizara kwa kufanikiwa kukusanya asilimia 98 sawa na shilingi 20,938,760,995.65 ya Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli hadi kufikia mwezi Aprili, 2004. Halikadhalika, Kamati imeridhishwa na Matumizi ya kawaida yaliyofikiwa shilingi bilioni 20.3 sawa sawa na asilimia 76.9 ya Makadirio ya mwaka mzima wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeridhishwa na mafanikio mbalimbali ambayo Wizara imeyapata kutokana na utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

- (i) Kufanya mapitio ya Sera na kurekebisha baadhi ya Sheria na Kanuni katika sekta mbalimbali za Maliasili;
- (ii) Kuimarisha utendaji wa Watumishi katika Idara mbalimbali;
- (iii) Kuimarisha ulinzi wa Maliasili za majini na zile za nchi kavu kwa kuweka doria na usimamizi madhubuti;
- (iv) Kuimarisha na kuboresha Miundombinu, ikiwemo kujenga Ofisi na nyumba za wafanyakazi, ukarabati wa majengo ya Ofisi za Vyuo mbalimbali chini ya Wizara yake;
- (v) Kuimarisha utangazaji wa Utalii ndani na nje ya nchi; na
- (vi) Kuchangia katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado Wizara inaendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali, yakiwemo:-

- (i) Uvunaji haramu wa mazao ya Maliasili;
- (ii) Uvamizi wa maeneo ya Hifadhi kwa matumizi ya kilimo, makazi, uchimbaji wa madini na uchomaji wa misitu ya Hifadhi;
- (iii) Ukosefu na ubovu wa miundombinu; na

(iv) Uchache wa watendaji na vitendea kazi, kama vile nyumba za watumishi, magari, Ofisi, vifaa vya Ofisini katika baadhi ya Vituo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara kuendelea kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa na Wizara kuwa kwa kuzingatia dira na mwongozo wa Serikali, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kurekebisha Sheria za Sekta za Maliasili kufuatana na Sera mpya;
- (ii) Kuongeza ushirikishwaji wa wadau wa Sekta za Maliasili kwa kuhusisha jinsia zote;
- (iii) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, ikiwa ni pamoja na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha;
- (iv) Kuimarisha utendaji wa Wizara na Taasisi zake ili kuboresha utoaji wa huduma zake;
- (v) Kuimarisha ulinzi wa Maliasili, Mambo ya Kale na Vivutio vya Utalii dhidi ya matumizi haramu;
- (vi) Kuendelea kuitangaza Sekta ya Maliasili na Utalii na kuweka mazingira mazuri zaidi yanayovutia uwekezaji;
- (vii) Kuendeleza kudumisha ushirikiano wa Kimataifa; na
- (viii) Kutekeleza mkakati wa Wizara kuhusu kukabiliana na janga sugu la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshauri Wizara kuimarisha taratibu za kushirikisha wananchi katika kusimamia, kuhifadhi na kulinda maliasili kwa baadhi ya vijiji kwa kuvitengenezea *Forest and Beekeeping Management Plan*, kuwaelimisha wananchi kuhusu uharibifu wa mazingira unaotokana na kuchoma misitu ovyo. Pia Wizara iendeleze utaratibu wake wa kutoa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya husika ili kuleta maendeleo kwa wananchi waishio karibu na maeneo ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara yetu katika Mkoa wa Tanga, Kamati ilitembelea maeneo ya Hifadhi ya Msitu wa Amani na kushuhudia uharibifu wa mazingira ambao unafanywa na wachimbaji wadogo wadogo. Kamati inashauri Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini kuzuia uharibifu huu. Vinginevyo, Msitu wa Amani utatoweka na Mji wa Tanga kukosa maji kabisa au kupata maji yaliyojaa Zebaki yaani *Mercury* ambayo ina madhara makubwa kwa afya za binadamu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Wizara kuangalia upya mwenendo mzima wa uvunaji magogo katika maeneo ya Pwani, Mtwara, Rufiji, Urambo, Uvinza Kilwa na kadhalika. Kamati pia ilishauri Wizara kusitisha uvunaji na usafirishaji wa magogo katika maeneo yaliyotajwa kutokana na kuwepo uvunaji haramu na hata wenye leseni kuvuna kinyume na makubaliano wakati wa utoaji leseni kama vile idadi, aina ya size ya magogo yanayofaa. Kamati pia iligundua kuwepo kwa baadhi ya Maafisa Misitu, ambao si waaminifu na washirikiana na wafanyabiashara wa magogo kusafirisha nje ya nchi magogo hayo.

Kamati inashauri Wizara kuwafuatilia na kuwadhibiti na hata kutoa adhabu pindi wanapofahamika. Utaratibu makini uandaliwe ili wageni wasiruhusiwe kuingia vijijini kuvuna miti katika misitu yetu. Wageni hawa hawana uchungu kabisa na uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu hawa. Wavunaji na wauzaji wa maliasili za magogo waunde Chama chao ili waweze kushauri utaratibu mzuri zaidi wa kuendeleza biashara hii kwa manufaa ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inayo magofu mengi sana ya kihistoria kama vile magofu ya Mafia, Mikindani, Bagamoyo, Kilwa na kadhalika. Wakati umefika kwa Wizara kuyatambua magofu hayo na kuandika historia zake. Historia ya maeneo hayo imeanza kutoweka kutokana na kukosa kumbukumbu na wazee walioishi kipindi hicho kufariki. Utalii unaweza kuongezeka sana endapo maeneo hayo ya kihistoria yatakarabatiwa, kuhifadhiwa na kutangazwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hifadhi ya Bahari, kazi kubwa sana imefanya katika eneo hili. Watendaji katika maeneo haya wanahatarisha maisha yao katika kufukuzia meli ambazo zinaendesha uvuvi haramu katika maeneo yetu ya bahari na kuondoka na mali ya nchi hii kwa kiwnago ambacho hakitabiriki.

Kwa hiyo, tunashauri Watumishi wa Hifadhi ya Bahari wapewe boti za kisasa ili kufuatilia huu uvuvi haramu na ambao unalisababishia Taifa letu kupoteza mali yake. Pia, wananchi wa maeneo hayo washirikishwe na kupewa elimu ya faida ya Hifadhi hii ili waweze kuwa walinzi bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye uamuzi wa dhati kuweza kuimarisha Mradi wa Hifadhi ya Bahari kwa maana ya kupewa fedha za kutosha kwa shughuli za Hifadhi na miradi iliyo chini yake. Mradi ambao unatakiwa ufanywe kwa sasa ni kupata zana mbadala kwa wavuvi wanaoishi katika maeneo ya hifadhi. Utaratibu wa mikopo kwa wavuvi na wananchi wengine katika maeneo ya Hifadhi uandaliwe ili wavuvi hao waweze kuondokana na shughuli zao za zamani za uvuvi haramu na wajipatie riziki yao kwa shughuli halali, ikiwemo ya uvuvi na upandaji wa mwani.

Mheshimiwa Spika, utalii katika nchi yetu haujatoa matunda ambayo nchi hii inastahili kupata. Zipo nchi ambazo hazina kivutio chochote cha utalii, lakini zinategemea pato lake kubwa kutokana na utalii, kwa mfano, nchi za Mauritius, Lesotho, Seycheles, Afrika Kusini, Namibia, Kenya, Uganda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania si tu ina wanyaampori wengi katika Hifadhi zetu, bali ina misitu mikubwa, ina maeneo ya kihistoria, ina *beaches* nzuri sana, ina viumbe wengi wa baharini na ina mikoko ya Mtwara, Mafia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, utalii hautegemei sana kuwepo kwa mvua kama kilimo kinavyotegemea mvua. Hivyo basi, ni muhimu sana Serikali kuliangalia suala la Utalii kama eneo ambalo tumelishughulikia kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uchunguzi iliyofanywa na wadau wa utalii inaeleza mapungufu katika kuendeleza utalii, yakiwemo urasimu, miundombinu kuwa duni, zikiwemo barabara mbovu, hoteli zenye kiwango cha chini sana kwa huduma kama vile chakula, ukarimu na wahudumu ndani ya hoteli hizo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa kueneza shughuli za utalii katika maeneo mengine, yakiwemo ya Ukanda wa Kusini. Tatizo la utalii katika maeneo hayo ya Kusini ni ukosefu wa miundombinu ya usafiri, mawasiliano na hoteli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo wageni walioingia katika maeneo hayo ya utalii, lakini uwekezaji wanaofanya kwa kweli ni utani tu. Wakati umefika kama kuna watu wanakuja kuwekeza, basi wawekeze kweli na si kama watu ambaa ni *speculators* tu, kwani wanachukua ardhi kwa kununua kutoka kwa wananchi, lakini hakuna kitu cha maana ambacho kinafanya. Watu hawa waangaliwe kwa makini, upo uwezekano wakuchukua maliasili zetu bila sisi kujua au kuhamisha mapato yetu kwenda nje kwa njia ya kutoa Ankara za uongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiamua kushughulikia utalii kwa nguvu zote, nchi hii itainua kwa haraka sana ukuaji wake wa uchumi. Kwani mazingira yetu ya kuwa na amani yanaweza yakatumika kama chanzo kizuri cha wageni kutembelea kwetu.

Mheshimiwa Spika, utangazaji wa nchi yetu pia haufanywi kwa ukamilifu wa kutosha. Nchi jirani inaendelea kuchukua idadi kubwa ya watalii kwa kutumia kutangaza vivutio vya Tanzania kuwa vipo nchini kwao.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya Kamati kuhusu suala hili la utalii ni kwamba tunaweza kufanya zaidi kuliko tunavyofanya sasa, hebu tuzamie huko kama Serikali na wadau wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo hayo, Kamati yetu inakubaliana na Mpango wa Maendeleo pamoja na Makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005. Hivyo, Kamati inaomba Bunge lako Tukufu liyapitishe Makadirio ya Wizara hii. Aidha, Fedha zinazoombwa na Wizara chini ya Fungu Na. 69 ni jumla ya shilingi 47,123,892,100/= . Kati ya hizo shilingi 28,153,392,700/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 18,970,499,400/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu kumshukuru na kumpongeza Waziri Wizara hii ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, Katibu Mkuu wake Bwana Solomon Odunga, pamoja na watendaji, wataalam wa Wizara yake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa mpango wa Bajeti hii kwa makini na ufanisi wa hali ya juu na hivyo kuifanya kazi ya Kamati kuwa rahisi na ya mafanikio makubwa katika kuipitia Taarifa ya Utekelezaji wa mwaka 2003/2004 na Makadirio ya Bajeti kwa Kipindi cha Mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira waliohusika na zoezi zima la kujadili na kuchambua maelezo ya Bajeti ya Wizara hii ni pamoja na Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Shaib Ahmada Ameir, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ali Said Juma, Mheshimiwa Shariffa Mbarouk Khamis, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Lucas Selelji, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan na Mheshimiwa Martha Wejja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa hadi kuniwezesha kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Namshukuru pia Katibu wa Bunge Ndugu Kipenka Mussa na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Sam Manamba, kwa kazi nzuri iliyofanyika ya kuratibu shughuli zote za Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea nitambue kuwepo katika *Gallery* ya Bunge, Mbunge wa Bunge la Marekani, ambaye amefuatana na Balozi Mdogo wa Ubalozi wa Marekani hapa nchini.

I wish to recognize the presence in the gallery of the United State Congressman, Mr. Wang Zang Xuam, accompanied by his delegation. Karibu.

Tunaendelea sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO - MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5)(b)(c) cha Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004.

Napenda pia kuungana na wenzangu kwa niaba ya Wapigakura wa Jimbo langu la Moshi Mjini, kutoa rambirambi zetu za dhati kabisa kwa wananchi na familia za hayati Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na hayati Mheshimiwa *Comrade Capt.Theodos James Kasapira*, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa msiba mkubwa wa kuondekewa na waliokuwa wapendwa Wabunge wao. Mwenyezi Mungu awalaze Marehemu mahali pema peponi. Pia natoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mbunge wa Pandani kwa kufiwa na baba yake mzazi juzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Zakia Meghji, jinsi alivyoweza kuiongoza Wizara hii muhimu kwa miaka mingi bila msaada wa Naibu Waziri na kuifanya Tanzania kujulikana duniani kote kama moja ya nchi zenye vivutio vya utalii na ushahidi uko tele jinsi utalii ulivyokua chini ya uongozi wake. Hongera sana.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani mtanisamehe kwa sababu Kiswahili cha kichaga ni kigumu kidogo hapa na pale huenda nikafanya makosa. (*Makofiki cheko*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina eneo la kilometra za mraba 58,000 za uvuvi kwenye maji baridi na eneo la kilometra za mraba 64,000 kwenye maji ya bahari. Uvuvi unaochangia Pato la Taifa hufanywa na wavuvi wadogo wadogo wasio na nyenzo bora ambaao ni kama asilimia 95 ya uvuvi wote unaofanyika Tanzania. Karibu uvuvi huo wote unatokana na kuvua kwenye eneo la maji baridi ambayo mchango wake ni zaidi ya asilimia 80 na uvuvi wa baharini maji chumvi ni chini ya asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, kwa mlinganisho wa maeneo ya uvuvi kati ya maji baridi na maji chumvi katika Pato la Taifa, ni rahisi kutoa hitimisho kuwa Tanzania inakosa mapato mengi kutoka kwenye uvuvi wa baharini na hili ni tatizo kubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, takwimu za mwaka 2003 zinaonyesha kuwa ukuaji wa sekta ya uvuvi ulipungua kwa asilimia 0.1%. Hapa tunashindwa kuelewa ilikuwa vipi samaki walikwisha au wahusika walishindwa kukusanya mapato au wawekezaji walionunua kiwanda cha *TAFICO* wameshindwa kufanya kazi?

Mheshimiwa Waziri, tunaomba atupe taarifa, ni lini *TAFICO* iliuzwa na hadi sasa imezalisha kiasi gani? Ukiangalia mgao wa fedha katika kuendeleza sekta hii ni shilingi 300,000,000/= ambazo ni ahadi /msaada wa *UNDP*. Bajeti ya fedha za ndani haipo kwenye kuendeleza uvuvi katika nchi hii. Hapa inaonyesha ni jinsi gani umuhimu wa sekta hii kwa Serikali ulivyo mdogo katika vipaumbele vyake, kwa maana nyingine Serikali haina nia ya dhati ya kuwandeleza raia wanaoishi ukanda wa pwani ambaao ni moja ya tatu ya Watanzania wote. (*Makofiki*)

Mheshimiwa Spika, nchi kama Ushelisheli na Madagascar, uchumi wa nchi hizo unategemea uvuvi wa baharini na Utalii wa ufukweni. Hapa itabidi tukubaliane kuwa

Tanzania bado tumelala sana hasa uvuvi wa baharini ambao hata robo yake hatujaweza kuitumia kama inavyotakiwa na badala yake wanaonufaika ni wafanyabiashara toka nje ya nchi wanaotumia meli na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaanmini kuwa kama mikakati endelevu itawekwa kwenye sekta hii ya uvuvi hasa baharini basi kwa kiasi kikubwa matatizo yetu kiuchumi tungeyapunguza kwa kiasi kikubwa na lishe ingeongezeka. Kwa sababu hiyo ya kuachwa uvuvi wa bahari leo kuna meli za kigeni zinazovua katika bahari yetu kinyume cha sheria zisizopungua 70 kutoka Japan, Kenya na kadhalika maana wenywewe tumelala.

Mheshimiwa Spika, inakisiwa kuwa kati ya hekta 130,000 na 500,000 za misitu hupotea kila mwaka nchini Tanzania, kwa uvunaji ambao hauangaliwi na hivyo Serikali kupoteza pato lake kutoka kwenye maliasili.

Mheshimiwa Spika, katika jarida liitwalo *Cut and Run, Illegal Logging and Timber Trade in the Tropics*, imeonyesha kuwa Tanzania ni mojawapo inayofanya biashara haramu ya mazao ya misitu, kitu kinachowanufaisha watu wachache na Taifa kukosa stahili yake ya kodi. Mbali ya Mapato ya Taifa, idadi kubwa ya wanyamapori ambao wametengwa Kimataifa kwenye *Red-Listed Species* wanahama na kupotea kabisa kutokana na makazi yao kuvurugwa na wakataji magogo na wakataji mbao. Hii ni hasara nyngine kwenye Utalii na Utafiti wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu za biashara ya mazao ya misitu kutoka *World Resources 2000 - 2001* zinaonyesha kuwa Tanzania inapata *6 million dollar* kutokana na mauzo nchi za nje ya mazao ya misitu wakati wenzetu wa Kenya wanapata *30 million dollar*. Wakati sisi tuna eneo kubwa zaidi la misitu. Tuna misitu na kila kitu lakini miti yetu inapitia Kenya na kupotea.

Mheshimiwa Spika, biashara ya uchongaji vinyago (*Wood Carving Industry*) inaingizia nchi yetu dola milioni 1.5 kwa mwaka wakati Kenya wanapata dola milioni 20 kwa mwaka. Nchini Kenya biashara hii imeajiri kati ya watu 60,000 - 80,000 lakini Tanzania haijulikani ni watu wangapi wanajishughulisha na bidhaa hii, kitu ambacho kinapelekeea kukosa mapato au nchi nyngine kunufaika na bidhaa hizi zitokazo Tanzania. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na *record* nzuri ya watu wanaojishughulisha katika biashara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maliasili ambayo nchi yetu imejaaliwa kuwa nayo ni wanyama pori, kwani tunazo mbuga zenye wanyama wa kila aina. Tuna uhakika kabisa mapato ambayo yangetsha yanatokana na uwindaji pekee (*Hunting Profit*) yangetsha kuwaendeleza wananchi pamoja na Serikali katika ujenzi wa miundombinu itumiwayo kwenye Mbuga zetu.

Mheshimiwa Spika, kuna tabia moja mbaya sana ambayo Serikali inaikumbatia katika biashara ya uwindaji inayowanyima wazawa haki kwa kuwamilikisha wagoni

hunting blocks nyingi, mgeni anakuwa anamiliki *blocks* kama sita mpaka kumi na leseni yake ni ya muda wa miaka mitano. Sasa kwa utaratibu huu tutapata nini?

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uombaji na utoaji leseni za kuwinda una ukiritimba mwingi na hauko wazi hivyo kuzidisha mazingira ya rushwa, kitendo cha mwombaji kuambiwa kwanza awe na vifaa vya kuwindia kabla ya leseni kutolewa ni kitu cha ajabu sana. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali, kwanza kuwapa kipaumbele wazawa katika shughuli za kuwinda kitu kitakacho saidia kuiongezea mapato na kupunguza matukio ya kuwaweka wananchi wanaokutwa kwenye *hunting block* za wageni na kuwekwa kizuizini kama majangili.

Pili, kubadili utaratibu wa sasa unaomtaka mwombaji leseni kuwa na vifaa vya uwindaji kabla ya kupata leseni. Waombaji wapewe leseni halafu wapewe muda kununua vifaa na muda ukipita kabla ya kutimiza masharti basi leseni zao zifutwe!.

Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu ambao umeanzishwa katika Mkoa wa Tabora ambapo *block* 16 zimetengwa na kugawiwa kwa wawindaji chini ya utaratibu shirikishi kwa wananchi waliokwenye maeneo hayo chini ya mpango wa *Tabora Wildlife Management Area*. Tunashauri utaratibu huu utumike nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja kati ya watu wenye *interests* katika *Tourism Industry*, hivyo ninayoyasema ni ukweli na nasema kwa kufuatia uzoefu nilionao. Utalii unaongelewa na nchi yetu ni katika nyanja za kutembelea Mbuga za wanyama na kupanda Milima iliyomo nchini mwetu tu, ndugu zetu wa Zanzibar wametuzidi kwa kukuza utalii wa mila na tamaduni za Visiwa hivyo pamoja na bidhaa za asili visiwani humo bila kusahau fukwe za bahari.

Mheshimiwa Spika, utalii ni moja ya vyanzo vikubwa vinavyoiletea nchi yetu fedha nyingi za kigeni. Hakuna ubishi, Serikali inaelekeza nguvu nyingi ili kukuza sekta ya utalii. Ni kweli Serikali inanufaika, lakini ni wananchi wangapi wananufaika na sekta hii ya utalii?

Katika nchi yetu yako makampuni 148 na kati ya hayo ni 48 tu ndio yanamilikiwa na wazawa, yaliyobaki yanamilikiwa na Watanzania ambao si wazawa. Hivyo nitakuwa sijakosea nikisema kuwa biashara ya utalii katika Tanzania bado haimnufaishi mwananchi wa Tanzania na kati ya makampuni 148 yanayofanyabiashara hiyo, 110 yanafanyabiashara katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kuwa mfanyabiashara wa utalii unahitaji leseni zifuatazo:-

- | | | | |
|----|------------------------------|---|---------|
| 1. | <i>Tour Operator Licence</i> | - | \$2,000 |
| 2. | <i>Travel Agent Licence</i> | - | \$2,000 |
| 3. | <i>Mountain climbing</i> | - | \$2,000 |

- | | | | |
|----|--|---------------|----------------|
| 4. | <i>Tourist Hotel Licence</i> | - | \$1,000 |
| 5. | Leseni ya Biashara ya Wizara- | shs.190,000/= | |
| 6. | Leseni ya Biashara toka
Ofisi ya Biashara Mkoa | - | shs. 200,000/= |
| 7. | <i>TALA Licence</i> za magari na kadhalika zaidi ya shilingi bilioni nane kabla hujapata leseni ya kufanya utalii. | | |

Je, ni Watanzania wangapi wana mtaji wa kuwekeza katika biashara hii ya utalii? Sisi tunashauri, leseni ya utalii iwe moja na sio mlolongo wa leseni. Karibu biashara zote hapa nchini hulipwa kwa fedha halali za Kitanzania ambazo ni *Tanzanian shillings (Legal Tender)*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina sababu gani za msingi za kuwatoza Watanzania leseni kwa kutumia fedha za kigeni na sio fedha zetu? Leseni isiwe ni chanzo pekee cha mapato cha Wizara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro na maeneo yanayouzunguka mlima huo ni kivutio kikubwa cha watalii. Katika *Master Plan* ya *Tourism* yaani mpango kamambe wa sekta ya utalii Kitaifa, nilitazamia kuona Moshi Vijijini, Moshi Mjini, Hai, Rombo na Upareni ikiwa *declared* kama *Tourist Area* na kupewa kipaumbele katika *development* ya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza sera ya Serikali sio kukuza utalii katika eneo hili, bali kuhamishia utalii Mkoani Arusha. Watalii wanapenda maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro lakini wanakatishwa moyo na Serikali. Mfano hai ni kiwanja cha ndege cha Moshi ambacho miaka ya nyuma kilikuwa maarufu katika usafiri wa watalii kutoka Nairobi, Kenya. Hivi sasa kiwanja hicho kimekufa kabisa na watalii sasa wanalazimika kuja Mkoani Kilimanjaro kwa kutumia mabasi au kupitia uwanja wa ndege wa Arusha ambapo safari huwachosha kabla ya kazi ngumu ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa barua yake *TAA/ENG.40/17/17/12* ya tarehe 16 Julai, 2003 ilitoa *tender* kwa *Ravji Construction Co. Limited* kukarabati *potholes* kwenye *Runway 08/26*, kwa shilingi 11,668,800/= lakini, kwa sababu zisizojulikana hadi leo, hakuna kazi yoyote imefanyika na watalii, wanashindwa kutumia kiwanja hiki. *Precision Air*, waliokuwa wanatoa huduma kwa watalii hapa Moshi, lakini kwa kuwa kiwanja hiki hakijafanyiwa ukarabati, wamefuta safari zote na wamehamia Arusha, je, hii ni kufuatia sera ya Serikali ya kutaka Watalii wapande Mlima Meru badala ya Mlima Kilimanjaro?

Mheshimiwa Spika, Serikali imediriki hata kugawa sehemu ya kiwanja hiki kuwa makazi na kujengwa nyumba. Kwa nini Serikali haitamki wazi kuwa haitaki Moshi iendelee? Kuua kiwanja cha Ndege kilichokuwa maarufu ni kuua Moshi Mji wa Mlima Kilimanjaro. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizofuutilia ni kuwa Serikali ina mpango wa kukarabati uwanja wa ndege wa Arusha kwa kutumia fedha za Hazina kiasi cha shilingi bilioni 18. Ni kichekesho cha aina yake, kwani tuna uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (*KIA*) kwa ajili ya maeneo ya utalii Kanda ya Kaskazini. Kwa nini mgao huu usizingatie kiwanja cha ndege cha Moshi ambacho ni Mji wa Mlima Kilimanjaro ambacho ni kilele cha Bara la Afrika. Kama ni mgao wa haki wa fedha za walipa kodi uwanja wa ndege wa Moshi katika ukarabati nao ujumuishwe katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuifahamisha Serikali kuwa kuutelekeza mji wa Moshi ni hatua mojawapo ya kuutelekeza Mlima Kilimanjaro ambao ni kivutio muhimu cha utalii na kitega uchumi thabiti kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutangaza rasmi kuwa Moshi ni Mji wa Mlima Kilimanjaro. Nakiri tena kwa makusudi kabisa kuwa Moshi ni Mji wa Mlima Kilimanjaro sio Arusha. Toka tupate Uhuru katika awamu zote za uongozi tumekuwa na viongozi wengi kutoka Mkoani Kilimanjaro. Kutoka Kilimanjaro tuna Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Charles Keenya, Mheshimiwa Daniel Yona, Mheshimiwa Zakia Meghji na wengine kama nimewasahau wanisamehe. Kwa kuwa sina sera ya Majimbo, lakini nyumbani ni nyumbani hata ndege kamwe hawasahau viota vyao. (*Makofsi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtakubali kweli kuona Mkoa wa Kilimanjaro unakufa na raslimali ya asili ya Mlima wetu ipo lakini Serikali haijali thamani yake, *this is very serious* au tunarudi kule kule katika sera zile kuomba walioendelea wapige *marktime* kusubiri wale walioachwa nyuma? Kumbukeni Mlima Kilimanjaro ni pamoja na ajira kwa vijana wetu. Tanzania, utalii ni Kilimanjaro, bila Kilimanjaro hakuna utalii Tanzania. Matangazo yote ya Utalii yanasema Tanzania ni nchi ya Kilimanjaro na Zanzibar. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, *Tourism Master Plan* iliyotolewa na Serikali mwaka 2002 inasema *Moshi Town of Kilimanjaro, Mt. Kilimanjaro is over used* na kuiachia *Management* kuangalia uwezekano wa kuhamishia wageni Mlima Meru. Siyo hiyo tu, hata katika *National Tourism Policy* ya Wizara haionyeshi kama Mlima Kilimanjaro uko katika *Northern Tourist Circuit*. Hali hii inaonyesha wazi, Serikali haina haja ya kuendeleza utalii Moshi. Kwa hiyo, kwa makusudi kabisa, Moshi inakufa *at the expense of Arusha*.

Mheshimiwa Spika, sera hii ni sawa na kumuua ng'ombe anayetoa maziwa na kumlea kichanga chake kwa matumaini ya kupata maziwa mengi.

Mheshimiwa Spika, kama nakumbuka vizuri na naomba radhi kama nimekosea, wakati mmoja Rais wa Afrika Kusini, Mheshimiwa Nelson Mandela, aliwahi kumwambia Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, wakati akiwa ziari na hapa Tanzania kuwa, kama ningekuwa na Mlima Kilimanjaro, ningepata fedha za kutosha kwa nchi yangu na nisingejishughulisha na biashara nyingine. Sisi badala ya kukuza kile kinachotuletea fedha sasa tunaua.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wabunge wote tujue na tujiulize maana ya *mass tourism* na *quality tourism*. Nchi hii ni maskini, tunahitaji pesa kwa maendeleo yetu, tunakwenda kukopa mchana na usiku ili tuletee wananchi wetu maendeleo, lakini tunakataa pesa za watalii kwa kisingizio cha *quality tourism* na kupandisha bei zetu kwa watalii, eti watachafua milima wetu na mbuga zetu. Mifano ya *mass tourism* iko mingi na nchi hizo zimeendelea sana, kama Spain na nchi zote zinazozunguka *Mediteranean Sea*, Kenya hata Afrika Kusini.

Sisi Watanzania ni maskini wakutupa, tunafunga milango ya fedha kuingia hapa kama njugu, eti kwa kisingizio cha *quality tourism*. Hao wataalamu wanotuambia tufanye hivyo nia yao ni kutufanya tubaki hohe hahe, fukara tena wa kutupa. Inaelekea hapa nchini tuna *double standards*, Zanzibar kuna *mass tourism*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hili la *mass tourism* kwamba litachafua mazingira ya Mlima Kilimanjaro ndio maana katika *tourism master plan* ukurasa wa 48 wataalam walishauriwa, kutokana na *feedback* ya soko ku-divert watalii kupanda Mlima Meru. La muhimu hapa ni kufungua njia mpya katika zile zilizopo kuupanda Mlima Kilimanjaro na kushawishi wenyeji kutoa msukumo mbadala katika sekta ya utalii nje ya mipaka ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna miondoko mipy ya vivutio kwa watalii unaoitwa *cultural tourism* au utalii wa kitamaduni, huu ndiyo utakuwa mkombozi katika jamii nyingi za watanzania kwani unahusisha mambo yaliyomo kwenye mila na tamaduni zetu, kitu ambacho ni wale tu waliomo kwenye hiyo jamii ndio watakuwa wahusika wakuu katika utalii wa namna hii na kitakachopatikana asilimia kubwa itabakia kwenye jamii husika.

Mheshimiwa Spika, watu wa nchi za nje wanapenda sana kuelewa vitu vyetu vya kiasili na wangependa kuviboresha zaidi ili viweze kutumika katika mazingira ya sasa ya sayansi na teknolojia. Tatizo watoaji wa taarifa hizo hawazifahamu au wanazipotosha kwa maksudi kabisa, hivyo kwa njia hii jamii mbalimbali Tanzania zinaweza kuandaa *tour package programme* zao kulingana na nini wanadhani watu wa nje wanawenza kuja kuangalia na kujifunza mengi yahusuyo jamii hiyo.

Kambi ya Upinzani inaamini kabisa jamii ya watu wa Same, Marangu, Lushoto, Kibondo, Urambo, Sumbawanga, Kondoa, Kilwa, Bukoba, Masasi, Kahama na kadhalika wana vivutio vyao vya asili ambavyo ni vya jamii hizo na huwezi kuvikuta katika jamii nyingine popote duniani. Kama ikiandaliwa vizuri utalii wa aina hii utalinufaisha Taifa na jamii husika na vile vile vikundi vya maeneo vitakavyohusika katika mtando mzima wa kuwapokea.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mkoani Kilimanjaro kuna mapango ya kale ya Wachaga yaliyokuwa yanatumiwa wakati wa vita, Mwanga na Same kuna *warm spring water* karibu na bwawa la Nyumba ya Mungu ambapo mamba wanapatikana, bila kusahau milima na Miamba ya Mawe na bwawa lenyewe ambalo mandhari yake ni

kivutio kikubwa kwa watalii. Vyote hivi vingeratibiwa na kusimamiwa vizuri wenyeji wangenufaika moja kwa moja na utalii huu wa kitamaduni.

Wakati wa kuachana na sera zisizowaletea wananchi faida ni sasa. Katika *Master Plan*, wataalamu hao walioandika na wanasema wazi kuwa bei zetu ni *over priced*, wanasema wazi kuwa, bei zetu ni *over priced*. Wanasema wazi kuwa *there is no value for money what they pay* na sisi ni *worse than other competing destinations*. Kwa nini bei zetu zisipunguzwe ili tushindane na wenzetu na watalii watakuja kama upupu katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri aagize ada za *rescue fee* wanayotozwa wanaopanda mlima bila hata kupata faida yake zifutwe mara moja. Sioni mantiki ya kumtoza mtu wakati wana *insurance* za kuweza ku-*claim* wanalipa na ndiyo inayofanya bei zetu ziwe kubwa mpaka tunaambiwa hatuwezi kuwa na *competition* na wenzetu.

Mheshimiwa Spika, bei zetu za kupanda Mlima tunatoza *entry fee \$30 per person per day, camping fees \$40 per person per night, but fees \$50 per person per night* na *rescue fees \$20 per person*.

Mheshimiwa Spika, bei zetu za kutembelea mbuga za wanyama ni *Lake Manyara*, Tarangire na *Arusha National Park - \$25 per person per day*, Serengeti *\$30 per person per day*, Ngorongoro *\$30 per person per day* na *crate fee \$15 per vehicle per day*.

Mheshimiwa Spika, bei za wenzetu kwa Uganda, *entry fees* kwenye mbuga zao na hata milima yao ni kati ya *US\$5* mpaka *US\$17* kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Kenya *entry fees* za Kenya zinategemea sehemu unayokwenda lakini ziko kati ya *US\$15* mpaka *US\$27* kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kwa bei hizi, tunategemea kweli kupata wageni wengi. Ni miaka nenda rudi, Waziri ameahidi kuwa Hoteli zitafanyiwa *grading* kufuatana na *number of stars*. Lakini hadi leo hakuna kilichofanyika. Kwa kuwa wenzetu wanafuata Stars za hotel, huwa wengine hawaji kwa kufikiria hapa hakuna hoteli wakati ukweli ni kwamba ziko kibao.

Mheshimiwa Spika, maonyesho ya utalii yako mengi sana duniani lakini, uwezo wa wazalendo kwenda huko ni mgumu sana. Ni wachache sana, *Tour Operators* wazalendo waliowahi kwenda kwenye hizi *Trade Fairs*. Sasa ni wakati muafaka Serikali ingewawezesha *Tour Operators* wachache waende kwenye hizi *Trade Fairs*, badala ya kupeleka watendaji wa Wizara, ambao si wauzaji wa utalii. Sera ya Serikali sio kufanya biashara, kwa hiyo wafanyabiashara ndio wangeweleshwa na sio watumishi wa Serikali.

Kuhusu *Amani Reserve* ina vipepeo na nyoka ambao hawapo popote duniani. Nchi jirani ndio inafaidika na urithi huu wa ajabu. Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kukuza biashara hii.

Vyura wa Kihansi waliopolekwa Marekani wameleta faida gani mpaka sasa kwa Tanzania?

Mwisho, je, wale watuhumiwa wa wahujumu uchumi waliokamatwa katika hifadhi zetu wako wapi, kesi zao zinaendeleaje? Taarifa nilizo nazo, kuna wengine wamekaa rumande zaidi ya miaka mitano bila kesi zao kusikilizwa. Haki za binadamu ni sehemu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nikiwa kama mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji na watendaji wake katika Wizara, nikitarajia kuwa changamoto na ushauri nilioutoa unazingatiwa na kutekelezwa bila kuonekana kuwa ni hoja za kisiasa zilizoja madongo na vijembe. (*Makofi*)

Mimi ni Mbunge wa Moshi Mjini na Mheshimiwa Zakia Meghji ni Mbunge na Waziri kutoka Moshi, pia ni Diwani mwenzangu wa Manispaa ya Moshi. Mheshimiwa Waziri, usione soo, kusema Moshi ni Mji wa Mlima Kilimanjaro na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, mlezi wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro naye pia asione soo, kusema Moshi ni Mji wa Mlima Kilimanjaro. Narejea tena kauli mbiu katika hotuba hii kuwa Moshi ni Mji wa Mlima Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kama mchangaji wa kwanza asubuhi hii.

Kwanza kabisa na mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Zakia Meghji na wataalamu wake kwa kuandaa bajeti hii vizuri pamoja na kuwa Mheshimiwa Waziri katika jitihada yake amefanya kazi nzuri katika mazingira magumu kwa sababu, sote tunajua kuwa bado yuko katika majonzi ya kupotelewa na mume wake, Marehemu Profesa Ramadhani Meghji, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema, peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa kupewa tuzo hivi juzi, tuzo ya *Distinguished Tourism Personality of The Year Award*. Vile vile natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri George Kahama na kwa Bwana Gabriel Mawalla kwa kupewa tuzo ya *Tourism Pioneer Award*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba niungane na wenzangu kwa niaba ya familia yangu na kwa niaba ya wanawake wenzangu natoa pole sana kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego pamoja na Marehemu Mheshimiwa *Comrade Capt. Theodos Kasapira*, aliyetutoka hivi karibuni. Nziombea roho zote mbili za Marehemu Mwenyezi Mungu azipokee aziweke pahali pema. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba sasa nianze kuchangia mimi katika sehemu ya hifadhi ya Mbuga za Wanyama na hasa katika sehemu ya mipaka.

Kama tunavyojuu kumekuwa na kilio kikubwa katika sehemu mbalimbali wanazoishi wananchi. Vile vile kulikuwa na hoja zilizojitokeza hapa Bungeni kuhusu malalamiko ya wanyama kuvuka mipaka na kuingia katika maeneo ya makazi ya wananchi. Mheshimiwa Waziri nadhani amelifanyia kazi au atalifanyia kazi lakini nilikuwa nikijaribu kutoa msukumo aliangalie vizuri kwa makini ili tusiendelee kuhatarisha maisha ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, ningetaka kuzungumzia mpakani mwa Kenya na Tanzania sehemu ya *Gate* la Masaimara. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri angalau atujulishe shughuli hii imefikia wapi kutokana na ndugu zetu wa Kenya walijaribu kuomba ili tufungue *Gate* hili. Kutokana kuwa mimi nilikuwa miiongoni mwa wenzangu katika sekta ya Kamati ya Biashara iliyopita tulifika sehemu ile, tulichokiona pale ni kuwa katika eneo letu la Mbuga zetu za Serengeti sisi tukiwa na *airstrip* moja tu na hoteli mbili tu za maana.

Kwa upande mwingine tuliona wenzetu wana mahoteli mengi, wana *airdromes* nyngi kuliko sisi. Sasa mimi nilikuwa natahadharisha tu iwapo tutakubali kuwa tunafunga *Gate*, wasi wasi ni kuwa tuwe tayari katika ushindano wa biashara. Kwani tunawaelewa wenzetu ni hodari na wana watalii wengi. Kwa hiyo, tuwe makini katika eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka pia kuzungumzia kuhusu *conservation area* ya Vikindu na Kisarawe. Maeneo haya si makubwa, lakini ni maeneo ambayo yanahifadhi wanyama. Ni maeneo yaliyo katika Mkoa wa Dar es Salaam mpakani na Mkoa wa Pwani. Katika eneo la Vikindu ni eneo peke yake ulimwenguni ambalo linahifadhi vinyonga wenye pembe tatu. Ni eneo pekee ulimwengu.

Mimi wiki mbili zilizopita nimepita na ni mtu ambaye napita sana lakini kitu kinachostaajabisha sana sasa hivi ni kuwa wananchi pamoja na kuwa kuna wanyama, wananchi bado wanadiriki kutafuta, wanapita katikati kwenda labda kutafuta kuni labda kufanya shughuli zao nyngine. Sasa mimi hofu yangu ni kuwa tusipokuwa macho au tusipoangalia tutawapoteza vinyonga hao ambao tunaambiwa wako katika sehemu hii pekee. Kwa hiyo, nilikuwa nikimwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hili kwa ukaribu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kuhusu mimea asilia. Kama tunavyojuu Wizara hii ni Wizara ambayo wengi wanaitegemea. Binadamu wanaitegemea, wanyama wanaitegemea lakini vile vile na mimea inaitegemea. Sasa naomba nizungumzie mimea ambayo ninaiona ina umuhimu kwa ajili ya faida ya kutuletea fedha kwa biashara. Kule Usambara kwa Mheshimiwa William Shellukindo, kuna maua mazuri sana ambayo yanaitwa *The African Violet*. *The African Violet* yali-originate *Usambara Mountains*. Kwa kweli yangepaswa maua yale yaitwe *Usambara Violet*. Kitu kinachoshangaza sana ni kuwa hakujakuwa na msukumo wa kutosha katika kuhakikisha kuwa tunatumia nafasi hiyo. Ndugu zangu, wakwe zangu Wasambaa wameliangalia eneo lile wakaona haya ni

maua ya kipuuzi tu ambapo wangepaswa hivi sasa ku-*propagate* wayazalishe ili waweze kujipatia fedha ya kuwasaidia kujikimu katika maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sio eneo moja tu, mirudi Kitulo kule Mbeya. Eneo la Mbeya lina eneo ambalo lina *orchids* nzuri mno ambazo zinafahamika ulimwenguni. Kwa bahati mbaya si watalii wengi wanaokwenda pale na ziko juu ya *plateau*. Wananchi wanapita na mimea hii ya *orchid* inajilea yenyewe. *Orchid* moja nani asiyejua hata Dar es Salaam kununua *orchid* moja ni shilingi 3,000. Leo tunalia na umaskini lakini kumbe tumeilalia fedha.

Ndugu zangu wa Dodoma, watani zangu. Waheshimiwa Wabunge wote wanapopita kwenda barabara ya Dar es Salaam wanaona mibyu mingi imejaa. Juu ya mibyu hiyo kuna mimea midogo midogo inayoitwa *The African Leopard Orchids*. Miaka mitatu iliyopita, lile moja tu ua ni shilingi 1,000 miaka mitatu iliyopita. Hawa Wagogo ndugu zangu nilipoongea nao waliniambia wao wanaitumia dawa hii ya shingoni mtu akipata mafindofindo.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nawaomba watani wangu Wagogo waachane na dawa hiyo kwa muda, wazalishe, wauze, wapate fedha za nje ili iweze kuwasukuma katika maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisiende mbali naomba niende katika Jimbo la Mheshimiwa Anatory Choya, Jimbo la Mheshimiwa Gwassa Sebabili na Jimbo la Mheshimiwa George Kahama, Karagwe.

Mheshimiwa Spika, *Burigi Game Reservation area* ni sehemu pekee ambayo ina ua linaloitwa *protea* na yanaota kwa wingi sana na wala hayahitaji maji. *South Africa* ni nchi kubwa duniani ya kwanza kuzalisha *protea* na kuziuza na mpaka sasa hivi *protea* moja ni dola 13. Lakini ndugu zangu, wakwe zangu bado wamelalia nchi hii na mimea, akiwemo Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, hawajafikiria kufanya jambo lolote na bado tumekalia utajiri lakini tunalia na umaskini.

Mheshimiwa Spika, nisingetaka kuchukua muda mrefu, lakini nina mapendekezo. Pendeleko la kwanza napendekeza kwamba Vikindu na Kisarawe wangepatiwa wanyama wa kutosha ili watalii wanaopita Mkoa wa Dar es Salaam badala ya kwenda *all that way* mpaka Mikumi, basi waweze kupata nafasi ya karibu kwenda kutembelea wanyama walio karibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pendeleko langu la pili kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba azidi kuendelea kuhamasisha Wananchi kwa wingi sana ili na wao waweze kujifunza utamaduni wa kutembelea maeneo haya. Lakini tunamwomba Mheshimiwa Waziri pia kwamba, atakapofanya hivyo basi ajitahidi angalau kuwawezesha waende kwa bei iliyo nafuu isiwe ni bei ambayo imewekwa kwa watalii wa kutoka nje. Pia, kwa kuwa wanawake ni hodari sana wa kuhamasisha, basi aanze na wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam tutaweza kumsaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pendelezo lingine ni kuwa tuna maporomoko mazuri sana katika nchi yetu. Ukienda *Usambara mountains*, ukienda Upareni, ukienda Ngara na maeneo mengi tu, lakini maporomoko haya kweli hayajafanyiwa kazi ya kutosha ili kuita au kuleta watalii waweze kuja kuyaona, kustarehe na ku-enjoy mandhali nzuri ya maporomoko hayo. Kwa kweli utalii katika *Lake Victoria* haujawekewa mkazo wa kutosha. Tuna kisiwa chetu, kweli ni kidogo, watalii wanakwenda katika kisiwa hicho cha Saa Nane, lakini bado kuna maeneo mengi ya *Lake Victoria* ambayo tungeweza kuyatumia. Pamoja na kuwa na mandhali ya mawe mazuri na makubwa, tungeweza kuhakikisha kuwa watalii tunawavuta hata kutoka Uganda, hata kutoka Rwanda, Burundi, tuwadake hao na pia watalii wanaopitia huku kwetu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri aliangalie sana suala la *the Southern* ... kwani kule tuna Ruaha, tuna *Selous* na tuna Rukwa. Hayo kwa kweli ni maeneo mazuri hata kwa kuwinda na kuangalia, lakini ninasikitika kuwa mpaka hivi sasa bado hatujaweka hasa umakini wa kuwapeleka watalii wengi na kwa sababu huko ni *Southern Area*, siku hizi watu wa kutoka *South Africa* wanakuja wengi katika shughuli za utalii na kuona nchi yetu, basi tungejitahidi katika eneo hilo tukwapeleka sehemu ile ili kusudi tuhakikishe nchi yetu pande zote tunapata ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika*)

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii moja kwa moja. (*Makofi*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nami niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa vifo vya wenzetu ambaao ni Marehemu Mheshimiwa Yetete Mwalyego pamoja na Marehemu Mheshimiwa Captain Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga kwa jinsi ambavyo alitetea kiti chake katika Jimbo la Bariadi Mashariki na baadaye kurudi tena hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe Mheshimiwa Waziri sifa ambazo nashindwa hata jinsi ya kuzihesabu kwa jinsi ambavyo anachapa kazi. Maneno haya tunapoyasema wengi tunayasema kutoka moyoni na mwenye kuona wivu aone wivu, labda yeeye hafanyi kazi vizuri. Lakini Mheshimiwa Waziri ni mwanamama ambaye ni mchapakazi, ambaye ana uzalendo na anajua kazi yake kikamilifu. Nampa hongera nydingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yake ya Maliasili na Utalii ni moja ya Wizara ambazo zina mianya mingi ya kuwa na rushwa. Watendaji wengi katika Wizara hiyo kwenye Idara mbalimbali wameshiriki katika rushwa na wengine wanaishi maisha ya peponi ingawa najua wataviacha hapa hapa duniani. Matokeo yake, watoto wao na vizazi vyao kesho na kesho kutwa watanyooshewa vidole na watapaswa kuwajibishwa na Watanzania kwa mali hizo walizowapora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kwa kiwango kikubwa na ninyi ni mashahidi kwa kujaribu kuwadhibiti, ni wengi sana. Ndiyo maana tunapompatia sifa, tunampatia sifa za dhati. Ingawa pia napaswa kutoa sifa hizo kwa baadhi ya watumishi katika Wizara hiyo, hawawezi wakawa wameoza wote, wapo wazuri ambao kwa kweli nafasi yangu ni ndogo kuweza kuwataja, lakini baadaye nitawataja kwa barua yangu rasmi na wenyewe nitawapongeza kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri kufanya kazi yake vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati huu kuna maboresho ya sheria ya wanyamaporii ambapo Watanzania mbalimbali na wadau mbalimbali wanaichangia. Ninashauri katika sheria hiyo, elimu kwa Watanzania na hasa Wananchi izingatiwe zaidi ili kusudi Watanzania waweze kufahamu sheria hiyo, lakini pia waweze kufahamu ni jinsi gani ya kutunza wanyamaporii wetu.

Mheshimiwa Spika, kubwa katika sheria hiyo ni kwamba, naomba sheria inayohusiana na masuala ya ujangili iwekwe, lakini pia iwe kali kwa wale majangili ambao ni wa nje ya Tanzania. Kwa mfano, pamoja na wema wetu tuliofanya wa kuwakaribisha wakimbizi na hasa wa kutoka huko Burundi, wema wetu umegeuka kuwa ni ajali na hasara kwetu maana wao wanapoingia kwenye mbuga hizo za wanyama wanazoa kila kitu. Kwa hiyo, hiyo ni shukrani ya punda, sisi tunachoambulia ni mateke. Wanaua watu wetu, wanapora watu wetu, wanapora na mali zetu za asili na kuzipeleka kwao na sisi tumetazama tu.

Ningeomba sheria iwe kali ya kutokuwahurumia, tena ikiwezekana hata kama haikutamkwa, wanapokutwa kwenye ujangili mle porini na wao wawe ni chakula cha wanyama. Nadhani nimeeleweka nina maana gani.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna Maafisa mbalimbali wanaohusiana na Idara mbalimbali za maliasili ambao ndiyo chanzo kikubwa cha magendo. Wanashirikiana na watu mbalimbali iwe ni majangili au watu wanaoharibu maliasili zetu, wao wanashiriki kwenye magendo hayo na ndiyo wanakuwa ni msaada mkubwa wa kuwalinda hawa wahalifu na wao sheria yao itungwe iwe kali sana, siyo ile ya kukaa kubembelezana kama ambavyo tumezoea kwenye ofisi zetu maana ndiyo wanaotumaliza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbuga za wanyama, kila mtu anajua kwamba Tanzania ni moja ya nchi ambazo zina vivutio vingi. Tuseme ni nchi ambayo ina mbuga nyingi kuliko nchi nyingi duniani na mbuga hizo ni za kuvutia maana zina wanyama mbalimbali, lakini bahati mbaya sana hatujatajirika na mbuga hizo. Watu wenyewe mbuga chache kama vile Kenya na nyinginezo wametajirika na mbuga zao katika kuimarisha utalii. Lakini pia hatujali mbuga zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa suala hili ninaiomba Serikali yote kwa ujumla waone umuhimu wa kuisaidia Wizara hii kwenye mbuga zetu kuchimba malambo ya kutunza maji kwani mvua si nyingi na tunajua hilo. Kwa hiyo, mito mingi inakauka, hata ile

inayopita kwenye mbuga za wanyama. Matokeo yake wanyama wengi wanahama kuelekea maeneo ya makazi ya watu na huko wanauawa kwa wingi. Kwa hiyo, upo umuhimu wa makusudi wa kuhakikisha kwamba malambo kadhaa yanachimbwa katika mbuga za wanyama ili kutunza maji, pamoja na kukinga baadhi ya mito ili kutunza maji kwa mwaka mzima ili wanyama wasiathirike. Suala hili ninaliomba kwa Serikali yote kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mbuga zetu mbili ambazo ni Urithi wa Ulimwengu. Kuna Serengeti na kuna hifadhi ya Ngorongoro.

MBUNGE FULANI: Mikumi je?

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mikumi haipo duniani. Ngorongoro pamoja na Serengeti ndiyo hifadhi au mbuga ambazo ni Urithi wa Kimataifa wa Ulimwengu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niongelee angalau hii Ngorongoro ambayo ndani yake kuna wafugaji. Yaani ndiyo mbuga pekee duniani ambayo wanyama wanaishi humo, watu wanaishi humo na mifugo wanaishi humo humo. Ni vitu vya ajabu! Lakini huo ndiyo urithi wenyewe na hiyo ndiyo sababu mojawapo ya kuwavuta labda watalii au watu mbalimbali duniani waje washangae mambo hayo. Inawezekanaje wanyama, mifugo na watu wote waishi kwa pamoja?

Kwa hiyo, inaonekana kama vile tunavyosoma kwenye vitabu mbalimbali vya Mungu kwamba kuna Eden na kweli ukienda Ngorongoro ni Eden kweli. Ukiona *Ngorongoro crater*, ukiona maeneo mengine kama kule Endulen, Embaruui ni maeneo ya kuvutia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kukisema hapa ni kwamba, hapa katika sheria ya Ngorongoro hakuna mahali panaporuhusu kilimo, maana ukisharuhusu kilimo kinaharibu ardhi, kinaharibu mazingira na hasa kikianza kuwa kilimo kikubwa. Lakini kwa nia nzuri tu Serikali kupitia aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo, Mheshimiwa Malecela, aliweza kuruhusu kwamba wafugaji wenyeji kwa yule anayetaka lakini, anaweza akalima angalau kabustani ili kamsaidie.

Mheshimiwa Spika, kuruhusu huko siyo kubaya na baadhi ya wenyeji wanafanya hivyo ingawa wenyeji wa asili kwa maana ya Wamasai wengi hawajishughulishi sana na suala hilo. Kuruhusu huko kumesababisha baadhi ya Wananchi kutoka nje ya mbuga hiyo ya Ngorongoro ambao siyo wenyeji kuvamia na kuingia katika mbuga na kuanza kulima, tena kulima hata kilimo kikubwa na kuanza kujenga nyumba za kudumu. Matokeo yake sasa wameanza kuziba hata zile *corridor* za kupitisha wanyama wanapo-*immigrate* kwenda au pengine kutoka Kenya na kwa hiyo wanyama wengi wamekwishaanza kupungua kwa sababu ya njia zao hizo kufungwa, kama vile simba na wengineo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kwa kupitia vyombo vyake iwe makini na hata watendaji watakapokuwa wameamua sasa kuwafukuza kikamilifu wale ambao si

wenyeji Serikali ifumbe macho, maana wanajulikana. Kuwepo kwao ndiyo hatari ya urithi wa mbuga hii ya hifadhi ya Ngorongoro. Kama Serikali itafumba macho kwa kupiga siasa siasa tu hizi za kubembeleza kwamba wacha wakae, maana yake tunaua urithi ule wa ulimwengu ambapo walimwengu wana haki ya kutunyang'anya kwamba: "Kama ninyi mmeshindwa kuilea na kuitunza hii kwa siasa zenu, tunainyang'anya kwa sababu tayari ni urithi wa ulimwengu na tunaiendesha." Hapo ndipo itakuwa mbaya zaidi, tunaweza tukajikuta tunaipoteza na hata wenyeji kabisa wanaoishi mle wakafukuzwa. Kwa hiyo, naomba sana hili lizingatiwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika dakika hizi za mwisho mwisho, niongelee utalii ambapo hata kama tungesahau kilimo tukaamua kuweka mbinu, mikakati na michakato kadhaa kuhusiana na suala la utalii Tanzania, tunaweza tukawa kama siyo wa pili, wa tatu, hata ikiwezekana wa kwanza duniani kupata pato kubwa linalotokana na masuala ya utalii kwa sababu tuna vitu vingi, vingi, vingi kupita kiasi ambavyo ni vivutio vikubwa kwa utalii. Kwa hiyo, Serikali yote kwa ujumla, siyo kuiachia Wizara peke yake kwani tunapomsifu Mama Zakia Meghji namna hii, ndiyo wengine wanaona hata vivu kwamba hawawezi wakatoa hata mawazo mazuri wakidhani eti wanamsaidia Mama Zakia Meghji kumbe wanamsaidia Watanzania wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tufanye mikakati na mipango madhubuti ya kusaidia utalii ili itusaidie katika mbuga zetu na mambo mengine yote yanayohusika. Tuwaimarishe hawa *Tour Operators* ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kusaidia utalii wetu nao pia tuwasaidie ili waweze kutusaidia. Vile vile, kuweka matangazo mbalimbali katika ndege, kutengeneza *CD*, tovuti mbalimbali na hata kutengeneza nyimbo/miziki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu zitumiwe kikamilifu huko nje ya nchi, pamoja na Watanzania mbalimbali walioko nje ya nchi hata wale ambao wanasona na pia tutumie *agents* mbalimbali walioko huko nje kutangaza utalii wetu. Ni jambo la kusikitisha kwamba katika Balozi zetu huko nje wengi katika Ubalozi hawajui masuala ya utalii kabisa! Nadhani wakati umefika kila Balozi popote nje, pawepo na mtu ambaye anashughulikia masuala ya utalii kikamilifu katika kutangaza. Tuliwahi kutembelea Ubalozi wetu Kenya, Kenya hapa hapa karibu na wao wakawa wanalamika masuala ya utalii hawayajui na wala hakuna hata angalau *brochures* mbalimbali zinazotangaza utalii wetu. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni la kushangaza!

Mheshimiwa Spika, mwisho ninamwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie pale Wilayani Nkasi, hatuna gari la maliasili. Hatuna kabisa, iwe ni wanyamapori, iwe misitu, iwe uvuvi, hakuna gari hata moja, wanajaribu kudoweadowea tu gari ya Halmashauri na wanapata shida.

Kwa hiyo, ninatoa ombi maalum hata kama kuna kagari kachakavu chakavu pale Wizarani basi mtusaidie kagari hako ili waweze kufanya kazi kubwa tukijua kwamba tuna maeneo pale kama Rwamfi ambayo ni *Game Reserve* na msitu pia ambao ni mkubwa sana, lakini unavamiwa na majangili pamoja na watu mbalimbali wanaopora nyara mle na wanashindwa kufanya kazi yao kwa sababu hawana gari wala pikipiki. Kwa hiyo, naomba ombi maalum, kwa kweli, naomba sana mtusaidie hilo gari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono kwa dhati kabisa hoja ya Wizara hii. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa maoni yangu na kuchangia hoja katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nami pia naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Mzee wetu; Captain Theodos James Kasapira, Mbunge wa Ulanga Mashariki na kuwafariji wafiwa wote kwa maana ya ndugu na Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki pamoja na Mkoa mzima wa Morogoro kwa msiba uliowapata kwa sababu nasi pia umetugusa kama kiongozi mwenzetu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nimpongeze sana, sana, sana Mheshimiwa Waziri kama alivyomwagiwa sifa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami ambaye amemaliza kuchangia sasa hivi. Sifa zote, ujasiri na utendaji wa kazi amezionyesha katika Serikali hii na ninaamini Wananchi wote wanaridhika na utendaji wake wa kazi katika nchi yetu hii ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninaamini kwamba, utekelezaji wake mzuri pia ni kutokana na yeye kuweza ama kutoa ushirikiano au kupata ushirikiano kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara yake, Wakurugenzi wote wa Idara zake pamoja na Mameneja wa Vitengo vyote vilivyo chini ya Idara za Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Ninaomba niwapongeze sana wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza kuchangia mimi nitaingia kidogo katika ukurasa wa 22; paragraph ya 45, upande wa Sekta ndogo ya Uvuvi. Kwanza naomba tu niseme kwamba uvuvi siyo Sekta ndogo. Naomba hili neno ‘Sekta ndogo’ liondolewe kwa sababu uvuvi ni Sekta mojawapo kubwa kabisa inayochangia mapato katika nchi hii kutokana na hali yake ya uvunaji wa mazao ya bahari ama ya maji chumvi au maji baridi au mitoni. Ninaamini inachangia kabisa kwa sababu hata ukiangalia kwenye jarida la kitabu hiki uvuvi unachangia zaidi ya bilioni 8 na wanyamapori nao bilioni 8. Sasa sijui ni Sekta gani ambayo utaisema kwamba hii ni Sekta ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, katika ukurasa wa 22; kwenye hii *paragraph ya 45*, Waziri amesema kwamba: “Katika mwaka huu wa fedha, katika kipindi hiki Wizara itaendesha doria ya siku 12,000 za kazi ili kudhibiti uvuvi haramu.” Ninaomba sana hizi doria kama ni chache basi wajitahidi sana kuziweka katika mpango mzuri ili doria hii isiwe sehemu moja, iwe katika ukanda mzima wa nchi yetu, japokuwa tuwe na *points*. Kama upande wa Kaskazini maeneo ya Pemba na Tanga, katikati iwe Dar es Salaam na Mafia na Kusini iwe katika maeneo ya Mtwara kwa sababu humu ndimo kunapovuliwa samaki wengi sana, meli kubwa kabisa zinakuja kuvua. Sijui kwanza hii doria wataifanyaje, maana doria ya kwenda bahari kuu inabidi upate vyombo vikubwa kabisa nya kuweza kukusaidia. Lakini naomba tu kwamba Wizara ijitahidi

katika kuboresha doria hii ili iweze kutoa maboti makubwa yenyewe kuweza kwenda kwa kasi na kuhimili vishindo vikubwa vyatia mawimbi ya bahari kuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kwamba Serikali safari hii imeweza kuruhusu uuzaaji wa samaki wa maji-chumvi kupeleka nje. Kwanza ninaishukuru kwa sababu tulikuwepo wote katika kuchangia mawazo haya na sasa Serikali imeona kwamba sasa umefika wakati na samaki wa maji-chumvi waweze kuchangia kama wanavyochangia samaki wa maji-baridi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kikubwa katika kuijandaa na mpango huu ni kwamba, ninaiomba sana Wizara ijaribu kukaa na kuongea na hao wenye viwanda. Kwanza viwanda visiwe vingi, vitafutwe viwanda viwe kama miradi ile ya kuangalia. Kinachaguliwa kiwanda kimoja au viwili vyatia kuweza kukaa na kuangalia kwamba wakati watakapokuwa wanunua samaki mapungufu yatakuwaje au hali ya kitoweo itakuwaje, baadaye ndipo zile leseni ziweze kutolewa kwa kiwango ama cha miezi sita au mwaka na baadaye hali ikiwa nzuri basi waweze kuendelea kama Serikali mtakavyoweza kupanga utaratibu wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, halafu wenye viwanda wasiruhusiwe wao kwenda kuvua kwa sababu hii ndiyo italeta balaa kama ilivyotokea kwenye magogo. Watu ambao wana viwanda wakitaka kuuza samaki nje, basi waandae zana na kuwapa Wananchi katika maeneo husika. Wanavijiji wapewe nyenzo na zana ili waweze kuvua halafu waende wakawauzie wale wenye viwanda ili wao ndiyo wanunue, lakini wao wasiruhusiwe kwenda kuvua, Wananchi ndiyo wavue ili waweze kufaidika.

Mfano katika *Lake Victoria* wavuvi wadogo wadogo walianzia tu kwa mitaji ya Sh.50,000/= na kwa kutumia mitumbwi midogo, lakini viwanda viliweza kuwapa nyenzo.

Sasa hivi Wananchi wale wameshakuwa matajiri na wanaweza kumudu kabisa maisha na hata ukiangalia hali ya mvuvi wa ukanda ule huwezi kumfananisha na mwananchi wa kawaida ambaye labda anashughulika na biashara nyingine.

Kwa hiyo, naomba Wizara mliangalie suala hili, muwe waangalifu katika utoaji wa leseni na kuweka masharti au kanuni ndogo ndogo kwa ajili ya Wananchi wetu wa vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la ruzuku. Kwa mfano, Idara ya Kilimo huwa inatoa pesa nyingi sana katika pembejeo za zana za kilimo. Nami naomba tu Wizara hii nayo ijaribu kutenga fungu maalum kwa sababu ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo ili na wenyewe kuweza kumudu kuweza kununua zana za uvuvi na waweze kufika katika bahari kubwa na kuweza kupata samaki na waweze kujiedhesha kimaisha.

Kwa mfano, Wizara ya Kilimo kuna yale matrekta *power tillers*, zile *power tillers* bei ya wauzaji ni Sh.5,000,000/=, lakini Serikali iliweza kuweka ruzuku asilimia 50.

Sasa *power tiller* ukiitaka unaipata kwa Sh.2,500,000/= kwa sababu Serikali inatoa hiyo ruzuku ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ikiwezekana ijitahidi kuhakikisha kwamba na zile zana za uvuvi kwa wale watu ambao wanataka kufanya biashara au kazi ya uvuvi wanapojiandikisha katika vikundi vilivyokubaliwa na kusajiliwa, basi Serikali nayo iwasaki.

Kama mashine *outboat engine* inauzwa Sh.3,000,000/=, basi Serikali nayo ichangie Sh.1,500,000/= ili Wananchi au vikundi vile viweze kumudu kununua na kuweza kufanya biashara hii vizuri bila ya kuleta athari nyingine na ninaamini hata masuala haya ya mabomu, makokoro na kadhalika yataopotea, yataondoka kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi ni hayo tu. Lakini suala lingine ni kwa upande wa magofu. Nataka nizungumzie kidogo tu kwamba, ni kweli kuna magofu ya aina nyingi na Serikali imeyaona magofu yaliyopo Mafia.

Mheshimiwa Spika, huwezi kufananisha magofu ya Mafia na magofu ya Kaole! Sijui kwa nini Serikali iliyaona yale ikashindwa kuyaona haya ya Mafia.

Lakini kwa kuwa tayari sasa kazi imeshaanza, naomba sana hata huo mpango wa kuweka maeneo yale ya Kimataifa kama Kilwa na Bagamoyo, basi kama utakwenda katika Kisiwa cha juani pale pana magofu hata hayo ya Kilwa sijui kama yatayafikia, labda yatashindwa kwa ule Msikiti mkubwa tu na ile ngome iliyopo pale. Lakini pana magofu mazuri kabisa na sasa nayapotea, yanaanguka.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali itafute mfadhili haraka sana kwenda kuyahui magofu yale. Juzi juzi tu katika Vyombo vya Habari tumesikia kwamba kuna hili sakata la magogo. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyokwenda pale bandarini na kuweza kuzuia ili kuionyesha jamii kwamba hata yeye yalikuwa yanamuuma.

Sasa kikubwa tu ni kwamba, wote hata sisi Wanakamati, nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira na mimi haya yalikuwa yananikera sana kwani ulikuwa ukipita barabarani unaona mamia ya magari yamebeba magogo yale na yanakwenda, lakini sasa magogo haya yamezuiliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama alivyo sema Mbunge wa Nkasi; Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kwamba labda kuna rushwa au nini. Mimi nasema hakuna rushwa, lakini kuna neno ambalo aliliongea kwamba, kuna kitu kinaitwa wivu.

Sasa huu wivu naomba sana Wakurugenzi wakubwa mkae muwaangalie hawa watendaji wenu wa chini labda wana mpango wa kutaka kukuharibieni ninyi kazi.

Kuna watu hawa ambao wanatoka katika Idara zenu ndogo ndogo ndiyo wanaofanya mambo haya, kama *licence* wao ndiyo walikuwa wanapitisha, kama kufanya *grading* wao ndiyo walikuwa *wana-grade*. Sasa leo magogo yamekwenda pale bandarini yamezuiwa na Waziri kazuia kama Kiongozi, kama Mtanzania ambaye roho inamuumma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, lakini magogo yale yalishakatwa, tuyafanye nini sasa au mtayafanya nini magogo yale? Je, yapigwe moto? Kwa sababu kila yanapokaa pale yanakauka, matokeo yake yatapinda, yatakosa thamani na hakuna lolote lile ambalo tutakaloweza kupata. (*Makofi*)

Yale magogo wenyewe ni Watanzania, lakini yanasarifishwa kwenda nje. Kwa hiyo, biashara hii uelewe kwamba kuna baadhi yanafanya na Watanzania. Lakini kuna baadhi ya wageni ambao wanawatumia Watanzania kwa ujanja kwenda kufanya biashara hii kihuni na matokeo yake ili kuweza kuwabana ndiyo wakaanza kuchochearna na hata yakakufikia wewe kwenda kukamata ili hawa Watanzania waweze kushindwa. Magogo yale wapoteze zile fedha wakati wao wamekopa kwenye mabenki, wanadaiwa maporini, wanafanya kila kitu. Sasa wakishafilisiwa wale wageni wapate *chance* ya kuweza kuifanya biashara hiyo. Kwa hiyo, naomba sana kwanza biashara hii ya magogo kwanza nakushukuru kwa kuizua (*ku-block*) lakini naomba sana haya yaliyokuwepo waonee huruma hawa Watanzania wayaondoe, yaondoke yasafirishwe wapate kulipa madeni ya watu, benki pamoja na hata vijijini kule kwa wale wakataji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninachosema wageni wakiyatka magogo katika nchi yetu basi wayachukulie bandarini kwa maana *FOB* au wawe wanatumia *Letter of Credit (LC)* watumie *LC* katika kupata kama zamani. Mimi nimepata fahamu magogo yanakatwa. Lakini hii fujo imekuja juzi tu baada ya watu wageni kuivamia mpaka vijijini wanakwenda kufanya hii biashara. Biashara hii ni ya mtu mdo go wa kijijini, leo anatoka mtu sijui kutoka Korea, kutoka China na kadhalika anakuja mpaka kijijini kukata magogo. Kwanza hivi vibali Wizara ya Mambo ya Ndani inatoa vipi vibali vyta Mchima anakuja na *mobile sawmill* na *mashine kruuu* linaunguruma pale anakata gogo tayari keshakuwa mwekezaji, sijui hivi kwa nini? Hivi kweli *machine* zile hatuwezi kuwa nazo sisi Watanzania? (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana kwamba magogo haya yaliyokatwa yaruhusiwe, miti imeshakatwa haiwezi tena kurudi waende wakailipie kwa sababu pana hasara pale. Pana karibu dola 160 zinalipwa bandarini nani atabeba mzigo ule? Kwa maana hiyo yule maskini mfanyakibashara ndiyo anaangamia au wewe kwa ushauri uliopata kutoka kwa watalaam wako tena hawa wa kati siyo wale Wakurugenzi basi wameweza kukushauri maskini ya Mungu ukaenda kuyazuia Serikali inapata hasara dola 160 kwa kila kontena. Hivi huu mzigo ataubeba nani? Kwa hiyo, yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Waacie hawa wauze hii biashara waweze kulipa madeni, lakini wakati huo ikiwa vibali vyote umezuia mpaka haya magogo yaondoke upange utaratibu mpya wa kuweza kuhakikisha kwamba hakuna uvunaji ovyo wa magogo. (*Makofi*)

Lakini tuelewe kwamba asilimia karibu 70 ya uchafuzi na uharibifu wa misitu jamani wanababisha wachoma mkaa. Ukipanda kwenye ndege Mheshimiwa Waziri,

kutoka Dar es Salaam kwenda Mafia, au Mafia/Dar es Salaam eneo la Wilaya ya Mkuranga limeteketea, ni jangwa. Sasa pia tuangalie upande wa Idara ya Misitu naomba sana hawa mabwana *forest* sijui wanajiita wakae sana waangalie katika huu uchomaji ovyo wa mkaa. Jamani tunaangamia. Kwa hiyo, Wizara ya Madini na Nishati ikae iangalie tunataka kushauri kwamba mimi na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. ESHA H. STIMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwanza mimi natoa pole kwa watoto, mke na familia ya marehemu Mheshimiwa Capt. Kasapira kwa kifo cha ghafla kilichotokea hapa Dodoma na naomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu kaka yetu Mheshimiwa Kasapira mahali pema peponi. Amen.

La pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dada yangu Zakia Meghji, kwa kazi nzuri anayoifanya akawa Waziri pekee asiyekuwa na Naibu Waziri, lakini anafanya kazi nzuri yenyé kuleta matunda kwa taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nichangie katika vipengele vifuatayo katika hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri. Kwanza, nichangie hali ya uvuvi, hali ya maliasili, misitu, nyuki na wanyamapori kwa sababu hizo ndiyo nyenzo zetu nzito ambazo zinatuletea uchumi ndani ya nchi yetu na tunapata fedha za kigeni kutokana na rasilimali hizo. Tulitembelea maeneo ya mwambao kama Tanga, Mafia, Mtwara na tukaona jinsi Wizara hii ilivyoweza kuweka mandhari nzuri ya mazalio ya samaki wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sasa hivi samaki wanapatikana wa kutosha na ni wavuvi wachache ambao wanapiga vita utaratibu huu kwa sababu walizoea kuvua kwa kutumia mabomu, kwa kutumia sumu na sasa hivi hayo yote yamedhibitiwa na Wizara hii na wao wanaona ni hasara lakini kwa taifa letu tumepata faida sana. Nampongeza Waziri na watendaji wote akiwemo Katibu Mkuu, watumishi ngazi ya Mkoa, Wilaya na maeneo yote ambayo yanashughulikia shughuli hizo hapa nchini. Kwa kweli wanajitahidi ingawa wapo wachache katika maeneo mengi ya shughuli zao muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikizungumza suala la nyuki, asali tunayopata na nta inayopatikana, Mheshimiwa Waziri, nilikuwa namWomba aone uwezekano wa kutafuta masoko ya uhakika kwa sababu ukisafiri kwa treni utaona akina mama na vijana na wazee wanavyohangaika kuuza asali hizo kwenye galoni, kwenye chupa wakati mwingine wanadhulumiwa watu wanachukua asali na treni inaondoka hawapati mapato yote kwa sababu ya kutokuwa na soko maalum. Kwa hiyo, hilo nilikuwa naomba aone jinsi gani atakavyoweza kulitatua tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jingine nisingependa kurudia sana yaliyosemwa, lakini kuna vipengele ambavyo na mimi naona nivielezee vinahuusu uvunaji wa miti. Kwanza nimpongeze Waziri kwa kusimamisha uuzaji wa magogo nje na kusimamisha makontena yaliyopo bandarini Dar es Salaam. Ujasiri huo umemwezesha yeye na taifa hili kujua mahasidi wa uvunaji wa miti yetu Tanzania wakiwemo watu wa nje ambao hawana uchungu na mali zetu. Lakini katika hilo Mheshimiwa Waziri, ninamwomba pamoja na

Serikali yetu ingawa Kamati yetu ya Mazingira, Maliasili na Utalii ilitoa agizo hilo na ye ye akatekeleza mara moja bila kuchelewa. Lakini hali imeathiri kwa kiasi ambacho sasa hivi tunaona wafanyabiashara wadogo wadogo wa magogo wameathirika wengine wanaumwa wale wenye *BP* haziteremki, watoto wamesimama kwenda shule, sasa kwa misingi hiyo ubinadamu na sheria vinasaidiana katika maamuzi mazuri kwa wananchi wa Tanzania. (*Makofî*)

Mimi nilikuwa naomba waruhusiwe wafanyabiashara wetu wa Kitanzania wamalize bidhaa zao zilizopo misituni wasafirishe wazilete bandarini, zikaguliwe kwa uhakika na watumishi wahakiki kwa ukweli. Safari hii wasifanye utapeli watamalizika kwa kufukuzwa kazi na Mheshimiwa Waziri hana mchezo na kazi. Wasimamie vizuri hiyo, wataona maendeleo yatakayowaletea katika utumishi wao. Wapewe muda wafanyabiashara hawa waongezewe kama itawezekana miezi sita kwa sababu hivi sasa malori ni ghali na walikokuwa wameacha magogo ni mbali wengine mpaka Kyela, Sumbawanga, Mpanda huko kote magogo yameenea kutokana na hali ya mstuko walioupata.

Mimi nasema wafanyabishara hao kwa lugha nyingine ya kizamani kidogo nitaikumbusha wamepata mfadhaiko wa biashara kwa sababu ukipata kitu cha kukushtua na wewe huna nyingine yoyote na ni Serikali lazima uitii, lazima utavurugikiwa hata kama ulikuwa mtu una *degree* zako ngapi lakini kitu kikiingia mkono wa Serikali lazima unapata mshtuko na naiomba Serikali na Waziri pamoja na Kamati iliyotoa amri hii wasamehewe hawa watu wamalize shughuli zao na waanze utaratibu mpya wa kutengeneza dhana kama inavyotaka Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilikuwa naomba Waziri alifikirie suala moja wafanyabiashara wetu hawa hawana uwezo mkubwa, mashine za kuwawezesha kuranda mba, kutengeneza bidhaa vizuri pia zinatakiwa pesa. Hakuna hata mfanyabiashara wa magogo mdogo ambaye ana uwezo wa kuchukua mashine kama ilivyokuwa kwa Wachina wanatembea nazo kwenye *mobile* zao za magari wanapita kukereza huko huko porini wao hawana uwezo huo. Itabidi mabenki hayo hayo yaone uwezekano wa kuwakopesha pesa tena wanunue mashine ndiyo waanze kutekeleza lile ambalo Serikali imeagiza. Kwa misingi hiyo, mimi naona kuna umuhimu wa kuwasamehe watu hawa kwa biashara zao za magogo ili waweze kuendelea vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nimeona ni muhimu ni kuhusu ushauri tulioutoa wana Kamati mwaka jana. Mwaka jana kama alivyosoma Makamu Mwenyekiti, wetu wa Kamati alitoa ushauri wa aina mbalimbali na sisi tulikuwepo kwenye kuchangia maamuzi hayo. Sasa tulikuwa tunaomba utekelezaji ufanyike kwa sababu nimeangalia kwa haraka haraka kwenye vitabu hivi sikuona yote ambayo tulikuwa tumeomba Waziri ayaweke vizuri. Inawezekana ni hali ya kiuchumi.

Kwa mfano, tulisema watumishi ni wachache mno katika Wizara hii, kama ilivyokuwa ye ye mwenyewe hana Naibu Waziri wa kumsaidia hali kadhalika na watumishi ni wachache. Kazi hii ni nzito sana, wanatakiwa watumishi wengi, nyenzo, magari na kadhalika. Tulitembelea Kisarawe kule Kazimzumbwi tukaonyeshwa misitu

ambayo ilivamiwa na wananchi na baadhi ya viongozi jinsi wanavyowindwa watumishi walioko kule ni hatari kwa sababu ni wachache hawana nyenzo za kujilinda. Sasa kweli askari wa pori yuko pale Kazimzumbwi anawezaje kujilinda ikiwa hana nyenzo za kupambana na watu ambao wanadai hayo ni mashamba yao ya tangu asili na asili? Hilo naomba Waziri alifikirie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho nilikuwa naona ni vizuri Mheshimiwa Waziri angeweka mpango wa kudumu wa kutoa semina na mafunzo kwa wananchi kwa sababu wananchi wengi hawaelewii mipaka yao katika masuala haya ya uvunaji wa magogo, mambo ya uvuvi, masuala ya mashamba, wapi wanaruhusiwa na wapi hawaruhusiwi. Lakini kukiwa na mafunzo kuititia vyombo vyetu vya habari kama redio, *television* kama inavyofanyika hivi sasa itaturahisishia wananchi kutokuwa na makosa ya hapa na pale kwa sababu makosa yanatokea kwa sababu ya kutofahamu mambo gani wanastahili kuyafanya na mambo gani hawastahili kuyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba ombi moja tu labda halitawezekana lakini nilitaje tu labda linaweza likawezekana baadaye. Tuna wanyama wengi na wanakuwa tunawaona wakati wa mafuriko na mvua kubwa. Je, Mheshimiwa Waziri, haiwezekani ukapata wafadhili ukawaomba wakaweka kiwanda cha kusindika nyama za wanyamaporili wale ambao tunakaa mbali ya maeneo hayo tuweze kufaidi hizo nyama? Hali kadhalika wanyama wengine kwa Tanzania ni kero lakini kwa nchi za kigeni ni chakula cha heshima sana, pia wangeweza kuwatayarishia kwa mfano nyani, ngedere, tumbili.

Nchi zingine ni chakula cha heshima kuandaliwa mgeni. Basi vitengenezwe *wavi-pack* kwenye makopo waweze kula. Masuala ya dini kila mtu ataona ni kipi hakimfai na kipi kinamfaa ataweza kufaidika na chakula chetu cha wanyamaporili kuliko ilivyo hivi sasa wanakula vyakula na mashamba ya wananchi, inakuwa kero kwa upande wa kilimo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa hayo machache nirudie kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache kuhusu Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote napenda niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, kwa kazi zake nzuri kwa kweli anastahili pongezi kwa matendo ambayo anayafanya katika Wizara hii. Ni Waziri, pekee naye anafanya kazi vizuri. Kwa kuititia hotuba hii mambo mengi ameyaeleza pia, ningeomba niwapongeze vile vile Katibu Mkuu wa Wizara hii, Wakurugenzi wote wa Wizara, watendaji wakuu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa kweli Wizara hii inaendelea vizuri na kuingiza pato kubwa la nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo ningependa nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri kuwa mpango madhubuti ambao ameuandaa wa sera ya (*WMA*) *Wildlife Management Areas*. Naamini mpango huu madhubuti ukiendeshwa vizuri unaweza ukasaidia kupanua uwigo wa utalii na uhifadhi kama ulivyokusudiwa. Lakini nimeona nishauri kitu kimoja kidogo sana, kamati ya ushauri ngazi ya Wilaya ukiisoma unaona kwamba wale wajumbe ambao wanatakiwa waingie kwenye kamati hiyo ya ushauri sana sana ni watumishi wa Serikali kitu ambacho isingefaa kuwa na watumishi katika wote kamati hiyo. Mimi naomba kwamba kamati hiyo, iongezewe na wanasiwa baadhi, kama Madiwani wa maeneo husika na wakizingatia jinsia. Waingie Madiwani wanawake na Madiwani wanaume ili waweze kuwa na utaratibu unaofaa katika kushauri katika kamati hiyo ya ushauri ya Wilaya. Hili naomba kwa sababu ukiacha kamati hiyo peke yake ya watumishi, Serikali ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya, naamini kutakuwa na malumbano kwa wale wanaongozwa katika maeneo hayo kwamba hawaridhiki kwa sababu ni watumishi wa Serikali wote. Ningombaa ushauri huu uweze kuwa muafaka kwa maeneo yote ambayo ni maeneo ya WMA yatakayotengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo ningependa kuzungumzia suala la utafiti. Utafiti ni muhimu sana katika masuala yote tunayoyaendeleza hapa nchini. Bila utafiti mambo mengi yatakuwa yanakwama. Mimi nimeangalia katika maeneo ya vitabu vyote hivi, nimeona maendeleo ya utafiti ni kidogo mno. Ukiangalia tuna mambo ya *TAWIRI*, mambo ya *TAFORI*, *TAFIRI* hawa wanahitaji utafiti wa kina. Mambo yakifanyiwa utafiti huwa ni mazuri kwa sababu yanaonekana wazi walivyofanya utafiti wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 1999 katika Bunge hili, Kituo cha Nyuki cha Tabora, kiliunganishwa na Shirika la *TAWIRI*, kikiwa kitu kimoja. *TAWIRI* wanatafiti masuala ya wanyamapori, lakini wa Tabora wanatafiti masuala ya nyuki na miti. Sasa katika kuunganishwa wamekuwa na kazi kubwa, kimekuwa chombo kikubwa cha kuangalia maeneo yote, wanyamapori pamoja na misitu na nyuki.

Sasa basi tusipofanya utafiti maendeleo yao yatakuwa duni. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba suala la utafiti katika maeneo haya yazingatiwe sana. Nimesoma kwa mwaka huu mchango wa utafiti ulikuwa unachangiwa na sehemu kama tatu sehemu ya *TAWIRI*.

Kwanza Ngorongoro ilikuwa inachangia shilingi milioni 40, *TANAPA* walikuwa wanachangia shilingi milioni 60 kwa mwaka. Idara ya Wanyamapori ilikuwa inachangia shilingi milioni 100 zote jumla zinakuwa shilingi milioni 200. Kwa mwaka huu nimeona zimetengwa shilingi milioni 50 kitu ambacho kimeshuka kwa kiwango kikubwa sana kutoka shilingi milioni 200 kuja mpaka shilingi milioni 50 ni pengo kubwa sana. Kwa hiyo, hawa watashindwa kufanya utafiti wao. Ukitumbuka mambo yamepanuka zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba suala la utafiti lizingatiwe sana na kama kuna fungu ambalo linaweza likaonekana basi waongezewe hao watu waweze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya suala la utafiti ningependa tena nijielekeza kwenye suala la utalii, mambo mengi hapa tunazungumza suala la utalii ni kama kuona sana sana ni watu wa kutoka nje ya nchi. Watu wetu wa ndani suala la utalii hawalifahamu na wala hawajishirikishi kwa sababu ya kutokuwa na elimu ya utalii. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba ni jambo jema suala la utalii likazingatiwa na kutolewa elimu, maeneo yote. Hatuwezi kuendelea tu utalii kutoka nje ya nchi bila Watanzania wenyewe kuwa na watalii humu ndani. Tunatakiwa sisi Watanzania tuwe watalii vile vile katika maeneo yetu kufahamu urithi wetu tulionao ili kuweza kufahamu mambo mengi. Kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri kwamba suala la WMA litapanua uwigo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba niongezee sehemu moja kwamba katika miji yetu mikubwa kama Dar es Salaam pangetengwa eneo kubwa hekta kama 10 au hekta 20 au hekta 30 wakawekwa wanyama, kukawa na sehemu kama ya utalii kwa sababu ni jiji, watu wengi watakwendwa kuona pale kabla ya kwenda kuona mahali pengine kama alivyoshauri Mheshimiwa Janeth. Kabla ya kwenda sehemu nyingine unaweza ukaenda pale ukaona kwa kutembea karibu tu kama kilometra moja, mbili ukaona wanyama, ukaona miti aina mbalimbali, ukaona samaki, ukaona nyoka, ukaona ndege ukajiridhisha pale. Kama kuna maeneo zaidi hapo basi hata wanafunzi watakwendwa. Kwa sababu tunataka tuwarithishe watoto wetu urithi ambao. Ni vizuri watoto wakawa wanaingia bure pale bila malipo, wakawa wanajifunza uhifadhi tulionao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nasema hilo kwa sababu moja, ukifika kwenye maonyesho ya Saba Saba Dar es Salaam, ule msululu wa watu wanaokwenda kuangalia mabanda ya utalii ni watu wengi sana, mamilioni ya watu wanakwenda kuangalia mabanda hayo. Pengine inawezekana hata mtu mzima hajawahi kuona mnyama wa aina yoyote kwa mfano, simba, nyoka, au ndege. Kwa hiyo, ni vema kama tungetenga maeneo hayo kwenye miji mikubwa kama vile Mwanza, Arusha, Mbeya na hapa Dodoma kwa sababu Dodoma ndiyo Makao Makuu ya nchi tunasema hivyo. Sasa hapa tungkuwa na mambo ya kuangalia, hata sisi Waheshimiwa Wabunge, pengine kama kuna maeneo hayo siku za *weekend* mnakwenda kuangalia wanyama hao kwa kutembea tu siyo kwamba lazima muende kwenye mbuga za wanyama kama Mikumi ambapo ni gharama kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza ushauri wangu kwamba katika miji mikubwa yangetengwa maeneo hayo ya kuweza kuangalia maonyesho ya kutembelea kuona wanyama hao. Hifadhi hiyo itakuwa muhimu kwa mambo mengine tutakuwa tunaangalia kwa sababu na utaalam upo pale wa kuelezwu kwamba hapa kuna vitu ambavyo vinatunzwa. Hata yale mazingira yataonyesha kwamba hapa kweli kuna elimu inayotosheleza kuelewesha jamii kwa suala la utunzaji wa mazingira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala hili ningependa kwamba niombe pamoja na kwamba lina gharama si mwaka huu lakini tuanze kuona umuhimu wa kutenga maeneo hayo miaka ijayo. Lakini suala la elimu katika upande wa mazingira pamoja na utalii lizingatiwe sana kwa sababu bila elimu hata watu wengine hawana ufahamu, lakini siyo kosa lao kwa sababu ya kuona kwamba ukitaka kwenda Mikumi ni mbali kutoka kwa mfano Dar es Salaam. Ukitoka hapa kwenda Tarangile nako ni mbali, uende Ruaha ni

mbali. Kwa hiyo, ni gharama kubwa sana kusafiri kwenda kuangalia utalii wetu. Vile vile gharama za kuingilia kwenye hifadhi zetu, kwa sisi tunafanya shilingi 1500/= kama umesafiri masafa marefu hiyo ni gharama kubwa, kwa hiyo ni vema zikapunguzwa gharama hizo kama mtu amesafiri masafa marefu, kwa sababu ya gharama alikotoka kwenda anakokwenda kuangalia masuala ya uhifadhi. Kwa hiyo, ningeshukuru sana kama ushauri wangu ungezingatiwa na ninaomba haya yote ambayo nimesema mambo muhimu matatu yazingatiwe. Ushauri, Kamati ya Wilaya kwenye WMA isiwe ya watalaan wote wa Serikali, waingizwe na wanasiasa, utafiti uongezewe fedha na wapewe vitendea kazi wasije wakabaki wanakaa bila kufanya kazi zao wanazotakiwa wazifanye kwa kukosa vitendea kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache nashukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole Ndugu wa Mheshimiwa Marehemu Capt. Kasapira kwa msiba uliowapata na vile vile Ndugu wa Marehemu Yete Mwalyego. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Meghji kwa hotuba yake nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwapongeza Mheshimiwa Meghji, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Wizara zake pamoja na wafanyakazi wote wa Maliasili kwa kazi nzuri waliyofanya mwaka 2003/2004 kwa sababu walivuka malengo ya ukusanyaji wa mapato, walidhibiti ujangili na hii Wizara sio mara ya kwanza kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato. Mwaka 2001/2002 walivuka; mwaka 2002/2003 na mwaka huu nao unaoishia sasa wamevuka. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja mia kwa mia na baada ya kuunga mkono hoja, ninayo machache ambayo nataka kuyaongea. (*Makofi*)

Kwanza kabisa nataka nimpongeze Mheshimiwa Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa ujasiri wake aliochukua kupiga marufuku upelekaji magogo nje. Tumekuwa tukilalamika hapa kwamba Mawaziri huenda hawachukui hatua, lakini Mheshimiwa Meghji kuna wakati alikuja hapa tukamwambia *Sao Hill* kule kuna matatizo, alichofanya alikwenda kule na akasambaratisha wale waliokuwa wanataka kufanya matatizo kule. Aliposikia kuhusu magogo, moja kwa moja amewasambaratisha. Magogo yako pale Bandarini na amewaambia waliohusika waje kukagua na wasipokuja *yata-be confiscated*. Hapo ndio anaonyesha uongozi halisi. Kwa hiyo, mimi nampongeza. Sio hivyo tu, kuna panga lake limewapitia waliokuwa wanafanya uharibifu, kuna watu sasa hivi wako hatarini na wameshasimamishwa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Meghji ninachosema ni kwamba ni lazima *u-clean the house* bila kuogopa kwa sababu hii Wizara zamani ilikuwa na mambo ya uozo sana kabla hujaingia. Lakini baada ya kuingia ikawa imetulia kabisa. Sasa Mheshimiwa Meghji mama yangu, nakuomba usiruhusu mtu yejote kuchafua ile Wizara. Watu wanakuheshimu na miaka mitatu nimekuwa hapa kulikuwa hakuna kitu kama hicho. Sasa kitu hiki kilichojitokeza huko kimetusikitisha, tunaomba sana *u-clean the house without fear.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukataji wa magogo haya yana athari nyingi. La kwanza kabisa ni uharibifu wa mazingira. Pili, ni kwamba nimesoma katika gazeti hili la *East African*, wanasema kwamba sisi tunaiza *cubic meter* moja Dola 70, ndio maana Wachina wanakuja kila mtu anakimbilia hapa anakwenda kuuza *USD* 18,000. Sasa huo uwiano uko wapi? Kwa hiyo tunaomba hata bei nayo iangaliwe kama huko nje wanauza *USD* 18,000 sisi tuuze kwenye *USD* 13,000. Lakini hatuwezi kumpa mtu faida kubwa hivyo! Ndio maana watu wanakimbia kutoka China. Mimi sijasikia Mtanzania akikata magogo China, kwa hiyo wasije kukata magogo hapa. Tanzania sio mahali pa watu kufanya vitu ambavyo kwao tukienda hatutavifanya. (*Makofi*)

Kwa hiyo mimi nasema kwamba kitu cha kwanza kabisa hakuna mgeni kuja kukata magogo yetu. Sasa nimeambiwa kwamba kuna Watanzania ambao wamekopa kweli huko. Kama kweli walipewa vibali halisi wakakata hayo magogo, kwa hiyo makosa ni kwamba walifanya kazi hii wakijua kwamba wanafanya biashara ya halali. Waruhusiwe wayapeleke kwa sababu hata nyumba zao zitauzwa. Watauziwa nyumba, watoto wao, maana Benki haitawasamehe kulipa riba. Kwa hiyo, tunaomba kama kweli walipewa yaende lakini haya ndio yawe ya mwisho. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Baada ya hapo tutengeneze viwanda vya ndani. Tutengeneze hivyo vitu vinavyokwenda kuuzwa huko. Huyu anachukua magogo kwa sababu unapokata lile gogo kuna mambo mengi sana unaweza kufanya. Sasa tuuze *finished product* tuweke viwanda, tutengeneze hata wale Watanzania wakikata watengeneze twende tukauze kwa bei kubwa huko nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukumbusha kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu ilipoingia iliwekea mkazo sana kutafuta uwekezaji kutoka nje. Sehemu ya Utalii tumeona Hoteli za Serena, *Kilimanjaro Hotel* ambayo Waziri wetu Mheshimiwa Meghji aliisimamia. Watu walilalamika hapa siasa; ilikuwa ni gofu! Hata Mheshimiwa Masilingi naye kuna siku alijibu akasema jamani tuwaachie watu hao wawekeze. Sasa nenda leo pale karibuni *Kilimanjaro Hotel five star* inawekwa pale. Kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Mkapa na yeze mwenyewe nampongeza kwa kuleta Wawekezaji, ni jambo sahihi nichini. *Kilimanjaro Hotel* ilikuwa imeoza, sasa hivi karibuni tutakwenda kule kufanya Mikutano na kujipongeza. Lakini zaidi ni kwamba hata huko maporini tumeanza kupata faida.

Mheshimiwa Spika, Serengeti sio tumekuja kulalamika, mwaka juzi ilikuwa ni kampeni Serengeti itusaidie, inasaidia Arusha, sasa leo tumekuja kukueleza kwamba sasa

tumeanza kufaidika na Serengeti. Kuna Kampuni moja imekuja pale inaitwa *VIP* imefanya mambo makubwa. Kwanza imeajiri watu ambao kwa *Annual Salary* inafikia kama Dola 230,000; imepatia watoto 20 wa Sekondari *Scholarship*, wengine sita kwenye Vyuo na wawili *University*. Hiyo ni baada ya mwaka mmoja na nusu tu. Wamejenga Shule moja ya Sekondari pale Natu, halafu wamejenga *Primary* mbili kwa muda wa mwaka mmoja. Wametuletea vitabu 10,000 katika Shule nane za *Primary*; Wamechimba visima 11 katika Sekondari zetu na wanaendelea kujenga na wamenunua *rig* ya kuchimba visima. Wametununulia *Ambulance*, kama kuna matatizo unapiga simu tu *Ambulance* inakuja kukuchukua. Wamenunua greda la barabara, sasa hivi tunalima barabara zetu sisi wenyewe kwa Dola 150; Sasa hivi wanajenga five star. Sasa mimi namsifu Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi nzuri. Tuleteeni Wawekezaji wengi na Serengeti tunawahitaji na tutajenga kiwanja *International Airport Serengeti*. Sasa ule mchezo tulikuwa tunalamika Arusha, sasa tuna-*compete equally*. Ndugu zetu wa Arusha kaeni tu-*compete* pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba sana tumwombe tena Mheshimiwa Waziri aende huko apitepite atuletee Wawekezaji wengine. Tunataka watu kama hao tukiwapata Serengeti wawili kama VIP, sisi tutakuwa tumeamka. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kwamba zamani ukifika pale Serengeti ilikuwa uwindaji unaweza kwenda ukaua na ukapita na gari limejaa wanyama watu wanashangilia tu. Lakini vitendo vya ujirani mwema vilipoanzishwa katika Shirika la *TANAPA*, Idara ya Wanyamapori na Ngorongoro, limehamasisha wananchi sasa hivi huwezi kupita pale na mnyama unatoka kuwinda. Hawawezi kukuruhusu kwa sababu sasa wamejua kwamba wale wanyama ni mali na kwa nini wanyama wamekuwa ni mali kwetu na wamejua kwamba huna haja ya kumwua kwa sababu katika yale mapato yanayopatikana kuititia *TANAPA*, tumepewa Malambo, sasa hivi tuna malambo kama matano pale, wamelipa *TANAPA*. Ng'ombe walikuwa wanakufa, sasa hawafi. Kwa hiyo, naishukuru sana *TANAPA* na Mheshimiwa Waziri, wametujengea Shule kama tano, zipo. *Dispensary* wametuwekea, sasa hivi ninapoongea wanajenga Bweni la Wasichana wa Shule ya Sekondari ya Serengeti, halafu wanajenga *Primary School* kule Miseke. Kwa hiyo, naomba hivi vitengo vya ujirani mwema viimarishwe zaidi vihamasishe watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingi wananchi wanalima pamba, wanapanua wanakata miti wanalima tumbaku kule Mpanda na wapi. Sasa naomba Wizara hii ishirikiane sana na Wizara ya Kilimo na Chakula ili watu waweze kutumia kilimo cha kisasa, kutumia mbolea waweze kutumia ardhi ile ile sio kila mwaka kwenda sehemu nyingine huko kukata misitu na kuimaliza kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba mimi ni mwanamisitu niliyepo hapa tena niliyebobe. Kweli! Mtu kama una shahada tatu katika fani hiyo, *why!* *B.Sc.*, *Masters*, na *Ph.D.* ya Misitu. Sasa kinachonisikitisha wanamisitu wenzangu kuna waliopelekwa TAMISEMI, kule wamefika wanakaa tu hakuna nyenzo za kufanyia kazi na ndio hawa ambao hata wakati mwingine bado wanavitoa kiholela vibali maana wako katika watu ambao sio *professional* na kule Halmashauri za Mitaa hakuna kipato. Sasa wamekaa tu.

Tunasema wale watu warudishwe kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii ili waweze kufanya kazi vizuri. Pale Serengeti nampata mwanamisitu Mwenzangu siwezi kumlaumu, hana kazi lakini haachiwi hata senti moja! Sasa atafanyaje kazi? Naomba warudi waweze kufanya kazi twende leo na *Village afforestation* kama ilivyokuwa zamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeanzisha WMA. Hizi ni muhimu kwa sababu wananchi sasa watamiliki maeneo ya wanyama. Naomba sana pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Idara ya *Game*, naomba washirikiane tena waweke nguvu kuhakikisha kwamba hizi WMA zilizoanzishwa hivi karibuni zinafanikiwa. Ni kazi nzuri wanayofanya lakini tuweke nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna hoteli za *TAHI* zilizouzwa nazo ni Soronera, Lobo, Mafia na Manyara. Wafanyakazi wale wanalamika kwamba hawakulipwa mafao yao vizuri. Sasa namwomba Mheshimiwa Meghji kama Waziri wa Maliasili na Utalii tufuatilie kule na *PSRC* tuone kwa nini hawa watu hawajalipwa mafao yao kama hoteli zinauzwa ili familia zao zisiadhirike. Mimi wamekuja kuniona wana hali mbaya sana. Naomba tulifuatilie hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo namwombea afya njema Mheshimiwa Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mungu ampe hekima nzuri aweze kutekeleza hii mipango pamoja na Maofisa wake na Katibu Wakuu wake. Ninarudia kwamba hicho kitu kinataka kutokea hapo, uchafu katika nyumba yako, *clean it*. Sisi tuko nyuma yako tutakusaidia. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kabisa! Safi sana. (*Makofi*)

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii Bwana Odunga, Wasaidizi wao wote wa Idara mbalimbali katika Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Aidha, kwa namna ya pekee nimpe pole sana Mheshimiwa Mama Meghji kwa kauli zake alizozungumza hapa kwamba leo ni mara ya kwanza amewasilisha Bajeti yake bila kupigiwa simu na mumewe ambaye Mungu alimwita mbele ya haki. Tunampa pole, tunamwomba Mungu amjaze ujasiri na nguvu za kukabili hali hiyo kwani ni mapenzi ya Mungu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitoe pole kwa familia ya Waheshimiwa Yete Mwalyego na Mheshimiwa Comrade Kasapira pamoja na Wapiga Kura wao na hata

Watanzania wote kwa msiba mkubwa uliowapata wa kupotelewa na ndugu zetu hawa, tunaomba Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuonyesha wasiwasi wangu kuhusu majukumu ya Wizara hii. Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa raslimali nyingi na raslimali nyingi za Taifa letu ziko katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Kuna sekta nne muhimu mbali ya nyingine zilizoko chini ya Wizara hii, zikiwemo Sekta ya Uvuuvi, Utalii, Misitu na Wanyamapor.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya umaskini wa nchi yetu na uduni wa Teknolojia tuliokuwa nao hasa Tukijua kwamba tegemezi kubwa la uchumi wa nchi yetu litakuwa katika Maliasili ambayo tumejaliwa na Mwenyezi Mungu, tunaona na ninaamini kabisa kwamba bado Serikali inastahili kuongeza nguvu katika kuboresha, kupanua na kuimarisha Wizara hii kikamilifu ili iweze kuchangia katika pato la Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi na kwa kweli kwa upana wa kazi za Wizara hii, tunamhurumia na kipekee ninamhurumia sana Mheshimiwa Waziri na wenzake wote kwamba wanabeba mzigo mkubwa na mzito sana ambaao kwa kweli wangehitaji msaada wa kufikiria namna ya kuendeleza suala la Uvuuvi, Utalii, wanyamapor na hata misitu. Ukiangalia kwa kina utakuta Wizara hii inafanya kazi nyingi ambazo pengine zingeweza kufanyika kwa urahisi zikachangia pato kubwa la Taifa. Lakini katika mchango wangu baadaye, nitajaribu kuainisha kwa kutumia takwimu.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi za wenzetu ambazo zimeweza kuendeshwa kwa Idara hizi peke yake au Idara hizi kuweza kuchangia kwa kiwango kikubwa sana katika pato la Taifa, mathalan suala la Uvuuvi. Wenzetu wa Namibia Uvuuvi unachangia karibu nusu ya pato la Taifa kwa nchi ile na maeneo yao ya Uvuuvi bado ni pungufu sana, labda ni robo ya maeneo ya Uvuuvi ambayo Tanzania kama Taifa tunayo. Ukienda kwa upande wa Watalii, wenzetu wa nchi kama *Seychelles* na Mauritius ni visiwa vidogo lakini vimeweza kupanua Utalii kwa kiwango kikubwa mno na hawa Utalii wao zaidi ni Utalii wa bahari kwamba wanakuwa wana *beach resources* nyingi. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba tunahitaji sasa kama Taifa kufikiria kwa upana sana kwamba Wizara hii Waziri asaidiwe vipi iweze kuwa na wataalam wengi, iweze kuwa na Idara za kutosha kwa sababu ni Wizara ambayo kama ikiwezeshwa na ikafanyiwa kazi kikamilifu, ni Wizara ambayo inaweza kuwa chanzo cha mapato makubwa sana kwa Taaifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la misitu. Leo katika mchango wangu kwa sababu ya muda nitajaribu kuzungumzia maeneo mawili tu, eneo la misitu na eneo la utalii. Sasa kwanza nianze na eneo la misitu. Tumeona Waheshimiwa Wabunge wengi na hata wananchi katika ujumla wao wakilalamika kuhusu ufujaji na uporaji wa maliasili katika misitu yetu na pamekuwepo na shutuma nyingi kwa Serikali kwamba pengine Serikali haifanyi kazi vya kutosha. Mimi naamini kwamba pamoja na Serikali kufanya juhudhi zote, bado kuna umuhimu mkubwa wa kutafuta mkakati wa kushirikisha umma katika hifadhi ya misitu yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika hili ushirikishwaji umma hauendi kwa maneno mazuri na rai mbalimbali za kutolewa na viongozi. Katika hali ya kawaida ya binadamu ushirikishwaji umma unafanikiwa pale panapokuwepo na motisha ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika Hifadhi ya Msitu wa Mlima wa Kilimanjaro kule Rongai na maeneo mengine ya Wilaya za Hai na Rombo, uvunaji wa misitu ya hifadhi umekuwa ni kero kubwa sana. Kweli Serikali imejitahidi kwa kiwango fulani kuwashirikisha wananchi lakini bado naamini ushirikishwaji huu ukiweza kuongezewa motisha na wananchi wale wakawa wana mgao katika pato fulani linalotokana pengine na mlima wanaweza wakadhibiti hali hii, *otherwise tutajikuta tunaharibu mlima huu ambao kwetu ni urithi mkubwa na ni mojawapo ya World Heritage Sites. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 47 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna jedwali Na.6 linaloonyesha upandaji miti. Kwa kweli nimeangalia takwimu hizi na ninastahili kuwapongeza wenzetu wa Mkoa wa Tanga, Mwanza na Iringa kwamba kwa mfano Mkoa wa Tanga wameweza kupanda miti katika mwaka 2003/2004, wameweza kupanda miti 62,000,000 wakati huo huo Singida wakipanda miti 300,000. Wenzetu wa Mkoa wa Iringa wamepanda miti milioni 14 wakati wa Mkoa wa Dar es Salaam wamepanda miti 400,000.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hizi takwimu ina maana kuna tatizo na kuna ukiukwaji mkubwa wa maagizo ya Serikali kuhusu suala zima la upandaji miti kama sehemu muhimu ya uhifadhi wa mazingira. Ningombaa kabisa niitake na niiombe Serikali iweke msisitizo na ile Mikoa ambayo inapuuza zoezi hili la upandaji miti, wahusika wake waweze kuchukuliwa hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la misitu, pengine tungejadili kidogo suala la mapato yatokanayo na Idara ya Misitu. Mwaka jana nilibahatika kwenda katika maeneo ya Kilwa katika harakati zangu za kisiasa na nilikutana na uvunaji mkubwa wa magogo na hata nilifanya Mkutano na Waandishi wa Habari kujaribu kuelezea hali hiyo, Bandari ya Kilwa ikiwa imetapakaa magogo ya aina mbalimbali, Wakorea, Wachina, Wahindi, Waswahili, wanapishana katika msitu wa Selous wakivuna miti bila huruma wala bila hiana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwamba hatua alioichukua pamoja na kwamba imechelewa, lakini ni hatua madhubuti na ninaomba asilegeze kabisa mkakati huu. Lakini nielezee wasiwasi wangu upande wa pili kwamba kwa kasi ya uvunaji wa magogo na kwa kiwango cha mapato ambacho sisi kama Taifa tunapata, kuna mambo mawili. Aidha, kuna makosa katika uchapishaji wa kitabu hiki ama kuna wizi mkubwa na udanganyifu wa hali ya juu ambao umepata baraka za baadhi ya Watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiingia katika jedwali la tano ukurasa wa 46 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, magogo yote ya miti yaliyovunwa katika nchi hii yaliweza kuingizia Taifa pato la Dola milioni 2.5. Wakati huo huo, mbao ambazo

zimechanwa zimeweza kuingizia Taifa mapato ya Dola 140,000 tu kwa mwaka mzima. Ukija kwa mbao za sakafu hizi wanaziita *parquet flooring* ambazo mimi mwenyewe binafsi nina taarifa ya Makampuni mengi ambayo yanashughulika katika kuuza mbao hizi, yameweza kulipatia Taifa jumla ya Dola za Marekani 276,000 tu. Sasa nyumba ya kawaida ukiijenga kwa kutumia *parquet flooring* nyumba ya vyumba vinne, itaku-cost Dola 10,000 kuweka *floor* ya mbao. Sasa kwa idadi hii ya mbao hizi zilizouzwa nchi za nje ina maana ni nyumba kumi tu zilizoweza kuwekewa mbao kama hizi huko nchi za nje. Mimi nasema kuna udanganyifu mkubwa au pengine labda hizi takwimu sio sahihi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama mapato haya ndio mapato Taifa linapata, pengine basi tupige marufuku kabisa, hatuna faida hata moja ya uvunaji wa miti yetu wa mapato kidogo kama haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye upande wa vinyago, mapato kwa Taifa yaliyopatikana kwa vinyago ni Dola 190,000. Sasa kwa kuvuna mpingo, mti ambao unatumia miaka 200 mpaka 500 kukomaa, kwa mapato ya Dola 190,000 mimi nafikiri pengine ni bora tungepiga marufuku hata kukata miti yetu ya mpingo kwa sababu hii kamwe haitaota tena karibuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kumaliza mara moja lile tatizo la yale magogo ya Dar es Salaam. Yale magogo yaruhusiwe yamalizie kazi yake yauzwe, lakini baada ya hapo nimshauri kabisa Waziri na Serikali tupige marufuku kabisa uuzwaji wa magogo nchi za nje hasa magogo ya mbao ambazo ni za asili. Kama tuna-export magogo basi tuweze ku-export labda teak ambayo inaweza ikapandwa na ikavunwa katika muda mfupi. Lakini kwa magogo ya *hardwood* yanayotumia zaidi ya miaka 200 kukua hatuna sababu ya kuyavuna, bora tuyache yatusaidie kuhifadhi mazingira na tupate mvua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikimbie kidogo upande wa Utalii. Nikiri kwamba mimi mwenyewe ni mfanyakishara ya Utalii, kwa hiyo nina *interest* katika eneo hili la biashara.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni *expensive destination*. Ukirudi tena kwenye page 55 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukiangalia idadi ya watalii wa Kimataifa wanaokuja Tanzania, kuanzia mwaka 1999 walikuwa 627,000; mwaka 2000 walikuwa 501,000; mwaka 2001 walikuwa 525,000; mwaka 2002 walikuwa 575,000 na mwaka 2003 walikuwa 276,000. Ukiangalia hii *growth rate* hii tumedumaa katika Utalii. Tusipongezane kwamba Utalii unakua au Utalii unapanuka; Utalii unadumaa! Ama takwimu zilizotolewa katika kitabu hiki pengine zinatia utata. Ukiangalia idadi ya siku walizolala watalii, labda idadi ya vitanda imeongezeka kutoka 17,000 mpaka 55,500 kwa kipindi cha miaka mitano. Lakini ukiangalia mapato yaliyopatikana kutokana na Utalii bado mapato yako katika wastani ule ule. Lakini ukija tena kuangalia *average expenditure per person* ni kama Dola za Kimarekani 153.

Mheshimiwa Spika, sasa tuna tatizo kubwa hapa na ninachowenza kusema hapa ni kwamba kwa kutumia takwimu hizi katika ukurasa huu, Utalii katika nchi yetu umedumaa. Sababu moja kubwa mojawapo ya kudumaa kwa Utalii katika nchi yetu ni kwamba Tanzania ni *expensive destination*. Matumizi ya Dola 153 kwa siku kwa mtalii wa kawaida ni pesa nyingi sana katika mazingira ya kawaida. Ukienda katika nchi nyingine ambazo zimekuza utalii kama *Seychelles* na Mauritius, wageni wana-spend average ya Dola 50 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachokisema hapa, tuna umuhimu wa kuangalia tena viwango vyetu tunavyo-charge watalii wanaokuja katika nchi yetu kama alivyokuwa ameshauri Mheshimiwa Ndesamburo.

Kwa mfano ukiangalia gharama za kupanda Mlima wa Kilimanjaro kwa mtalii wa kawaida ni kama wastani wa Dola 800 za Kimarekani kwa mpando mzima wa mlima. Hii ni gharama kubwa sana na watalii wengi katika maeneo mbalimbali ambayo tunajaribu kufanya na kuuza nchi, wanalamika kwamba Tanzania ni *expensive destination*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda haunitoshi sana labda nizungumzie suala la kuuza nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wanazungumza suala la kutumia Ofisi zetu za Ubalozi katika kuuza utalii wetu. Ukweli ni kwamba tusidanganyane hapa, Ofisi za Ubalozi ni chache na watalii ...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)

SPIKA: Malizia tu sentensi yako, ni kengele ya pili.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Sawa Mheshimiwa Spika.

Nilichokuwa nataka kumaliza ni kwamba naishauri Serikali sasa ianze kutumia vyombo vyta kisasa vyta kiteknolojia katika kuuza utalii wa nchi yetu kwa kipitia mitandao ya *Television* kama *CNN*, *BBC* na *Sky News* kama nchi za wenzetu wa Thailand, Kenya na Mauritius wanavyofanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofit*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mjadala utaendelea mchana kama kawaida. Hadi kufikia hapo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni.

(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

(Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi naomba niungane na wenzangu kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Timu yake yote kwa kutuletea hotuba yenye mwelekeo na yenye matumaini. Hali kadhalika na mimi nitumie nafasi hii kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mbunge mwenzetu Kasapira ambaye ametutoka wiki ya jana. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja, nizungumzie kwanza suala la utalii. Kama alivyozungumzia Mheshimiwa Mulyambatte kwamba iko haja ya kuendeleza elimu ya utalii. Mimi nasema elimu tu haitoshi, iko haja pia kwa Mheshimiwa Waziri kutengeneza utaratibu ili sisi tunapotembea kwenye haya mahoteli ingawaje yamebinafsishwa tupate *concessional rate* kwa sababu wengine wanawenza wakamaliza miaka mitano hawajalala Serena, hawajaenda Ngorongoro, Seronera, Lobo, maeneo hayo bahati nzuri katika nyadhifa zangu za zamani ndiyo ilikuwa natembelea na kulala. Kwa hiyo, naona haja hiyo ipo. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atufikirie hivyo. (*Makofit*)

Nalisema hilo kwa makusudi kabisa kwa sababu unaogopa, kwa sababu chai 20,000. Wengine sasa tunaogopa hilo. Sasa kama kuna utaratibu maalum basi tufikiriwe kwa hilo. Punguzo maalumu ni muhimu sana. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kunizindulia mapango ya Milima ya Umatumbi. Mapango aliyazindua tarehe 22 Septemba, 2001 lakini bahati mbaya tangu wakati tumehangaika kupata mtu wa kutustiri ili kuyaendeleza na kuyaweka katika suala ya kivivatio imeshindikana. Kwa hiyo, namwomba basi kwa sababu iko chini yake atusaidie kwa hilo kama tunaweza tukapata *investor*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalofuata ni suala la Vita vya Maji Maji. Vita hivi mwakani inatimiza miaka 100 na maandalizi ya Sherehe yameshafanyika. Kwa masikitiko makubwa watu wa Songea walitaka kuidaka hii sherehe. Lakini labda ilikuwa yule kiongozi wao hakusoma historia vizuri. Kwa sababu vita vilianza kwa Wamatumbi, ikaishia kwa Wangoni mwaka 1907. Kwa hiyo, jukumu la maandalizi ni la kwetu na tunaomba msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa masuala ya maliasili, misitu. Kama walivyozungumza wenzangu waliopita, nasema kwamba haya mambo yalifanyika, mpaka ikatokea hii amri ya kusitisha, kwa kweli masuala haya yalifanyika na baadhi kwa kusaidiwa na baadhi viongozi ambao wanastahili kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Lakini labda kwa kutaka kujinufaisha ndiyo wamesababisha watu wapate hasara zote hizo mpaka leo hali iko kama hii. Lakini nafikiri jambo hili halina matatizo kwa sababu ukitazama Ilani ya Uchaguzi ibara ya 22 inazungumzia maliasili hasa misitu, lengo ni kuwanufaisha wananchi ili waweze kufaidi maliasili yake. Ni dhahiri kwa misingi hiyo tunaomba kwa heshima zote Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili ili hawa mwenzetu

walioingia kwenye matatizo haya wasiendelee kupata hasara. Mimi ni mbia, siyo mshika dau. Kwa hiyo, lazima masuala haya, viswahili hivi vinaleta matatizo. Mbia, yaani Shinyanga, almasi. Mwanza, pamba, kule kwangu misitu na bahari. Kwa sababu natoka kwenye misitu nakuwa mbia kwa lugha ya kibiashara, lakini sifanyi shughuli hizo. Lakini katika masuala ya kutaka kuliweka jambo sawa unapozungumzia biashara hii unazungumzia masuala ya siasa.

Kwa sababu tangu tatizo litokee yametokea mambo kama hayo kwamba magogo yalivyostishwa, wale wananchi kule vijijini wengine hawajalipwa, baba alikuwa anakata magogo, kijana anapata kazi ya kupakia, mama anapata kazi ya kupika chakula, mama lishe. Kwa haya yote yaliyotokea biashara hizo zote kijijini zimeshakwama na hivi tunavyozungumza hali inakuwa sio nzuri. Kwa hiyo, rai iliyotolewa na wenzangu na mimi namwomba Mheshimiwa Waziri alitafakari suala hilo ili si kwa sababu tu ya kutaka kujifagilia. Lakini pia kwa kuangalia hali ya kibinadamu kwa sababu watu wamepata matatizo makubwa sana kama wengi walivyozungumzia wengi wamekopa mapesa benki, wengine watoto wao wamefukuzwa shule, hali kadhalika. (*Makofi*)

Hili ni suala zito na halafu nasikitika mchangiaji wa mwisho asubuhi, yeye alisema tupige marufuku. Anaposema tupige marufuku na kwa sababu sisi watu ambao tunao, chama chetu kimoja, ndiyo waliopata haya matatizo. Yeye anatafuta hoja ya kutukaanga kwamba Serikali yenu mnaona imewatia hasara. Kwa hiyo, hiyo ikamsimamisha mahala sisi wananchi watuone hatuko nao pamoja. Kwa hiyo, katika kulifanyika suala hili uamzi lazima kuangalia nani anashika dola sasa hivi na nani ananyemelea dola. Lisiamliwe katika misingi kwa sababu mambo mengine yametokea kwa mambo ya kuchomana chomana, mambo ya fitina. Fitina, wivu wa kibiashara, wivu kati ya wawekezaji na *indigenous* hawa wazawa. Maana yake pamoja na kwamba misitu ni yetu lakini Wachina wanataka wao wafanye hapa ndiyo kwao. Halafu wameshaanza kuwazulumu baadhi ya watu waliowafanya *ma-Sub Contractor*. Nataka nitamke yule ambaye aliingia kuja kuwa mwekezaji kuititia *TIC* kampuni yangu ikawa kama mdhamini, kuanzia sasa hivi saa 11.10 namkana na sina haja naye na nitakwenda *TIC* kwenda kumshughulikia ili atafute dhamana mwengine. (*Kicheko*)

Hiyo ni rasmi kwa sababu kuna watu wamekuja ameshawazulumu, wamempelekea mizigo mara tatu mara nne sasa hivi wale watu wameshakuwa maskini. Wapo hapo kwenye *Gallery*. Kuanzia leo simjui na asinijue. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo langu lingine ni kwamba hapa nina *interest*, hapa nina maslahi napo kwa sababu mimi nilimwona Mheshimiwa Waziri, nilimwambia Mheshimiwa Waziri, tulikuwa na vitalu nya kuwinda, Kilwa *Open* ilikuwa *open* alikuwa anashughulikia mtoto wa Marehemu Sokoine, halafu baadaye tukagawa vitalu vikawa vitatu. *Kilwa South* tukaigawa kukawa vitalu viwili. Mimi nilimtafuta *investor* kule Arusha kwa kutaka watu wanaojua hizi shughuli ni lazima tukiri ni wenzetu wa Kakazini. Lakini pia na sisi, nimekaa Seronera, nilikuwa nashughulikia masuala ya wafanyakazi *Serengeti National Park*, *Seronera Wildlife Lounge*, *Lobo*, *Serengeti Research Institute*, nimekaa miaka miwili, najua mambo ya uihifadhi, nilikuwa na Stephen Babu, Metili, Ndosi na Kishe yule wa *TANAPA* mpaka sasa yupo.

Kwa hiyo, masuala ya uwindaji siyo kwamba mimi ni mtu wa kaswida, nataka niingilie mambo ya *hunting*. Nilikuwa namwambia Bwana Severe, kwa sababu mama alishajivua kwamba kuna Kamati. *Chairman* Bwana Mlay, yule Bwana Severe, yuko Bwana Lyimo. Mimi naomba wasiniwekee mizengwe. Nataka nikistaafu sura yangu isikunjike. Nataka nikistaafu niendelee kuishi maisha yangu kama ninayoishi na kwa sababu wawekezaji wengi wametoka huko *North* basi jamani hata hili hamtuachii jamani? Hebu tuhurumiane, Bwana Severe mimi nakufahamu ni mchapa kazi, lakini tuangaliane jamani. Mama amesema masuala haya unayo wewe. Sasa tusigombane bwana vile vitalu navitaka. (*Makofi*)

Vitalu viko kwangu, viko nyumbani kwangu, viko katika maeneo yetu. Mwenzetu kule una vitalu mia sita kidogo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, naomba uongee na Spika au umwa-address Waziri kuliko watu wa nje.

MHE. OMAR S. CHUBI: Naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

Ninachosema Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kuweka sawa ili usinielewe vingine kwamba nasisitiza tu yaani badala kwamba Mheshimiwa Nkumba huwa anatumia kulia. Mimi siwezi kulia kwa sababu mimi ni mtu mzima. Na Mheshimiwa Profesa Mgombelo naye kaingia mkumbo wa kulia. (*Kicheko*)

Lakini *sincerely* nasema kwa moyo mmoja kabisa naomba hivyo vitalu nilivyoomba nipewe. Kumetokea jambo ambalo mimi silifurahii kwa kweli hawa Waheshimiwa wanamharibia dada yetu kazi. Kumeanzishwa *operation magogo* kuna Afisa mmoja ambaye bahati mbaya nimefutilia nasikia kaondoka mchana, kaamuru Askari Wanyamapori wakamate watu kule na kuna wananchi wapiga kura wangu wamepigwa, Askari Wanyamapori wameweka vizuizi bila hata alama mpaka mfanya biashara mmoja alivyoona magogo yamewekwa akatoa bunduki, alifikiri anavamiwa na majambazi. *Details* naweza kuzitoa kwa Afisa anayetaka.

Lakini kuhusu mtu aliyempiga wananchi wangu, namwomba Mheshimiwa Waziri umshughulikie. Siwezi kumtaja hapa. Lakini nafikiri hata wewe umeshasoma magazeti, umesikia mambo yanayofanyika kule. Huyu anatuharibia mwelekeo wetu wa Uchaguzi wa 2005. Ili wananchi watuchukie tunafanya mambo holela holela. Mimi kilio changu katika yote naunga mkono mia kwa mia masuala ya Wizara. Lakini yule aliyepiga watu ashughulikiwe na kama Wizara itaona haifai kufanya hivyo mimi na wananchi wangu tuutamshughulikia kupitia vyombo vy'a dola. Hii nataka iingie kwenye *Hansard* tutamshughulikia kupitia kwenye vyombo vy'a dola. Hiyo ndiyo kitu ambacho kusema kweli kimeniharibia *mood* hata mchana huu sijala na ninasikitika sana juu ya jambo hilo.

Lakini kwa ujumla mimi nataka niseme kutoka moyoni mwangu sina *grievance* na mtu yoyote wa Wizara, nina kwenye eneo la karibu na *Selous*, ule mpango wa ushirikishi wa kutunza hifadhi tumeupata kutoka Serikali ya Ubelgiji nashukuru. Kwa

sababu hilo tendo limeniongezea na mimi uhai wangu wa kurudi hapa. Lakini hivi vitu vidogo vidogo ambavyo vinataka kusababisha na sisi tuonekane siyo watu, naomba suala hili Mheshimiwa Waziri alitazame.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuomba kwa sababu misitu ni siasa, Mheshimiwa Mama, Waziri chonde, wale ambaa mizigo yao imekamatwa wahurumie, wape muda, waokote okote magogo yao kwa sababu maeneo yote hayana njia mpaka labda baada ya miezi mitatu minne ijayo ndiyo uje utunge hiyo Sheria. Tunazungumzia kama vile unavyoweza kutetea pamba kama inataka kunyeshewa mvua, usibishe naomba na hii ndiyo maana ya kuomba kidemokrasia. (*Makofi*)

Mbia kwa maana misitu iko kwangu na kwa taarifa katika Mkoa wa Lindi sehemu ambayo imebaki misitu ni Jimbo la Kilwa Kaskazini. Kule kote mambo yameshakwenda na ndiyo hivyo ilivyokuwa lakini hatutaki kumshika mtu hapa kama ndiye amekuwa chanzo. Yaliyopita kama alivyosema Mheshimiwa wa Mafia si ndwele, tugange ya sasa na yajayo. Naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa salamu zangu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Theodos Kasapila, naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa anayofanya. Naomba pia niwapongeze Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa na anaifanya kwa ufanisi na tungeomba kama inawezekana aongezewe Naibu Waziri kusudi waweze kusaidiana katika Wizara kuu hii ambayo ina Sekta nydingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kuhusu Idara ya Misitu. Tulipotembelea Tanga tumeona jinsi msitu wa Amani unavyoweza kusaidia kuingiza kipato katika nchi yetu na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuhakikisha kwamba katika hotuba yake mwisho wa jalada ni kwamba ameweeka msitu wa Amani kila mtu anaweza akauangalia. Ni msitu mzuri unapendeza na una viumbe vingi vyaa ina nydingi ambavyo kwa kweli ni kivutio cha utalii. Katika msitu huu kuna viumbe pekee ambavyo vinapatikana hapa Tanzania na haviko katika ulimwengu mwingine hasa kama alivyosema Mheshimiwa Janet Kahama, maua ambayo yanapatikana katika msitu huu hayapo popote duniani. Vile vile kuna nyoka wa aina nydingi. Kuna wanyama wanaotambaa chini. Kuna wadudu wa aina ya pekee. Kwa hiyo, msitu huu unahitaji uhifadhiwe, cha kusikitisha ni kwamba msitu huu unaanza kuharibiwa. Katika msitu huu kuna vyanzo vyaa maji ambavyo ndiyo tunapata maji yanayotumika katika mji wa Tanga pamoja na Muheza kwa ujumla. (*Makofi*)

Maji haya tayari yanaanza kuharibiwa, vyanzo vyaa maji vimeanza kuharibiwa. Kuna wachimbaji wadogo wadogo ambaa wanachimba dhahabu na ni dhahabu kidogo

sana wanayopata lakini uchimbaji huu umesababisha madhara makubwa katika msitu huu, cha kushangaza ni kwamba inaonekana hakuna mawasiliano au hakuna ushirikiano kati ya Wizara na Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona Wizara ya Nishati na Madini wanatoa vibali vya uchimbaji katika msitu huu sehemu ya Kisakale. Ni kwamba huu msitu utapotea, viumbe ambao wanategemea msitu huu watapotea. Lakini mbaya zaidi mji wa Tanga utapatwa na madhara makubwa kutokana na zebaki ambayo watakuwa wanatumia katika kusafishia madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini ifikirie upya katika utoaji wa leseni hizi. Naomba niongelee hifadhi ya bahari. Huko Mtwara kuna hifadhi ya mikoko na kwa kweli ina madhari mzuri ambayo haijatolewa kipaumbele kuwa kama kivutio cha watalii. Naomba Wizara ihakikishe sehemu hii ya Mtwara ambayo ina mikoko mizuri utafikiria ni barabara na *streets* ambazo zinakuwa katika mji wa bahari. Hii misitu izidi kulindwa lakini zaidi iwe kivutio kwa watalii. Iweze kutangazwa kusudi nchi ambazo zinakuja zinapeleka watalii huku waweze kufika kule Mtwara na kuona madhari mzuri ya bahari na misitu ya mikoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Mafia kuna hifadhi ya samaki. Kuna samaki wa aina mbalimbali, wazuri wa mapambo ambao kwa boti maalum unaweza ukachungulia ukawaona huko chini, kuna milima, kuna majani ya aina mbalimbali. Hiki ni kivutio kikubwa cha watalii na kinahitaji kulindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wananchi waweze kupata fursa ya kuona utajiri tulio nao hasa kule Mafia kwa wale samaki na milima chini ya bahari kusudi iwe vile vile ni kivutio kwa utalii wa ndani pamoja na utalii wa nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zakia Meghji, anafanya kazi kubwa nzuri. Lakini mazingira anayofanya kazi yanatisha. Hebu tuangalie jengo la Wizara lililopo pale Dar es Salaam, halilingani kabisa na Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo inavutia wageni, ambapo wageni wanafikia jengo hili linahitaji ukarabati wa hali ya juu na ama ikiwezekana basi wapatiwe sehemu nyingine wajengewe jengo la Wizara ambalo linalingana na Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi inasikitisha kuona vyombo na humu nadhani imetajwa kwamba vinaingia vyombo 87 ambavyo vinakuja kuvua katika bahari kuu. Tusipokuwa waangalifu samaki watatoweka na tutakuwa hatuna rasilimali ya bahari ambayo italeta maendeleo katika nchi yetu. Tunapashwa kudhibiti vyombo hivi ambavyo vinakuja nadhani ni vyombo haramu, vingine ambavyo vinakuja kuvua katika bahari yetu. Na kama tunatoa vibali basi tuwe waangalifu kujua ni vyombo vingapi na tuna samaki kiasi gani kusudi samaki wasije wakavuliwa kwa wingi tukabaki hatuna chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi unaingiza kipato katika nchi yetu. Fedha nyingi zimepatikana kutokana na uvuvi katika maziwa yetu hasa Ziwa Victoria. Naomba Waziri

ahakikishe kwamba uvuvi katika Ziwa Tanganyika linawaongezea kipato wananchi wa Kigoma. (*Makofi*)

Tunao dagaa ambao ni watamu sana, ni wazuri wanapendwa lakini wananchi hawajapewa kipaumbele katika kupatiwa mikopo ya kuweza kuvua hao dagaa ambao wangesaidia kuingiza kipato kwa wananchi wa Kigoma. Kwa sababu ndiyo tegemeo letu kama alivyosema Mheshimiwa Mayonga jana kwa kuwa tumeshindwa kupata miundombinu ya barabara, tumeshindwa kupata miundombinu ya umeme, basi tunaomba tufikiriwe na tupewe kipaumbele katika uvuvi katika Ziwa Tanganyika. (*Makofi*)

Inasemekana kwamba samaki wamepungua na mimi nakubali. Lakini bado tuna uwezo wa kuweza kuendeleza sekta hii ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa kusudi ili kuinua kipato cha mwananchi. Tunao samaki wa mapambo ambao kama watapewa kipaumbele vile vile wanaweza kuongeza pato la mwananchi wa Kigoma. Naomba uvuvi utiliwe maanani kama sekta muhimu ambayo inaweza ikainua kipato cha mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa magogo. Naomba nimpongeze Mhesihmiwa Zakia Meghji kwa kuzuia magogo ambayo yalikuwa yanasafirishwa kwenda nchi za mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kamati tulimshauri Mheshimiwa Waziri kwa sababu kila tulipokuwa tukitembea tunaona magogo yanazidi kusafirishwa kwa wingi, na hii inatishia uharibifu wa mazingira na nchi inaweza ikageuka kuwa jangwa kwa ukataji wa magogo. Inachosikitisha zaidi siyo hawa wafanya biashara wadogo wadogo ambao wanatishia ukame katika nchi yetu ni wafanya biashara wakubwa wakubwa ambao tumeambiwa kwamba hata hawa wafanya biashara wadogo wadogo wanafahamu wafanya biashara wa nchi nchi za mashariki hasa Wachina ambao wanakwenda kwa migongo ya wananchi wa humu humu Tanzania hasa wakubwa, vigogo kama magogo. (*Makofi*)

Tunaomba sana hawa Wachina ambao yanasafirisha magogo, ambao wanunua magogo, basi wayanunulie kule Dar es Salaam waletewe na wananchi wadogo wadogo. Siyo kwamba wenyewe waende msituni na kukata na kupima magogo na kukata kwa mashine. Wanachukua magogo yanayoruhusiwa na yale ambayo hayaruhusiwi. Tunaomba Serikali idhibiti ukataji miti wa namna hiyo. Na wale ambao wameisha chukua magogo ambayo yako Dar es Salaam, mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwamba hawa ambao wamechelewesha na meli hao waruhusiwe kuchukua magogo yao. (*Makofi*)

Lakini aangalie kama kuna magogo ambayo hayakuruhusiwa ambayo yamekwenda kwa njia za panya haya yasiruhusiwe, yabaki hapo hapo, yapigwe mnada, yaweze kusaidia humu humu nchini. Yale magogo ambayo ni halali waruhusiwe kupelekwa. Lakini vile vile hao wafanya biashara wadogo wadogo ambao walikuwa na magogo yao huko porini ambayo kwa kweli muda wao labda ulikuwa haujaisha kwa

sababu ya ukosefu wa mabehewa hao vile vile waruhusiwe kusafirisha magogo lakini wale ambao kwa makusudi mazima wamekata magogo wakati wanajua kwamba muda wao umekwisha, basi hayo magogo yasiruhusiwe kusafirishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijahitimisha kuipongeza Mikoa ya Tanga, Mwanza na Mikoa mitatu ambayo nimeona katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri imefanya vizuri kwa upandaji miti. Ninaomba Mikoa mingine ambayo upandaji miti unaenda unapungua waweze kuiga mifano ya Mikoa hii kusudi tuweze kuendeleza upandaji miti katika mikoa yetu. Kupanda miti kunasaidia kuhifadhi maji ardhini, vile vile kutasaidia kuongeza kipato cha mwananchi, kwa sababu kwa wakati huu jinsi miti inavyokatwa kwa ajili ya mikaa kwa ajili ya mbao, tunazidi kuteketeza miti na mwisho tutakuwa hatuna miti ambayo itahitajika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na vile vile kwa ajili ya kuhifadhi ardhni na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Nyuki. Nimesema mara nyingi hapa kwamba Tanzania wananchi wameitia sana ufugaji nyuki. Lakini wana ukosefu wa utaalam. Ufugaji nyuki tulio nao ni ufugaji wa asilia. Hatuna madawa, hatupulizii madawa na wala hatuweki mbolea. Kwa hiyo, asali inayopatikana ni asali ambayo ina umuhimu wa peke yake. Na faida ya asali ni nyingi, inatumika kama dawa, inatumika kama chakula, na inaongeza nguvu mwilini. Kwa hiyo, tunaomba Wizara iwasaide wananchi kwa sababu waweze kusafirisha asali nchi za nje, unahitaji kufanya uchunguzi kwa Mkemia Mkuu. Na hela za uchunguzi ni gharama kubwa. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwasaide wananchi kuweza kufanya uchunguzi wa asali yetu na vile vile kuweza kuwaunganisha na wanunuzi wa nje kusudi asali inayopatikana nchini isipotee bure na iweze kuwaongeza kipato wananchi. Baada ya kusema hayo Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja ya Mheshimiwa Waziri mia kwa mia.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote niungane na Wabunge wenzangu na wananchi wote wa Tanzania kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki kwa kupotelewa na mpendwa Mbunge wao Marehemu Comrade Capt. Kasapila, Mungu ailaze roho ya Marehemu mahala pema peponi, na Mungu awafariji wanafamilia maana wote tulishuhudia mshtuko ambao uliwapata wao hata sisi Wabunge tuliopo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Wizara yake ikiongozwa na Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi wetu, kazi kubwa ya Wizara hii ni kulinda na kuhifadhi maliasili ya Tanzania. Naipongeza kwa kuwa inatekeleza mambo yafuatayo kwa dhati kabisa. Kuhifadhi maliasili yetu na kulinda wanyamapori ambao ni vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuitangaza nchi yetu sehemu mbalimbali ulimwenguni. Tanzania sasa inafahamika mpaka hata Urosi ambapo ni soko moja geni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe pongezi za dhati kabisa Mheshimiwa Waziri kwa hatua aliyochukua ya kudhibiti uvunaji ovyo wa magogo. Kwa kweli kazi hii ilihitaji ujasiri. Siku ile nilicheka, yule kipanya alisema vizuri kuwa: “Askari wengine wa Miamvuli wangefanya hivi tungepiga hatua’ kwa hiyo lazima tumpongeze sana kwa kazi yake nzuri anayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, napenda kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo. Moja, katika uvunaji wa magogo, nakubaliana na wenzangu kwamba wale ambao magogo yao tayari yako bandarini, yamechunguzwa basi waruhusiwe kuyasafirisha ili waweze kupunguza makali ya maisha. Lakini sikubaliani kabisa kwamba kibali kiendelee kutolewa kwa miezi mitatu au sita ijayo. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunafunga *Pandora’s box* hata wale ambao walikuwa wameacha sasa wataanza upya na Serikali itakuwa inajikanyanga, itageuka jiwe ambapo siyo tabia ya Waziri Zakia Meghji wala sio tabia ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Nashauri kabisa uwepo msimamo wa dhati kukagua makontena yote yaliyo halali yasafirishwe kwa sababu wamechelewa kwa bahati mbaya, *deadline* ilikuwa tarehe 30 June lakini imewafikia mpaka hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili ni kwa Halmashauri zote hapa nchini. Wavuna magogo hawa walikuwa wanapitia katika Halmashauri zetu na Maafisa Maliasili wetu katika Halmashauri walikuwa hawasimamii kwa dhati. Pamoja na kwamba tutatupa lawama Wizarani lakini Halmashauri nayo ina mzigo wa kubeba hasa sasa wengi tunapodhani kwamba tumenyimwa vyanzo vingine vyaa mapato basi tunaona kuwaacha watu wavune magogo ni moja ya njia ya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa napinga na mpaka leo napinga. Nilifika kwenye Halmashauri moja iko katika Mkoa wangu wa Lindi nikakuta magogo yamejaa. Nikamuuliza Afisa Maliasili anasema aah, si kibali kimetoka Wizarami. Nikamuuliza wewe huna kauli hapa? Anasema, tunayo kauli. Mnapata shilingi ngapi? Anasema tunapata milioni mbili. Magogo yamejaa, yametapakaa kila kona ya bandari lakini yule bwana alikuwa hajali. Namuuliza umepima na umethibitisha kwamba magogo haya ndio *permit* walijopewa? Anasema aah, ukiangalia hivi tu kwa macho unaridhika. Kwa hiyo, sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana na Madiwani tunao wajibu kuhakikisha Maafisa Maliasili wanafanya kazi zao sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo napenda kuchangia ni suala la utalii. Nimesema kazi kubwa inayofanya na Wizara hii ni kulinda na kuhifadhi maliasili ambayo ni vivutio vyaa utalii. Utalii huu unavutia wageni wa nchi mbalimbali. Asubuhi kuna mmoja alisema kwamba sisi tunazingatia zaidi *quality* kuliko *mass*. Alishauri tungefanya utalii wa *mass* ili watu waingie tu waingie kama wanavyotaka kama wanavyofanya nchi jirani tungepata fedha zaidi.

Mimi naisifu Wizara na mashirika yote yanayosimamia utalii kwamba kwanza wanasimamia *quality* ya utalii ambao unaweza kupatikana ili iwe kivutio. Maana ukifungulia watu waingie tu waingie kwa *mass* utaponda Maliasili yote, utakanyagakanya nyasi zote, wanyama watakosa chakula na wanyama watakukimbia. Kwa hiyo, mimi nasema *quality tourism* ni jambo muhimu na lazima tulisisitize ili iwe kivutio kikubwa kwa nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuperomoko kwa utalii sio kwa sababu Tanzania ni *very expensive destination*, hapana, ni kwa sababu ya vita vinavyoendelea huko ulimwenguni. Bahati mbaya watalii wetu wengi kutokana na historia ya huko nyuma, bado wanapitia nchi jirani ndio wanaingia kwetu. Lakini sasa kwa jinsi Wizara hii inavyojitangaza nje, nina hakika wengi nao wanaweza kufanya *destination Tanzania*, wakaja moja kwa moja Tanzania badala ya kupitia nchi jirani. Kule kupitia nchi jirani ndio kunatukwamisha mpaka tunakosa mapato mengine ndio maana wengi wanatua Arusha kuliko miji mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivutio vya Tanzania sio Mlima Kilimanjaro peke yake, tuna wanyama sehemu mbalimbali, tuna hifadhi za *Selous*, tuna hifadhi za Ruaha, imeanzishwa Saadan sasa, tuna *coastal area* ambayo nayo inakuja juu kama maeneo ya Mkoa wa Tanga pale na Bagamoyo. Kwa hiyo, Tanzania vivutio ni vingi mno. Napenda nishukuru kabisa kwamba hata Mkoa wa Lindi sasa unafahamika katika ramani ya ulimwenguni kwa vivutio vya Kilwa ambavyo vimekuwa urithi wa Kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutegemea utalii wa nje, napenda kuwahimiza wananchi wa Tanzania na sisi tujitokeze, tukaangalie vivutio tulivyonavyo sisi wenyewe humu nchini. Maana wengine humu si ajabu tunaona simba kutokana na *video*, kwenye picha lakini hatujafika tukaona simba wanavyokaa msituni wanavyokuwa kivutio. Wanaweza kuja hata Mchinga pale wanaweza kuona simba lakini waangalie asiwararue, tunataka waende kwenye hifadhi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiingilio kwa Mtanzania ni Sh.1,500. Mtanzania kitakachomshinda ni namna ya kuzunguka ndani ya hifadhi. Ushauri wangu kwa Wizara na mashirika mbalimbali wangeandaa magari maalum ya kuwasaidia Watanzania wanaofika kwenye hifadhi zile kwa njia mbalimbali ili waweze kuzunguka ndani ya hifadhi na kiwango chao cha kuwatoza kisiwe kikubwa sana kama wanachotozwa wageni. Kwa njia hiyo tutaweza kukuza utalii wa ndani ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine katika Afrika kama Afrika ya Kusini utalii wao mkubwa ni wananchi mle mle ndani, ndio wanachangia zaidi kwa kutembelea hifadhi zao mbalimbali. Hata nchi za wenzetu zilizoendelea *America* na wapi wanakuja huku lakini wengi wao wanakuwa watalii nchini mwao zaidi. Kwa hiyo, na sisi tujifunze utamaduni huu. Kwanza itatupa muda wa kupumzisha *tension* ya shughuli zetu mbalimbali, tunganeza sisi Waheshimiwa Wabunge tuonyeshe mfano ili wananchi wengine wa Tanzania watufuate. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kugusia kidogo juu ya mambo ya kale. Kule kwetu Kilwa kama nilivyosema tayari wameshaanza kuhifadhi maeneo yale na imekuwa kivutio kikubwa cha utalii. Lakini siku moja nilipita kule Iringa ambako alizikwa marehemu Chifu Mkwawa eneo lile liko ndani. Ninashauri Wizara waweke vibao na watengeneze barabara ili wageni waweze kuona maeneo yale ambayo ni Mambo ya Kale lakini ni kivutio kikubwa vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza vivutio hivi vya kale kama Kilwa Kisiwani, Songo Mnara na kadhalika, Wizara hii inahitaji ushirikiano wa Wizara nyingine mbalimbali hasa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuendeleza viwanja vya ndege na Wizara ya Ujenzi kwa ujenzi wa barabara. Kwa mfano kiwanja chetu cha Kilwa, kweli ni kizuri lakini *reception* mahali ambapo wageni wanashukia *literary* hakuna. Sasa hivi pale Kilwa ndege zinazokuja ni nyingi na mji ule umeanza kuamka vizuri sana, ninaomba basi Wizara zinazohusika zichangie ili kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika utalii, napenda kuzungumzia yafuatayo. Balozi zetu pamoja na kwamba tunasema hawana uwezo lakini wengine wameonyesha mfano. Hapa napenda nichukue mfano wa Balozi wetu wa Urusi, Balozi Patrick Chokala kwa jinsi anavyojishirikisha kikamilifu katika kuitangaza Tanzania na kushirikiana na Watanzania wanaokwenda kuitangaza nchi yetu wanapofika nchi ya Urusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi Chokala *last time* nimeshuhudia ametengeneza bendera ndogo ndogo za Tanzania akawapa washiriki wa mabanda yote, maana kulikuwa na washiriki wa upande wa Serikali na *tour operators*. Kila *tour operator* alipewa bendera ya Tanzania ili aonyeshe kwamba anaiuza Tanzania. Sasa mfano huu ulioonyeshwa na Balozi Chokala ungeigwa na Balozi nyingine ili na wenyewe wasaidie hawa washiriki wa maonyesho wanaokwenda sehemu mbalimbali ili na wenyewe waonekane kwamba wanashiriki.

Sitaki kutaja nchi nyingine ninasema mfano mzuri niliouona sehemu nyingine sijaona, mfano huu ningeweza kushauri kwa sababu kazi hii ya kutangaza nchi ni *integration* ya Wizara zote, basi Wizara ya Mambo ya Ndani ihimize Balozi nyingine waige mfano wa Balozi Patrick Chokala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuomba Halmashauri zetu hasa zile zinazopakana na hifadhi zetu za wanyamapori, misitu, hifadhi za *Selous* na kadhalika wawahamasishe wananchi wajue umuhimu wa kuhifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naipongeza Wizara. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kongwa, napenda nianze kwa kutoa salamu za pole na rambirambi kwa wananchi wa Mbeya Vijiji kwa kuondokewa na Mbunge wao Ndugu yetu, Mheshimiwa Mwalyego, kwa wananchi wa Ulanga Mashariki kwa kuondokewa na Mbunge wao, Comrade Kasapira na kwako wewe Mheshimiwa Waziri na familia yao kwa kuondokewa na mzee wetu, Profesa Meghji tuliyejkuwa tumemzoea sana. Naomba wote hao Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri amekuwa akiifanya akisaidiwa na Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote katika Wizara hii na pia natoa pongezi kwa hotuba nzuri ilioandaliwa na kusomwa mbele yetu leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikisimamia vema majukumu yake kama ilivyoainishwa kwenye hotuba hii ya kuhifadhi, kulinda rasilimali za maliasili na hasa wanyamapori, misitu, samaki katika nchi yetu. Viashiria mbalimbali vinaonyesha kwamba kazi ambayo imekuwa ikifanyika ni nzuri. Kwa mfano idadi ya wanyamapori imekuwa ikiongezeko. Tutakumbuka miaka ya 70,80 wanyama hasa wakubwa kama tembo walipungua sana sana lakini sasa hivi wanaongezeka kwa kasi inayotia moyo katika karibu hifadhi zote nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamefanyika mapitio ya sera mbalimbali katika Wizara hii, marekebisho ya sheria mbalimbali yamekuwa yakifanyika kama mwaka juzi tuliletewa Sheria ya Misitu hapa *Forest Conservation Act, 2002* na natumaini sasa hivi imeanza kufanya kazi, najua kwamba Sheria ya Wanyamaporu inafanyiwa kazi huenda mwezi Oktoba tukakutana nayo hapa. Hivi vyote ni viashiria kwamba mambo mazuri yamekuwa yakifanyika, ni mengi kuyaeleza yote yamatiliza muda wako Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa haraka haraka ni kwamba sasa Sheria za Ngorongoro na *TANAPA* nazo zianze kuangaliwa taratibu ili nazo zije zifanyiwe marekebisho katika siku zijazo ili na zenewe ziweze kuendana na hali halisi ya mahitaji yaliyomo katika Sera ya hifadhi ya Wanyamaporu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuitia ile Sheria *Forest Act, 2002* tuliypitisha hapa imekuwa ikisisitiza kuhusu kuwashirikisha wananchi vijijini ili waweze kupata uwezo wa kusimamia, kutenga, kuhifadhi na kulinda maliasili zao kwenye vijiji vyao na vile vile kuwaelimisha wananchi kuhusu uharibifu wa mazingira na matatizo mbalimbali yanayohusiana na mazingira.

Lakini Wizara imekuwa ikifanya kazi sio kwa ukaribu sana na TAMISEMI ambao ndio wenye majukumu kule vijijini. Tungeomba ukaribu huo uongezwe kiasi kwamba Idara za Maliasili Wilayani zianze kupata msaada unaohitajika ili waweze kutekeleza jukumu hili muhimu la hifadhi mbalimbali za vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kazi hiyo iweze kufanyika kwa mfano katika Wilaya ya Kongwa, naiomba Wizara na hasa Profesa Iddi, Mkurugenzi wa Misitu kama itawezekana kutupatia pikipiki moja ili kazi hii iweze kufanyika vizuri sana ya kuainisha misitu yote ya hifadhi ya vijiji ili iweze kuhifadhiwa haraka. Kama mtakavyokumbuka kwamba maeneo haya ya kati ni makame, wenyewe wanasema ni *ecosystem* ambazo ni *fragile* ukiziachia zinaharibika kwa haraka sana na kurudi kwake ni kugumu kwa hiyo lazima tuwahi tuweze kuhifadhi kama tuna nia ya kupata uhifadhi wa maana katika nchi zetu ukiacha hifadhi zile za Kitaifa lakini hifadhi za vijiji nazo ni muhimu sana zinahitaji usaidizi wa aina yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 46 kuna jedwali pale kuhusu mauzo ya bidhaa za misitu na nyuki katika masoko ya nje. Bidhaa ya kwanza iliyooredheshwa pale ambayo ni magogo utaona kwamba kwa mfano mwaka 2000/2001, magogo yaliyosafirishwa yalikuwa mita za ujazo 1724 miaka minne baadaye 2003/2004 magogo yaliyosafirishwa ni mita za ujazo 8529. Kwa hiyo utaona ongezeko la usafirishaji wa magogo kwenda nje limeongezeka mara nne, ni kiwango kikubwa sana katika muda mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunakubaliana kabisa na hatua ambazo Mheshimiwa Waziri amezichukua kuhusiana na masuala ya magogo kwa sababu uvunaji huu ulishafikia hali ya hatari. Mimi mwenyewe nilijionea katika maeneo ya Rufiji, Kilwa, Liwale hali ilikuwa ni mbaya sana mpaka ikawa ni issue kwenye Kamati yetu kwamba kwa nini hali inakuwa hivi na tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuchukua hatua maana yake hilo ni ulikuwa haungalii idadi, aina ya miti, wala size ya mti sasa jambo hilo ni hatari sana. Kwa hiyo, tunaafiki kabisa hatua ambazo Mheshimiwa Waziri umechukua na tunajua kabisa Profesa Iddi, Mkurugenzi wa Misitu, ni mtu mwadilifu sana, safi kabisa, wako watu mahali ambao wanajaribu kufanyafanya haya mambo ya vurugu, naamini kabisa uwezo wa kuwadhibiti hao upo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa kama nilivyosema mwanzoni litakuwa liko TAMISEMI maana kuna baadhi ya leseni zinakatwa kule TAMISEMI kwenye Wilaya mbalimbali ndio wanatoa vibali vyta kukatakata miti haraka haraka ili Halmashauri zipate pesa bila kuangalia hatma ya uhifadhi na mahitaji ya miti katika nchi yetu. Sasa hilo nalo mliangalie namna ya kudhibiti kuanzia kule TAMISEMI ambako ndio kunasababisha ukataji mkubwa sana wa miti kwa maana ya Idara za Maliasili kwenye Halmashauri zetu za Wilaya. Maafisa Misitu walioko huko ambao badala ya somo la uhifadhi wao wameshikilia somo la kuvuna tu peke yake, inabidi waangaliwe vizuri, wazuri wapewe semina, wasiofaa kabisa basi tuondokane nao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika *item* hiyo magogo, mambo mawili wenzangu walisema na mimi niliyarudie tu kidogo, liangaliwe sana suala la wageni wanaokwenda hadi vijijini. Wageni hawa wakati mwingine hawaendi wao wanawatumia Watanzania kwa sababu ya umaskini wao kuanzisha vikampuni ambavyo ni vibaraka tu. Kwa hiyo, hili nalo litazamwe vizuri na wale Watanzania wanaotumiwa na wageni tujaribu kuangalia namna ya kuwadhibiti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama walivyosema wenzangu kwa wale ambao tayari wana leseni halali, walikata magogo kwa uhalali, magogo yao yako msituni, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri na Wizara mtaangalia namna na utaratibu wa kuwasaidia watu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sasa naenda ukurasa wa 61, ukurasa ule unaonyesha makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha mwaka 1992-2000 hadi 2004/2005. Utaona katika Idara karibu zote za Wizara hii, Idara ya Wanyamapor i imekuwa ndio inaingiza kiwango kikubwa sana. Kwa mfano mwaka 2004/2005 wao wanakadirwa kukusanya bilioni tisa na milioni mia nane na kitu, jambo ambalo ni zuri. Ukienda ukurasa wa 62 kwenye upande wa matumizi utaona kwamba katika mwaka 2003/2004, Idara hii ilipewa bilioni 7, mwaka 2004/2005 ile fedha ambayo wanatakiwa kupewa imepungua wamekadiriwa kupewa shilingi bilioni 6.5. Nafikiri ni vizuri wale wanaokusanya vizuri kama Idara hii ya Wanyamapor i na wao wakaendelea kuangaliwa vizuri zaidi kuliko tena bajeti zao kupungua kwa sababu nina hakika kabisa idadi ya hifadhi za wanyamapor i zimekuwa zikiongezeka na mahitaji yamezidi kuwa ni makubwa sana, basi tusiwapunguzie bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nizungumzie habari ya watumishi wa wanyamapor i walioko porini kwenye hifadhi za Taifa na kwenye mapori ya akiba, *national parks* na *game reserve*. Watumishi hao wanafanya kazi katika mazingira magumu kweli kweli. Ziko kada nyingi za watumishi hapa zimekuwa zikizungumzwa kwamba zinafanya kazi katika mazingira magumu lakini sijui kama wanazidi hawa, hawa wako kule porini kabisa, hakuna kijiji karibu, hakuna nini karibu, mbali kabisa na wanafanya kazi katika mazingira ya kuzungukwa na wanyama, mbung'o na matatizo mengine mengi. Juzi tumewakumbuka Walimu na Madaktari, naomba sana mama yangu, Mheshimiwa Mary Nagu, hebu wakumbuke na hawa wa hifadhi katika *aspect* ya mishahara ana marupurupu yao yaangaliwe kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni wachache sana, hizi mbuga ni kubwa kweli kweli, watumishi walioko pale ni kama watoto wakiwa walioko katikati ya hifadhi. Kwa kweli iko kila sababu ya kuongeza idadi ya watumishi katika kada hii ili watulindie dhahabu hii ya Tanzania ambayo tunaitegemea sana.

Maana tofauti ya maliasili hii ambayo anaisimamia mama Meghji ambayo ni *renewable natural resource* kwa maana wanyama hawa wanazaliana, ukiwatunza vizuri unaweza kuwa nao daima na ile maliasili ya Mheshimiwa Yona ya madini ambayo ukishachimba ndio imeondoka hiyo, hairudi tena, iko tofauti kubwa sana. Tuna wanyama kama faru leo wamepungua sana karibu hawapo kuwarudisha ni kazi kubwa kweli na ni gharama kubwa. Nakumbuka mwaka juzi walinunuliwa faru wawili *South Africa* wakaletwa Serengeti kule walipokelewa na Makamu wa Rais, marehemu Omar Ali Juma, faru wanapokelewa na Makamu wa Rais maana yake wameishi, hakuna. Kwa hiyo, wakishaisha kuwarudisha tena ni tatizo kubwa sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuangalie matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza sasa hivi ni historia kidogo inajirudiarudia. Kwa mfano walianza faru

wakawindwawindwa na majangili wakaisha, wamebakia wachache kweli. Kule mbuga za Kaskazini wakafuata mbwa mwitu, leo ukitaka kuona mbwa mwitu ni *Selous* na maeneo ya Kusini huku mpaka Tunduru kwa Mheshimiwa Naibu Spika unaweza kubahatisha kuona mbwa mwitu lakini Serengeti hata mtu akisema atakupa dola milioni 100 uzunguke mwezi mzima hutaona mbwa mwitu mmoja na walikuwa wengi kweli kweli. Simba ukaja ugonjwa wa kijingajinga tu karibu umalize simba wote kule Serengeti, sijui ulitoka wapi.

Sasa juzi tumeambiwa *flamingo* kule manyara wanakufa kwa maelfu. Sasa inaelekea kuna watu wanatuhujumu mahali au sijui kuna nini, naomba Wizara hebu angalieni haya mambo maana mbunga zetu ni nzuri dunia nzima na tuna majirani wengine ambaio sio wazuri sana isije ikawa kuna mbinu mbinu za kumaliza wanyama ambaio ni vivutio vizuri kwetu, vinavyosaidia kupata watalii wazuri zaidi ili wao waweze kufaidika na hali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho amezungumza Mbunge wa Serengeti hapa asubuhi, Dr. Wanyancha faida ambazo Wilaya yake inapata kutokana na wanyamapor wanajengewa shule za msingi, shule za sekondari kwa kushirikiana na wananchi, visima vya maji, malambo, barabara na kadhalika.

Mimi nilipata bahati ya kufanya kazi Serengeti katika *eco system* ile na hii kazi anayosema na mimi niliwahi kuifanya ndio maana hata jana niliposimama kuhusu *Ranch* ya Kongwa kidogo watu wa mifugo tunakuwa hatuelewani Kiswahili, huwezi kuwa na *Ranch* kubwa kama ile, 1/3 ya *District* ya Kongwa ni *Ranch* ile, haisaidii chochote, hakuna cha shule ya msingi hata bati mbili, hakuna cha nini cha nini, hivi sisi watu wa Kongwa tuendelee kuwa na kitu cha namna hiyo? Ndio maana nikasema iko pale kwa manufaa na mtazamo wa *NARCO*, ni lazima maeneo kama haya wananchi wafaidike nayo. Wizara ya Mifugo wanalo deni la kuwaambia wananchi wa *Kongwa justification* ya *Ranch* ile kuendelea kuwepo pale vinginevyo sisi wananchi hatuihitaji wanawenza kufuga mahali pengine. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa sasa hivi unapokuwa na eneo kubwa limetengwa kwa ajili ya mambo fulani fulani lazima wananchi wale ambaio wamekosa ile *opportunity, that's an opportunity lost to them*, ile *opportunity uliyo-lost* ile unairudisha kwa namna fulani ambayo ni ya manufaa kwa wananchi wale ili waipende ile hifadhi kuwepo kwake. Kwa hiyo, natoa wito sera hizi jamani zisiwe za Wizara moja Wizara nyingine ina sera zake tofauti sio vizuri, sera hizi ni za Serikali, Serikali ni moja, hifadhi ya wanyamaporinafanya mambo mazuri sana kwa wananchi walio jirani hifadhi za ng'ombe nazo zifanye mambo mazuri kwa wananchi jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kutokana na pengine dukuduku walio nayo wenzetu, wameomba angalau dakika tano, saba hivi wapate nafasi ya kuchangia,

kwa hiyo nitawapatia. Lakini pengine niwakumbushe tu kanuni ambayo inaweza kuhusika muda wa kusema Bungeni, kanuni ya 49(a), inasema: "Kila Mbunge anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15, usiozidi dakika 15". Sasa huu wa hawa Waheshimiwa wawili hautazidi wala hautafika huko. Kwa hiyo, nawapa dakika saba saba, naanza na Mheshimiwa Kone halafu Mheshimiwa Kwaangw'.

MHE. PARSEKO V. KONE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kuwapa pole familia ya Marehemu Capt. Kasapira na wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki na Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho ya Marehemu, Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi nzito anayoifanya. Nimpongeze Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa ufanisi na kwa kufuata ile wanayoita wataalam *Strategic Plan*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Wizara hii hasa *TANAPA* kwa kuanzisha Mfuko unaoitwa Mfuko wa Ujirani Mwema. Huu Mfuko ni kama alivyoeleza Mheshimiwa Wanyancha. Umebadilisha mtazamo wa wananchi kwa wanyamaporii kwamba sasa wanafaidi kuwa na wanyamaporii kuliko wakati ule ambapo wakiwa nao wanaona ni balaa. Lakini pamoja na pongezi na shukrani hizo kwa kifupi kwa sababu nimepewa muda mfupi nina yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa Marehemu Mwalimu Nyerere aliwahi kusema hivi: "Wizi mbaya kupita wote na mkubwa kupita wote ni kumwibia mwanao ambaye hajazaliwa". Kuharibu mazingira na kumaliza wanyamaporii ni kuwaibia watoto ambao hawajazaliwa. Nasema hivyo kwa sababu Wizara hii inajitahidi kwa hali ngumu sana kuhifadhi mazingira kwa ajili ya watoto ambao hawajazaliwa, lakini Watanzania wengine wao wenyewe ama kwa kutumiwa na wageni wanamaliza misitu na wanamaliza wanyamaporii. Najua Wizara hii itakuwa na kazi ngumu ya kufanya kazi hii peke yake hasa kwa sababu mbili, pamoja na jitihada zao. Kwanza hawana askari wanyamaporii wa kutosha, ni wachache sana. Kwa hiyo leo anayemsaidia Waziri wa Wizara hii ni Waziri anayehusika na Utumishi, nimwombe kabisa akumbuke Wizara hii waajiriwe askari wanyamaporii ili na sisi tusije kuhesabiwa kwamba tulishiriki kuwaibia watoto ambao hawajazaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika tatizo lingine kubwa ni suala la silaha, hawa askari wanafanya kazi katika hali ngumu. Kwa askari wa hifadhi ya Taifa *TANAPA* na hifadhi ya Ngorongoro wao wanatumia silaha za zamani, lakini majangili wanaopambana nao wanatumia silaha za kisasa. Mimi nafikiri Wizara inayohusika na kutoa leseni za silaha

ifikirie kuwapatia silaha kwa mfano *AK* 47, hiyo ingeweza kutumika kulinda hazina hii ambayo ndiyo hazina pekee ambayo tunaweza kupambana ua kushindana na nchi zingine za dunia hii ya sasa. Naomba pia Sheria ya Wanyamapori inayoandaliwa sasa kuletwa Bungeni, kwa kweli ilenge kabisa kukabidhi uhifadhi kwa wananchi na wananchi waone kweli hifadhi ni yao ndipo wataweza kushiriki vizuri katika kuhifadhi mali yetu hii tuliyonayo.

Mwisho, kwa kweli narudia hili la silaha kwa sababu bado nina dakika moja. Niliwahi kuuliza swali hili hapa Bungeni ikasemekana hii *AK* 47 ni silaha za kivita, lakini benki tunalinda kwa silaha kubwa kubwa. Sisemi silaha za kuwapa hawa askari zilingane na zile za kulinda benki, lakini zikaribiane kwa sababu wanyama watakapotoweka sijui sisi tunaweza kushindana na nini kingine katika dunia hii. Viwanda hatuna wala hatuna chochote kingine, lakini uhifadhi na utalii ungeweza kufidia pengo hilo la viwanda ambavyo hatuna. Naipongeza Wizara kwa hali inayojitahidi kuwalinda wanyama. Faru hawajawahi kupotea na sasa wanaongezeka pamoja na hali hiyo ngumu ya kutokuwa na uwezo wa vifaa na askari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na kwa niaba ya wananchi wa Babati Mashariki, naomba niungane na wananchi wa Ulanga Mashariki katika kuomboleza kifo cha mwenzetu Mheshimiwa Theodos Kasapira ambaye tumekuwa naye hapa kwa muda mrefu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mfupi nataka niseme hoja yangu kwa sentensi kama mbili, tatu au nne tu. Nitialekeza kwenye kifungu Na. 25, ukurasa wa 14, pale Waziri aliposema sentensi ya mwisho kwenye *paragraph* hiyo kwamba: "Mashamba Na. 1 mpaka Na. 3 ya Manyara kuwa sehemu za hifadhi na kwamba Wizara itawasilisha Muswada kwa ajili ya kuanzisha maeneo hayo". Kwa ufupi wa maneno yale yaliyokuwepo pale ambayo hayakuzingatia maslahi ya wananchi wa Wilaya ya Babati, wananchi wa Jimbo la Babati Mashariki na wala maslahi ya wananchi wa Kijiji cha Mayoka. Nataka nitamke rasmi kwamba tulikubaliana kuanzisha majadiliano juu ya maeneo hayo kwa sababu ya migogoro iliyokuwepo na Mheshimiwa Waziri aliwahi kuleta hapa Azimio la kutaka kupanua hifadhi hiyo. Mimi nikaomba kwamba sehemu hiyo ina migogoro, turudi kwanza tutatue na tushirikiane na *TANAPA*. Ushirikiano ule uliishia mahali na haujaendelea mpaka jana. Sasa leo nilipoona kuna sentensi inayoonyesha kwamba mashamba Na. 1 mpaka Na. 3 ya Manyara yatakuwa sehemu ya hifadhi ya Ziwa Manyara bila mawasiliano zaidi na Waziri anafahamu kwamba Jimbo la Babati Mashariki ndiyo *custodian* wa Hifadhi ya Tarangire kwa sehemu kubwa vile vile na sehemu ya Manyara, nashangaa. Kwa hali hiyo basi natamka wazi kabisa kwamba siungi mkono hoja hii na nitataka kupata maelezo ya kina kwa sababu yanahusu maslahi ya wananchi wa Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. SHAMIM P. KHAN: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kusema kwamba, naunga mkono hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kumudu Wizara hii akisaidiana na Katibu Mkuu na Wataalam wote.

Nimeridhika na jinsi Wizara hii inavyotangaza nchi yetu, hususan vivutio kama vile Mlima Kilimanjaro, Hifadhi zetu na kadhalika nje ya nchi. Wengi sana wanaelewa kwamba, mlima huu uko Tanzania na siyo nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama uwezo upo, basi ninashauri, *documentaries* zionyeshwe katika ndege (*Air Lines*) maarufu kama vile *Gulf Air*, *Emirates* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi ziongezeke kutunza makumbusho yaliyoko Ujiji - Kigoma. Yule *guide* (*Singing Guide*) anafanya kazi nzuri, lakini nashauri kuna haja ya kuandika vitabu vingi tu ili Watilii wa ndani na nje wafahamu kwamba, Dr. David Livingstone, alisaidiwa na Susi na Chuma katika misafara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua *status* ya *Mikumi Wild Life Lodge*. Je, huyu Mwekezaji ameleta maendeleo ya kutosha kufuatana na Mkataba?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, sasa *Kilimanjaro Hotel* imeanza kupata sura nzuri. Mwekezaji huyu angalau kwa nje ameonyesha kazi nzuri sijui kule ndani anaendelea kufanya maajabu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji tuwaenzi, kwani hata Ilani ya Uchaguzi ya CCM, inasisitiza kwamba, Sekta Binafsi ni wadau muhimu katika kuleta maendeleo katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusitisha zoezi la uvunaji wa magogo. Watekelezaji sasa wawe makini la sivyo, njia za panya zitatumika kusafirisha magogo. Watekelezaji Wakuu ni wanakijiji, wapewe semina ili waelewe umuhimu wa kutunza rasilimali ya nchi. Mabwana miti nao wawe makini, wababaishaji wachukuliwe hatua zinazostahili. Sisi wachaguliwa kutoka ngazi ya vijiji hadi ngazi za juu, tusiingilie kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera zifuatwe ipasavyo. Tusiwe wa kwanza kupinda sera zetu. Wapigakura wetu wakielimishwa, wanafahamu. Kazi yetu ni kuwaongoza bila ya kukiuka taratibu na Kanuni zetu.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa

namna hotuba yake ilivyoandaliwa. Ni bajeti maridhawa, yeny kina na yeny upeo wa kuendeleza uhifadhi Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wasaidizi wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Nasema, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kubuni Mpango wa *WMA*, kwani mpango huu utakuwa changamoto kwa kupanua wigo wa uhifadhi nchini hasa ikizingatiwa zaidi, kwenye maeneo yaliyo karibu na Hifadhi za Taifa. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwa hili kuwa, Kamati ya ushauri kwa ngazi ya Wilaya, imejielekeza sana kuwa na watumishi wengi na kuacha Viongozi/Wanasiasa nje, jambo ambalo litaleta kutoaminiana na Wajumbe wa Serikali na Wanasi. Naomba basi kama inawezekana wawepo Wajumbe wawili, watatu wa kisiasa, kama vile Madiwani wawili wa kike na Diwani mmoja wa kiume. Naomba hili lizingatiwe, yaani katika Kamati ya ushauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naishauri sana Wizara hii kwa suala zima la utafiti iongeze nguvu zaidi ili uhifadhi wetu uweze kuboreka na usitegemee watafiti kutoka nje ya nchi. Nasema hivi kwa kuwa kituo chetu cha Utafiti cha *TAWIRI* mwaka huu wa 2004/2005 bajeti yake ni jumla ya shilingi milioni 50 tu wakati michango hutolewa na sehemu tatu ambazo ni *TANAPA* shilingi milioni 60, *Ngorongoro CAA* shilingi milioni 40 na Idara ya Wanyama Pori shilingi milioni 100 na kufanya jumla ya bajeti ya *TAWIRI* kuwa shilingi milioni 200 kwa miaka ya nyuma. Kwa mwaka huu bajeti yake imeishia shilingi milioni 50 tu. Nimeangalia bajeti ya *TAWIRI* ya mwaka huu, sikuona ongezeko lolote na kuona fungu dogo mno, inasikitisha. Uhifadhi unaendeana na Utafiti wa mara kwa mara. Utafiti wa watu kutoka nje ni tegemezi mno. Tuongeze bajeti ya utafiti wetu. Watafiti wapewe usafiri na vitenda kazi.

Tatu, naomba kushauri kuhusu suala la kupanua wigo wa uhifadhi nchini kama vile, kwenye miji yetu mikubwa kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Morogoro na Tanga, uwepo mpango madhubuti wa kutenga maeneo ya uhifadhi kama hekta 10 - 15 ili kuanzisha utalii wa kutembelea Wananchi wetu kwa kulipia. Lakini kwa watoto wa shule waingie na kuona bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itawapa watoto hamasa zaidi na kuamsha ari ya uhifadhi kwa siku za usoni. Maeneo hayo wahifadhiwe wanyama wa aina mbalimbali, miti ya aina mbalimbali, ndege wa kila aina, majoka na samaki wa kila aina. Mpango kama huo utapanua sana wigo wa uhifadhi hapa nchini na ndiyo maana ya kurithisha watoto wetu urithi wa nchi yao. Elimu ya kusoma, kuhadithiwa bila kuona ni elimu nadharia. Elimu ya kuona kitu au kiumbe ni elimu ya vitendo kwani elimu hiyo, hubaki daima akilini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mpango huu uandaliwe katika miaka ijayo. Jamii yetu kwa siku zijazo itaongezeka sana na kushindwa kupata elimu ya uhifadhi na

utunzaji wa mazingira. Hivyo basi, yafaa kwa sasa kuanza maandalizi ya uhifadhi karibu karibu. Kuona ni kuamini, kuona ungali mtoto, kile ulichokiona, kitakaa daima kichwani. Tukuze utalii wetu kwa Wananchi wetu wa ndani kuliko hivi sasa utalii wetu ni wa kutegemea sana watalii kutoka nje. Tuanze na vituo vikubwa kupeleka watu wetu kwenye Hifadhi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuiingizia nchi hii fedha kupitia sekta ya maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara izingatie yafuatayo:-

- Ushirikiano uwepo kati yake na Wizara ya Madini ili leseni za utafutaji/uchimbaji madini usiingie ndani ya Hifadhi kwani wachimbaji huishia kuhatarisha maliasili zilizoko maeneo husika.
- Wizara ijihushe kikamilifu katika utoaji wa vibali vyatya uchomaji mkaa na uvunaji wa magogo hasa kwa wageni wasio na uchungu wa mazingira ya nchi yetu.
- Wananchi wahamasishwe kutembelea vivutio vyatya utalii kwani ni kwa njia hiyo tu wanawenza kuthamini na kutunza maeneo ya utalii.
- Asilimia 25 inayotolewa kama *royalty* ya uwindaji isicheleweshwe Wizarani ili isaidie maendeleo ya Halmashauri husika.
- Sheria za ufugaji nyuki na misitu hazijafahamika ipasavyo kwa Wananchi kazi ya ziada ifanyike ili kuwaelewesha nini wanatakiwa wafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo muhimu ya kihistoria yasibomolewe, kwa mfano, nyumba za soko la watumwa la Mikindani zimebekewa X, zisibomolewe ili kutunza historia ya eneo husika na nchi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya kihistoria Mkoani Kigoma kama Soko la Watumwa na *Livingstone Memorial* vitunzwe na watu wahamasishwe kujenga mahoteli maeneo hayo kama ilivyo Mikindani, Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wavuvi wa sangara wapewe msaada wa kupewa bei ya samaki wa minofu ambayo ni *predictable* badala ya kutegemea huruma ya wenye viwanda tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema na naunga mkono hoja.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nawatakia utekelezaji mwema wa malengo waliojiwekea kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri kuwa, mabaki ya Kaole yajengewe yawe ndani kama China ilivyojengea mabaki ya *Terra Cotta Warriors* huko Xian. Inavyoonekana kutokana na *weathering*, maandishi ya Kurani kwenye zile *column* yamefutika, yakiendelea kuwa nje hata zile *column* zitaanguka. Sehemu yenyewe haitunzwi vizuri. *Column* za magofu ya Kaole zinafanana pia na zile za *TAT MAHAL* huko *Agra India*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wataalam wazoefu wakaribishwe Kaole kuja kufanya utafiti zaidi. Ninaomba mambo ya kale yote yawekewe majengo ili kuzuia uharibifu. Pia UNESCO na Mashirika yanayohusika yahusishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji ya Kilwa/Bagamoyo na kwingineko, sharti itunzwe kwa histori yetu. Nawapongeza Watendaji wote wa Wizara na nawatakia utekelezaji mwema wa malengo waliojiwekea kwa mwaka 2004/2005.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwa makini hotuba hii, naunga mkono hoja.

Kwanza, nampongeza sana Waziri kwa kusimamia vizuri shughuli za Wizara kwa bidii na uadilifu mkubwa. Nampongeza Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote.

Pili, Wizara itapaswa kupambana kwa nguvu zake zote na ukataji miti ovyo na usafirishaji wa magogo, naipongeza Serikali (Wizara), kwa kulivalia njuga tatizo hili. Sisi kama Bunge, tunaunga mkono hatua hizo, pia uchomaji moto wa misitu na hasa mkaa ambao kwa sasa ni biashara kubwa kupita kiasi na vilevile udhibiti wa Maofisa ambao wanajinuifaisha kwa kutumia nafasi zao kuhujumu maliasili hasa mikaa na magogo. Hata hivyo, tungependa tupongeze juhudhi na hatua zinazoendelea kuhusiana na suala hili. Kuhusu biashara ya magogo na uchomaji moto misitu na mkaa kulikokithiri hivi sasa, ni vyema ikatungwa sheria itakayomruhusu Waziri na Watendaji kutoa adhabu za papo hapo au kumpeleka mhusika Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafutaji wa maeneo na aina nyingine ya utalii katika nchi. Tutumie Jiografia ya nchi yetu kutafuta maeneo mengine mapya yanayovutia, kwa mfano, Kusini mwa Tanzania na kadhalika, kwa mfano, ziko kazi za mikono ya binadamu au *physical geography*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa hakika Wizara nzima kwa ujumla, imefanya kazi ya kuigwa mfano. Nawatakia kila la kheri.

MHE. GEORGE F. MLAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitamke kuwa, naunga mkono hoja hii moja kwa moja. Vilevile nampongeza sana Mheshimiwa

Waziri, kwa uongozi wake mahiri na wenyе tija, pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote wa Idara mbalimbali za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara hii na Idara ya Mambo ya Kale, kwa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha kumbukumbu na habari cha Isimila - Iringa. Kituo hiki kiko katika Jimbo langu la Kalenga Wilaya ya Iringa Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hiki kikiwa *fully operational*, ni wazi kabisa kitasaidia sana kuvutia watalii wa mambo ya kale. Bila shaka kituo hiki kitatangazwa nje ya nchi ili kifahamike ipasavyo. Wakati huo huo natumaini *Transformer* ya umeme itakayowekwa hapo kituoni, itasababisha umeme utawanywe kwenye Kijiji cha Wenda ambacho kiko pembezoni mwa Kituo cha Isimila. Hali hiyo italeta hamasa kubwa na eneo hili litakuwa na biashara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri azidi kutusaidia kwa kuielekeza Idara ya Mambo ya Kale ikamilishe ukarabati pale Kalenga Kijiji cha kihistoria ambapo fuvu la Mtwa Mkwawa limehifadhiwa. Itapendekeza sana ikiwa watalii watakuwa wanafika kwanza Isimila, halafu Kalenga na hatimaye kufika *Ruaha National Park*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nitoe maoni juu ya Maliasili, hususan misitu. Hali ya uchomaji misitu nchini inatisha sana. Baada ya miaka mingi ya uchomaji misitu hauonyeshi hali hii ya hatari inapungua. Lazima tuokoe misitu yetu ili kuokoa maisha ya vizazi vijavyo. Kama ambavyo kwa uhifadhi wa wanayama tunao Askari hodari (*Garme Rangers*), vilevile tuunde jeshi dogo, jasiri na *mobile*, yaani *Forest Rangers*. Askari hawa wawatafute wachomaji wa misitu na ikibidi wapambane nao na kuwakamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hawa vilevile wawahamashe wanavijiji kupitia Serikali za Vijiji, wawe wanazima mioto hiyo haraka iwezekanavyo. Zaidi ya kuwa na *Forest Rangers*, vilevile Wizara ianzishe Kitengo cha Uendeshaji Mashtaka, yaani *Forest Public Prosecutors*. Hii itarahisisha wachoma mioto wakikamatwa wanakuwa *prosecuted* mara moja bila kutegemea *Police Public Prosecutors*.

MHE. OSCAR T. MLOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika kuchukua nafasi hii kushiriki katika kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ningependa nianze kwa kutamka kuwa naiunga hoja hii mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yake ni makini na imechambua kwa kina maeneo yote muhimu katika kukuza Utalii na kuzienzi Maliasili tulizonazo ambazo ni hazina tuliyopewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, ningependa kuulizia ahadi ambayo Mheshimiwa Waziri, alittoa siku za nyuma takriban miaka miwili iliyopita kuwa Milima ya Uluguru ambayo ni chanzo muhimu sana cha maji yanayotumiwa na Mikoa ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, itawekwa kwenye Mpango Kamambe wa Serikali wa kupata hadhi ya Hifadhi ya Taifa. Naulizia hili kutokana na umuhimu wake kwa Taifa ukizingatia kwamba, uharibifu unaendelea kwa kasi kubwa sna kwa ukulima duni wa milimani, uchomaji moto na hata udumishaji wa makazi ya binadamu kwenye milima hii inayotunza uhai wa Watanzania wengi wa Mikoa niliyoitaja hapo juu

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, napenda kutamka tena kwa mara ya pili kuwa, hoja hii ni muhimu kwa kuinua uchumi wa Taifa letu changa, hivyo, naiunga mkono mia kwa mia.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoapongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, pamoja na wataalam wao wote, kwa kuwasilisha hotuba yao ya bajeti ya mwaka 2004/2005 katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri aliyoiwasilisha pamoja na ile ya Kamati ya Maliasili/Mazingira kwa ujumla zimezungumzia mambo mengi ambayo kwa kiasi yanalingana kutokana na ukweli wake ulivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara ya Maliasili/Mazingira ilitangazwa kupiga marufuku usafirishaji wa magogo nje ya nchi na hilo limo hata kwenye hotuba yake Waziri aliyoiwasilisha asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huo mimi binafsi nakubaliana nao kwa manufaa ya nchi yetu na Wananchi wake na kutunza mazingira yetu yawe mazuri, kwani kutunza miti ndiyo manufaa ya nchi katika nyanja nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwa Wananchi wengi wanaofanya biashara za magogo ni maskini na wanategemea mikopo kwa kuweza kuendesha shughuli zao za kawaida za biashara, kwa hiyo, ningeliishauri Wizara kwa hivi sasa wale wote wenye magogo yao bandarini na msituni waweze kuruhusiwa kwani tutawaweka katika hali ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, ningeliomba Wizara iweke mkazo zaidi kwa wageni amba wao wenyewe au kuwatumia watu wengine kufanya kazi hiyo, ningeliishauri Serikali ikawazuia wageni wasiende vijijiini kukata au kununua magogo, watoe kazi kwa Watanzania ndiyo wafanye kazi hiyo wao kama wanahitaji basi wasubiri yafike katika sehemu ambayo itakubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niipongeze Wizara kwa kuchukua hatua thabiti katika kuhifadhi mazalio ya samaki ambayo yalikuwa yanatoweka kwa nguvu sana kutokana na kitendo cha ulipuaji wa mabomu katika mazalio ya samaki ambaa ulikithiri kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Nzega kuna tembo wengi ambao huenda na kurudi mara kwa mara na tembo hao huua hata watu kama swalilangu la nyongeza nilouliza hapa Bungeni, 2003. Je, Wizara ina utaratibu gani kutusaidia wakazi wa Nzega kuepukana na vifo vya kuuliwa na tembo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wananchi wengi hasa wahamaji kila maeneo wapo na hasa wanapokata misitu na kuhamisha huko na Serikali hutumia gharama kubwa sana kuhamisha wahamiaji. Je, watu wa Misitu wanaachaje mpaka Wananchi wanahamia maeneo hayo na wao wapo kwa maana hiyo watu wa Misitu hawatembelei maeneo ya kazi zao ndiyo maana Serikali hupata hasara kubwa ya kuhamisha wavamizi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengi sana misitu huchomwa, Morogoro, Tabora na sehemu nyingine na Wizara ipo. Je hii itakuwa ni Idara ya Misitu au ya Mapori?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya Wananchi kupata Semina juu ya maeneo husika kuhusu uhifadhi na bahari kwa kuwa Wananchi wanaelewa kuna hifadhi ya wanayama na Wananchi huishi huko huko, kwa hiyo basi, suala hili tuliangalie kwa kina kwa elimu, vipeperushi, vikao vya Serikali na vya Vyama. Mfano Mtware Kijiji cha Nalingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utaratibu wa magogo kupelekwa nje na suala hili lililaaniwa vikali sana. Je tuna utaratibu gani kuhusu magogo hayo hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na utaratibu, nguzo za umeme zinazotoka *South Africa* zisije tena hapa nchini na badala yake misitu yetu ikidhi mahitaji ya ndani ya nchi yetu ndipo tutafaidika Wananchi wote kwa ujumla katika kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Tabora kuna mambo ya kale chungu nzima na Mheshimiwa Waziri, aliahidi kuangalia mkoa huo na kuanza kuyakumbuka au kuyajengea mambo hayo na bado kihistoria baada ya miaka ijayo, Mkoa wa Tabora utasahaaulika kabisa sehemu ilipopigwa kura tatu. Pia shule aliyosomesha Mwalimu Nyerere na hata pia Viongozi wengi kusoma katika mkoa huo na mpaka sasa ni Viongozi

wa ngazi za juu. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wauone mkoaa huo ni ndani ya kihistoria ya nchi hii.

MHE. LYDIA T. BOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana hotuba ya Waziri, nampongeza pia kwa kazi zake nzuri, zenye matumaini wakati wote wa kuipatia Serikali kipato na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Katibu Mkuu, Watalaan wake kwa ushirikiano waliouonyesha kwa kipindi hiki, jitihada zao ziendelee na wasimamie mipango waliyojiwekea na nawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoaa wa Mtwara kuna maeneo mazuri sana kwa watalii kama *Old Boma*, Mikindani, Ruvula, Msanga Mkuu, lakini watalii wengi hawafiki sijui tatizo ni nini labda sababu ni ukosefu wa miundombinu ya uhakika nadhani ikiwemo na Serikali kutotangaza maeneo. Mimi naamini kuwa utalii ni kichocheo kikubwa cha Maendeleo hivyo, kustawisha maeneo ya Mtwara, uchumi utakua katika familia. Nashauri Serikali itupie jicho maeneo haya kuona kuwa yanaboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Marine Park*, kama Wananchi wataelewa itakuwa pia ni heshima kwa Mkoaa wetu, Wananchi wake watapata kipato ambacho nao watanufaika katika familia zao. Kuhusu Wananchi wake kwa maeneno haya kutopokea maelekezo ya Serikali, tatizo ni ukosefu wa uelewa (Elimu), kwani katika kanda hii Wananchi wake wamekosa elimu ya kusoma na kuandika toka enzi za mababu, hivyo, Serikali isikate tamaa, itafute kila mbinu za kuwashamasisha Wananchi kwa kuwapatia mafunzo ya semina, mikutano na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa kusitisha ununuza na usafirishaji wa magogo, aendelee na kazi na Mungu yuko naye, atampa kila msaada. Nasema hivyo sababu pamoja na kazi nzuri inayofanywa, maadui hawapendi, wataichukia pia Serikali, lakini siku ni leo ya kufichuliwa kwao na maovu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Maliasili walioko Wilayani chini ya TAMISEMI, wengi wao hawaajapandishwa vyeo kwa muda mrefu, halafu hawaungwi mkono katika Bajeti zao kupewa mafungu yao ya Idara ambazo zinaweza zikawasaidia kufanya kazi zao vizuri zikiwemo safari za vijijini, masurufu na kadhalika, pia uhamisho wengi wao wamekaa kituo kimoja kwa zaidi ya miaka 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ione kuwa watumishi wa Wilaya wakitumiwa vizuri hatutakuwa na tatizo lolote kama kuangalia vyanzo vya maji, kupanda miti na kadhalika, kuliko ilivyo sasa hawajaliwi na wala hawapatiwi nyenzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyamapor ni rasilimali ya Taifa ambayo tumebahatika katika nchi yetu; lakini wanyama hao wakati mwininge wanavuka na kudhuru watu au kuharibu mazao yao, naishauri Serikali iendelee kuwatambua

wanaoathirika na kubuni mbinu mbalimbali za kuweka sawa pande zote mbili, Serikali na wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri wanawake wasiachwe nyuma katika kuwashirikisha na mipango yoyote ya Hifadhi ya wanyama na misitu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuitakia kheri Wizara, naunga mkono mia kwa mia.

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika kuendeleza sekta hii ya Maliasili na Utalii. Mchango unaotolewa na sekta hii kwa bajeti ya Serikali umekuwa ukiongezeka siku hadi siku na huenda sekta hii ikawa tegemeo kubwa la Pato la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inaonyesha miaka ya nyuma Wizara hii ilikuwa imegubikwa na malalamiko mengi ya rushwa ambayo yalipelekea baadhi ya Viongozi Waandamizi kuwajibika kwa kuachia ngazi madaraka yao. Tuhuma za rushwa hazisikiki kama ilivyokuwa hapo awali, hata hivyo, hii haimaanishi kwamba, rushwa au dalili zake zimekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uvuvi sasa inatoa ajira kubwa ya muda (vibarua), kwenye maeneo ya Ziwa Victoria, Musoma, Mwanza na Bukoba, ambako kumejengwa viwanda vya samaki. Cha ajabu ni kwamba, viwanda vya samaki Musoma havitoi ajira ya kudumu kwa wafanyakazi, wengi wapo kama vibarua, hii ni hatari sana. Bei ya kununulia samaki haitolewi kwa haki kulingana na hali ya soko, isipokuwa inatolewa kwa vigezo vya kuelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wanatoa bei nzuri zaidi kwa wale Maafisa wa Serikali, ambao wanafanya biashara pale. Hali hii haitoi fursa sawa kwa wafanyabiashara wote na hii ni kinyume na taratibu nzima za biashara huru ambako nguvu za soko hutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uvuvi baharini hususan uvuvi wa *prawns* ni eneo jingine ambalo limejaa mashaka. Utoaji wa leseni za uvuvi wa kamba unatia mashaka sana, kwani kuna watu wachache ambao wamehodhi biashara hii kwa kushirikiana na baadhi ya Watendaji wa Wizara hii. Nashauri utoaji wa leseni za meli za uvuvi wa Kamba uwe wazi zaidi kuliko ilivyo sasa, ambapo dalili za wazi za matumizi ya rushwa katika upatikanaji wa leseni zipo wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko makubwa yanayotokea katika sekta ya uvuvi ambako wawekezaji wenye mitaji mikubwa wanaingia, hakuna budi kuwepo na mpango mkakati wa kuwawezesha wavuvi wadogo Wazalendo ili waweze kubakia katika sekta hii na kuwawezesha kupata ajira ambayo wamekuwa nayo kiasili kwa muda mrefu. Tusipofanya hivyo, tutajenga mazingira mabaya kwa wawekezaji ambao tunawahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikitoa leseni kwa wawindaji Wazalendo Mkoani Mara kuwawezesha kupata kitoweo na pia kujenga mahusiano na Hifadhi zetu. Hii imesaidia sana pia kuondoa au kupunguza Uwindaji haramu ambao ulikuwa umekithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibu Mwekezaji mmoja *VIP* amepewa kibali cha uwindaji ambacho kimemuwezesha kuchukua mgao wote wa Wananchi wengine. Hili ni tatizo. Faida ya mbuga hizi kwa Wananchi wetu ni nini na kwa nini Wananchi wanyimwe haki yao na apewe mtu mmoja? Je, ni Afisa gani aliyehusika na tatizo hili? Je hakujua kuna Watanzania ambao maisha yao yote wanahitaji kuwinda?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, asitishe kibali kilichotolewa kwa *VIP* ili Wananchi wengine waweze pia kunufaika na Maliasili ya nchi yetu.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na yenye maelezo ya kina. Pia niwapongeze Watendaji wote chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu, Ndugu Solomon Odunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni mmoja kati ya Wanawake jasiri na mahiri katika kutekeleza kazi zake na hivyo kujenga heshima ya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, ausaidie Mkoa wa Kagera, ambao una vivutio vingi vya utalii kama vile fukwe za Ziwa Victoria, Maporomoko ya Rusumo na kadhalika, ambavyo yeye mwenyewe alijiona, hivyo namwomba awaunge mkono Wana-Kagera ambao sasa nao wanajaribu kuutangaza Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hatua alizochukua kudhibiti uvunaji na usafirishaji holela wa magogo. Inaonekana wazi kuwa kulikuwa na uchafu mwingi unaofanyika hivyo hatua alizochukua ni sahihi. Kwa vile katika sekta hii ina wafanya biashara wadogo wadogo ambao baadhi yao wameshirikiana na wafanyabiashara wakubwa toka nje, ningeshauri ufanyike uchambuzi ili wale wanaofanya biashara kihalali wasaidiwe na kupewa msaada ili waweze kusafirisha bidhaa ambazo tayari walikwisha ziandaa na baada ya hapo wapewe utaratibu wa kuendelea nao. Lakini pia wafanyabiashara hao washauriwe kuunda vikundi vilivyo hai kisheria ili iwe rahisi kushughulika nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizidi kumpongeza Waziri na Wataalam wote. Naunga mkono hoja.

MHE. SAMUEL M. CHITALILO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na wafanyakazi wote walioko ofisini kwake, kwa ushirikiano wa kuweza kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utalii umeshamiri zaidi ya miaka kadhaa ya nyuma, ninaomba waendelee na kuitangaza nchi yetu kama wafanyavyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Waziri ni kuzidi kuomba kugawa eneo la kulima Wananchi kule *Maisome Island*. Pamoja na kuwa aliwahi kujibu swali langu kuhusu eneo hilo kuwa itakuwa vigumu kugawa eneo hilo kwa Wananchi. Mimi naomba Waziri atume watu wachunguze upya suala hilo, kwani pori lililopo halina kitu cha Utalii hata kidogo, miti ya maana haipo. Ninaomba kwa nia nzuri eneo hili la Kisiwa cha Maisome wapewe Wananchi ili waendeleze eneo hilo kwa kilimo na kupanda miti.

Mwisho, naunga hoja mkono mia kwa mia.

MHE. PHILIP A. MAGANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Wasaidizi wake wote, ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu wake, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya hususan katika Sekta ya Utalii na Wanyamapori. Hii imeelezwa vizuri katika Hotuba ya Waziri, kazi ambayo inajieleza yenye kwa matokeo katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kueleza masikitiko yangu na ya wale wakazi wa Mkoa wa Lindi, kutokana na uharibifu mkubwa unaofanywa na wakata magogo kwa fujo bila kuzingatia utaratibu wowote. Shughuli hii imeendelea kwa muda mrefu lakini imeongezeka kwa kasi miaka miwili iliyopita. Wakataji wa magogo siyo tu wanaathiri mazingira, bali wanafanya uharibifu mkubwa wa barabara, magari makubwa yanayosomba magogo na hivyo kuleta hasara kubwa kwa Halmashauri za Wilaya katika maeneo hayo kwa kuongeza gharama za ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama kuna utaratibu wowote wa kutoa vibali kuwaruhusu wakataji hawa wa miti. Wilayani na Mikoani wanasema vibali hutolewa Makao Makuu na wale wa Makao Makuu husema hutolewa huko huko Wilayani na Mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Mkoa wa Lindi, pamoja na wale wa Mkoa wa Pwani, ambako ndiyo hasa magogo yanaporomoshwa, ni maskini wa kutupwa, kama taarifa mbali mbali za hali ya uchumi nchini zinavyobaini. La kusikitisha ni kwamba, hafaidi chochote kutokana na biashara hii ya maliasili ya misitu. Hakuna ajira yoyote wanayopata. Ni ajabu kuwa badala ya kuwataka wawekezaji waanzishe viwanda vyta kupasua mbao na useremala ili wakazi wa huko wapate ajira na kuongeza teknolojia ya samani ambazo zingelitupatia ongezeko la mapato kutokana na uuzaji wa *finished product* badala ya magogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majuzi Bunge hili liliidhinisha ruzuku kwa Shirika la *TANESCO* ili kuziba pengo la uzalishaji wa umeme lililotokana na upungufu wa *hydrology* kwa vile hakuna mvua. Kwa upande mwingine ukame ultokana na kuathirika kwa hali ya juu kwa misitu katika *catchment areas* za Mto Rufiji (*Rufiji Basin*). Hii ni hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hatua ya kukataza au kusitisha ukataji wa miti ovyo na kuachana na biashara ya magogo. Hatua hii iwe ya kudumu na siyo ya zima moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampa hongera sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake ambayo imejaa hekima, busara na malengo ya muda mfupi na mrefu. Ni wajibu wake ingawa anastahili tuzo la haki kwa uwajibikaji, anafanya kazi yake vizuri sana, kweli kumbe mama hana mpinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna chombo chochote kinachosimamia mazingira ya milima yetu nchini ikiwemo milima ya Urugulu? Kama kipo chombo au kama hakipo, kwa nini Wananchi wa maeneo hayo kama vile Kinole, Kiziwa, Amini, Bamba na Kiroka, washirikishwe kuunda vikundi vyao vijijini kujenga ushiriki wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu na ushamba nchi kama Tanzania kuendelea kusafirisha (*export*) magogo nje ya nchi badala ya kusafirisha samani. Kuna baadhi ya watendaji wetu ndani ya Wizara siyo waaminifu. Naomba wajirekebishe au waachie ngazi mapema kabla ya awamu ijayo. Kwa nia safi kabisa, kama yupo Mtendaji ndani ya Wizara hii anajiona au anajihisi utendaji wake una walakini, hauendani na nia safi ya Waziri, basi huyo kiustaarabu aachie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iandae rasimu ya Sheria za Sekta ya Utalii upya kisha iandae Semina na kushirikisha wadau wanaojua mambo haya kuipitia kwa kina kabla ya kuletwa Bungeni uwakilishi mzuri wa wadau uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali yafuatayo:-

- (i) Je, uyoga ni maliasili?
- (ii) Je, makumbusho ni maliasili au utamaduni?
- (iii) Kwa nini Wizara inapendelea sana masuala ya Utalii badala ya Maliasili ambayo ni misitu?
- (iv) Je, kwa nini Wizara hii isijitwe Wizara ya Maliasili na Misitu tu ili Utalii uende Wizara ya Biashara, ili Biashara ya Utalii isihodhi Jina la Wizara na Uwajibikaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakumbusha Wizara ifanye Semina ya rasimu ya Sheria mpya za Utalii na Wanyama.

MHE. FTEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba kutoa pole zangu za dhati kwa familia, ndugu, jamaa pamoja na Wananchi wote wa Jimbo la Ulanga Mashariki Mkoani Morogoro, kwa kufiwa na Mbunge wao, Marehemu

Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Katibu Mkuu wake, Watendaji na Wataalam wake wote, kwa juhudhi na kazi nzuri ya kumudu vyema Wizara hii na kuweza kutufikisha kwenye maendeleo makubwa tuliyofikia hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaanza kuchangia kwenye Chuo cha Uvuvi cha Mbegani. Ninashauri umefika wakati sasa tukiimarishe Chuo kifiki kwa cha Kimataifa na tuweze kuona uvuvi wa kitaalam na kuweza kupata mavuno mengine mazuri ya kutupatia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa uvuvi haramu pamoja na wizi wa mali za baharini kama samaki na vinginevyo, ninashauri ulinzi wa vyombo vyta baharini vyta kisasa vipatikane na vilivyopo viimarishwe na vifanye kazi baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukataji ovyo wa Mikoko na miti iliyo mwambao wa bahari, unasababisha bahari kupanda juu na kula eneo kubwa la ardhi yetu, cha kusikitisha zaidi kisiwa kizuri cha Maziwe kilichoko Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga, kisiwa hicho ni kizuri na cha historia kubwa mwambao wetu wa bahari aidha kina historia ya Kasa wengi kukitumia. Kutokana na kukata miti na mikoko ya kisiwa hicho, sasa kimezama na kimekuwa kama fungu la mchanga tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Watendaji wake wote, lakini bado ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aongeze juhudhi katika kuangalia maeneo hayo. Mwisho, ninaomba kushauri kuwa, tuangalie zaidi uvuvi katika bahari yetu ya Hindi na Maziwa yetu ya Victoria na mengineyo. Ninaamini kwenye bahari kuna mali zetu nyingi ambazo bado hatujazishughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa sasa, ninaomba kuiunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa asilimia kwa mia kwa mia.

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na sina budi kuiunga mkono hoja hiyo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi binafsi sina pingamizi lolote lile kuhusu Bajeti yake, lakini kero yangu kubwa kwa hivi sasa ni kuhusu soko la kisasa la samaki lililokuwa lijengwe pale Kilimani. Jimbo la Kikwajuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni la muda mrefu sana na ninasikitika ya kwamba, mpaka hivi sasa suala hilo halijapata ufumbuzi wowote ule. Nafahamu fika jinsi Mheshimiwa Waziri, anavyolihangaikia suala hili. Pamoja na juhudhi zake hizo, ningemwomba sana atoe kauli kuhusu soko hilo la Kilimani ili Wananchi wa Jimbo la

Kikwajuni tuweze kuelewa hatua iliyofikiwa katika mazungumzo yake na Balozi wa Japan mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kumpongeza tena Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake wote, walioandaa hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri. Asante.

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa Hotuba nzuri. Aidha, kwa utekelezaji wa majukumu waliyopewa na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nachukua nafasi kuwakumbusha mambo machache yanayohusu Wizara hii.

Kwanza, imekuwa ni ajabu kwa upande wa Kanda ya Ziwa Nyasa kwa kutokuwepo na usafiri wa Ziwani kwa ajili ya usimamizi wa maliasili zinazopatikana Ziwani kwa maana ya samaki na mazao yanayotokana na misitu inayopatikana kwenye miteremko ya milima *Livingstone*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutoimarika kwa usafiri mwambao wa Ziwa Nyasa, makampuni kadhaa za ndani na nje ya nchi yetu, yameendelea kuvua samaki wa mapambo bila ya kuchunguzwa mienendo yao. Makampuni hayo yameendelea kuvua samaki bila leseni halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mazalio ya samaki kama Mto Ruhuhu, Nchuchuma, Kenju na Lumbila, yameendelea kutumika vibaya, hadi sasa aina fulani ya samaki inatishia kupotea kabisa katika eneo hili. Samaki hao wanaotoweka ni pamoja na mbasa, mbelele, ningu ngumbu na matuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lote la kuanzia Mto Ruhuhu hadi Kyela halina usafiri wa Maliasili na usimamizi wa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Wizara kusaidia boti kwa ajili ya Maafisa Maliasili wachache waliopo Manda na Makonde kuweza angalau kupita kwenye mwambao huo wa Ziwa Nyasa kufanya *supervision*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii katika kulinda uchumi wetu wa maliasili ya bahari (uvuvi). Kuna haja ya kuwa na udhibiti mkubwa wa uvuvi unaofanywa na meli za nje kwa kuhakikisha kuwa kunakuwepo *Radar* ya kumulika bahari yetu ikiambatana na ulinzi wa boti za mwendo wa kasi kufuatilia meli

zitakazoonekana kuonwa katika bahari yetu bila ya kibali. Morocco wanayo *facility* ya *Radar* inayoweza kumulika Afrika nzima na kuwapa taarifa ya wizi wa uvuvi unaofanyika nchi inayoibiwa. Mwaka 1995, Morocco iliikaribisha Zanzibar kutumia fursa hiyo lakini kwa bahati mbaya hakuna mazungumzo yaliyofanyika.

Nashauri Wizara ya Maliasili na Utalii, ifuatilie hili na Wizara ya Uvuvi ya Morocco ili kulinda maliasili yetu.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Waandaaji wote kwa kazi nzuri anayoifanya ya kusimamia kazi za Wizara hii kikamilifu. Baada ya kusema haya, naishauri Serikali yafuatayo:-

Kwanza, misitu inatisha, miti inayopandwa haikui yote, hakuna uoto wa asili. Sababu kubwa ni moto, uchungaji ng'ombe, kuni na kadhalika. Naishauri Serikali kwamba, utafutwe ufumbuzi wa nishati ili iwe mbadala wa kuni kama vile mkaa wa mawe au wataalam wafanye utafiti wa kutengeneza pumba za mbao ili iwe nishati ya kupikia. Kuhusu ng'ombe ufanyike utaratibu wa matumizi bora ya ardhi ili kila Mfugaji awe na eneo lake ili apange jinsi ya kutumia ardhi hiyo ambayo itamlazimisha apunguze ng'ombe. Serikali iandae mpango kama huo na elimu itolewe kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutunza misitu kwa ajili ya kuvuna asali ni muhimu kwani ni moja ya zao muhimu kwa Wananchi. Wizara iwe na mpango mkubwa na mzito ili Wananchi waweze kufaidika nao. Ili misitu iendelee, walio na tabia ya kukata kuni za kuuza wapewe mashamba wapande miti kwa ajili ya kuvuna kuni na papo hapo tutafuga nyuki na misitu ya asili itabaki na nyuki wengi watakuwepo huko na Wananchi watafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kukamata magogo na kupiga marufuku ukataji wa magogo na kuyasafirisha nchi za nje na kuwawajibisha watumishi waliohusika na kutoa vibali. Mimi namtia moyo Waziri aendeele na kazi yake na afanye kazi kwa kufuata sheria. Mwenyezi Mungu, atamlinda pamoja na watendaji wazuri ambao wanajua na kupenda kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo juu ya hatima ya Hoteli ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii bila kigugumizi chochote.

Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa bidii na juhudhi zake nzuri katika Wizara hii. Amefanikiwa sana katika utekelezaji wa majukumu yake yote yaliyopangwa.

Tatu, namshukuru sana kwa kuwa karibu sana na Wananchi wa Jimbo langu, hususan miradi ya *TANAPA*. Pamoja na kumshukuru Waziri, pia nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Balozi Lusinde, Mwenyekiti wa Bodi ya *TANAPA*, kwa juhudhi zake nzuri zilizofanikisha miradi hiyo. Pia namshukuru Mkurugenzi Mkuu wa *TANAPA* kwa utendaji wake mzuri na ufuatiliaji makini.

Nne, Miradi iliyoshirikisha Wananchi ni ujenzi wa Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Aman Abeid Karume (Pahi), ujenzi wa Hosteli ya Wasichana katika shule hiyo na kukamilisha nyumba ya *Headmaster* katika shule hiyo. Wananchi wanatoa shukrani nyingi sana.

Tano, Wananchi wanaomba mambo yafuatayo, ambayo tayari Mwenyekiti wa Bodi amepelekewa kwa hatua zaidi nayo ni: Tatizo sugu la barabara ya Chubi - Itaswi - Kisaki. Kimsingi tumekubaliana sasa barabara hiyo ipite Chubi - Itaswi - Mauno na kuunganisha na barabara iendayo Kondoa toka Busi. Barabara hii sasa itakuwa na kilometra 22. Kinachokwamisha kuanza ni nini kwa sababu makadirio yalikwisha letwa sehemu zote?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ALLY A. KARAVINA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze moja kwa moja kwa kusema kwamba, Maliasili na Utalii ni sekta ya uchumi kwa nchi yetu ambao unaweza kuwa na uwezo wa kuondoa umaskini, kwani si nchi nyingi katika Afrika na Dunia zina maliasili na vivutio vya utalii kama Tanzania. Nakiri kwamba, bado hatujatoa tafsiri sahihi ya sekta hii sasa na baadaye, jinsi gani tutaitumia kuongeza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba leo hii nizungumzie Mfuko wa *WMAs* na jinsi gani hizi zinaweza kuondoa umaskini na niseme *Wildlife Management Area* ya Uyumbu huko Urambo Tabora. Mimi ninaona malengo mawili makuu: Kwanza, kuhakikisha kwamba Maliasili hizi (*WMA*), zitatoa faida kwa Wananchi maskini wanaozunguka au kuishi pembezoni mwa misitu hii ya asili. Pili, ulinzi au jukumu la kulinda maliasili zetu kwa maana ya *WMA* ya Uyumbu na kadhalika, litakuwa la Wananchi wenye ambao malipo yake ni ruhusa ya kuvuna na kufaidika na mazao ya *WMA* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uyumbu *WMA* ina *C.B.O.* na sasa imepata usajili wa kuendesha *WMA* hiyo. Bado vitambulisho vya walinzi na mambo mengine madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haileweki pale Afisa wa Hifadhi ambaye bila kushirikisha wadau wengine wote pamoja na Halmashauri husika katika kubadili mipaka iliyokubalika na kuigawa sehemu hiyo kwa wagoni wawindaji mimi na wenzangu mpaka

leo hii hatujui mazingira yaliyopelekea Bwana Midala, Meneja wa Ugalla, kupunguza kilometra 10 kutoka kwenye mpaka uliokubalika kwa sababu tu aliona tuko *serious* na *speed* ya mafanikio ilikuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe sehemu iliyopunguzwa ndiyo ile inayokaliwa na wanyama (mbuga/misitu) halafu baya zaidi huyu Meneja Mfalme akavunja na kuiba asali yote ya Wananchi wangu wa Nsogolo (mizinga zaidi ya mia moja hamsini) na kuwafukuza na kuwatia ndani walioendelea kudai mali zao ambazo walikuwa wameruhusiwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri na kuridhiwa na Meneja huyu kama ilivyokuwa kawaida kwa kipindi kirefu hapo nyuma na kwamba, Wananchi hawa walikuwa hawana tegemeo lingine lolote zaidi ya kurina asali. Watoto wao wamefukuzwa shule na familia hizi takriban 50 hazina namna nyingine ya kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri yafuatayo:-

Kwanza, tunaomba Meneja Midala aondolewe katika Ugalla pamoja na mambo mengine, usalama wake mwenyewe kwa athari alizoleta ni pamoja na vifo.

Pili, Wananchi wale wanadai fidia halisi inaelekezwa kwa Mbunge, mimi nifanye nini? Namwomba Mheshimiwa Waziri awafikirie.

Tatu, kama kawaida ya Askari wa Miamvuli, namwomba Mheshimiwa Waziri atutembelee angalau kwa muda wa siku moja, ili ajionee mwenyewe haya tunayoyasema mimi na mwenzangu Mheshimiwa Jma Nkumba, Mbunge wa Sikonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. ABDILAH O. NAMKULALA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii lakini kuna maelezo ya kuongezea hoja hii.

Kwanza, Wanakijiji cha Nahingu hawatoki katakata *Marine Park*, tunafanyaje?

Pili, nini hatima ya Shamba la Kabisera la Mkonge ambalo Mwekezaji anataka kuweka *zoo* kinyume cha Sheria, tunafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba nzuri na mipango mizuri ya Wizara. Nawapongeza Ndugu Odunga, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kuishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutusaidia na kuchangia miradi yetu ya Maendeleo katika Tarafa ya Lembeni. Nawashukuru pia kwa ahadi ya kuisaidia shule ya Sekondari ya Kigononi, Tarafa ya Jipe-Ndaa kuweka simu za *solar*.

MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kutekeleza ipasavyo Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa CCM 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Uongozi, majemedari na wapiganaji wote wa Wizara, kuendeleza utalii, kulinda na kuhifadhi maliasili baharini, Maziwa na nchi kavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Jimbo la Rarya walinituma kwa Mheshimiwa Waziri niwafikishie kilio chao kuhusu msaada wa kusaidiwa kuchimba malambo kama mchango wa Wizara yake kwa Wananchi wa Wilaya ya Tarime, kama sehemu ya mchango wa Wizara yake kwa Wilaya zinazopakana na Hifadhi za mbuga za wanayamapor.

Katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anatoa hotuba ya 2002/2003 na 2003/2004, nilimwandikia barua kuhusu ombi la Wapiga Kura wa Jimbo la Rarya. Nina imani kubwa kwa utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kwa niaba ya Wapiga Kura wa Kilombero, kutoa pole zetu za dhati kwa kifo cha kaka yangu, Marehemu Mheshimiwa Kapteni Mstaafu Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa jirani zetu Wapiga Kura wa Jimbo la Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa Wizara yake kuandaa hotuba nzuri, fasaha na kwa lugha nyepesi. Naomba pamoa na pongezi zilizotangulizwa, niunge mkono hatua ya Waziri ya kusitisha biashara ya magogo, kwani baada ya kuangalia Jedwali Na. 5 ukurusa wa 46, inaonyesha kwa kutisha ongezeko kubwa la uvunaji wa mazao ya misitu. Kutoka takribani \$ 6,697 hadi kufikia \$ 2,544 milioni kati ya mwaka 2000 na 2004, kwa vyovoyote uvunaji umezidi zaidi ya urejeshaji wa hali ya misitu ya awali kabla ya uvunaji. Hivyo, uamuzi ni sahihi na madhubuti. Naomba kwa mantiki hiyo hiyo, Wizara isitishe uvunaji wa mali ya misitu na magogo kule Kilombero hususan Kata ya Mkumba kwenye Vijiji vya Malema, Utengule, Masagai na Taweta. Habari kutoka Jimboni kuwa biashara hiyo bado inaendeshwa hata baada ya tamko la Waziri. *Station* ya Mlimba ya Reli ya Tazara bado imeandika magogo kwa kusafirishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mwaka 2004/2005, Serikali imeandaa taratibu za kutoa leseni kupitia Serikali za Wilaya na Vijiji. Kwa Kilombero ambayo iko kwenye

Ramsar Site Area ambapo Tanzania ilisharidhia Mkataba wa Ramsar wa mwaka 2002, umakini uchukuliwe ili kuhifadhi umaarufu wa Vinamasi vyake. Faida zake ni nyingi pamoja na uzuiaji wa mafuriko nchi za Kusini mwa Tanzania. Hifadhi ya maji na mazingira hayo Kilombero ni muhimu.

Sehemu nyingine ya kuchangia ni juu ya mgao wa 25% kutokana na Uwindaji wa Kitalii. Marekebisho yafanyike juu ya mgao angalau kipato kwenda kwenye sehemu zile zihusuzo uhifadhi wa wanyama. Kwa Kilombero ni muhimu vijiji vya Mofu, Ikwambi, Utengule na Masagati, vipewe gawio sawia badala ya *effective rate* ya 7.25% yote kumezwa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia Hotuba ya Waziri, nimebaini kuteremka kwa kipato cha Serikali kutoka kwenye makampuni ya Uwindaji, uliteremka kutoka \$ 9,012,960 hadi \$ 8,824,305 kati ya mwaka 2000 na 2004, sababu moja kubwa ni ujangili. Kati ya mwaka 2003 na 2004 ujangili uliongezeka toka majangili 512 hadi majangili 607. Pamoja na vita vya Ghuba, sababu moja ni kuwa sheria hajakuwa kali kwenye kutoza adhabu. Katika kesi za ujangili theluthi moja ya kesi zote hutozwa tu faini. Kifungo kichukue nafasi ya faini ili kukabiliana na majangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengi ya kuchangia kwenye Wizara hii lakini muda ni mdogo. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri na *Selous Game Reserve Management*, kwa msaada wake wa Tingatinga kwa ajili ya utengenezaji wa tuta kati ya Kisauriwa na Kijiji cha Mpanga kwenye Tarafa ya Chang'ula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kumwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, aweze kukaa na Wizara ya Ujenzi, kuzungumzia suala la *Bonn Pits* kwenye barabara ya Kidatu/Ifakara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie hotuba ya bajeti ya mwaka 2004/2005 iliyotolewa na Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri mno, inayoipa Wizara hii mwelekeo sahihi kwa mwaka wa 2004/2005. Ninawapongeza sana wataalam wa Wizara hii nyeti kwa kufanya kazi usiku na mchana kizalendo na kwa lengo moja tu la kuinua uchumi wa Serikali yetu kwa njia ya Maliasili kwa Utalii. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napendekeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake, wapitie upya maoni na mapendekezo yaliyokwisha tolewa tangu mwaka 2001 hadi 2004, kwa kutumia vitabu vya Bunge (*Hansard*) na kuona ni yapi yameteklezwa na ni yapi hayajatelezwa ili utekelezaji uendelelezwe kikamilifu.

Pili, Wizara iangalie jinsi ya kusaidia miradi ya wadau (walengwa) wanaozunguka maeneo ya Utalii ili iwanufaishe wadau hao na waone umuhimu wa kulinda na kuhifadhi vizuri zaidi maeneo hayo. Kwa mfano, maeneo ya *KINAPA*, ambapo Wananchi wanaazima moto mara kwa mara ajali ya moto inapotokea na kuashiria kuteketeza msitu.

Tatu, ninaomba ule msaada wa kujenga bwalo la *Mwika Day Secondary School*, shilingi milioni tisa, ambapo umefikisha jengo hilo kwenye madirisha tu tangu mwaka 2003 uendelee kwa kasi zaidi ili wanafunzi hao wapate mahali pa kulia chakula.

Nne, *Ashira Government Secondary School* ni moja kati ya Shule kongwe za Sekondari za Serikali hapa nchini lakini imedumaa kimajengo. Ninaomba mchanganuo wa uendelezaji wa shule hiyo utakapoletwa Wizarani. Wizara ione jinsi gani ya kuisaidia Shule hiyo na kwa jengo lipi. Yako mengi sana.

Tano, kumekuwepo ukataji miti ovyo kwenye msitu wa Kilimanjaro. Askari Bwana Miti na Askari wa *KINAPA* ni wauzaji wakuu wa miti hiyo kwa watu kimagendo/kiwizi. Napendekeza Askari Polisi na hawa Askari wa *KINAPA* wawe pamoja na kwa zamu katika kulinda msitu huu ambao kwa sasa umeisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninamtakia Mheshimiwa Waziri afya njema na maisha marefu na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake, kwa hotuba nzuri. Hata hivyo, ningependa kusitiza kuhusu juhudhi zinazostahili kuchukuliwa katika maeneo muhimu mawili kuhusiana na Mkoa wa Kigoma na hususan Mji wa Kigoma Ujiji, ili nasi tufaidi juhudhi za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, anazungumzia utekelezaji wa mpango kamambe (ukurasa 20). Nikimnkuu, anasema: “Vilevile ilianza kutekeleza mradi wa kuhifadhi mazingira ya Ziwa Tanganyika pamoja na kuendeleza huduma za kiuchumi kwa wavuvi na huduma za jamii, ambao unahuishwa nchi zinazomiliki ziwa hilo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii si sahihi kwa asilimia mia moja. Hii ni kwa sababu kuwa nielewavyo mimi, hata Mkataba huo wa Ziwa Tanganyika haujasainiwa mpaka hapo utakaporidhiwa na nchi husika, ni dhahidi kuwa mkakati tajwa hapo juu hautatekelezeka. Vipi sasa utangazwe kama upo, wakati masharti ya kisheria hayajakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara isilisahau eneo hili kwa makusudi. Ili kuwaweka wenyeji wa huko katika hali ya matumaini, ni bora Wizara angalau ingeongea na Benki ya *CRDB*, ambayo imeweza kuendesha mradi wa mikopo kwa wavuvi Mkoani Kigoma siku za nyuma, ili wakati tukisubiri huo mradi kamambe, watu wa Kigoma waanze kupata matunda ya jitihada za Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuliongelea ni suala la *Livingstone Memorial* pale Ujiji. Ieleweke pia kuwa *Livingstone Memorial* haisimami peke yake na ikumbukwe pia kuwa kivuko cha watumwa halisi kilikuwa eneo la Bangwe na kwa hiyo ipo barabara ya ufukweni toka Bangwe hadi soko la Ujiji na kisha kuendelea hadi Tabora na hatimaye kufika Bagamoyo. Ni vyema *route* hii ikaboreshwa kabla ya kuanzia Ujiji na kuelekea Bagamoyo, kama Waziri alivyooonyesha katika hotuba yake kifungu cha 62, ukurasa wa 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata wasiwasi kidogo kuhusu utekelezaji wa mradi huu wa uboreshaji *route* hii, pamoja na *Livingstone Memorial*, kwani sioni fedha ya uhakika iliyotengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niikumbushe Serikali yetu kuwa, tunategemea kuleta maendeleo kwa uwiano. Kitendo kwa mfano, cha Wizara hii kuonekana kuweka umuhimu mkubwa kwa suala la ufgugaji samaki kabla ya kuonyesha jitihada za dhahiri za kukuza uwezo wa wavuvi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa na Ziwa Nyasa, kinatia shaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maziwa hayo niliyoyataja, si kwamba wanapatikana samaki wa chakula tu, bali hata wale wa mapambo ambao hupatikana huko tu ulimwenguni. Watanzania wengi hawajawezeshwa kutumia chanzo hiki kizuri cha mapato kama Jedwali Na. 7 (ukurasa 40) linavyooonyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kuwa naunga mkono hoja hii.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Hongera sana Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wananchi wa Jimbo la Siha, tunatambua uwezo alionao Mheshimiwa Waziri katika kuiongoza Wizara yake na kwa hiyo, hatuna shaka yoyote ile kuhusu umahiri wake kiutendaji. Tunamuunga mkono. Hata hivyo, tunaiomba Wizara yake ione umuhimu wa kutoa mgao wa haki na usawa kwa Wananchi wote, hasa wale wadogo wadogo ambao wamejiunga katika Chama chao cha *NOFIA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara Wananchi hawa wameonekana katika Ofisi za Serikali na kupitia wawakilishi wao (yaani Wabunge), wakilalamikia hali ya kupungua kwa mgao wao bila ya maelezo ya kuridhisha. Ilani ya CCM ya mwaka 2000, inatamka waziwazi kuwa, itatoa kipaumbele kwa Wananchi wenye uwezo mdogo ili kuweza kukabiliana na umaskini. *Commitment* ya aina hii inajitokeza pia katika *Vision* ya Taifa ifikapo mwaka 2025, kuwa tutakuwa tumekabiliana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kuwa Serikali ipo tayari kukutana na Wananchi hawa tarehe 3 Agosti, 2004 ili tuweze kuondokana na matatizo ya mara kwa mara. Aidha, ni vyema Serikali ikaheshimu makubaliano mbalimbali ambayo yamefanywa kati ya Serikali na wavunaji (*Saw Millers*) wadogo wadogo kama *NOFIA*, ili kuepukana na migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa hotuba yake nzuri. Naunga mkono hoja hii.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwuliza Waziri wa Maliasili na Utalii, mambo matatu yanayonikera mimi pamoja na jamii ya Tanzania, juu ya Mlima Kilimanjaro na mrabaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba, nimewahi kuhoji sana hapa Bungeni juu ya Sheria ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Na. 320 ya mwaka 1994, ikitaka asilimia 25 kwa yejote atakayeruhusiwa kukusanya fedha kutoka kwa watalii watakaotembelea Mlima Kilimanjaro, zilipwe kwa Halmashauri hiyo. Kinachosikitisha ni kwamba, hadi leo sheria hiyo haijafutwa na wala haijatekelezwa, japo ipo hai kwenye vitabu vya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mambo kama haya, ndiyo yanayotupelekea kusema vibaya juu ya Utawala Bora Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara iliona kuwa sheria hiyo haifai au haitekelezeki, basi ingeweka utaratibu wa kuifuta ili isiwachanganye watendaji na endapo watafanya hivyo kwa sasa, hawana budi kulipa malimbikizo. Kwani sheria ni sheria, haichagui mdogo au mkubwa, kwani ni Rais peke yake ndiye yuko juu ya sheria. Tunaomba utekelezaji wa mara moja kwa hilo, kwani linadhalilisha dhana ya uUwala Bora Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, magogo yanayokatwa au kuvunwa ovyo Tanzania chini ya vibali vinavyotolewa na Wizara hii, halafu Wizara hii hii inakuja kulalamika na kufukuza Viongozi wake Waandamizi, kuwafukuza Maafisa hao ni kuwaonea sana kwa kuwa kanuni za Wizara zilikuwa zinaruhusu. Hivyo, jambo kama hili la aibu la kuvuna miti wakati mazingira yaliyoachwa na babu zetu na kusaidia kupata mvua nyingi nchini na kuacha nchi yetu ikiendelea kuwa jangwa bila mvua, ni wajibu wa Waziri mhusika kujizulu ili kuonyesha uwajibikaji na siyo kuwafukuza Waandamizi amba siyo walioweka kanuni hizo!

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri afute kanuni hizo, naye ajiuzulu mara moja. Ileweke kuwa misitu ni urithi wa Taifa (*National Heritage*). Pia ningependa kuona kuwa Wizara ya Mazingira chini ya Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, iwe na jukumu la kutoa vibali vya kuvuna miti, kwani ndiyo wenye jukumu la kupanda miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa baadhi ya *Game Reserves* au *National Parks* kama vile Mikumi, kumeanza kuwa na hali mbaya ya upatikanaji wa maji kwa kunywa wanyama amba hutuletea fedha nyingi za utalii. Ningependa kuishauri Wizara hii iangalie uwezekano wa kuelekeza miti inayopita kandokando ya pori, kuingia kwenye

vijito ambavyo sasa hivi vimekauka na kusababisha wanyama kufa au kuhama. Nimepita Mikumi juzi na nimekuta vijito vyote vikiwa havina maji. Kama tunapata fedha nyingi hivyo, kwa nini tusielekeze hata bomba moja kumwaga maji kwenye vyanzo vya hivyo vijito, ili wanyama hao waendelee kufaidi, kwani kuna hatari ya kutoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Wizara hii ilituambia kuwa, Kilimanjaro Hoteli itavunjwa yote na kuanza upya, jambo ambalo siyo kweli. Je, Serikali iko tayari kutueleza kilichotokea?

Mheshimiwa Waziri, tunaomba maelezo ya kina juu ya Moshi Hoteli iliyopo Moshi Mjini, kwani ni miaka mingi haifanyi kazi, ni nini matatizo yake? Sisi wawekezaji tupo, tuambiwe tufanye nini ili tuweze kufufua hoteli hiyo muhimu na ya kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kupata majibu yote haya.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, lakini nashauri na kuomba ufanuzi kwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamaporini yangetusaidia sana Wilaya ya Bariadi, hasa vijiji vya mpakani kama Shishani, Longalimbogo, Ndolelezi, Nkuyu, Lug'wa, Ng'walali, Ng'wamtani na kadhalika. Je, ni lini Mradi huu utafika Bariadi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyamaporini wengi sana wanatoroka kwenye hifadhi na kuingia maeneo ya Wananchi na kuharibu mazao mengi mashambani na wengine wanashambulia binadamu na kusababisha ukosefu wa amani. Je, Wizara inasema nini kuhusu kuwafidilia Wananchi walioathirika na matatizo haya hasa mwaka huu wa 2004?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba, Mheshimiwa Waziri anakumbuka suala/kero ya wafugaji wa vijiji vya mpakani na mbuga zetu sasa hawana mahali pa kulisha mifugo yao na sasa mifugo inakufa. Hivyo, Mheshimiwa Waziri zingatia ombi langu na la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte na utusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, maduka ya nyama za wanyamaporini Wilaya ya Bariadi hatuna. Tafadhalii Mheshimiwa Waziri, atoe maelekezo ya kutosha ili nasi tupate faida ya maliasili hiyo.

MHE. LUCAS L. SELELI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nzega mara kwa mara imekuwa ikivamiwa na wanyama waharibifu kama Tembo. Inawezekana kuwa Tembo hao wameongezeka sana huko porini. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwaua? Je, ni idadi gani iliyopo kwa

sasa? Je, Mheshimiwa Waziri, unategemea tuwaelekeze nini Wananchi wanaoharibiwa mazao yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la magogo lina athari kubwa ya mazingira na pia tumekuwa *very loose* kwenye biashara zetu. Wizara ipige marufuku wageni (China, Korea na kadhalika) wasiingie hadi vijijini na kwa kuwa hadi sasa yapo magogo bandarini, yaruhusiwe yaliyo na leseni halali. Marufuku yaendelezwe kwa wale waliokiuka sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mgogoro wa Bahari ya Hindi kati ya SMZ na Serikali ya Muungano, lifikie muafaka haraka. Bila ya kutatua zogo hilo, litafanya tuendelee kukosa mapato kwa kuendeleza ugomvi usio na maana. SMZ wala Serikali ya Muungano, haifaidiki na chochote kutokana na ugomvi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iendeleze mafanikio iliyoyapata hasa katika nyanja ya utafiti na maliasili. Nawatakia kheri na baraka za Mwenyezi Mungu.

MHE. MARTHA M. WEJJA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia juu ya magogo. Naomba niishauri Wizara iwahurumie wavuna magogo wa Tanzania. Kisha Wizara iwasaidie kupata mashine za kununua, ziwasaidie kukatia magogo. Wasaidiwe kupata mikopo kwenye Mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hawa Wachina wasiruhusiwe kuingia msituni kukata magogo. Waajiri Watanzania waingie misituni kukata magogo, wakizingatia utaratibu na masharti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wachina/Watalii, hawa watu wamekuwa na mbinu za kurubuni Watanzania hata kuwachochea kuzungumza kwenye Vyombo vyta Habari (*Television*), ili waonekane kuwa Serikali inawaonea Wananchi wake. Hali hiyo inaipaka matope Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafanyakazi, nampongeza sana Waziri kwa uamuzi wa kuwafukuza hao wafanyakazi, kwani hao ndio wanaoruhusu kusafirisha magogo bila kupigwa mihuri. Nina hakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kima, naiomba Wizara isaidie ukuzaji wa kima wa rangi. Wanyama hawa wapo Zanzibar tu na ni wachache sana. Ingefaa wafanyiwe utaratibu wa kuwazalisha wengi, ili waletwe na huku Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja hii.

MHE. OMARI S. KWAANGW': Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika hotuba ya Waziri, kifungu cha 25, ukurasa 13 - 14, sentensi ya mwisho inayosema

“Mashamba Na. 1 - 3 ya Manyara kuwa sehemu za hifadhi”, inaruhusu eneo la Kijiji cha Mayoka katika Jimbo langu la Babati Mashariki, haijafafanuliwa ipasavyo na wakati huo huo inaonyesha Muswada unaandalowiwa kwa ajili hiyo na kwa kuwa huko nyuma Waziri alishawahahi kuleta Azimio la kutaka kupanuliwa kwa Hifadhi ya Ziwa Manyara na ikaonekana ni muhimu wadau wote wahanishwe, ikiwa ni pamoja na mashauriano kati ya *TANAPA*, Halmashauri ya Wilaya ya Babati na Wanakijiji cha Mayoka na kwa kuwa hadi sasa siiiona kama juhudhi tulizoanzisha za majadiliano zikiendelezwa kama tulivyokubaliana huko nyuma, basi kwa msingu huo, mimi Mbunge wa Babati Mashariki katika hatua hii ya Waziri kuleta jambo hili bila mawasiliano, siungi mkono hoja yake na nitahitaji maelezo ya ziada kuhusu jambo hili. Ahsante.

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote ndani ya Wizara hii. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, kwa kuwa yeche na Askari wa Mwamvuli na ameshuka chini anachapa kazi. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja ya kuchepusha barabara ya Mikumi. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwenye hotuba yake, ametenga Sh. 202,000,000/= kwa kazi ya upembuzi yakinifu, kuchepusha barabara ya Mikumi - Kilosa - Dumila. Naomba tuanzie Mikumi, tumalizie Handeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kwamba, Wizara ya Ujenzi watakapomala mchanganuo wao, tutumiwe na sisi Wizara ya Maliasili na Utalii, tutafute wafadhili kuweza kuchangia utengenezaji wa barabara. Tunaipongeza Wizara kwa kutia msukumo kwa Serikali mpaka kukubali kujenga barabara ya lami toka Mikumi - Kilosa - Dumila.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo niombe na tatizo la Hoteli ya Mikumi, tusaidiane kutafuta wawekezaji wazuri amba siyo wababaishaji. Tujaribu kumwona kama yule aliyepata Kilimanjaro Hoteli ili asaidie katika mazungumzo ya kuelewana na wateja wake, baadaye wateja wake watapenda kwenda pale *Mikumi Lodge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mipaka ya Hifadhi ya Mikumi, bado halijaisha. Mipaka imeanza kutazamwa upya, baadhi ya vijiji wameketi na Viongozi wa Vijiji, kama vile Vijiiji vya Ruembe na Kitete na Kielelezo. Mikumi na Rumango bado. Naomba wapatiwe fedha ili wamalizie shughuli hiyo ya upimaji . Naomba sana waongezewe fedha ili waondoe kero ya mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa kazi nzuri ambayo inafanyika na mhifadhi wangu wa Ndugu Shemkunde, nampongeza sana. Nimeomba maombi yangu kupitia kwake na nimeomba visima vitano nichimbiwe na nimepita kwa Bwana Miyombo Safari. Nimewomba asaidie kuchimba na mitambo yake. Sasa naomba visima vitano tu kwa Mji wa Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeomba msaada wa ujenzi wa Sekondari ya Tarafa ya Ulaya, inayojengwa katika Kata ya Ulaya. Hivyo, tunaomba mchango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Waziri binafsi, kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii. Pongezi hizo ndizo zinapelekea kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja bila kupunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa pongezi kwa Katibu Mkuu, Watendaji Wakuu na Mameneja wa vitengo mbalimbali katika Wizara yake, ambao kwa kuwa nao karibu sana, ndiyo maana utendaji wao umekuwa na maendeleo ya hali ya juu. Lakini yote hayo yanatokana na uongozi bora ambao anauonyesha Mheshimiwa Zakia Meghji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia katika Wilaya yangu ya Geita, kuhusu Kijiji cha Mgusu ambacho kiko Wilayani kwetu na kinachotambuliwa katika shughuli za maendeleo. Tatizo ni kwamba, kijiji hiki hakijasajiliwa kwa kuwa kiko kwenye hifadhi. Tulitoa ombi maalum la kuomba Wizara iwaruhusu Wananchi hawa waendelee kukaa ndani ya hifadhi. Hilo nashukuru sana kwa kuwa hawasumbuliwi mpaka sasa hivi. Naomba Waziri atamke kuruhusiwa Wananchi hawa waendelee kukaa na kufanya shughuli zao za uchimbaji mdogo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba wafanyakazi wa Hifadhi ya Rubondo, wapewe upendeleo maalum kwa kuwa wafanyakazi wa hifadhi hii muda wote wako vitani kutokana na eneo lenyewe. Naomba yafuatayo:-

(i) Wafanyakazi wapewe motisha au *special allowance* kwa kukaa upweke.

(ii) Watoto wa wafanyakazi hawa wajengewe huduma za jamii kama hospitali na shule, kwa kuwa eneo hili halina hospitali wala shule. Lakini kwa nafasi ya pekee, ningependa nitoe shukrani zangu za dhati kwa kutoa kiasi cha Sh. 2m./= kwa ajili ya ujenzi wa *dispensary* ya Nkome. Ombi langu naomba katika Kata ya Nkome, tumejenga Sekondari, hivyo, Wizara itujengee hospitali ili isaidie watoto wa wafanyakazi kupata elimu.

(iii) Kuwe na usafiri wa uhakika kutoka hifadhini hadi Makao Makuu ya Wilaya, ili kuwawezesha wafanyakazi wawe na urahisi wa kupata huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GIDEON A. CHEYO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa jitihada kubwa za kuboresha huduma katika Sekta ya

Maliasili na Utalii. Mafanikio yanaonekana na mchango kwa uchumi wa Taifa unaongezeka. Nawatachia shime waendelee na jitihada za kuboresha zaidi huduma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo kwa eneo la misitu, Wizara iendelee kudhibiti kwa makini zaidi uvunaji wa miti, unaohatarisha kumaliza misitu yetu, unaohatarisha ardhi yetu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kueneza shughuli za utalii sehemu mbalimbali hapa nchini, naiomba Wizara na Taasisi zake zinazohusika, kufanya uchunguzi katika Mkoa wa Mbeya, hususan Wilaya ya Ileje. Katika utafiti usio rasmi uliofanyika katika Wilaya yetu, umeonyesha vivutio vifuatavyo:-

(i) Katika baadhi ya misitu yetu, wapo mbega weupe na weusi, ambao hawapatikani kwa urahisi hapa nchini.

(ii) Yapo maporomoko ya maji ya Lusalala na mapango ya kale katika eneo hilo la Kata ya Sange, Wilaya ya Ileje.

(iii) Katika baadhi ya misitu yetu, yapo maji safi na meupe, ambayo yanafaa kwa utengenezaji wa maji ya chupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwa na hakika na manufaa ya vivutio hivi, tunaomba wataalam wa *TANAPA* wafikirie kutembelea maeneo hayo, wajionee wenyewe na kushauri ipasavyo. Hizi ni jitihada za kupanua maeneo ya utalii, hususan Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatachia mafanikio mema. Naunga mkono hoja hii.

MHE. SUMRI A. S. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla ya yote, naomba nitoe pongezi tele kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kazi ngumu na ya ufanisi mwangi katika Wizara nzima na Idara zake zote.

Pili, niishukuru Wizara juu ya malengo yote juu ya wanyamapori, utalii, uvuvi, misitu na nyuki. Wizara imeahidi kupanua wigo wa maendeleo ya sekta hizo ili kuleta manufaa kwetu na vizazi vijavyo. Kwa yote hayo, nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, nazidi kuiomba Wizara ifikirie kutupatia msaada wa uchimbaji wa mabwawa katika eneo la Kakese, eneo ambalo linapakana na Hifadhi ya Katavi. Eneo hilo, sehemu linalofikiwa na wanyama toka Hifadhi ya Katati na ni eleo la kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya uvuvi, tunaiomba Wizara iwasaidie wavuvi wetu wa Karema na Ikola, kandokando ya Ziwa Tanganyika, ili waweze kupata ruzuku ya Serikali kwa ajili ya zana hizo za uvuvi, angalau kwa asilimia 40 ya bei. Hali hiyo itaongeza ajira kwa wavuvi wetu na lishe bora kwa walaji wa samaki katika eneo lingine lisilokuwa na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru sana Wizara hii kwa kutusaidia Zahanati pale Jimboni kwangu Sibwesa, Kapalamsenga na maeneo mengine. Nazidi kuiomba Wizara juu ya barabara. Kijiji cha Kapalamsenga kipo kama km. 100 toka Mpanda Mjini. Kijiji hiki kipo katika ufadhili wa *TANAPA*. Ombi la wakazi wa kijiji hiki pamoja nami, tusaidiwe *grader* liweze kuchimba barabara itokayo kijijini hapo hadi Ifume, umbali wa km. 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya inaweza kuchangia mafuta. Eneo hilo ni kiungo kikubwa kwa Wananchi wa kijiji hiki na eneo la Ziwanu Ikola na Karema, ambako kuna kituo cha Afya. Kwa ajili hiyo, tunazidi kuomba msaada wa *TANAPA* kupitia kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nazidi kumtakia afya na furaha Mheshimiwa Zakia Meghji na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa siku hii ya leo, ili niweze kuchangia hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa umahiri wake wa kuiongoza Wizara hii inayoonekana kuongeza mapato nchini. Pia niwapongeze Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mchango mdogo wa kuboresha hotuba hii. Wizara iangalie uwezekano wa kuboresha Pori la Lukwati, kwa kuweka barabara na pia kuboresha maisha ya Wananchi wanaozunguka pori hilo, kwa kupeleka miradi ya ufugaji nyuki na kusaidia kuendeleza uvuvi kwa wale waliopo mwambao wa Ziwa Rukwa, ambako wanyamapori huenda mara kwa mara kunywa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isaidie kujenga Shule ya Sekondari pale Kapalala kama vile Shirika la *TANAPA* lilivyosaidia kujenga darasa moja ambalo limemalizika, kwani eneo lile halina Shule ya Sekondari, licha ya kuwa na Shule za Msingi zaidi ya nane. Tunalishukuru sana Shirika la *TANAPA* kwa msaada ule wa Sh. 3m./=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba kwa heshima kubwa Wizara isaidie kuchimbwa kwa kisima pale Shule ya Kapalala/Kininga, kwani juhudhi za kupata wahisani zimeshindikana na ni eneo ambalo akina mama wanapata tabu sana. Kwa Kijiji cha Gua, tayari wahisani wametusaidia visima viwili ambavyo vinafanya kazi vizuri. Wahisani hao ni wale wa pori wawindaji (*Safari Royal Arusha*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa ushauri kwa Wizara hii kuwa pamoja na pori la Lukwati kuandikishwa rasmi, ninapendekeza kama nalo lingepewa Bodi kama vile *Ngorongoro Conservation* na kadhalika, ingawa pengine utaratibu hauko hivyo. Hii itawenza kuliendeleza pori lile haraka zaidi kuliko kutegemea *TANAPA* au Katavi, kwani Uongozi utakuwa karibu sana na pori lenyewe. Naomba suala hili liangaliwe, siyo tu

kwa pori la Lukwati, hii ni kwa mapori yote yanayoanzishwa kama ilivyo Lukwati. Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara chini ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kulitambua pori hili lenye wanyama wengi na pia kuruhusu kujengwa kwa Ofisi katika eneo la Ngwara. Matatizo kimsingi ni kama ifuatavyo:-

Radia calls, solar power kwa vile hakuna umeme, upatikanaji wa gari la Pori la Lukwati kwa ajili ya doria na matumizi mengine na kusaidia kuboresha barabara ya Saza/Kininga/Gua au Ngwara, ili eneo hili liweze kuitika muda wote. Naomba msaada wa jambo hili ili kuwepo na watalii wa kutosha pamoja na wawindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri pia aangalie uwezo wa kutupatia gari la Maliasili Wilaya ya Chunya. Suala hili lipo mikononi mwake. Namwomba msaada huu haraka ili kudhibiti hali ya *control* ya Wilaya. Hatuna gari na eneo la kudhibiti ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lile zuri, nami nitakuwa bega kwa bega kuendeleza pori lile, tena haraka kama mambo niliyoyaeleza yataweza kusikilizwa. Naomba Waziri na Katibu Mkuu, watilie maanani hayo. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuimudu vizuri sana Wizara yake, licha ya kuwa peke yake. Lakini sote tunaona jinsi anavyochapa kazi pamoja na Katibu Mkuu na Watendaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Naomba Mheshimiwa Waziri ukipata bahati au nafasi ya kutosha, ututembelee kufungua jengo linalojengwa la Meneja wa Wanyamapori wa Lukwati.

MHE. RAPHAEL N. MLOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, Ndugu Solomon Odunga, Katibu Mkuu, Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanazofanya za kusimamia, kuendeleza na kuboresha rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ninataka kuzungumzia masuala mawili au matatu kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, Wizara ya Maliasili na Utalii mpaka sasa haijaweza kutoa ufumbuzi wa tatizo la Wananchi kuondolewa katika Vijiji vya Mgaya na Ng'wagimagi, Kata ya Bulungwa, Kahama. Vijiji hivi vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Kigosi, upande wa Kahama. Tangu waondolewe mwaka 1998, imekuwa kero. Japo nimewomba Mheshimiwa Waziri atoe jawabu, lakini mpaka sasa Wananchi hawajapata chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka huu, mimi mwenyewe nilahirisha kuja kuhudhuria Bunge la Februari, 2004, ili kuungana na Mtaalam wa Misitu kutoka Wizarani, Bwana Erasto Mpemba, ambaye pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa

Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, Diwani wa Kata ya Bulungwa, Maofisa Misitu wa Mkoa na Wilaya, pamoja na Wananchi waliohusika na uwekaji wa mipaka ya Msitu wa Kigosi kulingana na *GN* ya mwaka 1983, tulikwenda kuhakiki mpaka ambao unabishaniwa kati ya Wizara kwa upande mmoja na Wanavijiji na Halmashauri ya Wilaya kwa upande mwingine.

Mheshijiwa Naibu Spika, katika kufanya zoefi hili, mabishano makali yalijitokeza kati ya Bwana Mpemba, kwa upande mmoja na Wanavijiji na Maofisa wa Halmashauri ya Wilaya kwa upande mwingine, juu ya mpaka. Hatimaye uamuzi tuliofikia ni kwamba, Bwana Mpemba aliahidi kuwezesha Wataalam Huru (*Independent Boarder Verifiers*), wahakiki mpaka huo. Mpaka sasa zoezi halijafanikiwa na kila mara nikienda Bulungwa, suala la mgogoro wa mpaka huo limeendelea kuwa kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, nionavyo mimi, Wizara haiko wazi katika suala hili. Mimi naelewa umuhimu wa Hifadhi za Taifa kwa vizazi vijavyo. Naelewa pia kwamba, ardhi yote ya Tanzania ni mali ya Serikali na ina kauli ya mwisho kuhusiana na matumizi ya ardhi hiyo. Hivyo, namwomba Waziri wa Maliasili na Utalii, awe wazi kulieleza suala hili. Haijambo safari hii, katika aya ya 16 ya hotuba yake, Waziri amekuwa wazi zaidi alipotamka kupitia na kuchora upya mipaka ya mapori mbalimbali, pamoja na Pori la Moyowosi/Kagosi, japo haijullikani kwa kutumia *GN* namba ngapi zaidi ya ile ya mwaka 1983 ambayo bado inatambulika kwa Wananchi walio wengi huko Kahama.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tufuatane baada ya Bunge hili hadi Kata ya Bulungwa tukakutane na Wananchi wa Vijiji vya Nyawelwe, Nyamkende, Kagera na Mwadui, ili kwenda kulitolea suala hili ufumbuzu yakinifu.

Pili, Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani za dhati kwa Wizara kukubali kuisaidia Wilaya ya Kahama kukuza ufugaji wa kisasa wa nyuki, ili kuvuna mazao mengi ba bora zaidi yatokanayo na nyuki. Hapa pia nina maombi matatu: Wizara isichoke kuisaidia Wilaya ya Kahama katika kutoa elimu ya utambuzi ya umuhimu wa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi, pia elimu ya usimamizi shirikishi wa misitu na Wizara iwezeshe ujenzi wa barabara ya Bulungwa - Nandekwa, ili kukuza utalii wa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ningependa kurejea wasiwasi wangu nilioutoa mwaka 2003, wakati kama huu, kuhusu uvamizi wa Hifadhi ya Msitu wa Kigosi, unaofanywa na makampuni manne ya Kimataifa ya utafiti wa madini ya dhahabu. Kwa kuwa makampuni haya yanafanya utafiti kwa kutumia watu wengi na bila usimamizi mzuri kutoka kwa Maliasili, athari zinazotokana na zoezi la utafiti huo ni pamoja na uwindaji haramu na wa ovyo wa wanyamapori, ukataji miti ovyo wa msitu wa asili bila vibali na ucharibifu mkubwa wa mazingira. Kwa hili, napenda kurejea rai yangu ya mwaka 2003 kwamba: “*Are we so desperate and, indeed, has the pursuit of the dollar become of so paramount importance as to lead us to destroy, at the flicker of an eye-lid, this priceless heritage which nature has bequeathed to us, we Tanzanians, and only to us we Tanzanians and our posterity, for the human race?*” Mimi nakataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2004/2005.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wapiga Kura wa Jimbo la Lushoto, ninayo haya machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wavunaji wadogo wadogo wa mbao katika misitu ya Magamba Shume, wapewe haki yao ya mgao wa asilimia 40 kama mlivyokubaliana katika kikao cha Chama chao cha *NOFIA*. *Tembo Chipboard* wapewe asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utalii na kuitangaza Tanzania, ni budi lipewe msukumo zaidi. Bado Tanzania haifahamiki huko nje. Nchi jirani zinatambulika kuliko Tanzania, kwa nini? Sisi tuna vivutio vingi, vipi wasio na vivutio wanatambulika kuliko sisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kusimamisha ukataji magogo ovyo na kupeleka nchi za nje. Huo ni moyo wa kizalendo. Usiogope kama unaipenda nchi yako. Tunaunga mkono sana. Ahsante.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii. Aidha, kumpongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Wizara hii imekuwa kioo cha nchi, kwani inahusika na wageni wengi toka nje ya nchi, hasa watalii. Pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii, ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utalii - Korogwe. Eneo la Kata ya Kizara, Wilaya ya Korogwe, linapakana na msitu mkubwa wa *East Usambara*. Lipo eneo zuri sana kwa utalii, ambalo halitumiki, licha ya mimi katika miaka yote kukuomba Mheshimiwa Waziri, unitumie Wataalam wako watembelee eneo hilo. Eneo la kutoka Kijiji cha Bombo - Majimoto - Kwamkale - *Kizara Mission* hadi katikati ya msitu mkubwa mpaka unafika Kijiji cha Kizurai hadi Amani, ni eneo la ajabu sana kwa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako, eneo hili ukipita katikati ya msitu, utaona maajabu yafuatayo: Kuna miti mirefu sana inatisha, kuna upepo wa aina yake, kuna vyura wengi sana sawa na waliopo Kihansi, kuna maua mengi ya ajabu, kuna vijito na mabonde ya ajabu, kuna mbega aina ya tumbili, anayependeza sana na ambaye hapatikani ovyo na vivutio vingi sana vya ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaamini kwamba, Wataalam wa Wizara wakienda huko, watakuliana na mimi kwamba, eneo hilo ni kivutio cha kuweza kuwavutia watalii wengi kutembelea eneo hilo. Uzuri wa eneo hilo unaanzia Kata ya Kizara Korogwe na kupitia katikati ya msitu mikubwa hadi Amani mpaka Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba safari hii mchango wangu huu ufanyiwe utafiti kwa kuwapeleka Wataalam wa Wizara hii huko. Ninashauri kwamba, Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa tayari, nishirikishwe kwa nia ya kuwasaidia na kuwashamasisha Wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kero ya Mamba Korogwe. Vifo vya Wananchi wanaoumwa na mamba, vimezidi hasa katika Vijiji vya Kilole, Korogwe, Maurui, Ngombezi, Lwengera Darajani, Relini, Hale, Kwakinyumbi Stesheni na Mswaha. Ninaomba Wizara ipeleke Wataalam wakawaue mamba hao ili kuwapunguza. Hali ni mbaya sana. Mto Luvu ndiyo tegemeo la Wananchi wengi wa Korogwe kwa maisha yao. Wananchi wengi vijiji vyao viro kandokando ya Mto Ruvu. Kwa hiyo, maji, kufua na kadhalika wanategemea mto huo. Suala hili ni kero, tunaomba sana msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Mkomazi Game Reserve*. Hifadhi ya Mkomazi ipo katika Wilaya mbili, Wilaya za Same na Korogwe. Lakini cha kusikitisha, eneo la Korogwe hatufaidiki na lolote kuhusiana na hifadhi hiyo. Ninaomba sana Korogwe nayo ifaidike na hifadhi hiyo. Pia Wilaya ya Korogwe na sisi tunahimiza hifadhi hiyo sasa itambulike Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii na Ndugu Solomon Odunga, Katibu Mkuu wa Wizara, kwa uongozi wao uliotukuka, wenye mafanikio mengi kwenye sekta hii na wenye upeo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hoja ya Wizara, nataka pia kutumia uzoefu wangu katika Sekta ya Utalii, ambapo ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii (*TTB*), kwa manufaa ya wengi ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ya *TTB* ni ku-*promote* ama kutangaza nchi yetu, ikiwa ni pamoja na vivutio vyake. Kufanya kazi hii, Bodi ya Utalii inashirikiana na wadau wake kwa mfano, *Tour Operators* na wenye Hoteli za Kitalii. Katika kutangaza (ku-*promote*) utalii, *TTB* inashiriki katika maonyesho makubwa (*exhibition*) mbalimbali na kuuza (*market*) Tanzania kupitia matangazo, vipeperushi na kadhalika na pia kutumia Wawakilishi (*Tourist Representatives*) ili kutangaza jina la Tanzania kama *tourist destination*. *Tour Operators* na Mahotelii, wanafanya kazi chini ya Banda la *TTB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya kazi ni ghali kwa mfano, kukodi *square metre* moja katika maonyesho London, Kiingereza ni *pound* 267 au fedha za Kitanzania Sh. 500,000/= . Kwa hiyo, kukodi eneo la *square metre* 200 ni Sh. 100m./= kwa onyesho moja. Pamoja na hayo, gharama za usafiri, vipeperushi na kadalika. Hapo hapo, matangazo ya kibashara ni ghali kwa mfano, *CNN* au *BBC* wanakodisha huduma zao kwa Sh. 25m./= kwa dakika tatu kwa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya soko letu ni moja na ushindani ni mkali. Hivyo, yule anayewavutia wateja wengi ndiyo anayepata watalii wengi zaidi. Katika soko hilo wapo Wamarekani, Waingereza, Wakenya, Waganda, Watanzania, Afrika Kusini na kadhalika. Kwa hiyo, asiyewekeza hapo hapati kitu, ama atapata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kukwepa ghamama na ndiyo sababu wenzetu wote wanatenga fedha za kutosha kushawishi watalii kutembelea nchi zao. Hivi sasa katika bajeti za Mataifa yaliyo karibu na Tanzania, yanatenga mwaka huu kiasi cha *US \$* zifuatazo: Afrika Kusini *\$ 40* milioni, Namibia *\$ 20* milioni, Kenya *\$ 10* milioni na Tanzania *\$1.4* milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia jedwali hili utaona sisi Tanzania tunafanya mchezo katika suala hili. Huwezi kutenga *\$ 1.4* milioni katika soko ambalo unaoshindana nao wanawekeza *\$ 40* milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwa Wizara iamue kwa makusudi kabisa, kuongeza bajeti ya *TTB* kutoka *\$ 1.4* milioni ili kufikia angalau *\$ 5* milioni, kuwawezesha *TTB* kushindana katika soko la utalii wa Kimataifa. Suala hili lisiwe na mjadala sana. Tutafute vianzio mbalimbali toka wadau kwa mfano, *TANAPA, Ngorongoro Crater*, Idara ya Wanyamapor, Misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika eneo la Wanyamapor, Waziri wa Maliasili na Utalii, anaelewa kuwa mwaka 2001 tulikubaliana kubadili mpaka kwa km. 6 katika Mbuga ya *Msanjesi Game Reserve* Masasi ili kuruhusu shughuli za kawaida za Wananchi wa Chingulungu na Namalembro.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi huu ulifikiwa baina ya Mheshimiwa Waziri, Mkurugenzi wa Wanyamapor na Mheshimiwa Mbunge wa Masasi. Uamuzi huu ulikuwa unaondoa malalamiko ya siku nyingi ya Wananchi kuhusu maingiliano kati ya Wananchi na wanyamapor. Ningombaa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ahakikishe mpaka huu unakuwa *demarcated* kabla ya mwisho wa mwaka 2005. Tafadhali naomba suala hili la siku nyingi likamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri sana ya kuongoza Wizara hii muhimu kwa uchumi wa nchi hii. Kazi yake na ya Watendaji wake ni mfano wa kuigwa.

Hata hivyo, nilitaka tu kujua kama kweli Msitu wa Luguza, Mkoani Tanga, wenyewe miti ya kipekee (*ma-tik*), unauzwa na Serikali? Nasema hivyo kwa sababu kuna wanaharakati wa hifadhi za asili walionilalamikia kwamba, msitu huo unauzwa kinyume cha maslahi ya Taifa.

Lakini, la pili, wanasema kuwa Serikali inataka kuuza msitu huo bila utaratibu na sheria za tenda. Wanasema wana habari kuwa msitu ule unataka kuuzwa kinyemela kwa bei poa ya Sh. 4bn./= tu, wakati wao wanakadiria thamani yake kuwa karibu shilingi bilioni 40. Wanaharakati hawa wanadai wataandamana kushinikiza msitu huo kuuzwa, tena kwa njia za kinyemela kwa bei poa. Naomba ufanuzi wa hali halisi.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na Watendaji wote, kwa kuiongoza Wizara hii kwa mafanikio makubwa sana. Wizara hii ni muhimu sana kwa nchi yetu, ambapo pia ndiyo kioo cha nchi yetu kwa wageni wanaotoka nje kuja kututembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, imetueleza kuwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itaendeleza ulinzi wa maisha na mali za Wananchi dhidi ya wanyamapori, kwa kuhakikisha upatikanaji wa risasi na kuwapatia mafunzo ya mbini mbalimbali za kudhibiti wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninaipongeza sana Wizara kwa kuelezea kuwa katika mwaka huu wa 2004/2005, itaendeleza ulinzi wa maisha ya watu na mali zao kutoptaka na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni jambo la kutisha sana tunaposikia au kuona katika vyombo vya habari, vikieleza kuwa wapo watu walioliwa na simba au wanyama wengine wa hatari katika vijiji vyao au mashambani mwao. Vile vile inasikitisha kuona mazao ya Wananchi, yanaharibiwa mashambani na wanyama hawa wa pori. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri na wahuksika wote wa Wizara hii, kulismamia suala hili kwa mafanikio makubwa ili kuwasaidia Wananchi kuepukana na majanga haya ya hatari na ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kuwa sekta ndogo ya uvuvi ina mchango mkubwa katika upatikanaji wa chakula nchini. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla, kulismamia suala hili kwa kuwaunga mkono na kuwasaidia wavuvi hapa nchini, ili kuleta mafanikio makubwa katika sekta hii pamoja na Wananchi wote wa nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, imeeleza kuwa katika kuendeleza kilimo cha mwani, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara itatoa mafunzo kwa wakulima wa mwani 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ukubwa wa nchi yetu na kwa eneo kubwa tulilonalo la bahari hapa nchini, idadi hii ya wakulima 70 wa mwani, ambao watapewa mafunzo mwaka huu 2004/2005, inaweza kuwa ni ndogo sana. Kwa hiyo, ninaiomba

Wizara kuliangalia suala hili na kuongeza idadi hii kwa miaka inayokuja. Pamoja na Wizara kuamua kutoa mafunzo hayo, pia ninaiomba kuwatafutia soko la mwani duniani wakulima hawa, ili waweze kuuza mwani wao bila ya usumbufu wowote na kwa bei nzuri ambayo inaweza kukidhi kufidia ghamama ambazo watatumia pamoja kuwaingizia faida ya kilimo chao hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninachukua fursa hii kuipongeza sana Wizara hii kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu uvuvi bora kwa kurusha vipindi 160 vya Redio na 10 vya Televisheni.

Pmoja na kazi hii nzuri iliyofanywa na Wizara ya kutoa elimu kwa umma kuhusu uvuvi bora kwa njia ya Redio na Televisheni. Ninayo hofu kubwa kama elimu hii iliyotolewa kwa wavuvi kwa kutumia vyombo hivi vya habari, sijui kama walengwa watakuwa wameipata vizuri. Kwani mara nyingi wavuvi huwepo mbali na maeneo yao, kwani mara nyingi huwa wapo katika maeneo yao ya uvuvi baharini au katika maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara kutumia pia mikutano mbalimbali na semina katika maeneo haya ya uvuvi kwa zile saa ambazo itaonekana kuwa wavuvi hao wamerudi katika kazi zao za kuvua. Kama tutaongeza mambo haya mawili ya mikutano na semina, tutaweza kufanikiwa zaidi katika kuwapatia elimu hii wavuvi wetu hapa nchini petu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimnukuu Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hii, amesema kuwa: “Utalii ni sekta ambayo inaweza kuchangia ukuaji wa kasi wa Pato la Taifa”. Katika kutekeleza majukumu yake, sekta hii itakamilisha maandalizi ya utekelezaji wa sera ya utalii, pia itatilia mkazo kukuza na kuimarisha utalii wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninampongeza sana sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii na kweli ninamtakia kazi njema na zenye mafanikio mazuri ya kuiongoza na kuisimamia vyema Wizara hii ambayo ni kioo kwa Taifa letu la Tanzania. Kama alivyotueleza kuwa utalii unaweza kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa kwa kasi sana. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ifanya kazi zake vizuri na kwa mafanikio makubwa ili kuleta mafanikio haya kwa Taifa letu na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hii, ameelezea suala la Utawala Bora. Ninamnukuu Mheshimiwa Waziri, mwaka 2003/2004, Wizara iliandaa mafunzo ya Utawala Bora kwa viongozi wa vyuo, tasisi, Mashirika na wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa mafunzo haya waliyotoa ya Utawala Bora kwa viongozi hawa na ninawataka wasisitize umoja zaidi katika hili kwamba, bila ya umoja katika eneo lolote lile, hatuna Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hii kwa kuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba ya bajeti ya Wizara yake. Aidha, ninampongeza kwa dhati, kwa uchapaji wake wa kazi katika Wizara isiyokuwa na Naibu Waziri. Ameweza kuibua maeneo mengi mapya ya utalii, licha ya yale yaliyozoleka ya Mbunga za Wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa vivutio vimekuwa vingi. Pia jitihada za kufanya utafiti mambo ya kale na kuhifadhi majengo na maeneo ya kihistoria, ni kazi ya kupongezwa. Kazi hii nzuri, naamini haifanyi peke yake, kwa hiyo, ninawapongeza wataalam wanaomsaidia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nipongeze ongezeko la mavuno ya samaki nchini, hasa kutoka maji baridi. Limekuwepo ongezeko la uzito toka tani 26,000 mwaka 1999 kwa thamani ya Sh. 44,018,000/= hadi kufikia tani 301,855 kwa thamani ya Sh. 141,073,500/. Hili ni ongezeko kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko hili, ninapenda kujua wavuvi wadogo wadogo wanashirikishwa kwa kiwango gani katika uvuvi huo. Nashauri waanzishe umoja wao na wasaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuiomba Serikali kudhibiti hali ya amani na maelewano katika visiwa vinavyochangia uvuvi kwa wingi katika Ziwa Victoria, ambavyo ni Kerebe, Makibwa na Bumbire. Visiwa hivi ni maarufu kwa uvuvi wa samaki wazuri, lakini hali ya amani si ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, umbali wa visiwa hivi na Makao Makuu ya Wilaya ya Muleba na Mkoa wa Kagera (Bukoa), ni mbali mno. Napendekeza paanzishwe Kituo cha Ulinzi na Usalama pale pale kisiwani. Pia pawepo vyombo vyta mawasiliano ya kuaminika kama redio na simu, ili wapate msaada wa haraka pale panapotakiwa hivyo. Aidha, wataalam wa samaki waongezwe ili wasaidiane na wavuvi katika uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleweshwe kuhusu watalii wa Kimataifa. Ziko hoteli kubwa za kitalii, lakini utakuta baadhi ya watalii hufikia hoteli ndogo au nyumba za kulala wageni, zisizo na hadhi ya kitalii, hali ninayoiona kwamba, inapunguza mapato ya nchi. Nashauri wageni wote wa kutoka nje wafikie katika hoteli za kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii. Pia napenda kumpongeza Waziri na Wataalam wake wote, kwa hotuba yao nzuri iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina jambo moja tu ambalo ninamwomba anipatie usafanuzi, ni nini kinaendelea. Suala lenyewe ni kuhusu *Moshi Hotel*. Mimi kama mkazi wa Moshi, sielewi nini kinaendelea, ila ninachokiona ni uzio wa mabati katika jengo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli hiyo imefungwa kwa muda mrefu na hii imechangia sana Mji wa Moshi na Serikali kwa ujumla kukosa mapato na siyo mapato tu, hata ajira kwa Wananchi wetu wa Mji wa Moshi wamekosa kutokana na kufungwa kwa hoteli hiyo kwa muda mrefu. Hivyo basi, namwomba Waziri atupatie majibu ili tuelewe kinachoendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, langu ni hilo tu, sina zaidi. Ila ninampongeza Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii, kwa kuitangaza nchi yetu ya Tanzania katika dunia.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ina maelezo ya wazi na takwimu muhimu zinazojibu maswali mengi.

Naunga mkono hoja hii kwa dhati. Kwa upande mwingine, napenda kumpongeza Katibu Mkuu, Bwana Solomon Odunga, pamoja na Wakuu wa Idara na Mashirika ya Umma chini ya Wizara hii, kwa kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na uaminifu uliomjengea Mheshimiwa Waziri mazingira mazuri na hatimaye kumjengea heshima kubwa humu Bungeni na nje ya Bunge. Hongereni sana na endelezeni mambo haya mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii.

MHE. HALIMA O. KIMABU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu na wengine wote wa Idara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ningependa kuanza kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono, ninayo machache ya kushauri, pamoja na yale yote yaliyoongeleta juu ya wavuvi kupatiwa nyenzo kwa bei nafuu na pia uuzaaji wa minofu ya samaki wa maji chumvi, uanze haraka. Ila Wananchi wapewe mikopo ili nao wavue na viwanda wafanye *processing* tu.

Pili, kuna akina mama wanaotengeneza vifaa vya nyumbani (*furniture*) kwa kutumia magugu maji. Hawa wako Bukoba. Naomba hawa akina mama, hebu Wizara iwe karibu nao ili waone jinsi gani ya kuboresha jambo hili. Hawa akina mama wanastahili sifa, kwani wanasaadia kuvuna magugu haya, lakini pia kuongeza ajira na hatimaye kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mkaa kwa Mkoa wa Pwani, sasa limekithiri, miti mikubwa inaisha sasa. Hivyo, tunahama kwenye mkaa, tunaenda kwenye kuni. Mheshimiwa Waziri na hizo kuni zimeenda kwenye kuni zinazoitwa nyasi. Nyasi ni vile vipande vyembamba, yaani vichipukizi vya miti, ambavyo hata havichanjiki wala havichomeki mkaa. Hivyo, vinauzwa na kutumika kama vilivyo. Hii ni kwamba miti hii haipewi nafasi hata ya kuchipua na kuota tena. Sasa naishauri Wizara kwamba, undwe Mfuko wa Mikopo wa Nishati. Nina maana Wananchi wakopeshwe vifaa vya *solar* na *biaogas*, walipe kidogo kidogo hasa Wananchi wa vijiji. Tusaidiane kwa hili, tunanusuru miti kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kazi njema na mafanikio makubwa kwa yote wanayoyafanya. Narudia tena kusema kwamba, naunga mkono hoja hii.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara, kwa kutuandalia hotuba nzuri, yenye kina na kueleweka kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, napenda kupata ufanuzi juu ya nini kinaandaliwa (mpango/mkakati) kwa kuimarisha miundombinu na majengo ya eneo la kihistoria la Ujiji/Kigoma, sehemu ambayo Dr. Livingstone alikutana na Stanley. Endapo hakuna kilichopangwa katika bajeti hii ya 2004/2005, basi hili lizingatiwe katika bajeti ijayo ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa utekelezaji wa haraka wa kuzuia biashara ya magogo nje ya nchi. Hii imeonyesha uhodari wa utendaji wa Mheshimiwa Zakia Meghji, kwani suala lenyewe ni nyeti. Lakini kwa vile ni uamuzi wenye maslahi kwa nchi, ni uamuzi halali kabisa.

Hata hivyo, endapo kuna haja ya kulegeza uamuzi kwa wafanyabiashara wazalendo, ambao bado leseni zao zilikuwa hazijaisha, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa, wasamehewe kwa wakati huu ambao taratibu mpya zitaanza kuandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kuwa ni vyema Wizara ikapatiwa kibali cha kuajiri watendaji wengi zaidi kwa sababu Taifa limeamua kupanua sekta ya utalii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia haya machache, naunga mkono hoja hii na kuwatakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake katika kutekeleza majumu walijotueleza.

MHE. REMIDIUS EDINGTON KISSASSI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya yeze na Watendaji wake na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, pamoja na Wananchi wote wa Jimbo la Ulanga Mashariki. Mwenyezi Mungu, amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo kuhusu uthali: Jithada zaidi zifanywe ili kuitangaza nchi yetu nje, ili watalii zaidi waje kuitembelea nchi yetu, kote Bara na Visiwani. Jithada zaidi zifanywe zipatikane fedha za kuimarisha miundombinu ya uthali, hasa barabara na kwangu Jimbo la Dimani, zipo barabara ambazo zinahitaji kutengenezwa ili tuweze kuimarisha uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kumwomba Mheshimiwa Waziri, atusaidie Zanzibar ili tupate zana za uvuvi wa kisasa kwa njia ya mikopo. Gharama za kuvua ni kubwa mno na wavuvi wetu wengi wameendelea kutumia zana duni na kipato kinachopatikana ni kidogo sana. Naomba sana Wizara zetu mbili, zishirikiane ili tuweze kupata Kiwanda cha Kusindika Samaki na mazao mengine ya baharini kama vile pweza, kamba, mwani na kadhalika ili wavuvi wetu wapate soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie mashine za kuleta ubaridi katika soko letu la kisasa tulilojenga Jimbo la Dimani (*Cold Storage Facilities*), kwani gharama zake ni kubwa mno kwa jimbo letu kuzimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nazidi kumpongeza Waziri na Mungu amsaidie. Ahsante.

MHE. CHARLES H. KAGONJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi nzuri na nzito anazozifanya. Nashukuru pia kwa kuwaruhusu watu wa *Celtel* kujenga mnara katika eneo la Msitu wa Hifadhi, ili jimbo langu lipate huduma hiyo ya simu za mkononi. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashamba ya miti, tunazo fununu kwamba, mashamba haya wangeweza kubinafsisha baada muda mfupi. Kama hivyo ndivyo, basi naomba wakati huo ukifika, wafikiriwe kwanza Wazalendo. Kama ilivyofanyika katika Ranchi za Taifa, basi ifanyike hivyo hivyo kwa mashamba ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vidogo vidogo vya mbao vya Wazalendo, visibanwe wala hata kunyanyaswa. Mheshimiwa Waziri unakumbuka malamiko ya watu wa *NOFIA*, naomba waendelee kupewa mgao wao wa miti ya mbao kama makubaliano yao yalivyokuwa hapo mwanzoni. Nafahamu utakutana nao hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukamata magogo bandarini, tunalipongeza sana. Hata hivyo, ni vizuri ukachukua hatua unazoona zinafaa. Kama uko wizi au uporaji wa maliasili hiyo, chukua hatua kali bila kujali. Kwa sababu jambo hilo ni la hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo kwa kweli ni lazima jambo lifanyike kuhusu kuchukua hatua dhidi ya ukataji ovyo wa miti kwa ajili ya mkaa. Kama hatutachukua hatua za dhati sasa, basi Taifa hili liko njiani kugeuka jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *cultural tourism* ni aina ya utalii unaochanua sana katika Mkoa wa Tanga na hasa Wilaya ya Lushoto. Hata hivyo, naomba msaada wa Wizara kuuweka sawa utaratibu huo, kwani inaonekana utaratibu mzuri kwa utalii wa namna hiyo haupo. Hivi sasa ni msimu hasa wa aina hiyo ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa tisa wa Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameелеza namna Wizara yake inavyotengeneza barabara katika maeneo ya utalii. Naomba barabara ya Mkomazi - Mnazi hadi Umba, iingie katika mpango huo. Barabara hii inapakana na Mbuga ya Mkomazi/Umba. Ingawa barabara hii kwa sasa imepandishwa daraja na kuwa ya Mkoa, lakini bado haijafaidika vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu moto. Hatua kali zaidi zichukuliwe kwa wale wote watakaokamatwa wakichoma moto misitu. Moto una msimu wake na wako watu ambao inaonekana wanafurahia kuchoma moto. Nashauri ziundwe Kamati za Kudumu za Serikali za Vijiji, ambazo siku hadi siku, wataangalia kuzuka kwa moto. Labda sheria ziimarishwe ili kama moto unaleta uharibifu mkubwa, basi Serikali za Vijiji zinaweza kuwajibishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao kwa Wizara yangu. Pia napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wote kwa mchango wao mzuri kwa Wizara yangu. Napenda kuahidi kwamba, mawazo na mapendekezo yao yote walijyota tutayafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue nafasi hii, kumshukuru Msemaji Mkuu wa Upinzani Bungeni kwa sekta hii, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mbunge wa CHADEMA, Moshi Mjini. Napenda kumshukuru kwa mchango wake alioutoa hapa leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii, kuwashukuru kwa dhati Wabunge wote waliochangia katika hotuba yangu na kama ulivyo utaratibu, Wizara imepokea mawazo na mapendekezo haya na itayafanya kazi. Siku zote tunasema kwamba, mawazo ambayo tunayapata ndani ya Bunge lakini hata nje ya Bunge ambapo tunazungumza na Waheshimiwa Wabunge ni mapendekezo mazuri na ambayo yanatoa

challenge kubwa kwa Wizara yetu. Kwa hiyo, yote ambayo mmeyazungumza kwa kweli tutayafanyia kazi na nasema kwamba, inatupa hamasa mpya, mimi binafsi pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa sekta hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwatambua wale ambao wamechangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na kwa kuandika. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Msemaji Mkoo wa Upinzani, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Maria Watondoha na Mheshimiwa Omar Kwaangw', ambaye alikuwa mchangiaji wa mwisho na alisema kwamba, haungi mkono hoja yetu. Tutajaribu kujibu hoja yake. Kwa hiyo, wote nawashukuru kwa michango yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwatambue wale ambao wamechangia kwa maandishi, nao ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, Mheshimiwa Parmukh Singh Hooga, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Eliachim Simpara, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na Mheshimiwa George Mlawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Shaib Ahmada Ameir, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Sumri Mohammed, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna wengine pia ambao napenda kuutambua mchango wao uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge hao wakati wakichangia Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Hotuba ya Bajeti na Hotuba ya Waziri Mkuu. Nao ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Christopher Wegg, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi. Nawashukuru wote hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba radhi kwamba, kama kuna wengine ambao sikuwataja, basi nitakuwa napokea karatasi na kuwataja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kushukuru kwa michango yote hiyo na pia kusema kwamba michango imekuwa *challenge*, michango ambayo kwa kweli nitaifanyia kazi katika kipindi hiki na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge, watakuliana na mimi kwamba, kwa muda niliokuwa nao, itakuwa ni vigumu sana na utakuwa ni unafiki kusema nitaweza kujibu hoja zote hizo. Kwa hiyo, nitajibu baadhi ya hoja lakini pia kwa wale walioandika tutajibu hoja hizi kwa maandishi kama ilivyokuwa desturi yetu. Kwa hiyo, nitagusia baadhi ya hoja hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia upande wa sekta ya utalii na hapa imetolewa *challenge* katika upande wa utalii kwamba, pengine ingewezekana kabisa utalii ungeweza kukua zaidi na kwamba sera yetu imekuwa ni sera ya *quality tourism* na sio *mass tourism* na kuna mifano mbalimbali ambayo imetolewa. Pamoja na hayo imezungumziwa kwamba, utalii wetu ni utalii ambao ni ghali sana kwa watalii ambao wanakuja nchini kwetu. Sasa labda niseme kwamba, kwanza kabisa ni muhimu kuelewa tunakotoka na hatua tulizopiga. Napenda kusisitiza kwamba, utalii wetu ni tofauti na nchi jirani, aina ya utalii tunaotilia msisitizo ni ule unaojali mazingira. Ningependa kusisitiza hapa kwamba, kwa kweli nafikiri tunakuwa tunajidanganya mara nyingine tukisema kwamba, kwa kujali mazingira au *quality tourism* ni kwamba, tunakuwa na watalii wachache na fedha chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni sekta ambayo inategemea sana mazingira, ndio maana hapa tumezungumzia maliasili, inategemea suala zima la wanyamapor, misitu, uvuvi na kadhalika. Leo hii tukimaliza misitu na nitakuja katika suala la misitu hatutakuwa na misitu hiyo na kwa maana hiyo, tukimaliza wanyamapor pia hatutakuwa na wanyamapor. Siku zote tunasema kwamba, wanyamapor hawana *passport*, wana-*move* kutoka nchi moja na kwenda nyingine na wana-*move* kutoka nchi ile ambayo *environment* si nzuri na kwenda katika *environment* ambayo ni nzuri. Kwa hiyo, kama tunazungumzia utalii ambao tunataka maliasili hii iweze kudumu kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo, lazima kwa kweli tujali utalii ambao unajali mazingira. Napenda hili tukubaliane nalo kama sera yetu, sera ambayo pia hata tukizungumzia Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia inajali mazingira katika sera yake na nashukuru kwamba, nilikuwa mmojawapo ambaye nilishiriki katika kuitengeneza sera hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sekta hii kwa kweli imejitahidi sana. Nakubali kwamba, kumekuwa na matatizo kidogo ya fedha ambazo pia zinatengwa katika upande wa utangazaji wa uthali na kweli mmeefananisha na nchi mbalimbali. Kwa mfano, Kenya wanatoa Sh. 10bn/= kwa ajili ya utangazaji wa uthali, Afrika ya Kusini ni Sh. 40bn/= katika utangazaji wa uthali, Tanzania ni Sh. 1.2bn/=, nafikiri mwaka huu. Kwa hiyo, ukifananisha fedha ambazo tunazo kwa utekelezaji wa uthali na kile kinachopatikana kwa kweli nafikiri ni vizuri kuwapongeza wale watu wanaofanya kazi hizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Tanzania Tourist Board* inashirikiana na *TANAPA*, kwa mfano, katika kutangaza uthali, wanashirikiana na Ngorongoro, lakini pia hushirikiana na sekta binafsi. Zote hizi kwa kweli zinafanya kazi nzuri na kubwa na kuna mifano ambayo ningependa baadaye kuitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mafanikio mbalimbali ambayo yamepatikana. Kwa mfano, kwanza kabisa, kuondoa dhana potofu kwamba baadhi ya vituo vyetu vipo nchi jirani. Hivi sasa wakala wengi wa nje wanajua kwamba, Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro vipo Tanzania. Hili linajulikana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwamba, kuna watalii wanaopitia nchi jirani. Zamani watalii hawa walipoteremka katika nchi jirani walikuwa kwanza wanaanza kutalii katika nchi ile baadaye labda ndio wanakuja Tanzania. Lakini hivi sasa kwa utafiti ambaao tumeufanya, ni kwamba, zaidi ya asilimia sitini ya watalii wanaoshuka nchi jirani ni kwamba, wanateremka tu kwa sababu ya bei au gharama ya nauli. Gharama ya nauli kutoka kwa mfano, Uingereza kwenda nchi jirani ambayo tunaizungumza ni chini ukifananisha na gharama hiyo hiyo kuja Tanzania. Kwa hiyo, watalii wengi wanakwenda nchi jirani na kwa utafiti uliofanywa wanasema mara nyingi sana siku hiyo au siku ya pili yake wanapanda magari kuja Tanzania. Mara nyingine pia tunajua kwamba, ndege zinajaa sana hivi sasa, kwa kweli ndege nyingi sana zinajaa. Nafikiri jana au juzi mlisoma kwenye gazeti kwamba, hata mahoteli katika *Northern Circuit* yote yamejaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta kwa mfano, *KLM* ambayo ilikuwa inakuja mara moja au mbili sasa hivi inakuja kila siku lakini inajaa. Kwa hiyo, inabidi watalii wanaotaka kuja Tanzania wapande ndege kwenda nchi jirani ili waweze kuja hapa. Nasema kwamba, hili bado tunalifanyia kazi na tunasema kwamba, Balozi zetu kwa kweli zinafanya kazi, tukisema hapa kwamba, Balozi zetu hazifanyi kazi si sahihi.

Kuna Balozi ambazo zinafanya kazi nzuri na hasa mwaka huu kulikuwa na mkutano wa Balozi kule Ngorongoro. Tulikwenda tukazungumza na tunatambua kwamba, kuna baadhi ya Mabalozi wanafanya kazi nzuri, wameleta *groups* za watalii na naweza kutaja, kwa mfano, Balozi wetu wa China. Kwa muda mrefu sana tumetaka watalii kutoka China, lakini utaratibu wa Wachina ili watalii waje nchini kwenu ni kwamba, kuna *MOU* lazima mtiliane Mkataba kati ya nchi na nchi, ndipo ambapo wanawenza kuja katika nchi hiyo ama sivyo atakuja labda mmoja, lakini hakuna utaratibu

ule wa *Tour Operators*. Nampongeza Balozi wetu wa China, Balozi Sanga amefanya kazi nzuri sana kwa kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnavyoolewa kwamba, Rais wetu alipokwenda China kipindi kilichopita, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alisaini makubaliano kati ya China na Tanzania kwa upande wa Utalii. Tayari tumeshapeleka majina ya kampuni zile ambazo watashughulika nazo na wao wametuletea pia majina ya kampuni ambazo tutashughulika nazo. Kwa hiyo, naamini kabisa muda si mrefu tutawaona Wachina nao wanakuja hapa nchini kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo ni kwamba, nchi yetu imeweza kupata tuzo mwaka 2003 kwa kuwa na vivutio bora kwa nchi za Kusini mwa Afrika. Mwaka 2000, pia Tanzania ilipata tuzo ya utalii unaomjali kila mtu (*To do 99*) iliyotelewa Ujerumani na hadi hivi sasa ndio nchi pekee Barani Afrika iliyopata tuzo ya aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hiyo, filamu bora ya kutangaza utalii ya dakika kumi na moja ya *CD Rom* yenye kauli mbiu "*Tanzania Authentic Africa*" ama kwa Kiswahili "*Tanzania Afrika Asilia*", ilishinda tuzo ya dhahabu ya *golden campus*. Hii ilikuwa mionganoni mwa kampuni za filamu za utangazaji wa vivutio vya utalii duniani. Tuzo hiyo ilitolewa mwezi Machi, 2004 kwenye maonyesho ya kule *Berlin ITP*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Visiwa vyetu vya Zanzibar vimepata tuzo ya kuwa visiwa vyenye vivutio bora zaidi Barani Afrika na Mashariki ya Kati, kati ya Visiwa vilyvypo kwenye ukanda huo. Kwa hiyo, hayo kwa kweli ni mafanikio na lazima tujivunie mafanikio hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni kuongezeka kwa idadi ya watalii wa nje kutoka watalii 230,000 mwaka 1993 hadi kufikia watalii 576,000 mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato pia kutokana na utalii yameongezeka kutoka dola za Kimarekani 146,000,000 mwaka 1993 hadi dola za Kimarekani 731,000,000 mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Freeman Mbwe, alizungumzia juu ya takwimu zilizokuwa katika kitabu na akaonyesha kwamba, mwaka 1999 takwimu zilikwenda juu. Lakini niseme kwamba, takwimu zilikwenda juu kwa sababu ulikuwa ni wakati wa *millennium* na watu wengi pia walikuja Tanzania na hata wengine walikuja kufunga ndoa juu ya Mlima Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Bodi imeweza kuanzisha Ofisi za Wakala mbali ya Balozi zetu kwa kusaidia kutangaza Tanzania huko Marekani, Ujerumani na Ufaransa na mwakilishi aliyepo Ujerumani atahusika pia na nchi ya Austria na Uswiss.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, ukuaji wa sekta ya utalii ambao kwa sasa unachangia kwenye Pato la Taifa zaidi ya wastani wa asilimia kumi na sita umekuwa chachu ya maendeleo ya sekta nyingine kama vile viwanda, kilimo, mawasiliano, usafirishaji na kadhalika, kwa sababu utalii kwa kweli ni *multisectoral*. Pale utalii unapokua basi sekta nyingine pia zinakua na pale sekta nyingine zikidumaa, utalii nao unakuwa *affected*. Kwa mfano, ukizungumzia *infrastructure*, kwa mfano, barabara zikiwa mbovu, watalii hawawezi kufika maeneo mengine na hivi sasa kama tunavyoolewa, kwa mfano, barabara ile ya Ngorongoro hivi sasa italeta mabadiliko makubwa sana katika sehemu za Kaskazini. Lakini pia upande wa Kusini au *Southern Circuit* ambapo tumetangaza Daraja la Mkapa pamoja na barabara, hayataleta mabadiliko makubwa sana katika sekta hii kwa Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo, nchi yetu imeathirika kwa sababu siyo kisiwa. *Tourism* ni sekta nyeti sana kwa sababu inahusu watu kusafiri kutoka nyumbani kwao kwenda nchi nyingine, kwa hiyo, ni nyeti. Pale ambapo wanaona kwamba, kuna matatizo kidogo hata duniani, basi watu hawasafiri, kwa mfano, vita vya Iraq ambavyo vilikuwepo au *Travel Advisory* ambazo zinatolewa mara nyingine na nchi hizo, kwa mfano, labda Marekani wanaweza kutoa *Travel Advisory* msiende nchi za *East Africa* labda na kadhalika. Kwa hiyo, hizi zote zinaathiri kuja kwa watalii, ni sekta nyeti sana na ndio maana tukasema kwamba, hivi sasa tunapanua wigo kwa maana moja, utalii wa ndani lakini pia utalii wa nchi zingine badala tu kutegemea nchi za Magharibi tu, tumeona pia tutegemee nchi za Urusi, China na kadhalika ili lolote linalotokea katika sehemu moja lisweze kuathiri utalii wetu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya jitihada hizo za kukuza utalii na kama Waheshimiwa Wabunge hapa walivyosema, kwa kweli mara nyingine katika hoteli zetu vijana ambao wanaajiriwa ni vijana wa nje. Kwa hiyo, Serikali ya Ufaransa kwa upande wake, imeshatenga *Euro 4.7* milioni ili kuweza kusaidia Tanzania kwa upande wa ujenzi wa Chuo ambacho kitachukua wanafunzi mia tano kwa mwaka katika ngazi ya cheti. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, amezungumzia suala la Makampuni ya Utalii. Ni kweli kabisa, Mheshimiwa Ndesamburo ni mfanyakibashara upande wa utalii, ana kampuni ya kupanda Mlima Kilimanjaro, ana hoteli nzuri pale Moshi, lakini nafikiri Mheshimiwa Ndesamburo, sijawahi kumwona mie hata siku moja katika maonyesho ya utalii au watu wangu wanasema hajawahi kwenda kwenye maonyesho ya utalii. Ningependa kwa kweli kumhamasisha Mheshimiwa Ndesamburo, aende katika maonyesho yetu na aone na tukijaliwa mwaka kesho tukiwa hapa, atawenza kuzungumzia ni nini ambacho kinafanyika. Mwaka 2003, Banda la Tanzania lilipata tuzo katika nchi za *SADC* kama Banda Bora kwa upande wa Tanzania. Kwa hiyo, ushirikiano mkubwa unapatikana kutokana na *private sector* na *private sector* hii niseme kwamba, wanasaidiwa, kwanza kabisa, msaada ambao unapatikana ni kwamba, wanalipia nusu tu ya malipo ya banda lile ambalo tunalikodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nauli za ndege huwa tunazungumza na kampuni za ndege, kwa mfano, *KLM* ambao wanatoa nusu au asilimia hamsini tu ya nauli kwa kwenda katika sehemu mbalimbali hizi ambazo kuna maonyesho haya. Kwa hiyo, tayari kwa kweli Wizara au Serikali inasaidia sana kwa vitu hivi.

Niseme kwamba, wengi wanataka kuja lakini mara nyingine wanachelewa hata nafasi wanakosa. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, kwa kweli ningekukaribisha uweze kuhudhuria. Lakini labda niweke takwimu sawasawa tu. Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, alisema kwamba, kuna Makampuni 148 na kati ya hayo 48 yanamilikiwa na wazawa na mengine na Watanzania wasio wazawa. Nataka kuweka sawa tamko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, sera ya uzawa siyo sera ya Chama cha Mapinduzi. Sera yetu ni ya kuwaendeleza Watanzania wote. Takwimu pia zinaonyesha kwamba, hadi tarehe 30 Juni, 2004 tuna Makampuni 282 na siyo 148. Kati ya hayo Makampuni 150 yanamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100 na zilizobaki kwa ubia. Aidha, huduma za kahawa ni kwa Watanzania tu. Kwa hiyo, kwa upande wa ukodishaji wa magari utaratibu ni kwamba, ni kwa ajili ya Watanzania pekee yao na pia vilevile Mheshimiwa Philemon Ndesamburo anaewela kwamba, shughuli za kupandisha Mlima wa Kilimanjaro ni kwa ajili ya Watanzania pekee yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilozungumziwa ni juu ya suala la leseni na labda niseme kwamba, hivi sasa tuko mbioni kurekebisha Sheria ya *TARA*. Napenda kusema kwamba, pamoja na Wizara ya Fedha kurekebisha mambo mengi tu katika leseni, lakini Sheria ya *TARA* nayo pia nafikiri itaangalia masuala mbalimbali na mapendekezo mengine ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine labda niseme kwamba, katika upande wa kutangaza matangazo, hapa lilizungumziwa kwamba, labda Wizara ingetumia *CNN* na kadhalika. Napenda kusema kwamba, *TTB* inayo Tovuti hivi sasa na pia imefanya Mkataba na *ATC* pamoja na *Commission Zanzibar* ili kutumia *CNBC* ambayo nayo pia itatumika kama kutangaza Tanzania kwa *Euro* 50,000 kwa miezi mitatu. Tulipouiza *CNN quotation* ambayo tulipewa japokuwa tulijaribu kujadiliana nayo, lakini hawakukubali wakasema *quotation* ni *Euro* 250,000 kwa miezi mitatu. Hiyo itakuwa *one third* ya bajeti nzima ya *TTB*, lakini *otherwise* kwa kweli *CNBC* tunafanya utaratibu wa kuweza kuitangaza Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa ni juu ya Mfuko wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo. Niseme kwamba, suala la wavuvi wadogo wadogo limekuwa linajitokeza mara nyingi sana na ni nia ya Wizara yetu na sera yake kusaidia wavuvi wadogo wadogo. Kwa hiyo, hivi sasa tuna Mradi wa *MASEP* na mradi huu wa *MASEP* utakuwa hasa na nia ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo ambao watakuwa na uwezo wa kununua vyombo imara na zana bora za uvuvi na vyombo hivyo vitawawezesa wavuvi kuvua samaki kwenye maji ya kina kirefu, ambayo yana samaki wengi na hivyo kuwaongeza mapato yao ya samaki. Kwa hiyo, tunatumai kwamba,

Programu hii ya *MASEP* itasaidia pia kuondoa umaskini kwa wavuvi na kutakuwa na Mfuko Maalum ambao utasaidia hasa hasa vikundi vya wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la doria, kulingana na Mkakati wa Doria Kitaifa, Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi kutakuwa na Vituo vitatu ambavyo ni Tanga, Bagamoyo Mbegani na Mtwara. Hivi sasa Kituo ambacho kimekwisha kuanzishwa ni kile cha Mbegani. Kituo hicho kina boti mbili za doria, moja ya mita saba na nyingine ndogo. Aidha, meli ndogo ya Chuo cha Uvuvi Mbegani, pamoja na ndege ndogo ya kukodisha kutumiwa kufanya ukaguzi wa meli baharini. Pia boti 13 za Hifadhi za Bahari na maeneo tengefu hutumika kufanya doria katika maeneo ya Hifadhi yaliyopo Dar es Salaam, Mafia na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, labda niseme aliulizia juu ya suala la kujenga soko kule Kilimani Zanzibar. Mtakumbuka kwamba, nilijibu swalii hili hapa Bungeni. Tumezungumza na wenzetu wa Japan na hata juzi juzi wakati niko Mwanza tulizungumza na Balozi wa Japan akasema kwamba, tusubiri. Kwa hiyo, hatuna la zaidi isipokuwa kuweza kusubiri. Hilo ndilo naweza kulisema, sitawenza kusema zaidi ya hapo kwa sababu ni maombi ambayo tumeomba kutoka nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mkakati gani wa ufuatiliaji wa udhibiti wa meli za uvuvi eneo la *deep sea* na nje na zipo boti ngapi za uvuvi kwenye Bahari Kuu. Niseme kwamba, utaratibu ambao unafanywa ni kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, *Navy, Marine Police, TRA* na KMKM kwa upande wa Zanzibar, kwa ajili ya kufanya doria za pamoja umeanzishwa. Utaratibu wa kuendesha doria za pamoja na nchi jirani umeanzishwa. Kwa mfano, hivi karibuni mwezi wa Septemba, 2004, zitafanyika doria za pamoja kati ya nchi yetu na Msumbiji na pia umeanzishwa utaratibu wa kupeana taarifa kuhusu meli zenye sifa mbaya kutoka nchi mbalimbali. Meli zipatazo 73 zimepewa leseni kutoka Tanzania Bara kwa ajili ya kuvua kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma meli nyingi sana zilikuwa zinavua bila ya kuwa na leseni, lakini tumekuta kwamba, baada ya kufanya *patrol* na hasa kwa msaada wa programu ya *EU* katika masuala ya *surveillance* kwa kutumia boti, lakini pia kutumia ndege, tulipotumia ndege walishanka. Kwa hiyo, hivi sasa kwa kweli leseni zimeongezeka zaidi. Hivi sasa niseme kwamba, kuna mkakati wa kuzungumza wa *EU* katika programu ambayo *EU* itahakikisha kwamba, inalipa kabla meli hazijavua katika Bahari Kuu. Mkakati huu kwa kweli ambao tumezungumza na *EU* na hivi sasa tumewaandikia pia wenzetu wa Zanzibar na tutazungumza baada ya hapo kwa upande wa *EU* katika Mabaraza yao pamoja na Tanzania pia kwenye *Cabinet* yetu kabla ya kufanya maamuzi yoyote yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nizungumzie juu ya masuala ya magogo ambayo kwa kweli yamezungumzwa sana hapa. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa wote ambao wameniunga mkono. Nikawa najiuliza nasema kama ingekuwa hatujafanya hivi sijui ingekuwa vipi? Lakini labda niseme kuwa, naelewa hisia mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge waliozungumza juu ya msamaha. Lakini labda niseme kuwa, Sheria ya Misitu tulipitisha sisi Wabunge hapa na kilichofanyika *actually*

ni kusimamia na kutekeleza sheria hii. Si sahihi na napenda kusema kwamba, hakuna mtu aliyekuwa anamtafuta mtu. Mimi nilikuwa simtafuti mtu yeyote. Sheria tulipitisha hapa na taratibu pia zilitolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi tarehe 29 Januari, 2004, nilionana na wafanyabiashara wa magogo, tukazungumza kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, 2004, ndiyo mwisho wa kusafirisha nje magogo ya aina yoyote. Kwa sababu sheria ya zamani ilikuwa inaruhusu kusafirisha nje magogo ya aina mbili tu, magogo mengine yalikuwa hayasafirishwi, tulikuwa tunasafirisha aina mbili tu, mitiki na pangapanga. Sasa tukasema kwamba, kama vile tunavyofanya kwa maliasili, sisi hapa tunapiga kelele siku zote kwamba, tuongeze thamani, korosho tuongeze thamani, kahawa tuongeze thamani, samaki tuongeze thamani na pamba tuongeze thamani. Sasa magogo kwa nini tusiongeze thamani? Ni suala la kuongeza thamani ili Wananchi wetu waweze kupata kazi pia katika viwanda vyetu na ili tupate fedha zaidi kwa maendeleo ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, tulipitisha hapa sisi sote. Kwa hiyo, ilipofika tarehe 30 Juni, 2004, ndiyo ilikuwa siku ya mwisho. Lakini kama vile Waheshimiwa Wabunge walivyozungumza ni kwamba, kuna baadhi ya watendaji amba walikiuka mambo haya na katika kukiuka hata kama huwezi kumkamata ukasema ni rushwa lakini kuna viashirio vya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *authorization* inasema mpaka tarehe 30 Juni, 2004, Profesa Idd na napenda kumtetea alisema, *authorization* mpaka tarehe 30 Juni, 2004, lakini baada ya hapo ikatolewa *export permit* na hizi *export permit* ni za mwezi mmoja mmoja. Kwa maana hiyo, mtu aliyetoea *export permit* angetakiwa iishie tarehe 30 Juni, 2004. Lakini kitu cha ajabu hata *export permit* zilitolewa mpaka tarehe 30 Juni, 2004 na zile *export permit* kitu cha kuchekesha, badala ya *export permit* kuwa tarehe 30 Juni mpaka tarehe 30 Julai, 2004 labda zilikuwa tarehe 30 Juni, mpaka tarehe 17 Julai, 2004. Kwa hiyo, zile karatasi hata kisheria hazina maana ni karatasi tu. Ni kama vile uwe na *passport fake*, haina maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukasema tusimamie na hasa Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Kamati ya Maliasili na Mazingira, wamefanya kazi nzuri kwamba, magogo yanakatwa kila siku tumezungumza hapa Waheshimiwa Wabunge, ukigeuka huku magogo, ukigeuka huku magogo, tukasema hapana, basi kwa hiyo siku ile tarehe 2 Julai, 2004, nikaona tayari nikaenda *Port* na kufika *Port* tukakuta makontena pale, kwa hiyo, ikabidi tuyazuie. Kwa sababu kuruhusu ni kusema kwamba, mimi nimevunja sheria pia. Lakini katika kuzuia ikabidi tuangalie kwa sababu sheria inaruhusu, Sheria hii ya Misitu inaruhusu na yote tuliyofanya ni ya kisheria, inaruhusu kama Serikali ina wasiwasi na kitu basi inaweza kufungua na hilo ndilo tulilofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukasema kwamba, wenye makontena wawepo na tukawapelekea barua, mimi kila siku nahakikisha barua zimewafikia mkononi na kusaini kila kitu by *dispatch* kwamba, ikifika tarehe 26 Juni, 2004, jamani wanapigiwa simu njooni, wanasema tunakuja kesho hawaji, ikaja Kampuni moja, halafu juzi Kampuni

ya pili. Tukasema sisi ikifika tarehe 26 sheria tunayo kwamba, tutafungua bila ya wao kuwepo. Lakini pia sheria ni kwamba, baada ya siku 30 basi makontena yote yanataifishwa na utaratibu wa kuyataifisha utafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa kwa makontena yale ambayo tumefungua ni kwamba, kwanza tumeona kwa sababu kuna watu wengine walisema hawatukuja, kuna makontena matatu yameanza kufunguliwa lakini nusu ya makontena yana magogo ambayo hayajapigwa nyundo maana yake ni kwamba, hayakulipiwa. Mheshimiwa Freeman Mbewe, anauliza juu ya fedha kwa upande wa misitu, basi tufanye hivi halafu tuone mwaka kesho tutakuwa na fedha kiasi gani. (*Makofi*)

La pili, mengine yakaonekana kwamba, kulikuwa na magogo ambayo hata sheria ile ya zamani hairuhusu mbali na hii mliyotunga juzi. Kwa sababu sheria hii ya zamani kuna magogo ambayo yalikuwa hayaruhusiwi. Kama nilivyosema kulikuwa na magogo ya aina mbili yanaruhusiwa. Kwa hiyo, magogo ya aina nyingine yalikuwa hayaruhusiwi, lakini *still* kwenye makontena kukaonekana magogo hayo bado yanasafirishwa nje. Lakini jana tarehe 26 Julai, 2004, makontena manne yalihakikiwa na yalipatikana pia magogo ambayo hayaruhusiwi kwa sheria ile ya zamani. Lakini pia ndugu zangu kuna magogo mawili ambayo yameonekana yana vifuniko haijulikani kwa sababu wale wakisogeza kifuniko kinaenda ndani. Kwa hiyo, leo wanachunguza kule ndani kuna kitu gani? Sasa hayo ndiyo ambayo kwa kweli mpaka sasa hivi yanaendelea na ndugu zangu kwa kweli naomba kama mlivyosema, mniunge mkono. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wamezungumza kwamba, kuna makontena yaliyokuwa pale bandarini yakishahakikiwa yasafirishwe. Kisheria ni kwamba, kontena likikutwa na magogo ambayo hayana nyundo ni makosa, kwa hiyo, inabidi kupelekwa Mahakamani na tayari mwenye makontena matatu ya kwanza utaratibu wa Mahakama umeshachukuliwa. Mmesema kwamba, kwa yale ambayo hayana matatizo basi yaruhusiwe na kwamba kuna mengine yako kwenye misitu na kadhalika. Kama nilivyosema awali ni kwamba, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inajali mazingira, inajali Wananchi wake na inataka kuondoa umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kwamba, tukisema *blank statement* kwamba tutoe miezi sita, tutapata matatizo ndugu zangu. Kwanza, misitu ndiyo itaisha kabisa lakini *blank statement* kama hizo kutakuwa na rushwa nyingi tu. Mimi ningefikiria kwamba, kama kuna watu wa aina hiyo na ambao tunasema kwamba, wamechukua mikopo kutoka benki na nyumba zao zitauzwa, Serikali haitaki kuleta umaskini kwa Wananchi wake. Tutakachowea kukubali ni kwamba, tuhakikishe basi hiyo *individual* mmoja mmoja. Mmoja mmoja nina mkopo benki, benki gani hii, haya tunapata maelezo. Magogo yangu haya yanakwenda kuangaliwa *physically* na halafu lini yanasafirishwa, yanasafirishwa tarehe fulani, meli gani, meli hii basi utaratibu huo utawezekana. Lakini kwa kweli kabisa mimi kama Waziri wa Maliasili na Utalii, nitaona vigumu sana kuweza kukubali *blank statement* ya kusema tuwape miezi sita wote wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la *hunting blocks*, ambalo lilizungumzwa. Niseme kwamba, kuna *hunting block* 42, wageni 15, Watanzania 19 na ubia 8. Lakini niseme kwamba, hivi sasa ni kama miaka hata minne au mitano pale ambapo *hunting block* inakuwa *vacant* tumekuwa tunawapa Watanzania na tunawapa Watanzania ndugu zangu bila kujali Mtanzania ametoka Kaskazini au Kusini. Kwa sababu tukisema *blocks* za Kaskazini watu wa Kaskazini na *blocks* za Kusini watu wa Kusini, tutapata matatizo katika nchi hii. Kwa hiyo, *blocks* zitakapokuwa *vacant*, kwa kweli Watanzania ndiyo ambao wanapata nafasi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mheshimiwa Omar Kwaangw', alieleza kutokuunga mkono hoja yangu hii. Labda niseme kwamba, suala la Mheshimiwa Omar Kwaangw', kama tunalikumbuka lilikuwa kama miaka minne au mitano iliyopita. Lilikwishawahi kuzungumzwa hapa Bungeni na kuna wakati liliuja Azimio hapa tukalirudisha Azimio hilo, lakini baadaye utaratibu ukaonekana kwamba, maeneo yale yalikuwa katika iliyokuwa Wilaya ya Mbulu. Kwa hiyo, mawasiliano yakafanyika na Mashamba Na. 1, 2, na 3, hivi sasa hati zimeshapelekwa *TANAPA*, baada ya mazungumzo kufanyika na baada ya maelewano kupatikana. Kwa hiyo, mtakumbuka hata Mheshimiwa Omar Kwaangw', kwa kweli mwaka 2003 na mwaka 2003, hajalizungumzia suala hili, kwangu mimi lilikuwa ni suala ambalo limemalizika. Baada ya kusema hayo, namwomba Mheshimiwa Omar Kwaangw', aiunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nirudie kuwashukuru tena nyote kwa mawazo yenu ambayo tutayafanya kazi, najua kwamba, mengi hatujayajibu, lakini tunayo kwenye makaratasи hapa tutawaandikia. Naomba kwa heshima na taadhima, mniunge mkono ili tuweze kufanya kazi iliyokuwa mbele yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, yuko pale alikuwa ananisaidia kuandika andika. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii

Kif. 1001 - *Administration and General* Sh. 1,632,956,400/=

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 1001, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Wakati nachangia nilimwomba kwa heshima zote kwamba, katika utekelezaji wa *operation* ya magogo Wananchi walipigwa na kwenye pacha ya kwenda Nanjilinji au Nainokwe na Njinjo imewekwa *block* ambapo Wananchi wanadhalilishwa. Bahati mbaya wakati Mheshimiwa Waziri, anafanya majumuisho hajanipa jibu. Naomba maelezo.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba, nisingeweza kujibu yote japokuwa nilikuwa naye hakunieleza. Lakini niseme kwamba, hili la Mheshimiwa Omar Chubi la kupigwa, nimelisikia sasa hivi na labda kwa wale ambao walipigwa pengine wangeweza kutumia sheria kwa maana ya kwenda Mahakamani ili kwa wale ambao walihusika wafanyiwe hivyo kwa sababu hatuna taarifa yoyote ile. Taarifa ninaipata hivi sasa.

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni nchi ya amani na utulivu, kama Serikali imetoa kibali kufanyika *operation* maalum na kama Wananchi wanapigwa halafu tunaambiwa waende Mahakamani, jambo hili kwa kweli linatisha! Mimi bado nataka Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba, kama hilo limetokea kama Maafisa wake walitoa hilo agizo au ni watu tu ambao wanajifanya Maafisa wa Wanyamapor, wanadhalilisha watu kwenye Jimbo langu, jambo ambalo kusema kweli linakatisha tamaa. Kwa sababu *Star TV* inafika kule kwangu wananiangalia, naomba Mheshimiwa Waziri, aseme juu ya hili jambo kwa sababu ninao watu wamekuja kunilalamikia na hilo ni tatizo la kutaka kutuchafulia mambo yetu yanayokuja. Naomba maelezo ya kina.

MWENYEKITI: Ningependa sana kumruhusu Mheshimiwa Waziri ajibu kwa sababu ni kweli wanatuangalia, lakini kwa sababu amesema ndiyo amelipata sasa hivi, sasa katika mazingira hayo sijui unafanyakanyaje? Amelipata sasa hivi, amesema kwamba ataliangalia. Sijui ungependa aseme nini wakati amelipata sasa hivi? (*Makofit*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nisingependa kuchafua hata kidogo kwa sababu mimi pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Ndiyo maana nikasema nimelipata sasa hivi, kwa sababu Mheshimiwa Omar Chubi, tumekuwa tunaonana hapa Bungeni na kwa sababu hakunieleza juu ya suala hili, nilikuwa silijui. Sasa labda kama anaweza kunipatia majina ya hao waliopigwa halafu na mimi nitalifuatilia. (*Makofit*)

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo jibu nililokuwa ninalitaka. (*Makofit*)

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi niko kwenye *Programme 10, Administration, subvote 1001*, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzoefu wangu mdogo hapa Bungeni, mara nyingi Mheshimiwa Spika wetu, anapotoa maamuzi mazito huangalia pande zote mbili za Muungano wetu. Je, Mheshimiwa Waziri, anafanya jitihada zipi ili Balozi wa Japan pamoja na Serikali yake, nao waweze kuona umuhimu wa upande wa pili wa Muungano wetu na hatimaye waweze kujenga soko la samaki la kisasa kule Kilimani kama walivyofanya *ferry* Dar es Salaam na Kirumba Mwanza? Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunashirikiana sana na katika sekta mbalimbali. Lakini hata katika uvuvi

nilijitahidi mpaka fedha zikapatikana Ubalozi wa Japan huo huo kwa kujenga soko pale Malindi Zanzibar. Hili nimejibu kwamba, tunalifuatilia na tumezungumza na Balozi wa Japan. Sikutaka kulijibu kwamba, labda Wizara hii si ya Muungano, lakini kama Waziri, mimi nitalifuatilia, nimezungumza na Balozi wa Japan na ninaahidi kwamba, nitazidi kulifuatilia hili suala. (*Makofi*)

MHE. ISAAC M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kuchangia kwangu, nilikuwa na kitu kimoja kwamba, pamoja na kumsifu Mheshimiwa Waziri na kazi yake nzuri aliyoifanya kule Bariadi, wakatujengea shule watu wa *National Parks* na kutuchimbia visima na vitu vingine, lakini kuna tatizo moja kubwa ambalo ni la muda mrefu halijapata jibu, ambalo linahusu watu ambaao walikamatwa kwenye *National Parks* na wako rumande kwa muda mrefu zaidi ya miaka kati ya mitano na kumi, lakini kesi haisikilizwi wala watu waliowakamata hawawapeleki Mahakamani. Sasa nasema kama Serikali inaona hawa watu kuwaweka kule hakuna sababu ya kuendelea na kesi, basi watamke waachiwe hawa watu warudi majumbani. Kuwaweka rumande bila kupelekwa Mahakamani ni kuwanyima haki yao kimsingi. Kwa hiyo, nilikuwa nataka jibu tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na suala hili.

MWENYEKITI: Kesi hii haijafika Mahakamani, maana tusijiingize kwenye Mahakama?

MHE. ISAAC M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba hapa imetajwa kwamba kuna kesi kama 98 za kati ya mwezi Julai hadi Septemba, anasema ziko Mahakamani na nyingine 96 Jumla 329. Lakini hizi ni za miaka ya hivi karibuni. Ninachozungumza ni kwamba, watu wako kule kwa muda mrefu na hakuna Mahakama inayokwenda kuwachukua wale watu na kuweza kuwasikiliza na kupewa haki yao ya msingi. Ndiyo nilikuwa nauliza kama Serikali haiwezi kuendelea hakuna njia yoyote ya msingi ya kuweza kuwatoa wale watu au Mahakama haiwezi kusikiliza hiyo kesi basi hawa watu waachiwe watoke ndani ya rumande.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba, hawa watu walismewa kesi kwa sababu Polisi haiwezi kuwaweka muda mrefu hivyo. Kwa hiyo, suala lao litakuwa bado liko Mahakamani na sijui kama nitawenza kulizungumzia suala ambalo liko Mahakamani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Isaac Cheyo, nadhani umeridhika. Kitu kikiwa Mahakamani hatuwezi kukizungumza?

MHE. ABU T. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie. Kama unavyojuu kuna huo mradi wa barabara kati ya Kidatu na Ifakara, ambaao umefadhiiliwa na Serikali ya Uswiss. Utalii bila barabara hautakamilika. Lakini kabla ya Udzungwa kufanywa *National Park* mwaka 1992, kuna *bonn pits* nyingi zilikuwa zinamilikiwa na *TANROAD*. Sasa hivi wakandarasi wameshachaguliwa lakini kwa sababu ile ni sehemu ya hifadhi, zile *bonn pits* haziwezi kutumika. Kwa hiyo, naamini kabisa Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Maliasili na Utalii, wote wanakuwa na *responsibility* hamna tatizo kati ya hizo Wizara mbili. Sijui kwa

kuzuiwa wakandarasi kutumia hizo *bonn pits* kwa ajili ya kuchukua kifusi na changarawe kutengeneza barabara, Wizara ya Maliasili na Utalii na Ujenzi sijui watatupatia ufumbuzi gani ili huo mradi ambao unafadhiliwa na hawa wenzetu usije ukasitishwa.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri anazungumzia juu ya *Udzungwa National Park*. Katika *National Park* kuna sheria zake kwa kweli. Kwa hiyo, baada ya kuwa *National Park* eneo hilo, suala la kupata kifusi katika eneo hilo haliruhuswi kisheria. Nilimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, haitawezekana. Kwa hiyo, Makampuni yale matatu au wakandarasi watatu itabidi kwa kweli wapate kifusi katika sehemu nyingine.

MHE. ABU T. KIWANGA: Hilo nalielewa vizuri na mimi nilikuwa kwenye *National Park* naelewa kabisa taratibu. Lakini kama nilivyosema hii barabara imefadhiliwa na watu na kiwango maalum cha fedha. Sasa iwapo kama kibali maalum hakitatoka ina maana kuwa lazima tutafute gharama zingine ili kukamilisha uwezekanaji wa kupata kifusi kutoka sehemu nyingine. Sasa Serikali haiwezi kuona umuhimu wa hizo Wizara mbili kukaa na kutafuta ufumbuzi ili kukamilisha huo mradi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri Mheshimiwa Abu Kiwanga, suala hili asiwe na wasi wasi nalo. Kwa sababu Wizara ya Ujenzi ndio iliyotoa tenda na Wizara ya Ujenzi, linapotokea tatizo hilo inawasiliana na Wizara nyingine. (*Makofsi*)

MHE. ALLY A. KARAVINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001. Lakini sina nia ya kushika mshahara wa Waziri, kwa sababu ni mchapakazi sana. Isipokuwa nataka maelezo tu ambayo ni nyeti kidogo kwa ajili ya *WMA* ya Uyumbu. Juu ya yule Meneja wa Ugala aliypunguza kilomita 10 za *WMA* wakati alipoona sisi tunafanya kazi kwa haraka haraka kupata kibali na kutimiza masharti yote yanayotakiwa na Wizara. Bwana Midala akampa mzungu huyo kilomita 10 kwa viashirioshrio vya rushwa. Sasa nasema maelezo huyu Bwana Midala. Mimi na mwenzangu Mheshimiwa Juma Nkumba ambao ndio tumeathirika na huyu Bwana, namna gani maelezo mpaka sasa, maana yake Wilaya ililalamika inaomba aondolewe, Viongozi wote wa Wilaya wote waliomba aondolewe mpaka sasa hakuna kilichofanyika kutoka Wizarani?

La pili, huyu Bwana katika kutimiza malengo yake hayo alivunja na kumwaga takriban mizinga 150 ya asali ya Wananchi ambao walikuwa wamepewa vibali maalum na vibali ambavyo huwa vinatolewa na Halmashauri na huyu Bwana ni *signatory* na akachukua uamuzi *unilateral* wa kufanya hivyo. Sasa nauliza kwa sababu hawa Wananchi wanandidai mimi hiyo asali, sasa maelezo kutoka kwa Waziri juu ya *compensation* au nini itakuwaje? Mimi nataka maelezo na huyu bwana mshahara wake kwa nini usitumike kulipa asali hii? Ahsante sana.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mpaka tumesema tutaliangalia tena. Kwa sababu kilichotokea ni kwamba, kulikuwa na mpaka lakini Afisa Wanyamaporu alipopelekwa kwenye maeneo yale alipunguza eneo hili la mpaka. Huyu bwana aliyelewenda hivi sasa Bwana Midala akataka kuweka

mipaka sawa. Kwa hiyo, kukawa na matatizo pale. Sasa tumesema kwamba, tuta-revisit mpaka wote ili kuangalia ukweli uko wapi na nilisema kwamba, ningependa Waheshimiwa Wabunge pia wakati tunafanya *exercise* hiyo pia wangeweza kuwepo.

Suala la asali au suala la kumwondoa Bwana Midala, ningesema labda pengine tuanze kwanza hili la mipaka halafu baadaye tuangalie suala hilo la Bwana Midala kwa shughuli hizo alizofanya.

MHE. ALLY A. KARAVINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja dogo amesahau juu ya mizinga 150 ya asali. Sasa mimi nilikuwa naomba huu mshahara wa huyu Bwana ungetumika hata kama ni mwaka mzima wa kulipa asali hii ambayo aliimwaga tu na ku-*destroy* hiyo mizinga *unilateral* kama fundisho kwake na wengine wote watakaokuu alipe Wananchi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mimi nafikiri ndugu yangu Mheshimiwa Ally Karavina tukubaliane kwamba, twende mapema sana kati ya eneo lile tuangalie suala la mpaka. Halafu baada ya hapo tuta-*deal* nalo hilo suala lingine. Naomba tukubaliane hivyo kuliko mimi sasa hivi kusema juu ya kumwaga asali.

MHE. OMAR S. KWAANGW: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme nadhani kauli ya Mheshimiwa Waziri sasa ndiyo imeleta utata zaidi. Kwa sababu kilichoko Mbulu ni msitu wa Marang na sio mashamba, Shamba Na. 1, 2 na Na. Labda kama Serikali imefanya kinyemela kubadilisha mpaka wa Wilaya ya Babati. Kwa hiyo ninafahamu kabisa kwamba, mpaka ulioangaliwa upya ni mpaka wa *Marang Forest* ambaao ndio imeonekana kwamba, *Marang Forest* iko Mbulu. Lakini mashamba haya aliyoyataja hapa Mheshimiwa Waziri kwamba yanataka yawe sehemu ya *Lake Manyara National Parks* yako Wilaya ya Babati. Kwa sababu na Waziri ye ye mwenyewe hajafika na pengine taarifa alizopewa sina hakika kama ni sahihi. Ndiyo maana wakati mwingine inatokea hata ile ya magogo, Waziri hapewi taarifa sahihi, Maofisa wanafanya mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati utakapofika nitaomba Kamati Maalum Teule iende kule kwa sababu mgogoro huu ni wa miaka ya kutosha na Waziri alikuwa na nafasi ya kuniuliza kabla hata ya kuandika hotuba yake na ajue hii kitu iko wapi. Waziri hajafika Babati katika muda wote huu. Jimbo langu ndilo lina hifadhi mbili. Sehemu kubwa *headquarters* ya *Tarangire National Park* iko kwangu na sehemu ndogo ya *Lake Manyara National Park*. Kwa hiyo, mgogoro huu naufahamu vizuri sana. Sasa kwa sababu siridhiki, naomba maelezo ya ziada Waziri anasemaje, hajafika ye ye, hajaona kama kweli Marang na sehemu hizi zote ziko Wilaya ya Mbulu, sasa nataka kujua anasema nini?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, suala hili lilikuwepo miaka mitatu, minne, iliyopita na lilifanyiwa kazi kwa kuwaelimisha Wananchi kufanya mikutano nao na nimekuwa napata taarifa zote. Hata Mwenyekiti wa Bodi ya *TANAPA*, kwa wakati huo Mheshimiwa Lusinde, alifika kule pamoa na Viongozi wa *TANAPA*. Wakafanya vikao pamoa na uongozi wa Wilaya na

Mkoa. Kwamba, Shamba Na. 2 na 3 yana hati miliki hivi sasa. Upande wa Shamba Na. 1 lina nyaraka ya kulitoa kwa *TANAPA* tayari. Pia shamba Na. 1 liko katikati ya Shamba Na. 2, lenye hati na mpaka wa sasa wa hifadhi ya Ziwa Manyara. Mashamba yote hayo matatu yaliombwa hasa kwa madhumuni ya uhifadhi na yalikubaliwa kwa sababu hiyo. Vikao kwa mfano vya Wilaya, Mkoa, vya kuidhinisha mashamba hayo yafanywe hifadhi ya Manyara vilifanyika pia. Sasa sijui na kwa sababu najua kikao cha Wilaya na Mkoa kilifanyika pia na imeungwa mkono.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, hajajibu swali langu. Yeye amesema maeneo haya sasa yapo Mbulu na kwamba haya mambo yalikwisha. Mimi nataka kumhakikishia kwamba, haya anayoyasema ya sisi kukutana na *TANAPA* tunayafahamu. Lakini tulikubaliana sasa yaende Halmashauri ya Wilaya kwa sababu yanahu su ardhi ya sehemu ya Wilaya ya Babati. Tukakubaliana kwamba, yakitoka Halmashauri ya Wilaya, basi tuendeleze mazungumzo twende tupate maoni ya Wananchi wa Kijiji cha Mayoka kabla mambo haya hayajakamilika. Mimi nina hakika kuna utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata namna *TANAPA* ilivyonunua haya mashamba yana utata. Hili Shamba Na. 1 Serikali mwaka wa 1972 iliipa Kijiji kipywa cha Mayoka pamoja na Na. 4. Kwa hiyo, historia hii ni ndefu. Sasa kama Waziri anadhani kwamba, hili limekwisha mimi nataka kumwambia kwamba, halijaisha na ndiyo maana naendelea kusema mimi siungi mkono. Ndiyo maana nikasema, kwa kuwa na yeye hajafika na anaonesha hataki *ku-review* hii kitu. Basi mimi niko tayari kusema wakati muafaka nilete hoja hii. Kamati Teule iweze kwenda kule na ni muda sasa Kamati za Bunge ziweze kufanya kazi sawa sawa. Kwa sababu yako mambo mengi ambayo yanafanywa na Serikali bila kuhusishwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya mwisho ya Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Omar Kwaangw', aridhike kwamba, Waziri atalifuatilia hilo jambo na atakuja katika eneo hilo ili waliangalie. Kwa hiyo, naomba aunge mkono hoja ya Waziri na nataka kumhakikishia kwamba, Waziri atafika katika eneo hilo. (*Makofi*)

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Kiongozi wa Serikali hapa Bungeni, nakubali kurudisha shilingi au naunga mkono hoja hadi hapo Waziri atakapofika na tuone jambo hilo upya.

MWENYEKITI: Lakini ulikuwa hujatoa shilingi bwana, lakini imeelewka. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. OMAR S. KWAANGW': Si Shilingi, samahani. Nilisema siungi mkono hoja na kwamba nitakuwa tayari kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule. Sasa kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi mimi nakubali kwamba, sasa jambo hilo liangaliwe upya. (*Makofi*)

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kupitia kifungu 1001 nitafute maelezo tu. Napenda kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hatua kubwa alizochukua kuhusu suala la magogo. Kwa kweli tungependa uzi ukazwe zaidi kwa sababu suala hili la magogo linafanya jangwa lienee kwenye nchi yetu. Uvunaji wa misitu unafanywa sio kwa magogo peke yake lakini uchomaji wa mkaa kwa watu ambao hata hawakuuziwa miti ya Serikali unafanyika kwa kiwango ambacho kinatisha.

Lakini nilikuwa naomba maelezo katika kuvuna malihali na bioanuwai zetu kuna mavuno pia sio ya mbao, sio ya magogo. Kwa mfano, kuna Makampuni ya Kenya yanaendesha uvunaji wa mti wa msandali katika mikoa kama Singida, Arusha nje ya *National Parks*. Mti huu sasa unatoweka. Wanavuna mizizi wanachukua pamoja na mti mzima (*complete tree harvesting*), wanang'oa kabisa mizizi na kubeba kupeleka nchini mwao. Wanatengenezea manukato na madawa mengine. Sasa watu hawa kwanza hatuelewi hivi wana kibali cha kuvuna na kwa nini wavune *complete genetic resource?* Kwa hali ilivyo sasa ni miti tu ambayo iko ndani ya *National Parks* na tuwasifu sana hawa watu wa *National Parks* na *Game Reserves*, kwa kuweza kuhifadhi *genetic resource* hii. Nje ya maeneo haya miti hii karibu inamalizwa kabisa, *complete harvesting* ya *genetic resources* zetu. Sasa tungependa Waziri atupe maelezo kwamba ni hatua gani zimechukuliwa? Kama ikiwezekana basi uvunaji huu na wenyewe upigwe marufuku wa kuondoa mali ambayo haikuwa *processed*, kuiondoa kupeleka nje ya nchi na wenyewe upigwe marufuku kama usafirishaji wa magogo nje ya nchi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Bunge lako Tukufu lingependa kuelewa kwamba, kilo moja ya mti huu wa msandali una thamani ya dola 25. Kwa hiyo, ni mali ambayo kwa kweli ina thamani kubwa ambayo tunahitaji tupate maelezo na kama ikiwezekana Serikali ichukue hatua ya kuilinda. Ahsante sana.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna taarifa kwamba, kuna hizo *sandal wood* ambazo zinavunwa katika maeneo ambayo kama alivyosema nje ya *National Park*. *National Park* mojawapo ni *National Park* ya Manyara. Ndiyo maana tulifikiria pia hata hii *extension* tuliyokuwa tunazungumzia ya mashamba haya ingesaidia maeneo haya kuingia ndani ya *National Park* na kwa hiyo, kuweza kudhibiti. Lakini hata hivyo, tukatumai hivi karibuni kutoa *regulation* ambayo Waziri ana kibali cha kufanya hivyo ili kupiga marufuku usafirishaji wa aina yoyote ya *sandal wood*.

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kifungu hicho hicho 1001. Lakini sina nia ya kushika mshahara wa Waziri. Waziri yeeye ananifahamu kwamba, pale mwisho alipokuwa anamalizia, tulijua alikuwa na muda mdogo sana, sasa hakuweza kutamka kwamba wengine nitawajibu kwa barua matatizo yao. Sasa nataka tu anijibu hoja hizi mbili. Ya kwanza, nimpongeze kwa kazi kubwa aliyoifanya kuchapisha ...

MWENYEKITI: Nafikiri unaelewa kwa nini?

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Naelewa na mimi sikuwafanya hayo.

MWENYEKITI: Nenda moja kwa moja kwenye hoja.

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Ndiyo hoja yenewe Mwenyekiti, kumpongeza. Mimi siwezi kuwafanya hayo nashangaa wao wana-*panic* tu. (*Makofi/Kicheko*)

Nimpongeze kwanza, kwa juhudi kubwa tulizoshirikiana mimi na ye, kuchapisha barabara ya Mikumi mpaka Handeni. Kazi kubwa ni kuokoa wanyama, nampongeza sana. Sasa hawa wanaguna hawaelewii hata faida za wanyama. Kwa hiyo, nimeomba mle kwamba tushirikiane kutafuta na wafadhili kushirikiana na Ujenzi. La pili Mwenyekiti, ni suala la Hoteli ya Mikumi. Hili suala linazungumzwa lakini linaishia hewani na watu wanateta teta wanasema ni hoteli ya wakubwa. Basi wamalize hao wakubwa hiyo hoteli. Kama ni wakubwa kweli kweli wajenge hoteli basi. Wasiwe wakubwa wa kubabaisha. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, atafute wafadhili. Tunao wafadhili kwa mfano yule mfadhili anayemalizia Hoteli ya Kilimanjaro Dar es Salaam pale. Wateja wengi watapenda kwenda Mikumi. Angempa akarabati na hiyo Hoteli ya Serikali ili wakitoka Dar es Salaam wamalizie Mikumi. Mwisho, visima vyangu nimeomba vitano naomba majibu. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namhakikishia Mheshimiwa Christopher Wegga na nilisema pale kwamba, tutajibu kwa maandishi, lakini tunapenda kusema kwamba, tutazidi kushirikiana. Kuhusu Hoteli ya Mikumi ni kwamba, mwenye hoteli alikwenda Mahakamani na hukumu ikatolewa juzi Ijumaa kwamba, alipwe shilingi 3,000,000,000/=. Lakini Serikali ita-*appeal* kwenye *High Court*.

MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amebomoa hoteli alipwe Sh. 3,000,000,000?, ni Mahakama gani, naomba maelezo hiyo Mahakama? (*Makofi/Kicheko*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote na shemeji yangu Mheshimiwa Christopher Wegga, namwomba kabisa atulizane tu. Maadam Serikali imeshatoa taarifa ya kusudio la kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu, basi wasi wasi wake alionao ndio wasi wasi wetu pia na sisi. Kwa hiyo, tutafanya kila linalowezekana angalau Serikali iridhike kweli kile ambacho kimetakiwa kulipwa katika ngazi hiyo ya Mahakama ni halali. Kwa hiyo, naomba tusiwe na wasi wasi, ni taratibu zetu ambazo tumejiwekea za kupata maamuzi kuititia Mahakama.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii. Mimi nikoo katika *Vote 69 - subvote 1001*, lakini pia sina nia ya kushika mshahara wa Waziri. Lakini nataka tu maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Kuna mwekezaji mmoja alipewa shamba la *Mikindani Sisal Estate* miaka mitano iliyopita.

Yule Bwana mwekezaji baada ya kupata lile shamba la Mkonge pale ndani ya lile shamba kulikuwa na mashamba ya baadhi ya wakulima wa maeneo yale wanayoishi ndani ya lile eneo la Kabisera. Kulikuwa na majumba ya watu pamoja na nyumba ya Mungu (Msikiti). Yule Bwana alipopewa lile eneo alichokifanya ni kuchukua tingatinga kubomoa majumba yote ya watu waliokuwa wanaishi ndani ya eneo lile na akabomoa nyumba ya Mungu (Msikiti) pia ameubomoa kwa tingatinga.

Sasa nataka nimweleze Mheshimiwa Waziri kwamba, miaka yote yule mwekezaji eneo lile alilolipata hakuna alichokifanya zaidi ya kuweka uzio wa umeme. Ni hatari kweli Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majirani wanaoishi karibu na lile eneo. Sasa hivi majirani wanaoishi karibu na eneo lile, watoto wao sasa hivi wanawaweka kwenye matenga. Kwa sababu ni hapa na pale tu ukiwaachia tu wamekwenda kukutana na uzio wa umeme na hakuna maendeleo yoyote aliyoafanya. Sasa tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kila Bunge la Bajeti leo karibu miaka mitatu Wabunge wanalamika kuhusu suala hili lakini majibu tunayoyapata haturidhiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tena kwamba yule Bwana sasa anabadili matumizi ya lile eneo. Mwaka 2003 tuliambiwa kwamba, sasa nataka kufanya *zoo* alete simba pale. Sisi tuna simba *natural* pale. Unataka kuleta simba wa nini, tunashangaa! Lile ni eneo la shamba la mkonge, anataka kuleta simba. Kwa taarifa nyingine nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri sasa hivi amebadilisha mpaka biashara, sasa amejiingiza katika biashara ya utalii. Sisi Mtware tuna maeneo ya utalii ambayo maeneo mengine hamna. Sisi tunapewa sehemu ambayo inaitwa *White Sand*, yaani Msimbati Uvura, kuna *White Sand pure*. Yakitoka tu maji yakichelewa dakika ile unaweza ukapita na gari kwenye ule mchanga.

Sasa yule mzungu alichokifanya ni kwamba, kutumia eneo lile la mkonge yuko karibu na bahari amenunua boti yake na amefungua baa moja sasa hivi anavusha watu. Lakini ile boti sasa hivi inavusha watalii kutoka Msumbiji kuwaleta Uvura pale Msimbati na kuwarudisha tena Msumbiji. Kwa hiyo, watalii wengi wanaokuja eneo lile wanashukia Msumbiji kuja pale na kurudi tena Msumbiji. Yule Bwana ndio anatumia boti yao. Sasa tunaomba tumpe taarifa hii Mheshimiwa Waziri na kwa kweli ni kero kubwa. Waheshimiwa Madiwani, wamekaa kwenye Mabaraza ya Madiwani wamepitisha, lakini watendaji hawataki kuleta yale maamuzi ya Madiwani kwa Mheshimiwa Waziri. Sasa tunaomba awaagize au kama yuko tayari basi akakutane na wale Waheshimiwa Madiwani ili wamwambie ukweli uliokuwepo. Kwa sababu wanazuiwa na wale watendaji. Kwa hiyo, tunaomba majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka shamba hilo mimi binafsi baada ya kipindi kilichopita, nililitembelea shamba hilo pamoja na Uongozi wa Wilaya. Lakini niseme kwamba, mwekezaji wa shamba hilo hakupewa kibali chochote cha *zoo*. Kwa hivyo, hakuna kibali kutoka Wizarani kwangu ambacho kimempa uwezo wa kuwa na *zoo* katika eneo hilo. Labda niseme kwamba, itabidi kuwasiliana na Uongozi wa Wilaya na Mkoa ambao ulikuwa katika sehemu hiyo. Lakini Wizara haijatoa kibali hicho.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini nafikiri alipotembelea lile eneo ameona na kuna uzio wa seng'enge wa umeme ambao umewekwa katika eneo lile ambalo ni hatari sana kwa Wananchi wanaishi jirani naye. Sasa tunaomba atusaidie, amwagize yule Bwana ile seng'enge umeme ule auzime. Ni hatari kwa sababu watu wanashindwa hata kwenda kulima. Sasa kama mtu utashindwa kwenda shambani kwako ni hatari. Watakuwa wale watu Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tunaomba kwamba, lile eneo lililozungushwa na seng'enge ya umeme basi pia atoe tamko hapa kwamba, Bwana mara moja ile seng'enge iondolewe.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Niseme tutafutilia maana yake ni sehemu ambayo ni *private property*, lakini tutafutilia juu ya hili.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 - *Finance and Account* Sh. 711,722,700/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* Sh. 494,671,900/=

(Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2001 - *Wildlife* Sh.7,033,537,900/=

MHE. GWASSA A. SEBABILITY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naafiki kifungu hicho mara mia moja. Lakini kwa sababu kuna uharibifu mkubwa unaofanya katika Pori la Akiba la Kimisi kule Ngara na kwa bahati kwa sababu Mheshimiwa Waziri, alikuwepo kule tarehe 21 mpaka 22 Mei, 2004 na ameshuhudia mwenyewe uharibifu uliopo na kwa bahati nzuri sasa wawili wapendanao na wanaofanya kazi kwa kuaminiana na ndio wanasa Diana hapa, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi yuko pale anasikia.

Naomba tu kusaidiwa iwapo Waziri anaweza kutamka kuwa, watashauriana na kushirikiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuweza kutuma watumishi kuja kuokoa ile mali ya Taifa ambayo inateketezwa na wahujumu kutoka nchi ya jirani. Ni hilo tu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ameniambia tutashirikiana. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping* Sh.8,345,664,400/=
Kifungu 3002 - *Fisheries* Sh.5,998,210,400/=

Kifungu 4001 - *Tourism* Sh.2,815,766,100/=
Kifungu 4002 - *Antiquities Unit* Sh.1,120,862,900/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* Sh.3,319,541,400/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2001 - *Wildlife* Sh.2,709,102,000/=

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilichangia kwa maandishi na nilimkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, tunapakana na Hifadhi za Taifa moja ya Orumanyika Lugundu pamoja na ya Ibanda ambako niliwahi kuuliza swali hapa Bungeni na nikamwambia kwamba watu wake walikwenda wakajiwekea mipaka wakachukua ardhi ya Wananchi na akaahidi kwamba, angeunda Tume Ndogo ya kwenda kuchunguza hilo, lakini halijafanyika. Kwa hiyo, niliuliza amefikia wapi? Hilo la kwanza.

Lakini la pili niliuliza kwamba, kuna ardhi ambayo iko katika eneo la Kimisi inapakanana na Jimbo la Mheshimiwa Gwassa Sebabi, ambayo asubuhi Mheshimiwa Janet Kahama, alikuwa anatutania kwamba, kuna rasilimali hatujazitumia. Sasa Council pamoja na mimi nilikuwepo, Wajumbe walikataa na ushahidi upo, lakini Uongozi wa Mkoa ulilazimisha kwamba, eneo hilo liwe Hifadhi ya Taifa, wakati sisi tuna upungufu wa ardhi. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri katika hilo amechukua hatua zipi?

NAIBU SPIKA: Ninataka kutoa tahadhari, bado dakika mbili tu kwa majadiliano haya.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, anaweza kurudia sijasikia vizuri, angezungumza kidogo kidogo?

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nimechangia kwa maandishi, nimekukumbusha kwamba, mwaka 2001 wakati wa bajeti niliuliza swali kuhusu Orumanyika Lugundu, ambako wapimaji wako walichukua ardhi ya Wanakijiji na ukaahidi kwamba, ungeunda Kamati Ndogo ya kufuatilia na hukuunda. Sasa ninauliza umefikia wapi?

La pili ni kwamba, kuna ardhi ambayo ilikuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ambayo sasa imeamuliwa, lakini siyo na Halmashauri yenyewe bali na Uongozi

wa Mkoa kwamba, iwe *game reserve*. Sijui kama umepata taarifa hizo na unachukua hatua zipi?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kama halijafanyika basi tutaagiza watu wetu wafanye. Lakini hili la pili juu ya *game reserve*, utaratibu wa sasa ni kwamba, kabla ya eneo kuwa *game reserve* ni lazima mikutano ifanyike katika ngazi ya Vijiji, ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa, ndipo ambapo inakuja kwenye Wizara. Kwa hiyo, kwa upande wetu kama haijapitia katika ngazi zote hizo, basi Wizara haitaweza kukubali jambo hilo. (*Makofii*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 3001 - *Forestry and Beekeeping* Sh.10,387,011,800/=
 Kifungu 3002 - *Fisheries* Sh. 300,000,000/=
 Kifungu. 4001 -*Tourism* .. Sh. 668,436,600/=
 Kifungu. 4002 -*Antiquities Unit* .. Sh. 1,586,407,600/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2004/2005, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio hayo.

Mhesimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa
Mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, makadirio ya Wizara hii yamepitishwa rasmi na Bunge hili. Baada ya kufika hapo tumemaliza shughuli za leo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 01.37 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano

tarehe 28 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)